Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 1

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page A

بسم الله الرحمن الرحيم

KANUNI ZA NDOA

NA

MAADILI YA FAMILIA

Kimeandikwa na:
Hujjatul-Islam Ibrahim Amini

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page B

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 9987-427-12-X

Kimeandikwa na:
Hujjatul-Islam Ibrahim Amini

Kimetajumiwa na:
Al-Akh Salman Shou
S. L. P. 19701, Dar-es-Salaam, Tanzania
Email:info@alitrah.org
Website:www.alitrah.org

Kimehaririwa na:
Dr. M. S. Kanju
S. L. P. 19701, Dar-es-Salaam, Tanzania
Email: mokanju2000@yahoo.com
Website:www.alitrah.org

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Ukhti Pili Rajab

Toleo la kwanza: Agosti 2005
Nakala: 2000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Al-Itrah Foundation
P. O. Box 19701, Dar-es-Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Fax: +255 22 2113107
Email: info@alitrah.org
Website: www.alitrah.org

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page C

YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA

Wajibu wa wanawake

Misingi ya ndoa na maadili ya familia 2

Utangulizi 4

Wajibu wa wanawake 9

Kuishi na Mume 13

Wema 15

Heshima ya Mume 17

Malalamiko na manung'uniko 19

Tabia za kupenda 22

Matarajio mabaya 26

Uwe faraja kwa Mumeo 28

Uwe mtu wa kuonesha shukrani 30

Usitafute dosari za mwenzako 32

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page D

Usimwangalie mtu yeyote isipokuwa Mumeo 35

Vazi la hijabu la Kiislamu 37

Samehe makosa ya Mumeo 41

Kuweza kuishi na ndugu wa Mumeo 42

Kuvumilia kazi ya Mume wako 44

Endapo mnatakiwa kuishi nje mji wa nyumbani 48

Kama Mume afanya kazi nyumbani 50

Msaidie Mume wako kupata maendeleo 52

Kuwa mwangalifu kwa Mume wako asipotoshwe 54

Wenawake wenye dhana 58

Kumridhisha Mume wako na si mama yako 73

Uwe safi na mrembo nyumbani 78

Uwe kama mama kwake 80

Hifadhi siri za familia 81

Kubali Uongozi wake 82

Uwe Muelekevu wakati wa hali ngumu 85

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page E

Usikatae kusema na usinune 87

Mume wako akikasirika, wewe nyamaza 90

Burudani za Wanamume 92

Utunzaji wa nyumbani 93

Usafi 95

Nyumba nadhifu 98

Kutayarisha chakula 102

Kupokea Wageni 107

Mdhamini wa nyumba 113

Kazi za wanawake 115

Usipoteze muda wako wa akiba 119

Umama(utunzani wa mtoto) 121

Lishe na Afya 125

SEHEMU YA PILI

Wajibu wa Mwanamume 129

Mlezi wa Familia 129

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page F

Utunzajiwa Mke wako 130

Mpende mkeo 131

Mheshimu Mke wako 135

Uwe na tabia njema 137

Kulalamika kusiko na lazima 143

Kuanzisha ugomvi 145

Mridhishe na mliwaze mke wako 147

Usitafute makosa yake 149

Puuza mazungumzo ya uongo ya wakosoaji 152

Samehe makosa ya mke wako 158

Uwe msikivu 166

Haki za kinidhamu za Mume 171

Wanamume wa kutuhumu 176

Mwanamke asiye mwaminifu 184

Usitamani Wanawake wengine 186

Uwe mwenye kushukuru 190

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page i

Pia uwe msafi nyumbani 192

Mtunze mke wako 194

Uchumi wa Familia 196

Saidia kufanya kazi za nyumbani 199

Rudi nyumbani mapema 201

Uwe mwaminifu 202

Elimu na mafundisho 204

Kupata mtoto 207

Ujauzito na kuzaliwa Mtoto 216

Kikwazo kikubwa katika kusuluhisha tofauti 220

Talaka 222

Ufafanuzi wa hadithi 229

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page ii

بسم الله الرحمن الرحيم

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza, kwa jina la ***"PRINCIPLES OF MARRIAGE & FAMILY ETHICS"*** kilichoandikwa na Mwanachuoni: **Ibrahim Amini.**

Ni ukweli ulio wazi kwamba katika jamii yetu hatujishughulishi sana na somo hili, kana kwamba Uislamu hausemi chochote kuhusu maudhui hii. Ni jambo la kusikitisha kwamba tunawaozesha watoto wetu bila kuwafundisha kanuni za ndoa na maadili ya familia. Matokeo yake ni kwamba, kwa vijana wetu kukosa somo hili muhimu, kumekuwa na migongano mingi na mizozo isiyokwisha katika maisha yao ya ndoa, na hatimaye ni talaka zisizokifani na za kiholela mno katika jamii yetu.

Katika kitabu hiki mwandishi amefanya jitihada kubwa kufanya utafiti na uchunguzi wa kina wa somo la mfumo wa maadili ya familia na uhusiano wa mume na mke, kwa mtazamo wa Kiislamu. Tumekiona kitafaa sana katika jamii yetu hii ambayo imemomonyoka mno kimaadili kwa kuiga tamaduni za kimagharibi ambazo zimewapotosha wengi katika vijana wetu.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page iii

Kwa ajili hii tumeona tukitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili ili jamii yetu, hususan vijana wetu wanaotarajia kufunga ndoa na wale ambao tayari wako kwenye ndoa wanufaike na somo hili, ambalo kwa hakika ni muhimu sana. Na hili likuwa ndilo lengo kubwa la **Taasisi yetu ya 'Al-Itrah Foundation'** katika kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu **Salman Shou** kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vile vile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni mwanga kwa wasomaji wetu na kuzidisha upeo wao wa elimu katika dini.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S.L.P. 19701
Dar-es-Salaam. Tanzania.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page iv

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 1



Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 2

KANUNI ZA NDOA
NA
MAADILI YA FAMILIA

DIBAJI

Jamii ya binadamu ni mkusanyiko wa familia nyingi. Uislamu unatilia maanani sana kwenye furaha halisi na ufanisi wa wanadamu kwa njia ya ulinganifu wa Kiislamu, maadili ya hali ya juu, familia zenye elimu, na zenye tabia nzuri na nyumba zenye furaha. Kama ilivyo katika maeneo yote ya shughuli za binadamu, Uislamu umeweka wazi na kinaganaga haki na wajibu wa wanaume na wanawake, waume na wake (walio kwenye ndoa) na pia wazazi na watoto. Familia zenye furaha zilizo na mazingira yenye kufurahisha, ambamo mume, mke na watoto na ndugu wengine huishi pamoja kwa uchangamfu na uelewano wa pande mbili, ustahamilivu na heshima na kutimiza wajibu wao kwa ihusikavyo kwa kila mmoja wao, kwa hakika ni kielelezo cha hadhi ya juu zaidi ambacho Mweyezi Mungu Mweza wa yote amewabariki wanadamu miongoni mwa viumbe wote.

Kwa bahati mbaya, upungufu wa kutokufahamu vipengele hivi, hususan kwa waume na wanawake, husababishia kwenye matatizo mengi kwao wenyewe na halikadhalika kwa watoto - vizazi vijavyo. Kwenye nchi za magharibi zilizoendelea, zenye kupiga hatua zaidi, mafanikio makubwa zaidi ya kiteknolojia, kisayansi na mwenendo wa maisha ya kasi ya kisasa zaidi; huko kiwango cha kutalikiana na kutengena kinatisha.

Kwa kulichukulia umuhimu wa somo hili, ICRO (Kitengo cha utamaduni cha Kiislamu - Iran) kinachukuwa fursa ya kuchapisha kitabu hiki (kwa asilia katika lugha ya Kifursi) kilichoandikwa na msomi

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 3

maarufu wa Kiislamu, mwandishi mwenye kujulikana Profesa mwandamizi wa maarifa ya sheria za Kiislamu katika Hawzah Ilmiyah (Islamic Theological Centre), Qum, Iran, Hujjatul-Islam Ibrahim Amini. Mwandishi amefanya jitihada kubwa katika kufanya utafiti na uchunguzi wa kina wa somo la mfumo wa maadili ya familia na uhusiano wa mume na mke. Sehemu ya kwanza inaongelea wajibu wa wanawake na sehemu ya pili inaongelea wajibu wa wanaume. Pamoja na wajibu, haki za waume kwa wake na zile za wake kwa waume pia zimeelezewa kwa kunukulu Aya za Quran Tukufu na Hadith. Ni matumanini yetu kwamba kitabu kitakuwa chenye manufaa kwa wote na kila familia itakifanya kuwa hazina ya kupata faida ya upeo wa juu sana katika kuanzisha na kudumisha mazingira safi na ya kufurahisha, yaliyojaa baraka za Mwenyezi Mungu.

Department of Taranslation and Publication,
Islamic Culture and Relations Organization.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 4

UTANGULIZI

Hamu kubwa sana ya vijana wote wanaume na wanawake ambao hufikia umri wa balekhe ni kuoa au kuolewa. Kwa kuanzisha maisha ya pamoja ya ndoa, wangepata kujitegemea zaidi na pia kupata mwenza mwema na wa kuaminika. Wanaangalia maisha ya ndoa kama mwanzo wa ustawi wa maisha yao.

Mwanaume ameumbwa kwa ajili ya mwanamke halikadhalika mwanamke ameumbwa kwa ajili ya mwanaume. Kila mmojawao anao mvuto kwa mwenzake kama sumaku. Ndoa na kuanzisha maisha ya pamoja ni hamu ya kawaida ya mwanadamu na ya kukubaliana na silika zao. Ndoa inafikiriwa kuwa mojawapo ya neema kubwa sana kutoka kwa Mungu. Kwa kweli ni wapi kwingineko ambako mtu angeweza kupata hifadhi bora zaidi kwa ajili ya ujana kuliko kitengo cha familia yenye kuaminika? Ni hamu ya kupata familia ambayo humlinda kijana asifuatilie njozi zisizo na mantiki na duku duku la ndani. Muungano wa ndoa huwawezesha wahusika kupata mwenza mwema na mwaminifu ambaye ataweza kuwa tayari kushirikiana katika wakati mgumu na wa matatizo. Mkataba mtakatifu wa ndoa ni kamba ya Mungu inayoziunganisha nyoyo, huzibembeleza zinapokuwa zimefadhaika na kuzielekeza njozi zisizo na mantiki kwenye lengo lililo bora. Familia ni kituo cha mapenzi, wema na urafiki ambapo ni mahali pazuri zaidi pa kuishi kwa starehe. Mwenyezi Mungu Mweza wa yote ameitaja neema hii kwenye Qur'an Tukufu:

﴿ وَمِنْ ءَايَـٰتِهِۦٓ أَنْ خَلَقَ لَكُم مِّنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَٰجًا لِّتَسْكُنُوٓا۟ إِلَيْهَا
وَجَعَلَ بَيْنَكُم مَّوَدَّةً وَرَحْمَةً ۚ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَـَٔايَـٰتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١﴾ ﴾

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 5

"Na katika Ishara zake ni kuwa Amekuumbieni wenza kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila shaka zipo Ishara kwa watu wanaofikiri." (**Quran 30:21)**

Mtume (s.a.w) wa Uislamu alisema: "Mwanaume ambaye hakuoa hata kama ni tajiri kwa hakika ni masikini na mhitaji; na hivyo hivyo kwa mwanamke."

Imam Sadiq (a.s) alimuuliza mtu, "Je! Umeoa?" Mtu huyo akajibu, "Hapana" Imam aksema: "Nisingependa kuishi bila kuoa hata kwa usiku moja tu, hata kama ningekuwa nina miliki dunia yote."

Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema: "Hakuna taasisi katika Uislamu iliyobuniwa na Mwenyezi Mungu ambayo anaipendelea na kuipenda zaidi kuliko ndoa."

Pamoja na kwamba Mwenyezi Mungu Mwenye huruma amewajaalia wanadamu neema yenye thamani kubwa kama hii, wao hawaifurahii, na wakati mwingine kwa sababu ya ujinga na ubinafsi, huugeuza muungano huu wa upendo na ulio barikiwa kuwa jela yenye giza au hata jahanamu iwakayo moto! Hii ni kwa sababu ya ujinga wa mtu mwenyewe kwamba, jamaa wa familia wanalazimika kuishi kwenye jela hili yenye giza au kwamba mkataba huu wa ndoa takatifu unavunjiliwa mbali.

Kama wanandoa wanafahamu wajibu wao na kutenda kufuatana na maelekezo yake, basi nyumba itakuwa mahali pa urafiki na kufanana na Pepo. Lakini, kama zipo tofauti za kifamilia na mabishano, nyumba ya familia, kwa kweli itageuka kuwa jela. Tofauti za kifamilia huletwa na sababu mbali mbali, kama vile hali ya kiuchumi, historia ya familia ya mwanaume na mwanamke, mazingira ya maisha, uingiliaji usio na sababu

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 6

wa baba, mama na ndugu wa pande zote mbili, na sababu zingine nyingi. Lakini, kwa mujibu wa mwandishi, jambo muhimu zaidi ni ujinga wa mume na mke kuhusu wajibu wao na kutojitayarisha vya kutosha kukabiliana na maisha ya ndoa. Kwa jumla, ili kazi itimizwe, utaalamu na matayarisho ni sifa muhimu zinazohitajika. Kama mtu anakosa ujuzi muhimu na matayarisho, basi hawezi kufuzu katika kufanikisha lengo analo litaka. Hivyo, madarasa ya kuwafundisha na kuwaelimisha watu kwa ajili ya majukumu mbali mbali huanzishwa.

Utaalamu, utayarishaji na ujuzi ni sifa zinazohitajiwa pia katika ndoa. Kijana wa kiume lazima awe na taarifa za kutosha kuhusu kanuni za maadili ya mke wake na matamanio yake ya moyo. Lazima pia afahamu matatizo ya ndoa na njia za kuyatatua. Asifikirie ndoa kuwa kama kununua mali, kukodisha mfanya kazi wa kike, lakini akubali kwamba ndoa ni mkataba wa urafiki, uaminifu, wema, ushirikiano na muungano katika maisha ya pamoja ya familia.

Kijana mwanamke pia lazima afahamu falsafa ya maisha ya mume wake na matakwa yake. Asifikirie kwamba ndoa ni kama kumwajiri mtumishi kwa lengo la kutimiza mahitaji bila ya mapatano na masharti; lakini kama ahadi ya urafiki wa ushirikiano na muungano katika kufanya jitihada kwa ajili ya kuendesha maisha. Ili kuweza kupata ushirikiano ulio fuzu, ipo haja ya kuelewana, ushirikiano na moyo wa mapenzi.

Ingawa maisha ya baadaye ya vijana wa kiume na wa kike zaidi hutegemea ndoa ambayo inahitaji utambuzi wa umuhimu wa fikra za ndoa na matayarisho ya kuifanya kazi kama hii, kwa bahati mbaya jamii yetu hupuuza umuhimu wa masharti haya.

Zaidi wazazi huzingatia mambo kama mahari, uzuri wa sura na haiba. Hata hivyo, hupuuza kujiweka tayari kwa ajili ya kuanzisha maisha ya

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 7

ndoa kama sharti muhimu. Wanawaoza watoto wao wa kiume na wa kike bila kuwapa taarifa ya kutosha kuhusu maisha ya familia.

Matokeo yake, vijana wawili na watu wasio na uzoefu huingia kwenye maisha mapya na kukabiliana na matatizo mengi. Kutofautiana, mabishano na kupigana huanza kujitokeza. Hapo sasa wazazi wao ndio huingilia kati kwa lengo la kusaidia kusuluhisha migongano. Lakini kwa kuwa uingiliaji wao huwa wa upendeleo zaidi, migongano hukuzwa na hali huwa mbaya zaidi.

Miaka ya kwanza ya maisha ya familia huwa imejaa matukio na matatizo mengi. Hiki ni kipindi ambapo familia nyingi huvunjika kwa kutalikiana na kutengana. Baadhi yao huendelea na ndoa zao na kupendelea jela hii ya kujitakia wenyewe kuliko kutalikiana, na familia nyingine hujifunza zaidi kuhusu mwenziwe na hutengeneza kiasi fulani cha maisha ya starehe.

Ingekuwa ubora ulioje kama pangekuwepo na jinsi ya kuwaeleimisha na kuwafahamisha vijana wa kiume na wa kike kuhusu misingi na uanzishwaji wa ndoa katika namna ya madarasa yatakayoitwa **"matayarisho ya ndoa"** ambayo yangewatayarisha wao kuanzisha familia zao. Ninayo matumaini kwamba ipo siku ambapo utaratibu kama huo utaanzishwa.

Kitabu hiki kimeandikwa katika misingi ya umuhimu huu. Katika kuanzimia masuala ya kitabu hiki, nimetegemea Qur'an Tukufu, hadith za Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na Maimamu maasum (a.s.) pia na takwimu za kawaida na uzoefu wangu mwenyewe.

Ingawa miongozo fulani ya ndoa iliyo bora imeandikwa, siwezi kudai kwamba matatizo yote ya familia yanaweza kutatuliwa kwa kusoma kitabu hiki. Inatumainiwa kwamba kitabu hiki kitaonesha ujuzi na utambuzi ulio bora zaidi kwa wale wanaoyapitia matatizo ya ndoa na familia. Inategemea

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 8

sana kwa hao wenye madaraka ambao wataona umuhimu wa jambo hili, kuchukua hatua za maana ili kuweza kuwasaidia wale wanaosumbuliwa na maumivu na mateso ya kuharibika na migongano ya familia (Insha Allah).

Kitabu hiki kimegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu wajibu wa wanawake kwa waume zao na sehemu ya pili inazungumzia wajibu wa wanaume kwa wake zao. Lakini wanaume na wanawake wanatakiwa kusoma sehemu zote mbili ili waweze kupata ujuzi mzuri wa jambo hili. Kwa kusoma sehemu moja tu ya kitabu, msomaji anaweza kuhisi ubaguzi kwa kupendelea upande moja na kuchukia upande mwingine; lakini, kusoma sehemu zote mbili, msomaji atakiri kwamba hivyo sivyo.

IBRAHIM AMINI
Qum, July, 1975.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 9

SEHEMU YA KWANZA

WAJIBU WA WANAWAKE

Madhumuni ya ndoa

Ndoa ni haja ya kawaida kwa kila mwanadamu. Inayo manufaa mengi na mazuri, baadhi ya hayo manufaa mengi na mazuri yaliyo muhimu ni haya: Ujengaji wa familia ambayo kwayo mtu anaweza kupata usalama na utulivu wa akili. Mtu ambaye hakuoa au kuolewa hufanana na ndege asiye na kiota. Ndoa hutoa huduma ya hifadhi kwa kila mtu anayehisi amepotea kwenye maisha yasiyo na mpango; mtu anaweza kupata mwenzi wa maisha ambaye anaweza kushirikiana naye katika furaha na huzuni.

Matamanio ya kawaida ya kijinsia yana nguvu na yenye maana. Kila mtu anatakiwa kuwa na mwenzi kwa lengo la kujitosheleza kijinsia kwenye mazingira yaliyo salama na tulivu. Kila mtu anapaswa kufaidi raha mustarehe ya kijinsia katika namna iliyo sahihi na inayostahiki. Wale wanao jiepusha na ndoa mara kwa mara husumbuliwa na maradhi ya kimwili na kisaikolojia. Maradhi hayo na matatizo fulani ya jamii ni matokeo ya moja kwa moja ya vijana kujiepusha na ndoa.

Uzazi: Kupitia kwenye ndoa, binadamu wanaendelea kuzaana. Watoto ni matokeo ya ndoa na ni vipengele muhimu katika kuimarisha misingi ya familia na halikadhalika kama chanzo cha furaha kwa wazazi wao. Msisimko mkubwa sana umebainishwa kwenye Qur'ani Tukufu na Hadith kuhusu ndoa na kupata watoto. Mwenyezi Mungu Mweza wa yote anasema kwenye Qur'ani Tukufu:

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 10

﴿ وَمِنْ ءَايَـٰتِهِۦٓ أَنْ خَلَقَ لَكُم مِّنْ أَنفُسِكُمْ ﴿٢١﴾ ﴾

"Na katika Ishara zake ni kuwa Amekuumbieni wenza kutokana na nafsi zenu…" (30:21).

Mtume (s.aw) alisema: "Hapana muundo ulio bora zaidi ulio asisiwa katika Uislamu kuliko ndoa."

Imam Ali (a.s) alisema: "Shiriki katika ndoa; kwa sababu hii ni Suna ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w)."

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Yeyote anayefuata Suna yangu lazima aowe na kuzaa watoto ambao ni matokeo ya ndoa na kuongeza umma wa Waislamu ili kwamba katika Siku ya Ufufuo nitakabiliana na umma wa mataifa mengine nikiwa na idadi kubwa ya umma wangu."

Imam Ridha (a.s) alisema: "Mafanikio makubwa sana ya mtu ni kuoa mke mwaminifu, ambaye kila amuonapo anafurahi na hulinda mali yake na heshima yake mwenyewe wakati akiwa hayupo."

Kilichozungumziwa katika sura hii kwa upande wa ndoa ni mambo yahusuyo dunia na maumbile tu ambayo pia wanyama wanayo; manufaa ya urafiki na kuzaana. Kama ilivyo madhumuni ya kweli ya ndoa kwa jamii ya binadamu ni ya aina tofauti. Binadamu hakukusudiwa kuingia katika dunia hii kwa sababu ya kula, kunywa, kulala, kutafuta starehe au kuendekeza ashiki na halafu kufa na kuharibika. Hadhi ya mwanadamu ni ya juu zaidi kuliko matendo kama hayo. Wanadamu wanakusudiwa kujifunza wenyewe na roho zao katika kupata ujuzi, kufanya matendo

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 11

mema na kuwa na tabia njema. Binadamu amekusudiwa kuchukua hatua kwenye njia iliyonyooka ili apate ukaribu wa Mwenyezi Mungu Mweza wa yote.

Mwanadamu ni kiumbe ambacho kinaweza kusafisha roho yake kwa kuepuka matendo maovu na kujizoeza kuwa na tabia njema hufikia kiwango cha hadhi ya juu sana ambayo kwamba hata malaika hawezi kuipata. Binadamu ni kiumbe ambacho ni cha milele. Amekuja hapa duniani ili kwa mwongozo wa manabii na utekelezaji wa utaratibu uliowekwa na dini ya Uislamu, aweze kupata furaha yake hapa duniani na Peponi, ili kwamba aweze kuishi maisha ya amani katika dunia ijayo daima milele.

Kwa hiyo, madhumuni ya ndoa lazima yatafutwe katika muktadha huu wa kiroho. Lengo la ndoa kwa mtu wa dini lazima iwe ni njia ya kuepusha matendo maovu na kutakasa roho kutokana na madhambi. Lazima iwe ni njia ya kupata ukaribu kwa Mwenyezi Mungu Mweza wa yote. Ni katika muktadha huu kwamba mwenza anayefaa na mwema huchukua jukumu muhimu.

Waumini wawili wanapounda familia kupitia katika ndoa, uhusiano wao wa kijinsia utawanufaisha katika kuimarisha mapenzi na wema wao, kwa wanandoa wa aina hiyo hapangekuwepo na hatari ya kutishia potovu wa kijinsia, mazoea mbaya au matendo ya haramu. Mtume (s.a.w) wa Uislamu na Maimamu wote (a.s) wamesisitiza sana kuhusu taasisi hii ya ndoa.

Mtume (s.a.w.w) alisema: “Yeyote anayeoa amelinda nusu ya dini yake.”

Imam Sadiq (a.s) alisema: “Rakaa mbili za Swala ya mtu aliyeoa ni zaidi ya rakaa sabini za Swala ya mtu ambaye hakuoa.”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 12

Mumini mchamungu na mwenzi mpatanifu hutekeleza jukumu la maana sana katika kupata na maisha ya kuheshimika na kuaminika. Kwa kweli kuwa na mwenzi wa aina hii ni kipengele muhimu kwa mtu anapotaka kuepuka matendo maovu na kuwezesha msimamo wa mtu katika kutekeleza matendo ya wajibu ya ibada. Wanandoa wachamungu, si tu kwamba hawatakutana na vikwazo vyovyote katika kufanikisha malengo ya kidini, bali watakuwa chanzo cha kutiana moyo wenyewe kwa wenyewe.

Je, inawezekana kwa mtu muumini wa Mwenyezi Mungu kupigana kwa utukufu katika njia Yake bila ya uthibitisho wa mke wake? Je, inawezekana mtu yeyote mchamungu kupata riziki yake kihalali, kwa kuzingatia vipengele vyote vya kidini, kulipa sadaka iliyoamriwa kisheria ili kuepuka ubadhirifu, na kutumia katika kutoa msaada bila ya idhini ya mkewe?

Mchamungu kila mara angemlingania mwenzi wake kwenye wema, kama vile ambavyo mtu mpotovu angemshawishi mwenzi wake kuwa mpotovu. Halafu ni jambo la maana kwamba kwenye Uislamu wanamume na wanawake ambao wanataka kuoa au kuolewa wanashauriwa kuangalia usafi na tabia njema za wale wanaotaka kuwa wenzi wao katika maisha ya ndoa, kama masharti ya muhimu.

Mtume (s.a.w.w) alisema: “Kama ingetokea mimi nimpe mtu Mwislamu mazuri ya dunia na akhera, ningemjalia moyo wa unyenyekevu, ulimi ambao ungetamka sifa Zake mfululizo, mwili wenye kuvumilia maafa yote, na ningempa mwenza katika ndoa mchamungu ambaye akimuona tu anafurahi, na analinda mali yake na heshima yake mwenyewe asipokuwepo.”

Mtu mmoja alikwenda kwa Mtume na akasema: “Ninaye mke ambaye hunikaribisha nyumbani kila ninaporudi na hunisindikiza hadi mlangoni

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 13

ninapoondoka. Anaponiona mimi nimehuzunika na sina furaha, kwa kuniliwaza na husema: 'Kama unafikiria kuhusu riziki, basi usikate tamaa, kwa sababu Mwenyezi Mungu ndiye anayetoa riziki na kama unafikiria maisha yajayo, basi Mwenyezi Mungu na akuongeze akili yako na jitihada zako.' Halafu Mtume (s.a.w.w) akasema; "Hakika Mwenyezi Mungu anao watendaji na wawakilishi hapa duniani na mke ni mmojawapo. Mwanamke wa namna hii atazawadiwa thawabu nusu ya mtu aliyejitolea mhanga."

Imam Ali (a.s) alikuwa anafikiria haya haya aliposema kuhusu Hadhrat Zahra (a.s). Alisema kwamba mkewe alikuwa msaada mkubwa katika kumcha Mwenyezi Mungu Mweza wa yote. Historia inatuambia kwamba, siku moja kipindi kifupi baada ya harusi ya imam Ali (a.s) na Hadhrat Zahra (a.s), Mtume (s.a.w.w) alikwenda kuwapongeza nyumbani kwao na kujua hali yao. Alimuuliza Imam Ali (a.s): "Unamuonaje mkeo?" Imam akajibu; "Nilimuona Zahra kama msaada mzuri sana katika kumuabudu Mwenyezi Mungu Mweza wa yote. Halafu Mtume aliuliza swali hilo hilo kwa Zahra (a.s) naye alijibu: "Mwenzangu ni mume mzuri sana."

Katika sentensi moja, Imam Ali (a.s) alimtambulisha mwanamke bora katika Uislamu na akaelezea madhumuni makuu ya ndoa.

KUISHI NA MUME

Kazi ya mke ni kumtunza na kumlea mume. Si kazi rahisi. Wanawake hao ambao hawatambui sifa hii ya wajibu wao, wataona vigumu katika kutimiza kazi hii. Ni kazi ya mwanamke ambaye anatambua kwamba kazi hii inahitaji kiwango fulani cha busara, mtindo na ustadi. Kwa mwanamke kuwa mke aliyefuzu, lazima auteke moyo wa mume wake na kuwa chanzo cha furaha kwake. Lazima amtie moyo katika kutenda matendo mema na kumshawishi asifanye matendo maovu. Lazima pia mke achukue hatua za

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 14

kutosha kutunza afya yake na ustawi wake. Matokeo ya bidii yake yanaelekezwa katika kumfanya mume awe mwema na anaye heshimika ambaye atastahili kuwa mlezi wa familia yake, na baba mzuri ambapo watoto watapata mwongozo na heshima. Mwenyezi Mungu, Mjuzi wa yote amemjaalia mwanamke uwezo usio wa kawaida. Mafanikio na furaha, na pia mateso ya familia yapo mikononi mwake.

Mwanamke anaweza kuifanya nyumba kuwa pepo ya hali ya juu au jahanamu inayowaka moto. Anaweza akamfikisha mume wake kwenye kilele cha mafanikio au balaa isiyofaa. Mwanamke mwenye sifa alizopewa na Mwenyezi Mungu, ambaye anatambua wajibu wake kama mke, anaweza kumnyanyua mume wake kuwa mtu wa kuheshimika hata kama alikuwa mtu wa chini sana kuliko wote.

Mwanachuoni mmoja aliandika: Wanawake wanao uwezo wa ajabu ambao kutokana nao wanaweza kupata chochote wanachotaka."

Katika Uislamu, mke kumtunza mume kuna daraja la maana sana. Imelinganishwa na jukumu la Jihadi (vita takatifu katika njia ya Mwenyezi Mungu). Imam Ali (a.s) alisema: "Jihadi ya mwanamke ni kumtunza mume wake vizuri."

Fikiria kwamba Jihadi ni mapambano na vita vitakatifu katika njia ya Mwenyezi Mungu, pamoja na mapambano ya kuendeleza heshima ya Uislamu, kulinda nchi za kiislamu na kutekeleza haki katika jamii, ni mojawapo ya matendo ya kiwango cha juu sana ya ibada. Faida ya kutekeleza majukumu ya mke mzuri, vile vile huakisiwa wakati wa kufikiriwa kwa Jihadi.

Mtume (s.a.w.w) wa Uislamu alisema: "Mwanamke yeyote anayekufa ambapo mume wake yuko radhi naye, huingia Peponi."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 15

Mtume pia alisema: "Kama mwanamke hatatimiza wajibu wake kama mke, hajafanya wajibu wake kwa Mwenyezi Mungu."

WEMA

Kila mtu ana hamu ya urafiki na wema. Wote wanataka kupendwa na wengine. Moyo wa mwanadamu hunemeeka kwa hilo.

Mtu ambaye hapendwi na mtu yeyote anajifikiria yeye mwenyewe kama yupo peke yake na ametelekezwa. Bibi mpendwa! Mumeo hajawa tofauti. Yeye pia anahitaji mapenzi na huba. Kabla ya kuoa mapenzi na huba ya wazazi wake yalitimiza haja hii, lakini sasa, anayo matumaini kwamba wewe ndiye utakae timiza haja hii.
Mwanaume anategemea kwa mkewe kupata urafiki na mapenzi, ambyo ni haja ya wanadamu wote. Hujitahidi sana ili apate riziki na kukufurahisha wewe. Hushirikiana na wewe matatizo yote ya maisha, na kama mwenza wako wa kweli, anajali kukufurahisha wewe kuliko hata wazazi wako wafanyavyo. Kwa hiyo, onesha shukurani zako kwake na umpende yeye, atakupenda wewe. Mapenzi ni uhusiano wa huku na huku ambao huunganisha nyoyo.

"Mvulana wa miaka ishirini ambaye alikuja Tehran kusoma kwenye chuo Kikuu, alimpenda mjane mwenye umri wa miaka thelathini na tisa ambaye alikuwa mama mwenye nyumba wake." Hii ni kwa sababu mwanamke huyu aliijaza nafasi tupu iliyoachwa wazi na mama yake moyoni mwake kupitia wema wake.

Kama mapenzi yanatoka sehemu zote mbili, msingi wa ndoa unakuwa na nguvu na hatari za kutengana zinaepukwa. Usifikiri kwa majivuno kwamba mumeo alikupenda wewe alipokuona mara ya kwanza, kwa sababu mapenzi ya aina hiyo hayadumu. Mapenzi yanayodumu ni

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 16

yale yanayopitia kwenye wema na huba ya kudumu katika namna ya urafiki wa karibu sana.

Kama unampenda mumeo na unao urafiki mzuri naye, atafurahi na atakuwa radhi kujitahidi na kujitolea kwa ajili ya ustawi wako.

Mwanaume anayefurahia mapenzi ya mkewe, husumbuliwa na maradhi mara chache au matatizo ya mshtuko. Kama mwamaume hapewi uhusiano mwema na wa kirafiki na mkewe anaweza kukata tamaa na kuanza kuikwepa nyumba yake. Anaweza kujikuta anatumia muda wake mwingi sana katika kutafuta marafiki na watu wa kumjali. Anaweza akajisemea mwenyewe: "Kwa nini nifanye kazi na kuwasaidia watu ambao hawanitaki. Inawezekana labda nikajifurahisha mwenyewe na kujaribu kupata marafiki wa kweli."

Mwanamke anaweza akampenda mumewe kwa uaminifu, lakini mara nyingi haoneshi au kuyadhihirishi mapenzi yake. Haitoshi kuanzisha uhusiano wa kirafiki na kuchukulia kwamba hali hiyo ni sawa. Matamshi ya mara kwa mara kama vile, 'ninakupenda,' 'umepotea machoni kwangu sana,' Ninafurahi kukuona,' husaidia sana kuendeleza uhusiano mzuri. Mume anapokuwa safarini, mwanamke lazima amwandikie barua kuonesha kwamba haoni raha bila kumuona. Kama ipo simu ofisini kwa mwanamume, mke anatakiwa kumpigia simu mara kwa mara, lakini isizidi kiasi. Mke amsifu mumewe kwa marafiki na ndugu zake wakati hayupo, na kumtetea endapo mtu anamsema kwa ubaya.

Mwenyezi Mungu Mweza wa yote anazungumzia kuhusu mapatano haya ya mapenzi na huba ya mume na mke ndani ya Qur'an:

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 17

﴿ وَمِنْ ءَايَـٰتِهِۦٓ أَنْ خَلَقَ لَكُم مِّنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَٰجًا لِّتَسْكُنُوٓا۟ إِلَيْهَا
وَجَعَلَ بَيْنَكُم مَّوَدَّةً وَرَحْمَةً ۚ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَـَٔايَـٰتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١﴾ ﴾

“Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wenza kwa ajili yenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. hakika katika haya bila shaka; zipo Ishara kwa watu wanao fikiri. (30:21)

Imam Ridha (a.s) alisema: “Wanawake wengine ni baraka kwa waume zao ambao huonesha mapenzi na huba yao.”

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: “Watu walio bora sana miongoni mwa wanawake ni wale wenye mapenzi na huba.”
Imam Sadiq (a.s) alisema: “Ukimpenda mtu mwoneshe kwamba unampenda.”

HESHIMA YA MUME

Hamu ya kuheshimiwa ni jambo la asili, lakini si kila mtu yupo tayari kuitoa. Mumeo hukutana na watu wengi katika shughuli zake wakati hayupo nyumbani. Baadhi ya watu hao wanaweza kuwa hawana staha na kumfedhehesha hali ambayo hatimaye humtibua mtu. Wewe kama mke wake, anakutarajia wewe kuonesha heshima na ari akiwa nyumbani na kwa hali hiyo unaipandisha hadhi ya nafsi yake iliyokanyagwa.

Kumstahi na kumheshimu mume wako hakukudhalilishi wewe, lakini huongeza nguvu na mwelekeo kwenye harakati za kuyafanya maisha kuwa bora. Kila mara unatakiwa umsalimie na kwa hayo maamkizi yako mfanye ahisi unamjali. Usiingilie kati mazungumzo yake. Uwe na adabu na mpole

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 18

unapozungumza naye na usimpigie makelele. Inapotokea wote wawili mnakwenda kwenye mkutano ngoja mumeo aingie kwanza. Msifie mbele ya watu wengine. Waambie watoto wenu kumheshimu baba yao na uwakaripie kama hawaoneshi adabu kwake. Mheshimu mbele ya wageni na uwe makini kwa mahitaji yake, na yale ya wageni.

Anapogonga mlango jaribu kufungua mlango huku ukitabasamu na kuonesha uso wenye furaha. Tendo hili dogo la kuonesha furaha, athari yake ni kwamba huburudisha moyo na kumwondolea uchovu mumeo. Baadhi ya wanawake wanaweza kudhani kwamba tabia ya aina hiyo si ya kawaida. Fikiria unapomwamkia mumeo kama mgeni. Hii si tabia nzuri kwa sababu mumeo amekuwa kwenye harakati siku nzima kwa ajili ya ustawi wa familia yake na anastahiki kufikiriwa na kuheshimiwa anaporudi nyumbani. Maamkuzi hayo ya kwanza huleta picha nzuri sana, na lililo zuri kwa mgeni ni zuri pia kwa jamaa wa familia.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: “Wajibu wa mwanamke ni kujibu hodi ya mlangoni na kumkaribisha mume wake.”

Imam Sadiq (a.s) alisema: “Mwanamke anayemheshimu mume wake na hamsumbui, atapata bahati na mafanikio.”

Mtukufu Mtume (s.a.w) alisema: “Mke anawajibika kutayarisha beseni na taulo ili mumewe anawe mikono.”

Uwe mwangalifu usije ukamfedhehesha mumeo, usizungumze naye kwa ukali, usimtukane, uwe msikivu kwake na usimuite kwa majina machafu. Ukimkosea na yeye atakufedhehesha wewe. Hatimaye, moyo wa mapenzi na kuaminiana utamomonyoka. Kwa hiyo, mtagombana mara kwa mara na kubishana, hali ambayo itasababisha mtalikiane.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 19

Hata kama mtaendelea kuishi pamoja, maisha yenu kwa hakika yatajaa fujo. Hisia za uadui na usumbufu wa kisaikolojia unaweza kuanza kujengeka hadi kufikia kiwango cha kuhatarisha maisha ya wanandoa na hali hiyo inaweza kusababisha uhalifu. visa vifuatavyo vinaonesha baadhi ya mambo haya:

"Mtu mmoja mwenye umri wa miaka ishirini alimchoma kisu mkewe mwenye umri wa miaka kumi na tisa hadi akafa kwa sababu mke alimtukana mume. Mahakamani mume alisema; 'nilimuoa mwanamke huyu mwaka moja uliopita. Mwanzoni mke wangu alinipenda sana. Lakini baada ya kipindi kifupi mke wangu alibadilika na kuanza kunidhalilisha. Alianza kutumia lugha ya matusi kwangu kila ilipowezekana na kwa sababu ndogo sana, alianza kunikebehi. Kwa sababu jicho langu la kushoto ni kengeza, akawa na desturi ya kuniita mimi 'punda kipofu.' Siku moja, akaniita 'punda kipofu' nilikasirika sana hivyo kwamba nilimchoma kisu mara kumi na tano.' "

"Mtu mwenye umri wa miaka sabini na moja (71) ambaye alimuua mkewe, alitoa maelezo yafuatayo: 'Ghafla tabia ilibadilika kwangu na akaanza kutonijali mimi. Wakati mmoja akaniita 'mtu nisiyevumilika.' nikagundua kwamba alikuwa hanipendi tena, nikamshuku na nilimuua kwa kumkata shoka mara mbili."

MALALAMIKO NA MANUNG'UNIKO

Hakuna mtu yeyote asiyekuwa na matatizo na manung'uniko kuhusiana na maisha ya kila siku. Kila mtu hupenda kuwa na mtu wa kumhurumia ambaye anaweza kuwa mwandani wake na kumsikiliza matatizo yake. Lakini jambo la kukumbuka ni kwamba "upo wakati na mahali kwa kila jambo." Mtu lazima aelewe wakati muafaka na mahali pa kulalamikia. Baadhi ya wanawake wajinga na wabinafsi hawatambui kwamba waume

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 20

zao wanachoka sana na fadhaa baada ya kazi ya siku nzima. Badala ya kungoja kwa muda wa saa moja au mbili ili apumzike na kupata nguvu, huanza kumshambulia kwa mfululizo wa malalamiko. Mathalani mke anaweza kusema:

"uliniacha mimi na watoto hawa maluuni na ukaenda zako. Ahmad amevunja kioo cha mlango wa chumba cha mbele. Watoto wetu wa kike walipigana. Makelele ya watoto wa majirani zetu yananiudhi kweli. Hasan hajifunzi hata kidogo na amepata maksi za chini sana. Nimefanya kazi sana leo najisikia nimechoka. Hakuna hata mtu wa kusikiliza kilio changu!

"Watoto hawa hawanisaidii hata kidogo kwa kazi za hapa ndani. Afadhali nisingezaa watoto kabisa! Unayo habari dada yako alikuwa hapa leo? Sijui tatizo lake nini; alikuwa anafanya mambo kama vile nimemeza urithi wa baba yake.

"Mungu na aninusuru kutoka na mama yako! Amekuwa ananisengenya. Nimechoshwa na wote hao. Pia nimejikata kidole leo kwa kisu na kuumia sana.

"Ingekuwa vema kama nisingekwenda kwenye harusi ya Muhamedi jana. Ungemuona mke wa Rashid! Alivyopendeza, ungeshangaa! Mwenyezi Mungu angenipa na mimi bahati kama hiyo! Wanaume wengine wanawapenda wake zao na huwanunulia vitu vizuri. Hao ndio waoaji wa kweli.

"Rashid alipoingia kila mtu alimpa heshima. Ni kweli kwamba watu hupendelea kuona tu vazi ulilovaa. Anacho nini ambacho mimi sina? Kwa nini ajioneshe mbele yangu? Ndio, anayo bahati kuolewa na mume ambaye anampenda, yeye si kama wewe!

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 21

"Siwezi kuvumilia kuendelea kuishi kwenye nyumba iliyolaaniwa, kukutunza wewe na watoto. Kwa hiyo fanya utakalo!"

Msimamo wa namna hi si sahihi. Wanawake wa aina hii hudhani kwamba waume zao huondoka kwenda kwenye pikiniki au burudani kila asubuhi. Wanaume hukutana na mamia ya matatizo kila siku. Bibi mpenzi! Hujui mumeo amepita kwenye mambo gani anapokuwa katika kazi yake. Hujui ni watu fidhuli na wenye karaha kiwango gani mumeo ameshughulika nao siku nzima. Kwa hiyo, anapokuja nyumbani usiwasilishe malalamiko yako yote kwa wakati moja. Usimfanye ajihisi kuwa imekuwa hatia kuwa mwanamume.

Uwe na wastani na umfikirie. Endapo kwa kunung'unika kwako na kumsumbua, kutamuongezea wasi wasi na machungu, basi, ama anaweza akaanza ugomvi au akaondoka hapo nyumbani na kwenda kwenye mgahawa au filamu au hata kutembea tu mitaani.

Kwa hiyo, ewe Bibi mpenzi! Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, acha mazoea haya ya kulalamika hata wakati usio muafaka. Tafuta muda unaofaa na halafu mpe matatizo yako ambayo ni ya kweli, si kwa kulalamika, lakini fanya hivyo, kwa namna ya kushauriana. Kwa njia hii, hutasababisha yeye kuanza kujenga hisia za uadui na mapatano ya familia yanabaki kuwa salama.

Mtume (s.a.w.w) wa Uislamu alisema: "Sala za mwanamke anayemchokoza mume wake kwa ulimi wake, hazikubaliwi na Mwenyezi Mungu hata kama akifunga saumu kila siku, anaamka kila siku usiku kufanya ibada, anawaachia huru watumwa katika njia ya Mwenyezi Mungu. Mwanamke mwenye ulimi mbaya ambaye humuumiza mumewe kwa njia hii, ni mtu wa kwanza kuingia Jahanamu!"

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 22

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) pia alisema: “Wanawake wa Peponi huwaambia wanawake wanaowatukana waume zao kwa njia hii: ‘Mwenyezi Mungu na akuuweni. Msiwe watovu wa adabu kwa waume zenu. Mtu huyu (mume) si kiumbe wako, na wewe hustahiki kuwa naye. Muda mfupi ujao atakuacha na atakuja kwetu.’ ”

Sijui wanawake wa aina hii wanataka kujipatia nini kwa hayo manung’uniko yao. Kama wanataka kusikilizwa na waume zao au kujionesha, basi, hakika wanajipatia kitu kinyume chake kabisa na kumkasirisha. Kama wanakusudia mateso kwa mume, kumsababishia madhara ya kisaikolojia na kumuingiza kwenye mazoea bandia ya kuangamiza, basi wapo kwenye njia potofu.

Bibi mpendwa! Kama unamjali mumeo na familia yako, basi ni lazima uache msimamo huu usio na mantiki. Je, umewahi hata kufikiria kwamba mwenendo wako mbaya unaweza ukasababisha kuvunjika kwa maisha ya familia yako?

“Daktari mmoja alitoa ushahidi mahakamani: ‘Sijapata kumuona mke wangu akifanya mambo kama mke sahihi wa nyumbani wakati wote wa ndoa yetu. Nyumba yetu mara nyingi imekuwa katika machafuko.Wakati wote mke wangu anapiga makelele na kutukana. Nimechoshwa naye.’ Baada ya kumlipa mke wake fedha nyingi tu, akapata talaka. Akasema kwa furaha: ‘Kama angetaka na angeomba utajiri wangu wote na hata shahada yangu ya taaluma ya tiba, ningempa ili niachane naye haraka sana.’ ”

TABIA ZA KUPENDEZA

Mtu yeyote mwenye tabia njema na inayopendeza pia angepata dhiki na matatizo ya maisha kwa njia ile ile. Hawa ni aina ya watu ambao watu huvutiwa nao na wanawatafuta wakati wote. Tabia inayopendeza na

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 23

msimamo wa mtu utakuwa na kinga dhidi ya maradhi ya kisaikolojia kwa kuwa kuonekana kwao katika maisha ni kushinda matatizo yao kwa njia nzuri iwezekanayo.

Imam Sadiq (a.s) alisema: “Hakuna maisha yanayo kubalika zaidi kuliko yale ambayo yanatokana na tabia njema.”

Lakini mtu mwenye tabia mbaya naye pia angeyaona maisha hayafurahishi kwani uhusiano wa watu hao kuendeleza wasiwasi na fadhaa. Mtu kama huyu hupenda kulalamika na kupigia kelele maisha. Msimamo wa namna hii huepukwa na watu wengi ambapo mtu huyo hapati marafiki wengi. Hii ndio hali ambayo huathirika kwa urahisi na matatizo mbali mbali ya kisaikolojia na maradhi mengineyo kwa sababu ya wasi wasi na utupu ambao mtu mwenye msimamo mbaya anavyoyaona maisha.

Mtukufu Mtume (s.a.s) alisema: “Mtu mwenye tabia na msimamo mbaya atakuwa kwenye masumbuko na mateso wakati wote.”

Msimamo mzuri na unaopendeza ni muhimu kwa watu wote kwa ujumla na hususan baina ya wanandoa kwani wanandoa lazima wawe pamoja.

Mpendwa Bibi! Kama unataka kufurahia maisha ya furaha na mumeo na watoto wako, ufanye msimamo wako na tabia ya kupendeza vikubalike. Uwe na tabia njema na si mgomvi. Unao uwezo wa kuifanya nyumba yako kuwa Pepo ya hali ya juu au Jahanamu iwakayo moto. Unaweza kuwa malaika wa huruma ambapo mumeo na watoto wanaweza kupata amani kupitia kwako. Unajua utaacha mvuto wa kupendeza kiasi kwenye roho zao kwa huo msimamo wako wa kutabasamu na lugha nzuri. Mvuto wa kupendeza ni mbichi katika akili zao wanapoondoka kwenda shuleni au kwenye shughuli za kazi na unawasaidia wao kuwa na mwanzo mzuri wa siku.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 24

Kwa hiyo, kama unajali kuhusu sifa nzuri ya maisha yako na uhusiano ulio nao na mumeo, usiwe kinyume na tabia njema. Uwe dhahiri katika msimamo wako na tabia inayopendeza kwani nguzo bora zaidi ya kutegemea kwa usalama wa ndoa ni maadili mazuri ambayo yanaelekeza kwenye tabia inayopendeza.

Namna nyingi za talaka ni kwa sababu ya tabia zisizolingana za mume na mke. Takwimu juu ya talaka kwa uthibitisho zinaonesha kwamba msimamo wa kupatana, maadili mema na tabia ya kupendeza, hazikuwepo kwa wanandoa husika. Chanzo kikubwa cha ugomvi na kutokuelewana kwa wanandoa ni kwa sababu yakutolingana kwa tabia na kanuni za maadili za wanandoa. Takwimu zifuatazo zinavutia:

"Mwaka 1968 kesi za malalamiko ya ndoa zilizowasilishwa mahakamani zilikuwa 16,039, kesi 12,760 miongoni mwa hizo, misingi ya malalamiko yao ilikuwa kutokulingana kwa kanuni za maadili. Mwaka 1969 kesi za malalamiko ya aina hiyo hiyo 16,058 liziwasilishwa mahakamani, kesi 11,246 miongoni mwa kesi hizo, misingi ya malalamiko ilifanana na ile ya kesi za mwaka wa nyuma. Kwa hiyo, inathibitika kwamba zaidi ya asilimia sabini ya ugomvi wa kifamilia ulisababishwa na kipengele hiki."

Mwanamke alilalamika kwenye Baraza kwamba mume wake kila siku alikuwa na desturi ya kula chakula chake cha mchana na jioni nje. Halafu mwanaume akaeleza kwamba sababu iliyomfanya ale nje ni kwamba mke wake hakuwa mbunifu hata kidogo na alikuwa mwenye tabia isiyopendeza kuliko wanawake wote wenye tabia kama hiyo hapa duniani. Haraka sana mwanamke alinyanyuka na kuanza kumpiga mume wake mbele ya majaji."

Mwanamke huyu mpumbavu alidhani kwamba angebadilisha tabia ya mume wake ya kula chakula chake nje badala ya nyumbani kwa kulalamika,

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 25

kutukana na kumpiga. Lakini mwanamke huyu hakutumia mbinu rahisi na ya kiakili ambapo alitakiwa kuwa na busara zaidi na kuzingatia mwenendo unaostahili.

Mwanamke mwingine alipeleka taarifa mahakamani kwamba mume wake aliacha kusema naye kwa muda wa miezi 15 na kwamba alikuwa anatoa matumizi yake kupitia kwa mama yake (mume). Mume alijibu kwamba alikwisha kinai na msimamo usiopendeza wa mke wake ambao ulimfanya yeye asizungumze naye kwa miezi."15

Migongano mingi ya kifamilia inaweza kusuluhishwa kwa wema, huruma na tabia inayopendeza. Kama mume wako si mwema, kama anatoka kwenda kula chakula cha jioni peke yake, kama anapenda kutumia lugha ya matusi, anatumia utajiri wake wote vibaya, hupenda kusema suala la kutalikiana na kutengana au sababu kadhaa katika ugomvi wa kifamilia, ipo njia moja tu ya kusuluhisha. Njia hii ni kuwa mwema na tabia njema. Matokeo ya mazoea ya tabia kama hii ni ya kimiujiza.

Imam Sadiq (a.s) alisema: "Mwenyezi Mungu Mweza wa yote atampa mtu mwenye tabia ya kupendeza thawabu zinazolingana na zile za Jihadi. Atamneemesha kwa wingi mtu huyo usiku na mchana."

Imam Sadiq (a.s) alisema: "Mwanamke yeyote anaye msumbua na kumtesa mumewe yu mbali na neema za Mwenyezi Mungu na mwanamke yeyote anayemheshimu, anaye mtii na hamhuzunishi mumewe, ameneemeka na kufanikiwa."

Ipo hadith inayosema kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alipewa taarifa ya mwanamke mwema ambaye alifunga saumu kila siku na alikuwa anafanya ibada kila siku usiku akimuabudu Mwenyezi Mungu, lakini alikuwa na tabia isiyo pendeza ya kuwaudhi majirani zake kwa

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 26

maneno yake makali. Mtukufu Mtume alisema: “Hapana jema kwake huyo na yeye ni mkazi wa Jahanamu.”

MATARAJIO MABAYA

Mpendwa Bibi! Wewe ni mwanamke mkuu wa familia yako. Uwe na hekima na uweledi. Panga vizuri matumizi yako. Panga bajeti ya matumizi yako kwa njia ambayo haitasababisha hasara kwa utajiri na hekima yako.

Usishindane na wengine na uwaonee wivu. Kama unaona nguo nzuri imevaliwa na mwanamke, au kama unavutiwa na fanicha na vyombo ambavyo umeviona kwenye nyumba ya rafiki, usimlazimishe mumeo kununua vitu kama hivyo ambavyo vinazidi uwezo wake wa kifedha na pengine atalazimika kukopa. Je, si vema zaidi kungoja hadi hapo ambapo hali ya kipato itaruhusu au itakapopatikana akiba ya ziada ya kuwezesha kununua vitu visivyo vya muhimu?

Mara nyingi ni wale wanawake wajinga na wanaojipendelea ambao hushindwa, na kuwa wabadhirifu na kutaka kushindana. Wanawake wa aina hii huwalazimisha waume zao kuingia kwenye madeni na huchoshwa na kukasirishwa na kujaribu kuridhisha matakwa yao yasiyo weza kutoshelezwa. Wakati mwingine, ufumbuzi wa aina moja tu uliopo kwa wanaume wa kutatua matatizo haya ni uamuzi wa kumtaliki mke au kujiua.

Wanawake ambao hawatambui madhumuni ya kweli na maana ya ndoa na badala yake wanaifikiria kama utumwa ambapo mwanamume anapatikana kwa lengo la kutimiza matamanio yao ya kitoto na mahitaji ya kiulimwengu. Wanawake wa namna hii wanataka mume ambaye atawahudumia kama mtumwa na hawatapinga njia zao za matumizi. Wanawake wa aina hii mara nyingine huenda mbali zaidi. Wanawafanya waume zao watumie zaidi ya uwezo wao hali ambayo inaweza kuwafilisi, wanaweza kufanya mauaji au matokeo yoyote ya msiba.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 27

Wanawake wa aina hii ni aibu kwa wanawake wenzao. Endapo matarajio yake makubwa yanasababishwa kutalikiana, mwanamke atanyang'anywa mapenzi ya watoto wake na ataishi maisha ya upweke. Kwa wanawake wa aina hii si rahisi kuolewa tena kwa urahisi. Hata kama inatokea, hakuna uhakika wa ndoa ya pili kama itadumu, kwani binadamu wengi hawapendi kuwekwa katika utumwa. Na mume mpya inawezekana naye asiwe na uwezo wa kutimiza mahitaji yao kabisa kuliko hata wa mwanzo.

Mpendwa Bibi! Badala ya kuwa mwenye tamaa sana, jaribu kuwa mwenye busara. Tumia muda mwingi na juhudi kwa ajili ya ustawi wa familia yako na mumeo badala ya kujaribu kuiga mambo ya kila mtu. Kama mumeo anaumia kupita kiasi, mzuie na udhibiti matumizi yake yasiyo ya muhimu. Badala ya kununua bidhaa zisizo za muhimu, ni vema kuweka kiasi fulani cha akiba kwa ajili ya matatizo ya siku za usoni.

Katika hadith Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: "Mwanamke yeyote ambaye halingani na mume wake na humshawishi afanye mambo zaidi ya uwezo wake, basi matendo yake hayatakubaliwa na Mwenyezi Mungu, ataonja ghadhabu ya Mwenyezi Mungu mnamo Siku ya Ufufuo."

Katika hadith nyingine, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: "Mwanamke yeyote asiyelingana na mumewe, haridhiki na kile ambacho Mwenyezi Mungu amewajaalia na humtendea mume wake ubaya kwa kudai ampe zaidi ya uwezo wake, basi matendo yake (au ibada ya mke) hayakubaliki kwa Mwenyezi Mungu na Atamkasirikia mwanamke huyo."

Katika hadith nyingine, Mtume (s.a.w.w) alisema: "Baada ya kumwamini Mwenyezi Mungu, hapana neema iliyo kubwa zaidi ya kuwa na mume au mke mnayeelewana naye."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 28

UWE FARAJA KWA MUMEO

Uzito wa mzigo wa maisha huchukuliwa na wanaume kwa sababu wao wanao wajibu wa kutunza na kusaidia familia zao. Katika kutimiza wajibu huu, mwamaume wa familia lazima akabiliane na matatizo mengi na vikwazo vingi nje ya familia yake. Baadhi ya matatizo haya yanaweza kuwa ukubwa wa kazi, mizozo kwenye msongamano wa magari na usumbufu wa kungoja na kupanda mabasi kutoka nyumbani kwenda ofisini na kurudi nyumbani, wasiwasi kuhusiana na masuala ya marafiki nawafanyakazi wenzake na wasiwasi wa kiuchumi na kisiasa ya siku hiyo, wasi wasi wa marafiki na wafanya kazi wenzake, na wasiwasi wa kujaribu kuboresha hali ya maisha ya familia yake. Kiasi cha mishughuliko na wasiwasi wa mtu mwenye kuwajibika ni mikubwa na yenye sehemu nyingi. Si jambo la kushangaza kwamba wastani wa umri wa mwanaume ni mdogo zaidi ya ule wa mwanamke.

Ili mwanadamu aweze kwenda sambamba na mizigo ya maisha ni muhimu kuwa na mtu ambaye atakusikiliza na kukuhurumia. Mumeo ni mmoja wapo wa watu hao. Anaweza akahisi yu mpweke na akahitaji kupata kimbilio na faraja akiwa katikati ya misukumo hii. Ni kawaida kwamba mwanaume hutarajia kupata faraja na utulivu kutoka kwa mke wake na familia yake. Kwa hiyo, tazamia matarajio na mahitaji yake. Uwe mkunjufu na mchangamfu wakati ambapo kwanza ndio anarudi nyumbani kutoka katika kazi zake, na apate viburudisho au umfanye ahisi kwamba wewe upo tayari kusikiliza mahitaji yake. Jaribu kutokumwingiza kwenye shari kwa kuanza kumlaumu mara tu umuonapo. Ngoja apumzike na apate nguvu upya kabla ya kumweleza madai binafsi ya watu wa familia.

Mumeo anapokuja nyumbani, jaribu kutabasamu na kumsalimia kwa uchangamfu. Mtimizie mahitaji yake ya kimwili ya uchovu, njaa na kiu. Halafu muulize kuhusu matatizo yake. Kama hayupo tayari kusema uwe

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 29

msikilizaji mzuri na umhurumie. Jaribu kuonesha kuhusika kwako kwa dhati na halafu umsaidie kutambua kwamba matatizo si kwamba hayawezekani, na makubwa kama anavyodhani. Mpe moyo wa kumuunga mkono na kumsaidia aweze kukabiliana na masuala ipasavyo. Unaweza kusema kitu kama: "Matatizo haya yanawapata watu wengi. Kwa utashi na uvumilivu, inawezekana kuyatatua matatizo almuradi mtu asiruhusu yamshinde. Matatizo haya, kwa kweli ni mitihani na pia hujenga tabia ya kweli ya mtu. Usikate tamaa. Unaweza kuyatatua kwa kuazimia na ustahamilivu.

Kama unayo mawazo fulani kuhusu jinsi ya kuyashughulikia, mwaambie mumeo. Kama huna, labda unaweza kumshauri amuone rafiki mzuri ambaye anao ujuzi na sifa zaidi.

Mpendwa Bibi! Wakati wa matatizo, mumeo anahitaji sana umjali na mapenzi yako. Unatakiwa umsaidie na umtunze kama mtaalamu wa maradhi ya akili na mke mwenye huruma. Kiwango gani cha matunzo mtaalamu wa maradhi ya akili angempa ambacho na wewe ungempa? Usikadirie pungufu uwezo wako wa kumtuliza na kumpa nguvu. Hakuna mtu muaminifu na mwenye kuhusika zaidi kuhusu ustawi wa mumeo isipokuwa wewe. Ataweza kupata nguvu kutokana na mapenzi yako kwake na aweze kukabiliana na matatizo yake kwa hali ambayo itapunguza mhemuko wake na wasiwasi wa akili. Hatimaye, mapatano ya kuheshimiana na upendo utakuwa mkubwa zaidi.

Katika hadith, Imam Sadiq (a.s) alisema: "Hakuna kitu bora zaidi duniani kuliko kuwa na mke mwema. Na mke mwema ndiye huyo ambaye mume wake hufurahi pindi amuonapo."

Kwenye hadith, Imam Rida (a,s) alisema: "Lipo kundi la wanawake ambalo huzaa watoto wengi. Ni wanawake wema na wana huruma. Huwasaidia

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 30

waume zao wakati wa matatizo na katika mambo ya dunia hii na ile ijayo. Wanawake hawa hawafanyi matendo yoyote ambayo yangewapa hasara waume zao kuongeza matatizo yao."

UWE MTU WA KUONESHA SHUKRANI

Kama mtu ni mwema na mpaji wa utajiri wake ambao ameupata kutokana na kazi ngumu, shukrani na kuoenasha kufurahia kwako kwa matendo kama hayo ni hali ambayo itachangamsha hisia zake za ndani na kumfanya ahisi amefanikiwa. Matendo ya ukarimu yanaweza kuwa kawaida ya mtu ambapo hujenga mazoea kutumia na kugawana utajiri wake na wale wanao hitaji. Hata hivyo, kama matendo ya ukarimu yanapuuzwa na hayafurahikiwi, mhusika anaweza akapoteza utashi na msukumo wa kufanya wema. Itakuwa ni kawaida kwa mtu kuhitimisha kwamba ilikuwa ni kutumia vibaya kutoa fedha yake aliyoipata kwa jasho ambapo hakuna shukrani inayotolewa.

Shukrani na kufurahishwa ni tabia za kuvutia akiwa nazo mtu na ni siri ambayo kwayo mtu anaweza kuvuta matendo ya msaada.
Hata Mwenyezi Mungu ametaja kwamba shukrani kwa neema Zake ni sharti ambalo husababisha neema Zake kuendelea kutolewa kwa wanadamu:

﴿ وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِن شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ وَلَئِن كَفَرْتُمْ إِنَّ عَذَابِي لَشَدِيدٌ ﴿٧﴾ ﴾

"Na alipotangaza Mola wenu : Mkishukuru nitakuzidishieni; na mkikufuru, basi adhabu yangu ni kali." (Qur'ani 14:7).

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 31

Mpendwa Bibi! Mumeo naye pia ni binadamu. Kama mtu mwingine yeyote yule. Yupo tayari kusaidia familia yake na anaiona kama wajibu wa uadilifu na kisheria. Anapopewa shukrani na kufurahikiwa kwa kutekeleza kazi yake, kazi hizo haziwi tena mzigo kwake.

Wakati wowote anaponunua vitu vya nyumbani au kitu kama nguo na viatu kwa ajili yako na watoto, furahi na umshukuru yeye. Onesha shukrani zako kwa vitu vidogo anavyofanya kama kununua bidhaa za vyakula, kusafiri na familia na kukupa wewe fedha. Unapoonesha shukrani, unamfanya mumeo ajihisi kuwa mwema na kuzawadiwa kwa usumbufu uliompata. Uwe mwangalifu kwamba usizipuuze kazi zake na kuwa mtu asiyejali mchango wake kuhusu ustawi wa familia.

Anaweza akaanza kutumia fedha yake kwingineko au kwake yeye mwenyewe.

Ikiwa tu rafiki au ndugu amekupa zawadi ya jozi ya soksi au shada la maua, unatakiwa kumshukuru mara nyingi, hivyo, ni kawaida tu na ni haki kumfurahia mumeo kwa kukupendelea na kukufikiria. Usidhani kwamba utakuwa unajidhalilisha kwa kuonesha shukrani zako. Kinyume chake, utapendwa na kujaliwa kwa vitu vingi zaidi kwa sababu unafurahia juhudi ya mumeo ambapo dharau na ubinafsi ni tabia ambazo zinaweza kuipeleka familia kwenye mabalaa.

Zifuatazo ni Hadith zinazozungumzia tabia za shukrani:
Imam Sadiq (a.s) alisema: “Wanawake bora zaidi miongoni mwa wanawake wenu ni hao ambao huonesha furaha wakati waume zao huleta kitu nyumbani na hawaoneshi kutokuridhika kama hakuna kilicho letwa nyumbani.”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 32

Imam Sadiq (a.s) alisema: “Mwanamke yeyote ambaye husema kwa mumewe kwamba hajaona vitu vyovyote vizuri kutoka kwake basi anakuwa amekosa uaminifu na anavuruga ibada yake.”

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: “Yeyote asiye washukuru watu wanaomsaidia, kwa kweli, haoneshi shukrani zake kwa Mwenyezi Mungu kwa neema Zake.”

USITAFUTE DOSARI ZA MWENZIO

Hakuna mtu aliyekamilika. Watu wengine ni warefu sana au wafupi sana au wanene sana au wembamba sana, wanapua kubwa au pua ndogo, wanasema sana au wakimya sana, wana hasira zana au wanaelewana na watu haraka sana weusi sana rangi ya wastani au wanakula sana au wanakula kidogo na orodha inaweza kuendelea. Wanaume na wanawake wengi sana wanazo dosari hizi. Ni matumaini ya kila mwanaume na kila mwanamke kutafuta mwenzi aliyekamilika, lakini matumaini ya aina hiyo si sahihi. Hakuna uwezekano wa kumpata mwanamke anaye muona mumewe kama mtu aliye kamilika.

Wanawake hao ambao hutafuta makosa ya waume zao bila shaka watayapata. Wanaweza wakaona dosari ndogo na kuzikuza kwa kushughulikia jambo hilo hadi kiwango cha kuwa kipingamizi kisichovumilika. Dosari hii huchukua nafasi ya sifa zingine zote za mume. Kila mara huwalinganisha waume zao na wanaume wengine. Wameanzisha kitu kinachoitwa mwanaume anayefaa katika dhana yao kiwango ambacho hakiafikiani na waume zao. Kwa hiyo, kila mara wanalalamika kuhusu dosari ndani ya ndoa zao. Wanawake hao hujifikiria kuwa na bahati mbaya na kushindwa na maisha na pole pole huwageuza kuwa wanawake |wenye chuki.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 33

Tabia ya aina hiyo ya mwanamke humfanya nini mumewe? Anaweza kuwa ni mtu mvumilivu sana ambaye anaweza kustahamili ujeuri lakini upo uwezekano mkubwa atafedheheshwa na atakuwa na kinyongo kwa mkewe. Hali hii inawezekana ikawatumbukiza wanandoa husika kwenye mabishano na kuelezana dosari za kila mwanandoa. Wote wawili watadharauliana na maisha yao yatageuka kuwa na mlolongo wa ugomvi na mabishano. Hivyo, ama wataishi katika mateso wakiwa pamoja au wataamua kutalikiana. Katika hoja zote mbili, wote watahasarika, hususan ambapo hakuna uhakikisho kwamba ndoa nyingine inaweza kuthibitisha vinginevyo.

Inasikitisha kwamba wapo wanawake wasiojua na wanakaidi katika huo ujinga wao. Inawezekana kwamba wanaweza kuharibu maisha ya familia zao kwa jambo dogo. Ifuatayo ni mifano ya wanawake wa aina hiyo:

"Mwanamke alimwacha mume wake na akaenda nyumbani kwa baba yake kwa sababu mume wake alikuwa ananuka mdomo. Mwanamke huyo hakuwa tayari kurudi kwa mumewe hadi atatue tatizo lake. Kufuatana na malalamiko ya mume, mahakama iliwasuluhisha wana ndoa hao na mke akarudi kwa mumewe. Walipokwenda nyumbani, mke aligundua kwamba pumzi ya mumewe ilikua bado inanuka, kwa hiyo alihamia chumba kingine."

"Daktari wa meno mwanamke alimtaliki mume wake kwa sababu hakuwa katika kiwango kinacholingana na cha kwake; mwanaume alifuzu na kupata taaluma hiyo miaka mitatu baada ya mke wake."

"Mwanamke aliomba kumtaliki mume wake kwa sababu alikuwa na desturi ya kuketi chini na kula kwa kutumia vodole vyake, alikuwa hanyoi kila siku na hakujua jinsi ya kuishi na watu."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 34

Kama mambo yalivyo, si kwamba wanawake wote wapo hivi. Wapo wanawake wenye akili, wa kweli, na wanao utambuzi wa kutosha kwamba hawa hatarishi ndoa na furaha kwa kukuza dosari za waume zao.
Mpendwa Bibi! Mumeo ni binadamu kama wewe. Hakukamilika, lakini anaweza kuwa na sifa nyingi. Kama unapendezwa na ndoa yenu na familia yenu basi usitafute udhaifu wake. Usifikirie dosari zake ndogo kuwa muhimu. Usimlinganishe na mwanaume huyo ambaye umembuni akilini mwako. Inawezekana mumeo awe na udhaifu fulani ambao haupo kwa wengine. Lakini kumbuka kwamba wanaume wengine wanaweza kuwa na kasoro ambazo hazipo kwa mumeo. Ridhika na sifa zake. Hatimaye, utaona kwamba sifa zake zinazidi dosari zake. Zaidi ya hayo kwa nini utarajie kumpata mume mkamilifu ambapo wewe mwenyewe si mkamilifu. Kama wewe unajivuna kiasi cha kutosha kujiona wewe ni mkamilifu, basi waulize watu wengine:

Mtume (s.a.w.w) alisema: “Hakuna kitu kibaya zaidi kwa binadamu kuliko kutafuta dosari za watu wengine, ambapo hawajali mapungufu yao.”

Kwa nini ukuze dosari ndogo? Kwa nini uharibu maisha yako kwa kitu kisichokuwa maanani?

Uwe na busara, acha upuuzi! Puuza dosari za mumeo na usizitaje mbele yake au nyuma yake. Jaribu kutengeneza hali ya hewa ya uchangamshi katika familia yako na ufurahie neema za Mwenyezi Mungu.

Hata hivyo, inawezekana pawepo dosari katika tabia ya mumeo ambazo unaweza kuzirekebisha. Kama ni hivyo, unaweza kufaulu kufanya hivyo hapo tu ambapo utakuwa na busara na uvumilivu. Hutakiwi umlaumu au kuanza kumgombeza, lakini mwendee kwa njia ya kirafiki.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 35

USIMWANGALIE MTU YEYOTE ISIPOKUWA MUMEO

Mpendwa Bibi! Kabla hujaolewa inaewezekana ulikwisha chumbiwa na watu wengine. Posa za uchumba huu inawezekana zilitoka kwa watu matajiri, wasomi, wenye sura nzuri na kadhalika ambao ungependa wakuoe. Matarajio ya aina hiyo yalikuwa ni jambo la kawaida kabla ya kuolewa. Lakini sasa umechagua mwenzi wako na kuwekeana mkataba wa dhati naye kuwa wapenzi katika maisha yenu yote, hivyo, sahau yaliyopita kabisa. Lazima uyaweke pembeni matamanio yako ya zamani na usahau ofa hizo za zamani. Usimfikirie mwamanume mwingine yeyote isipokuwa mumeo na utafute amani naye. Kama ukifanya vinginevyo, utajiweka katika hali ya mashaka.

Sasa basi, umekubali kuishi na mumeo, kwa nini wakati wote uendelee kuwatilia maanani wanaume wengine? Kwa nini umlinganishe mumeo na wanaume wengine? Unapata manufaa gani unapowatazama na kuwatilia maanani wanaume wengine isipokuwa kujiweka katika hali ya mateso yasiyo na mwisho na kusababisha upate maumivu makali ya akili?

Imam Ali (a.s) alisema: “Yeyote anayeyaacha macho yake huru, kila mara atapata maumivu ya neva na atanasa kwenye mtego wa wivu wakati wote.”

Kwa kuwatazama waume wengine na kuwatilia maanani na kuwalinganisha na mumeo, utamuona mwanaume ambaye hana dosari za mumeo. Unaweza kudhani kwamba labda mwamaume huyo amekamilika kwa sababu huzijui dosari za mwanaume huyo. Utafikiria kuwa ndoa yako ina mushkeli, na fikira hii inaweza ikawafikisheni mahali penye mwisho wenye hatari.

Mke wa mtu, umri wake miaka 18 ambaye alitoroka nyumbani kwake alikamatwa na polisi usiku wa jana. Akiwa kituo cha polisi mwanamke

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 36

huyu alisema kwamba baada ya miaka mitatu ya ndoa, pole pole alihisi kwamba hampendi mume wake. Alisema: "Nilikuwa na tabia ya kulinganisha uso wa mume wangu na nyuso za wanaume wengine na nikajuta kwa nini niliolewa naye."

Mpendwa Bibi! kama unataka ndoa ya kudumu daima milele, kama hutaki mateso ya kiakili, na kama unataka muendeshe maisha ya kawaida, basi acha kuwa mbinafsi na sahau hayo matarajio yako yasiyofaa. Usiwapongeze wanaume wengine. Usimfikirie mwanaume yeyote isipokuwa mumeo. Usiendekeze fikira hizi:
'Afadhali ningeolewa na fulani'
'Ningependa mume wangu aonekane kama . . . . . .'
'Natamaani mume wangu angefanya kazi ya. . .. .'
'Natamaani….. Natamaani……. Natamaani….'
Kwa nini ujifunge jela kwa kuendekeza mawazo hayo? Kwa nini utibue misingi ya ndoa yako? Kama lolote kati ya matakwa hayo yangefanikiwa kwa kweli, ungejuaje kwamba ungefanikiwa kuridhika zaidi? Unao uhakika kwamba wake za waume wajulikanao kama 'hawana dosari; wanaridhishwa nao?

Mpendwa Bibi! Kama mumeo anashuku kwamba unaonesha kuvutiwa na wanamume wengine, atakata tamaa na kuacha kuvutiwa na wewe. Usitaniane na wanamume wengine au kufuatana nao. Wanamume ni wepesi kuhisi hivyo kwamba hawawezi hata kuvumilia wake zao kuonesha kuvutiwa na picha ya mwanamume mwingine.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: "Mwanamke yeyote aliyeolewa ambaye huwatazama wanamume wengine atakabiliwa na adhabu kali ya Mwenyezi Mungu."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 37

VAZI LA HIJABU LA KIISLAMU

Wanaume na wanawake, licha ya kwamba wanavyo vipengele vingi vinavyofanana, pia wanazo tabia za pekee. Mojawapo ya tabia hizi ni kwamba wanawake ni viumbe wa kuvutia, wazuri, na wanaopendwa. Ni wachangamfu, wanavutia na wanapendwa; ambapo wanaume huchangamshwa, huvutiwa na huwapenda wanawake kwa sifa zao.

Mwanaume anapomuoa mwanamke, hutamani uzuri wote na mapenzi yote ya mke wake visitiriwe kwa ajili yake tu. Hutumaini kuwa ni yeye peke yake ndiye anayefaidi uchangamfu, mapenzi, kujishaua, uzuri, ukunjufu na kadhalika na kuwaepuka wanaume wengine kabisa. Mwanaume kimaumbile yu moto moto sana na hamvumilii mwanaume mwingine kumtazama mke wake au kuanzisha aina fulani ya uhusiano naye. Mwanaume ataona uhusiano wa karibu na mke wake na wanaume wengine kuwa ni kukiukwa kwa haki yake ya kisheria. Mume anatarajia mkewe kufuata kanuni ya vazi la kiislamu la Hijab na kwa kuwa mwepesi wa kubadilika kufuatana na tabia na maadili ya Kiislamu atashiriki katika kutunza haki yake ya kisheria.

Mwanaume yeyote aliye mwaminifu na hamasa lazima atakuwa na hamu hiyo. Tabia ya kijamii ya mwanamke ambayo imeegemezwa kwenye maadili ya Kiislamu, itaweka akili ya mume katika hali ya utulivu; kwa hiyo atafanya kazi kwa shauku kubwa ili aweze kutunza familia yake, na mapenzi kwa mke wake yataongezeka. Mwanaume wa namna hii hatavutiwa na wanawake wengine. Kinyume chake mwanaume ambaye mkewe havai Hijab ambayo ni vazi linalovaliwa na mwanamke Mwislamu na badala yake huonesha uzuri wake kwa wanaume wengine au anachanganyika nao, atatibuliwa sana. Atamuona mke wake kuwa anahusika na kukandamiza haki zake. Mume wa aina hiyo kila mara atapitia kwenye mateso na taabu na mapenzi kwa mkewe yatapungua pole pole.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 38

Kwa hiyo, ni kwa manufaa ya jamii, na wanawake kwamba wanatakiwa kuvaa inavyostahiki na kuwa na tabia ya unyenyekevu, wanatakiwa kuonekana hadharani bila urembo na kuacha kuonesha uzuri wao kwa wengine.

Kuvaa Hijab ni wajibu wa Kiislamu. Mwenyezi Mungu Mweza wa yote anasema kwenye Qur'ani Tukufu:

﴿ وَقُل لِّلْمُؤْمِنَٰتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَٰرِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ
زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا ۖ وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ ۖ وَلَا يُبْدِينَ
زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ ءَابَآئِهِنَّ أَوْ ءَابَآءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ أَبْنَآئِهِنَّ
أَوْ أَبْنَآءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَٰنِهِنَّ أَوْ بَنِىٓ إِخْوَٰنِهِنَّ أَوْ بَنِىٓ أَخَوَٰتِهِنَّ أَوْ نِسَآئِهِنَّ
أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَٰنُهُنَّ أَوِ ٱلتَّٰبِعِينَ غَيْرِ أُو۟لِى ٱلْإِرْبَةِ مِنَ ٱلرِّجَالِ أَوِ ٱلطِّفْلِ
ٱلَّذِينَ لَمْ يَظْهَرُوا۟ عَلَىٰ عَوْرَٰتِ ٱلنِّسَآءِ ۖ وَلَا يَضْرِبْنَ بِأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِينَ
مِن زِينَتِهِنَّ ۚ وَتُوبُوٓا۟ إِلَى ٱللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهَ ٱلْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٣١﴾ ﴾

"Na waambie Waumini wanawake wainamishe macho Yao, Na wazilinde tupu zao, na wala wasioneshe uzuri wao isipokuwa unaodhihirika. Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao, wala wasioneshe uzuri wao ila kwa waume zao, au baba zao au baba wa waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au kaka zao, au watoto wa kaka zao, au wana wa dada zao, au wanawake wenzao, au iliyowamiki mikono yao ya kuume, au wafuasi wanamume wasio na matamanio, au watoto ambao hawajajua mambo yanayohusu

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 39

uke. Wala wasipige chini miguu yao ili yajulikana mapambo waoliyoyafisha. Na tubuni vyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waumini, ili mpate kufanikiwa. (Qurani, 24:31)

Kuchunga vazi la Kiislamu la Hijab na kuizingatiwa matumizi yake

katika jamii kuna manufaa kwa wanawake katika vipengele vingi:
Kwa kutumia vazi la Hijab, wanawake wanaweza kulinda uzuri wao wa kijamii na maadili ya ndani kwa ubora zaidi, na kujilinda dhidi ya kuwa tu kitu kilichopo kwenye maonesho.

Wanaweza kuthibitisha imani na mapenzi yao kwa waume zao, kwa ukamilifu zaidi na kwa hiyo kusaidia kutengeneza na kutunza familia yenye uchangamfu na kuzuia hisia mbaya na ugomvi wa kifamilia. Kwa ufupi, wanaweza kuvutia nyoyo za waume zao na kujiimarisha kwenye familia zao.

Kwa kuzingatia matumizi ya Hijab ya Kiislamu mitazamo isiyo ya kisheria yenye dokezo ya kutamani kutoka kwa watu wenye udhaifu huo, itakoma na kusaidia kupunguza idadi ya ugomvi, kuimarisha mizizi ya familia, na matokeo yake kutengeneza mazingira ya utulivu ndani ya familia.

Hijab ya Kiislamu ya wanawake pia itasaidia vijana wa kiume ambao hawajaoa, kutokana na kujiingiza kwenye vitendo viovu. Hivyo, kuwaepusha vijana dhidi ya mazingira yanayoamsha hisia za kutamaani mwanamke aliyevaa nguo isiyo sitiri umbo lake hali ambayo pia itawanufaisha wanawake katika jamii.

Kama wanawake wote wangefuata utaratibu wa Hijab ya Kiislamu basi, wanawake wote wangekuwa na uhakika kwamba waume zao wanapokuwa nje ya familia zao, hawangekutana na mwanamke asherati ambaye angewavutia na kumtoa nje ya familia yake.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 40

Uislamu unatambua lengo mahususi ambalo limesababisha kuumbwa kwa mwanamke na humuona yeye kama msingi muhimu wa jamii na kupewa wajibu kwa jamii. Jamii humtaka mwanamke ajitolee katika kutekeleza wajibu wake wa kuvaa Hijab ya Kiislamu, ambayo ingeepusha uovu na upotofu wa jamii na kutengeneza uimara, usalama na kutukuza taifa lake. Lakini kwa wazi wazi thawabu kubwa zaidi ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mweza wa yote kwa kutekeleza wajibu wake kwa dini.

Mpendwa Bibi! Kama unapenda uimara na amani kuwepo kwenye familia yako, na mumeo aendelee kukuamini wewe siku zote, kama unajihusisha na haki za wanawake katika jamii; kama unavutiwa na afya ya vijana kiakili na unao wasi wasi kwamba wanaweza wakaacha maadili mema, kama unataka kuchukua hatua za uhakika za wanaume waovu kuacha kuwatongoza wanawake; na kama unatafuta radhi ya Mwenyezi Mungu kwa kuwa Muislamu muaminifu na mwenye kujitolea, basi tumia vazi la Hijabu ya Kiislamu. Usioneshe uzuri wako na urembo wako kwa wageni, ama uwe ndani nyumbani kwako ukiwa na ndugu zako wa karibu, au kwenye mikusanyiko mingine ya kijamii nje ya nyumbani kwako. Lazima uvae ushungi mbele ya shemeji zako na watoto wao, waume wa wifi zako, waume wa shangazi zako, na binamu zako. Usipovaa Hijabu ya Kiislamu mbele ya watu waliotajwa ni dhambi na pia unaweza kusababisha mateso makubwa kwa mumeo, hata kama hatasema.

Mwanamke halazimiki kuvaa Hijabu kwa kiwango kile kile mbele ya baba mkwe, kaka yake, na watoto wa kiume wa kaka au dada yake, ingawa ni vema kwa kiwango fulani kuvaa Hijabu mbele ya watu hawa pia. Kwa usemi mwingine, wanawake wasionekane mbele ya watu hawa- ndugu zake- kama ambavyo anaweza kuvaa kwa kumvutia mumewe. Hii ni kwa sababu wanaume wengi sana hawapendi wake zao waonekane katika hali ya kuvutia kwa kuvaa nguo au urembo mbele ya

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 41

wanaume wengine, na kama mambo yalivyo isisahaulike kwamba utulivu wa akili na imani ya mume kwa mke wake ni muhimu sana kwa kudumu na usalama wa familia yote.

SAMEHE MAKOSA YA MUMEO

Kila mtu isipokuwa wale ambao Mwenyezi Mungu amewatangaza kuwa **'Maasum'** hufanya makosa. Watu wawili wanaopendana na wanashirikiana pamoja, hufanya makosa, lazima wawe wasemehevu. Kama hawatasameheana, basi ndoa yao itavunjika.

Wafanya biashara wawili ambao ni wabia, na jirani wawili, marafiki wawili na hususan mume na mke wanahitaji kusameheana. Kama watu wa familia hawasameheani na kufuatilia makosa ya kila mmoja wao, basi ama familia itafarakana au wataishi maisha yasiyovumilika.

Mpendwa Bibi! Pengine mumeo hufanya makosa. Anaweza akakutukana, akakufedhehesha, akasema uwongo, anaweza hata kukupiga. Matendo kama hayo yanaweza kufanywa na mwanamume yeyote.

Baada ya kufanya kosa, kama mumeo hujuta kwa kosa hilo au wewe unahisi anajuta kwa kosa lake hilo, basi msamehe na usilifuatilie jambo hilo. Kama anajuta lakini hayupo tayari kuomba msamaha, basi usijaribu kuthibitisha kosa lake. Vinginevyo, anaweza kuhisi anadhalilishwa na anaweza kulipiza kisasi kwa kukumbuka makosa yako na kwa hiyo, ikawa chanzo cha ugomvi mkubwa kwa hali hiyo, ni bora wewe unyamaze kimya hadi hapo atakapo jilaani mwenyewe kutoka kwenye dhamira yake na akaanza kuhisi majuto kuhusu kosa hilo. Hapo atakuona wewe kuwa ni mtu mwenye busara na mke wa kujitoa kwa mambo mema ambaye anavutiwa na mume wake, na familia yake.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 42

Mtume (s.a.w.w) wa Mwenyezi Mungu alisema: Mwanamke mbaya hatoi msamaha kwa makosa ya mumewe na hakubali hata kuomba msamaha."

Je, si ni jambo la kusikitisha kwamba mkataba wa ndoa takatifu unavunjwa kwa sababu mwanamke hayupo tayari kusamehe makosa fulani ya muewe?

KUWEZA KUISHI NA NDUGU WA MUMEO

Mojawapo ya matatizo ya kifamilia husababishwa na ndugu wa mume na mke wake. Baadhi ya wanawake hawana uhusiano mzuri na mama wa mumewe, dada au kaka zake mumewe. Kwa upande moja mke anaweza kujaribu kumtawala mume wake ili asiweze kumsikiliza hata mama yake au ndugu yake yeyote na anaweza kujaribu kuwafitinisha ili wasielewane wao kwa wao. Kwa upande mwingine, mama wa mume anajiona kuwa yeye ni mmiliki wa mwanae na mke wa mwanae. Mama hujaribu sana kuwa karibu sana na mwanae na kutahadhari kwamba mke wa mwanae asiweze kummiliki mumewe kwa ukamilifu. Anaweza kusingizia uwongo kuhusu mke wa mwanae au kumuona anayo makosa. Msimamo wa aina hii unaweza kufuatwa na mabishano mengi na hata chuki ya mara kwa mara. Hali inakuwa mbaya zaidi endapo watu hawa huishi kwenye nyumba moja. Hata kama ugomvi unaweza kutokea baina ya wanawake wawili, uchungu wa kiakili na dhiki hasa zaidi humpata mume aliyoko kati yao.

Mume ananaswa katikati ya mabishano ambapo hawezi kuegemea upande wowote. Kwa upande moja yupo mke wake ambaye angependa kuendesha maisha ya kujitegemea bila kuingiliwa na mtu yeyote. Kwa kawaida mume huhisi lazima amsaidie mke wake na amfurahishe. Lakini kwa upande mwingine, anafikiria wazazi wake ambao wamemsaidia kuingia katika maisha, wamemsomesha na wametumia muda mwingi wa maisha yao kumlea. Anahisi kwamba wazazi wake wanatarajia awasaidie wakati

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 43

wanahitaji msaada na kwamba haitakuwa busara kuwasahau. Zaidi ya hayo, kama yeye mwenyewe anayo haja ya kupata kitu fulani, hatakwenda kwingineko isipokuwa kwa wazazi wake, ambao watamsaidia yeye na familia yake. Matokeo yake ni kwamba anatambua kwamba marafiki zake wakuaminika ni wazazi wake na ndugu zake. Kwa hiyo, mtanziko kwa mtu mwenye busara ni ama kuwa upande wa mke na kuwaacha wazazi au kinyume chake, lakini hapana lolote kati ya haya mambo mawili yanawezekana.

Matokeo yake, atalazimika kwenda na pande zote mbili na kuziweza pande hizi katika hali ya kuridhika ambayo ni kazi ngumu. Njia moja tu inayoweza kurahisisha hali ni kwamba mwanamke lazima awe mwaminifu na mwenye hekima. Katika hali kama hii, mume anatarajia mkewe amsaidie katika kutatua tatizo. Kama mke anamheshimu mama mkwe wake, humtaka ampe ushauri wake, na anakuwa mtiifu na kufanya urafiki naye basi, mama mkwe wake atakuwa msaidizi wake mkubwa sana.

Je, si jambo la kusikitisha kuona mtu ambaye anaweza kuwavutia watu wengi kwa sababu ya wema wake na tabia zake, halafu awafukuze kwa ajili ya ukaidi na ubinafsi wake? Hutambui kwamba katika mazuri na mabaya ya maisha, mtu anaweza akahitaji msada wa wengine, na hususan ule wa ndugu ambao wanaweza kukusaidia ambapo kila mtu akiwa amekukimbia? Je, si ni jambo zuri zaidi kufurahia uhusiano mzuri na ndugu wa mtu kwa kutumia busara na tabia njema? Je, hivi kweli ni busara na haki kufanya urafiki na watu wengine ambapo unavunja uhusiano na ndugu zako?

Uzoefu unaonesha kwamba mtu anapotaka msaada kutoka kwa wengine, marafiki humkimbia lakini ndugu aliwo watupa huja kumsaidia. Hii ni kwa sababu mshikamano wa kifamilia unao asili na hauwezi kuvunjika kwa urahisi. Kuna methali isemayo: “Hata kama nyama ya mtu ingeliwa na ndugu zake, wasingeitupa mifupa yake”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 44

Imam Ali (a.s) alisema: "Mtu hawezi kamwe kuishi bila kuwa na ndugu zake, hata kama ni tayari na anao watoto."

Mtu atataka heshima na wema wa ndugu zake. Ni wao ndio watakao msaidia kimwili na kiakili. Ni ndugu ndio wanasaidia mara nyingi. Wakati wa shida ndugu huweza kusaidia haraka zaidi kuliko wengine. Yeyote anaye watupa ndugu zake hupoteza mikono mingi, ya kumsaidia.

Mpendwa Bibi! Kwa ajili ya mume wako na faraja yako mwenyewe na pia kutafuta marafiki wengi na wanao kuunga mkono, vumilia kuwa nao ndugu wa mumeo. Usiwe mbinafsi na mjinga; uwe na busara na usisababishe usumbufu wowote kwa mumeo. Uwe mke mzuri na mwenye kujitolea ili uweze kukubalika kwa Mwenyezi Mungu na watu.

KUVUMILIA KAZI YA MUME WAKO

Kila mtu anayo kazi na kazi hutofautiana; mathalan, dereva ambaye muda mwingi zaidi yupo barabarani na anashindwa kurudi nyumbani kila siku usiku; polisi ambaye anatakiwa kuwa kwenye zamu baadhi ya muda wa usiku; daktari wa tiba ambaye ana muda mfupi wa kuwa na familia yake, mkufunzi au mwanasayansi ambaye husoma sana muda wa usiku; makanika ambaye nguo zake ni chafu na hunuka mafuta, mfanyakazi kiwandani ambaye hufanya kazi usiku. Kwa hiyo ni mara chache sana mtu kuwa na kazi ambazo hazisumbui kwa namna moja au nyingine na kusababisha kero kwa familia.

Hakuna njia nyingine yeyote ya kupata riziki kihalali isipokuwa kufanya kazi. Ni muhimu kwa wanaume kuvumulia matatizo ya kazi zao. Hata hivyo, kuna tatizo lingine ambalo ni malalamiko ya familia.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 45

Kwa kawaida wanawake hupenda waume zao kuwa karibu nao na hupendelea wawepo nyumbani giza liingiapo. Wanawake hutaka waume zao kuwa na kazi nzuri yenye mshahara mnono. Wanapenda kuwa na muda wa kutosha wa kwenda matembezi ya jioni. Lakini bahati mbaya kazi za waume walio wengi, hazikidhi matamanio ya wake zao, na hii kwa baadhi ya familia ni chanzo cha ugomvi na mabishano.

Dereva ambaye amekuwa kazini kwa mausiku kadhaa, ambaye hajalala usingizi wa kutosha na amekuwa hapati chakula kwa wakati unaostahili, anaingia nyumbani kwake apumzike na apate amani na faraja akiwa na familia yake. Halafu mke wake, bila kumpa nafasi ya kupumzika hata kidogo, anaanza kupiga kite na kugumia: "maisha gani haya? Kwa nini unaniacha mimi na watoto hawa na ulikuwa wapi? Ninafanya kazi zote kwa sababu wewe haupo ambapo ungenisaidia. Nimechoshwa na hawa watoto watundu! Na kwa kweli udereva si kazi nzuri. Ama lazima ubadili kazi au tulizana na mimi hapa nyumbani. Siwezi kuishi namna hii zaidi ya hapa!" Masikini dereva huyu ambaye anaye mke wa aina hii hawezi kutegemewa kufanya vizuri kazi yake na anaweza kuhatarisha maisha yake; na maisha ya hao anao wasafirisha. Daktari ambaye tangu asubuhi hadi usiku, huwatembelea wagonjwa makumi kadhaa hawezi kuvumilia malalamiko ya mke wake. Daktari huyu ataweza kuendelea na kazi yake? Mfanya kazi ambaye hufanya kazi ya zamu ya usiku hawezi kufuatilia kazi yake kwa hamasa endapo mke wake ni mwanamke mjanja.

Mwanasayansi ataweza kufuzu katika eneo la taaluma yake ya utafiti endapo mke wake anamsumbua kila wakati? Hii ni mitihani inayo wabainisha wanawake wenye busara na wale walio wajinga.

Mpendwa Bibi! Hatuwezi kuitengeneza dunia iwe vile tunavyotaka sisi, na mazingira yaliyopo. Mume wako anahitaji kazi ili aweze kupata riziki halali kwa ajili ya familia yake. Kazi yake inayo masharti ambayo

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 46

yatakufanya ubadilike ili uendane nayo. Lazima upange utaratibu wa maisha ya familia yako kufuatana na kazi yake. Kwa nini ulalamike na umuone anayo makosa kwa sababu ya kazi yake? Mkaribishe nyumbani kwa uso wenye furaha na uwe mwema kwake. Uwe na hekima na uivumilie kazi yake.

Kama mume wako ni dereva ambaye muda mwingi yupo barabarani, basi, tambua kwamba anajaribu kuleta fedha nyumbani kwa ajili yako na watoto. Kazi yake si tatizo. Yeye ni sehemu ya jamii na anaihudumia kwa namna nzuri kadiri awezavyo. Ingekuwa bora kama angekuwa mvivu au kama angekuwa anafanya kazi isiyoendana na masharti ya dini? Kwa hiyo, yeye hana ubaya wowote. Kasoro ipo kwako, unatarajia awepo nyumbani kila siku usiku na wewe unashindwa au hutaki kubadilika kufuatana na hali iliyipo sasa.

Hivi si busara kuzoea hali ya wakati uliopo na kuishi kwa raha zaidi? Si ingekuwa bora zaidi kumkaribisha mumeo kwa uso wenye tabasamu na kumshawishi aendelee na kazi yake kwa kumpa 'kwa heri' ya kuchangamsha anapoondoka nyumbani kwenda kwenye kazi yake? Kama ukimfanyia wema, atazidi kuvutiwa na familia yake na anaweza kuzidisha bidii kwenye kazi yake. Hata farakana na wewe; atarudi nyumbani mapema kadiri iwezekanavyo; atajitahidi asifanye ajali na atakuwa imara kushikilia maadili mema.

Kama mume wako anafanya kazi ya zamu ya usiku, anakosa usingizi mzuri wa usiku ili aweze kumudu matumizi ya familia yake. Jaribu kuzoea hali hii na usioneshe kutokuridhika kwako. Kama unachoshwa na upweke, unaweza kufanya baadhi ya kazi za nyumbani, kushona na kusoma wakati wa usiku. Asubuhi tayarisha kifungua kinywa, mume wako anaporudi kutoka kwenye kazi, halafu tandika kitanda mahali penye kimya. Wanyamazishe watoto wawe kimya na uwafundishe wasimsumbue baba yao wakati anapumzika. Unaweza hata kulala nusu usingizi ili uweze

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 47

kupumzika na mume wako wakati wa mchana. Lakini usisahau kwamba amekuwa macho usiku kucha na usingizi wake wa mchana ni sawa na usingizi wako wa usiku. Wanawake waliopo kwenye hali kama hii wanatakiwa kuwa na mipango ya aina mbili, moja wa kwao na mwingine wa waume zao.

Kama mume wako ni dereva, dakitari, mfanya kazi au bingwa wa sayansi na kadhalika, basi lazima ujivune na sababu ya kuwa naye. Mume wako si mvivu, mzururaji au hafanyi kazi isiyo afikiana na mafundisho ya dini. Kwa hiyo, umthamini na kumshukuru.

Usimtarajie yeye au kumuambia aache kazi yake, lakini jaribu kuafikiana na kazi aliyonayo. Kama anasoma au anatafiti katika eneo fulani, basi usimsumbue. Wewe unaweza kufanya kazi ya nyumbani soma kitabu au kwa ruhusa yake, nenda uwatembelee marafiki au ndugu. Lakini, wakati anapumzika, jaribu kuwepo nyumbani. Tayarisha chakula chake na mahitaji mengine. Mpokee mume wako kwa tabasamu na tabia njema. Kwa kuonesha wema wako na kwa kumfurahisha, unaweza kumfanya asahau uchovu wake. Kama wewe ni mke mzuri, basi si tu kwamba utaharakisha kupandishwa kwake cheo, lakini unatoa mchango kwa huduma zake kwa jamii.

Si wanawake wote wanastahiki wanamume wenye bidii kama hao. Kwa hiyo, kwa kuwa na tabia njema na mwenye kujitolea, thibitisha kwamba na wewe unastahiki kuwa naye.

Kama kazi ya mume wako inamtaka avae nguo rasmi ambazo huchafuka, basi zifue nguo hizo mara kwa mara. Usilalamike na usimwambie mambo yasiyofaa kwa sababu ya kazi yake. Usimwambie abadili kazi. Kuna ubaya gani kuwa makenika? Kwa vyovyote vile, hili si jambo la umuhimu na familia zisivunjike kwa sababu hii.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 48

"Mwanamke alimwambia jaji mahakamani kwamba kazi ya mume wake, ilikuwa kuuza mafuta ya taa na kwa hiyo kila mara alikuwa ananuka vibaya na kwa hiyo alichoshwa na hali hiyo."

ENDAPO MNATAKIWA KUISHI NJE YA MJI WA NYUMBANI

Mtu anaweza kutakiwa kuishi nje ya mji wa nyumbani kwake. Mume wako anaweza kuwa anafanya kazi kwenye sekta binafsi au ya umma, na akahamishwa na kupelekwa kwenye mji mwingine. Watu wengine huishi hivi ama kwa muda au moja kwa moja. Wanaume wanalazimika kuvumilia hali hii lakini wanawake wengine hupenda kuwa karibu na wazazi wao na ndugu zao.

Wanawake hawa wamezoea mitaa, kuta ndefu na mazingira ya mahali walipozaliwa. Baada ya kuhama huanza kuwalaumu waume zao na kulalamika: "Kwa nini niishi mbali na nyumbani? Hadi lini nitakuwa mbali na nyumbani, na wazazi wangu? Sina mtu mahali hapa. Umenileta wapi hapa? Siwezi kuishi hapa; Kwa hiyo fikiria namna ya kutatua tatizo hili!"

Wanawake hawa hawatakiwi kuwatibua waume zao namna hii. Wanawake hawa ni dhaifu sana kiakili hivyo kwamba wanadhani mahali waliko zaliwa ndizo sehemu nzuri zaidi kuishi. Wanafikiri kwamba hawawezi kufurahia maisha mahali pengine. Binadamu haridhishwi hata na sayari yake, kwa hiyo, ameanza kwenda kwenye sayari nyingine. Lakini mtu anamuona mwanamke ambaye hafikirii, wakati ujao hata kidogo hivyo kwamba hayupo tayari kuishi umbali wa maili chache kutoka mji wa nyumbani kwake. Yeye anafikiri; "Kwa nini niwaache marafiki zangu na ndugu zangu wote niende ugenini?" Inakuwa kama vile mwanamke huyu hajiamini vya kutosha kuweza kupata marafiki wapya mahali pengine mbali na alikozaliwa.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 49

Mpendwa mama! Uwe na busara na mwenye kujitolea. Usiwe mbinafsi. Sasa kazi ya mume wako imekuondosha kutoka kwenye mji wa nyumbani kwako, usimsababishie usumbufu. Kama yeye ni mfanyi kazi serikalini, ameamuriwa kuondoka kwenda kwenye kazi na kama anayo biashara binafsi, basi kwa hakika ni kwa manufaa yake mwenyewe kuishi mahali pengine. Endapo mume wako anakutaarifu kwamba anakwenda kuishi sehemu nyingine, unatakiwa kukubali mara moja. Unatakiwa kumsaidia kufunga mizigo na kwenda mahali pa ugenini ambako lazima ujaribu kuhisi upo nyumbani. Panga maisha yako hapo ambapo ndio nyumbani kwako na ujirekebishe ili upazoee. Kwa kuwa wewe ni mgeni katika sehemu hii na labda huna mazoea na tabia za wakazi wa hapo, uwe na tahadhari nao. Baada ya muda, kwa msaada wa usimamizi wa mume wako, jaribu kupata marafiki kutoka kwa wanawake safi na wakuaminika.

Kila sehemu inayo sifa zake. Unaweza kujipumzisha kwa kuona sehemu za kuvutia na kutembelea majengo ya zamani. Lazima muweke familia pamoja na umtie moyo mume wako katika kazi yake. Baada ya muda utazoea nyumba yako mpya na inawezekana hata ukapapenda zaidi kuliko ulikotoka. Unaweza ukaona kwamba marafiki zako wapya ni bora zaidi kuliko wa zamani.

Endapo hiyo sehemu mpya itakosa starehe za mji wa zamani, basi zoea maisha mapya na tafuta sifa zake. Endapo hakuna huduma kama vile umeme, basi mazingira yenu yanaweza kuwa na hali ya hewa nzuri zaidi na mnaweza kupata vyakula vibichi na vyenye ubora wa kiwango cha juu. Kama hakuna barabara nzuri basi hamtavuta hewa yenye sumu kutoka kwenye moshi wa magari na hamtasumbuliwa na kelele za watu na magari.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 50

Wafikirie wanaume na wanawake wanaoishi vijijini kwa furaha kwenye nyumba za matofali ya udongo na hawatajali kwa vyovyote vile starehe za jiji na nyumba zao nzuri zifananazo na kasri. Fikiria mahitaji yao na yale wanayoyakosa. Kama unaweza kuwasaidia, basi usisite na mtie moyo mume wako kuwa na msaada kwao. Kama wewe unayo busara na unafanya kazi yako, basi utaishi kwa raha kwenye sehemu hiyo ya ugenini. Unaweza kuwa na msaada kwa maendeleo ua mume wako. Kwa njia hii utajulikana kama mke unayeheshimiwa na kujitoa katika mambo mema. Utapendwa na mume wako na utakuwa maarufu miongoni mwa watu. Zaidi ya hayo, Mwenyezi Mungu ataridhika na wewe.

KAMA MUME ANAFANYA KAZI NYUMBANI

Wanawake wale ambao waume zao wanafanya kazi nje wana uhuru nyumbani. Lakini baadhi ya wanaume wanafanya kazi nyumbani, kama vile watunzi wa mashairi, waandishi, mafundi rangi, au wanasayansi ambao huhitaji kusoma sana. Wake wa wanaume wa aina hii wana uhuru mdogo nyumbani na kwa hiyo maisha yao ni tofauti. Kazi zilizotajwa hapo juu zinahitaji umakini zaidi, kipaji na akili. Kwa hiyo, panahitajika faragha na ukimya. Saa moja ya kazi iliyofanywa mahali pa ukimya ni sawa na kazi iliyofanywa kwa saa kadhaa mahali penye shughuli na kelele nyingi. Tatizo liko wazi kwa upande moja, mwanaume anahitaji mahali palipo tulia afanye kazi yake na kwa upande mwingine, mke anataka apite hapa na pale ndani ya nyumba kwa uhuru.

Kama mwanamke anapanga mambo ya nyumba kama hiyo kwa namna ambayo kwamba mume wake anaweza kuendelea na kazi yake, kwa kweli atakuwa amefanikisha kazi ya manufaa. Mafanikio ya aina hiyo kwa hakika hayapatikani kwa urahisi, hususan pale ambapo wapo watoto. Lakini, hata hivyo, tatizo lazima litatuliwe, kwa sababu maendeleo ya mume katika kazi yake yatategemea kutokuwepo kwa tatizo hili.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 51

Kama mwanamke anashirikiana na mume wake, anaweza kumfanya awe mtu wa kuheshimiwa ambaye atakuwa na sifa kwake na jamii.
Mwanamke ambaye mume wake hufanya shughuli zake nyumbani, asije akamtarajia kumlea mtoto, kufungua mlango kwa ajili ya wageni, kwenda jikoni, kusaidia kazi za nyumbani, kukemea watoto…Lakini anatakiwa afikirie kana kwamba hayupo ndani ya nyumba ambapo anaendelea na kazi.

Mpendwa Bibi! Mume wako anapotaka kwenda chumba cha kusomea tayarisha kalamu, karatasi, sigara, kisahani cha majivu, kiberiti, vitabu na vitu vingine atakavyo vihitaji.

Ukishatayarisha chumba na vitu anavyo vihitaji, mwache peke yake. Usizungumze kwa sauti kubwa na usiwaruhusu watoto wapige kelele. Wafundishe watoto wako wasicheze kwa fujo na kelele wakati baba yao anaendelea na kazi. Usiseme naye kuhusu mambo ya kila siku. Jibu hodi ya mlangoni na simu. Kama mtu anataka kumuona au kuzungumza naye mwambie anashughuli. Wakirimu wageni wakati anapopumzika. Waambie marafiki na ndugu zako kumtembelea mume wako wakati hana shughuli. Marafiki zako wa kweli hawataudhika kwa taarifa yako hiyo. Wakati unafanya kazi zako za nyumbani, mtekelezee mahitaji yake, usimwingilie kati.

Labda baadhi ya wanawake wanafikiri haiwezekani kuishi kwa njia hii. Wanaweza wakasema: “Hivi inawezekana mwanamke kufanya kazi ngumu ya nyumbani na wakati huo huo amtunze mume wake pasipo kuruhusu kitu chochote kuingilia kazi zake?”

Ni kweli kwamba maisha ya aina hii si ya kawaida na huonekana magumu, lakini kama wanawake wahusika wanatafakari kuhusu umuhimu wa kazi za waume zao, wanaweza kuamua kutatua tatizo kwa kufanya mpango, bidii na hekima. Upekee wa baadhi ya wanawake hudhihirika katika

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 52

hali kama hii. Vinginevyo, kuendesha maisha ya familia ya kawaida ni kazi ya kawaida.

Mpendwa Bibi! Kuandika kitabu, makala nzuri ya kisayansi au tungo nzuri, kuandika shairi zuri sana, kutengeneza mchoro mzuri au kutatua matatizo ya kisayansi si kazi rahisi. Lakini, moyo kwa upendo na ushirikiano, hilo linawezekana. Je, huko tayari kuyatoa mhanga matamanio yako pamoja na mabadiliko kidogo tu katika maisha yako? Kwa kufanya hivyo utakuwa unamsaidia mume wako katika kazi yake. Kwa msaada wako huo, mume wako atapata hadhi kubwa na wewe utashiriki katika hadhi hiyo.

MSAIDIE MUME WAKO KUPATA MAENDELEO

Wanadamu kiasili wanazo nguvu zisizo dhihirika za kuwawezesha kupata maendeleo. Kupenda kupata ubora ni hali ambayo kila mmoja wetu anayo; na tumeumbwa ili tuweze kufanikisha ubora. Kila mmoja, ambaye anayo kazi yoyote katika umri wowote na katika hali yoyote anaweza kuendelea na kukomaa. Mtu hatakiwi kutosheka na hali ya yeye kuwepo tu na asisahau makusudio ya kuumbwa. Mtu lazima ajaribu kupata ubora katika kipindi cha uhai wake.

Licha ya kwamba kila mtu anafuatilia maendeleo, si wote wanaofanikiwa kupata maendeleo yanayohitaji malengo ya juu na juhudi kubwa ya kufanya kazi. Mtu lazima atayarishe uwanja na kuondosha vigingi na baada ya hapo anachukua hatua muhimu za kuelekea kwenye mkondo wa maendeleo. Umashuhuri wa mwanaume unategemea sana utashi wa mke wake. Mwanamke anaweza kumsaidia mume wake kupata maendeleo kama vile ambavyo pia anaweza kuwa mwenye kusababisha hasara kuhusu maendeleo ya mume wake.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 53

Mpendwa Bibi! Wakati ambapo unafikiria uwezekano, fikiria hadhi ya juu zaidi ya mume wako na umtie moyo wa kufanikiwa. Kama bado anataka kuendelea na masomo yake au kama anataka kuongeza ujuzi wake kwa njia ya kusoma na utafiti, basi usimsitishe. Mpe moyo wa kufanikisha matakwa yake Panga maisha yako kwa namna ambayo hayatakuwa kipingamizi cha maendeleo yake. Jaribu kumsaidia ili apate maendeleo kwa kutengeneza mazingira ya kuburudisha na kuliwaza ndani ya nyumba yenu. Kama mumeo hakusoma, mshawishi kwa unyenyekevu, mwambie aanze masomo yake ya usiku. Kama mumeo ni msomi, mtie moyo wa kuongeza ujuzi wake kwa kusoma zaidi.Kama mume wako ni daktari wa tiba, mhamasishe asome majarida ya tiba na makala zingine zinazohusiana na tiba. Kama mumeo ni mwalimu, mhandisi au jaji, basi mwambie awe anasoma vitabu na makala mbali mbali zinazohusiana na utaalamu wake. Unatakiwa kukumbuka kwamba katika kazi yoyote ambayo anafanya mumeo, ipo fursa ya kuendelea.

Usimruhusu mume wako aache mkondo ambao umewekwa na mpangilio kwenye muumbo. Mtumainishe asome vitabu. Usiruhusu umashuhuri wake usiendelee kuongezeka.

Kama hana muda wa kununua au kupata vitabu basi kwa kutumia ufawidhi wake wa rafiki yake, pata vitabu anavyo vipenda yeye. Mpe vitabu hivyo na mpe matumaini ya kusoma. Wewe pia unatakiwa kusoma vitabu na majarida yenye manufaa. Kama katika kusoma kwako unasoma makala ambayo ina manufaa kwa mume wako, basi mtaarifu. Kitendo hiki kina manufaa kadhaa:

Kwa kufanya hivi mara kwa mara, mume wako atakuwa mtu mwenye kuelimika ambaye atakujengea heshima wewe na yeye. Aidha, atakuwa bingwa mzuri sana ambaye huduma zake zita mnufaisha yeye na jamii yake.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 54

Kwa kuwa amekubaliana na sheria za muumbo, kupitia kwenye masomo na utafiti wake, hapatakuwepo na uwezekano yeye kupata maradhi ya akili na kuchanganyikiwa.

kwa kuwa yupo kwenye mkondo wa kuelekea kwenye maendeleo na anaonesha kupendelea kusoma, basi ataambatana zaidi na wewe na watoto, hatavutiwa kwenye uovu na hatanasa kwenye mtego wa mazoea ya hatari.

KUWA MWANGALIFU MUME WAKO ASIPOTOSHWE

Wanaume wanatakiwa kuwa na uhuru wao na ushirikiano wao katika shughuli ili waweze kufanya kazi na kuendelea kwa namna inayowafaa. Kama wanaume watawekewa masharti katika shughuli zao, basi, hawatakuwa na furaha. Mke mwenye busara hawezi kuingilia mambo ya mume wake. Mke hatakiwi kufuatilia nyendo za mume wake; kwa sababu lazima atambue kwamba kwa kumnyima mume wake uhuru anaouhitaji na kujaribu kumdhibiti katika shughuli zake anaweza kujibu kwa ukali sana.

Wanaume wenye busara na uzoefu hawahitaji kudhibitiwa.Wanaume kama hao kila mara kufanya mambo yao kwa busara; si rahisi kuwa danganya; wao wanawajua marafiki zao na maadui zao. Hata hivyo, wapo watu ambao ni wa kawaida; watu hawa wanaweza kudanganywa kwa urahisi na kuvutiwa kwa urahisi na watu wengine.

Wapo watu ambao ni laghai na wanangoja kuwadanganya watu wa kawaida. Mtu laghai, licha ya kujifanya kuwa mwema, humtega na kumnasa mtu mwingine na kumwelekeza kwenye uovu. Jamii iliyojaa uovu na tabia ya binadamu isiyokubali kushindwa haisaidii kurekebisha hali. Mtu wa kawaida anaweza asijue hali yake kwa kipindi fulani, lakini siku moja anashtuka na kujikuta yupo kwenye kina cha mtego na hawezi kujinasua.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 55

Ukiangalia kila mahali pale ulipo, utaona watu wengi wa aina hiyo wenye bahati mbaya. labda hakuna hata mmojawao aliye nuia kuanguka kwenye mtego au kuwa mwovu. Lakini kupitia kwa urahisi wao, ujinga na uamuzi wa pupa sasa wamekuwa mawindo ya waovu katika jamii.

Kwa sababu hii, watu wepesi wanatakiwa kusimamiwa. Kwa kufuatilia shughuli zao, watu wenye busara na wenye kuwatakia mema wenzao watakuwa wamewafanyia huduma kubwa.

Watu wazuri sana kwa kazi hii, hata hivyo, ni wake wa wanaume hawa. Mke mwenye busara na mwerevu anaweza kufanikiwa kazi kubwa sana kuhusu mume wake, kwa msimamo wa kumsaidia na busara. Wanawake wa aina hii, hata hivyo, lazima wakumbuke kwamba hawatakiwi kuingilia moja kwa moja mambo ya waume zao, au kuwaambia “Wafanye hivi” na “wasifanye vile”. Sababu yake ni kwamba wanaume mara nyingi hawataki kabisa kutumiwa kama kitendea kazi mikononi mwa wengine vinginevyo watajibu kwa ukali. Lakini mwanamke mwenye hekima angefuatilia shughuli za mumewe na kuwaangalia washirika wake bila kudhihirika, na mume asitambue.

Pia hutokea kwamba baadhi ya wanamume, wakati mwingine huchelewa kurudi nyumbani isivyo kawaida. Endapo jambo hili linatokea na idadi ya siku anazochelewa kurudi nyumbani imo katika kiwango kinacho kubalika, basi hapana haja ya kuwa na wasi wasi, kwa sababu upo wakati ambapo wanaume hujikuta wanajaribu kushughulikia mambo ambayo hawakuyategemea baada ya kazi zao. Hata hivyo, endapo idadi ya siku anazochelewa kurudi nyumbani inazidi kiwango kisicho kubalika, basi, mke wake atalazimika kufanya upelelezi. Lakini, upelelezi si jambo rahisi, unahitaji uvumilivu na busara, mtu lazima aepuke hasara na malalamiko. Kwanza kabisa, mke anatakiwa azungumze na mume wake kwa upole na wema: Mke amuulize mume wake kwa nini alirudi nyumbani kwa

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 56

kuchelewa kuliko jana yake na alikuwa wapi. Mke anatakiwa kufuatitilia jambo hili kwa busara na uvumilivu katika nyakati mbali mbali na fursa tofauti. Kama atagundua kwamba mumewe huchelewa kurudi nyumbani kwa sababu ya kazi yake au kuhudhuria mkutano wa kisayansi, kidini na kimaadili, basi amwache aendelee hivyo. Kama mke anahisi kwamba mume wake amepata rafiki mpya, anatakiwa ajue rafiki huyoni nani. Kama rafiki yake mpya ni mtu mwenye tabia njema na mwenendo safi, basi, asiwe na wasi wasi, kwa sababu rafiki mzuri ni neema kubwa.

Ukihisi kwamba mume wako anaingia kwenye upotofu au ameshirikiana na watu waovu na wasiofaa, basi unatakiwa umsitishe haraka sana. Katika hali kama hii, mwanamke anao wajibu mkubwa sana. Kosa dogo tu katika kushughulikia jambo hili, kwa kufanya uzembe, linaweza kuharibu maisha ya familia yao. Hii ni hali ambapo busara na werevu wa baadhi ya wanawake hutumika na kudhihiri. Mtu lazima akumbuke kwamba ugomvi na ubishi si suluhu na huweza kusababisha kinyume chake. Mwanamke nayepitia kwenye tukio hili anazo kazi mbili za kufanikisha:
kwanza anatakiwa kutathmini hali ya nyumbani; na ajipime yeye mwenyewe na msimamo wake. Lazima agundue sababu ya tabia ya mume wake. Lazima afanye uamuzi usio na upendeleo kwa nini haoneshi uchangamfu kwa familia yake na kuelekea kwenye upotofu. Mke anaweza akang'amua kwamba msimamo wake mwenyewe ndio umekuwa sababu; au labda alikuwa ndio sababu; au labda alikuwa hajali vyakula anavyo vipenda mumewe, jinsi anavyoonekana au mambo ya nyumbani. Mambo kama haya huwafanya wanaume wafarakane na familia. Wanaweza wakafuatilia mambo ya upotofu ya nje ili wasahau matatizo yao. Mke anaweza kumuuliza mume wake kuhusu matatizo yake na ajaribu kusaidia kuyatatua. Kama mwanamke alijisahihisha na kuibadilisha nyumba kulingana na matakwa yake, basi, awe na matumaini kwamba mume wake atarudi tena kwenye familia yake na kwamba ataepuka sehemu zenye uovu.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 57

Pili, mke lazima amwoneshe mume wake wema mwingi kadiri iwezekanavyo. Lazima amshauri mume wake na kumkumbusha matokeo mabaya na matendo yake. Anaweza hata kulia na kumwambia awaache marafiki zake wabaya. Lazima amwambie: Nina kupenda kwa dhati ya moyo wangu. Ninajivuna kuwa na wewe. Ninaona heri kuwa na wewe kuliko vitu vyote na nipo tayari kujitolea kwa ajili yako. Lakini nina huzunishwa na kitu kimoja; kwa nini mwanamume kama wewe, awe na marafiki kama, au ahudhurie dhifa ya aina hiyo? Matendo kama haya hayastahili kufanywa na wewe. Tafadhali acha kufanya mambo haya.

Mke lazima aendelee na msimamo huu hadi aushinde moyo wa mume wake. Inawezekana kwamba mume amezoea kuendekeza tabia zisizofaa na kwamba hawezi kuathiriwa kwa urahisi, lakini mke asikasirike. Lazima afuatilie lengo lake kwa juhudi na uvumilivu zaidi.

Wanawake wanao uwezo mkubwa kwa wanaume. Mwanamke anaweza kufanya lolote atakalo kama akili yake itamwelekeza kufanya hivyo. Kama mwanamke anaamua kumwokoa mume wake kutoka kwenye kinyaa cha maovu, anaweza kufanya hivyo. Upo uwezekano wa asili mia themanini kushinda, almuradi utekelezaji wake uwe wa busara. Kwa vyovyote vile, mke hatakiwi kutumia nguvu au msimamo wa ukali; isipokuwa tu kama haoni matokeo yoyote ya kuonesha wema na upole kwake. hata hivyo, hatakiwi agombane, aondoke nyumbani au atumie njia nyingine yoyote ile ya upole kadiri iwezekanavyo na si kulipize kisasi.

Ndio, kutunza mume ni kazi ya kila mke. Ni kazi ngumu na ndio maana Mtume (s.a.w) alisema: “Jihadi ya mwanamke ni kumtunza mume ipasavyo.”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 58

WANAWAKE WENYE DHANA

Si vibaya mwanamke kuwa na tahadhari kuhusu mume wake, lakini ni pale tu ambapo haitavuka kiwango cha dhana na kutokuaminiana. Dhana ni maradhi yenye uharibifu na yasiotibika. Bahati mbaya baadhi ya wanawake huathiriwa na ugonjwa huu (wa dhana).

Mwanamke mwenye dhana hudhania kwamba mume wake, hawi mwaminifu kwake kihalali au isivyo halali. Anadhani kwamba ameoa mke mwingine au anataka kuoa mke mwingine. Mke anatuhumu kwamba mume wake anao uhusiano wa kimapenzi na katibu mukhtasi wake au mwanamke mwingine. Hupoteza imani kwake kwa sababu huchelewa kurudi nyumbani au alionekana anaongea na mwanamke. Endapo atamsaidia mjane na watoto wake, mke anaweza kufikiria kwamba mume wake anavutiwa na mwanamke huyo, na si tendo la msaada. Kama mwanamke yeyote anampongeza mume wake, kwa kumwambia kwamba sura yake inapendeza au tabia yake ni njema, anamalizia kwa kusema kwamba yeye anavutiwa na mwanamke huyo. Kwa kuona unywele wa mwanamke ndani ya gari yake, mke anadhani yupo mwanamke mwingine katika maisha yake. Wanawake wa aina hii wenye fikira kama hizi na uthibitisho usio kamili, polepole kimakosa hupata uhakika kuhusu waume zao kutokuwa na uaminifu.

Huwaza kuhusu suala hili usiku na mchana. Pia huwaambia wengine, marafiki, na maaadui kuhusu suala hili; ambao kwa jina la huruma, wanaongezea nguvu shutuma zao na kuanza kuwaambia wanawake wahusika habari za wanaume wengine wasio waaminifu.

Ubishi na ugomvi huanza kutokeza. Mwanamke huanza kudharau mambo ya nyumbani na watoto na anaweza hata kwenda kwa wazazi wake.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 59

Atamfuatilia na kupekua mifuko yake. Atasoma barua zake na ataelezea kila jambo dogo kuwa ni kwa sababu ya yeye kutokuwa mwaminifu.

Kwa msimamo huu, atayafanya maisha ya familia kuwa magumu na kuigeuza nyumba kuwa jahanamu iwakayo moto na ambamo yeye pia atateseka. Kama mume wake angeleta uthibitisho wa yeye kutokuwa na hatia au kuapa kwamba hajafanya jambo lolote baya, au alie, bado hataridhika.

Msomaji bila shaka amekwisha waona wanawake wa aina hii, lakini inafaa kujua mifano ifuatayo:

"Mwanamke alisema kwenye mahakama: "msishangae kwa nini nimeamua kutengana na mume wangu baada ya maisha ya ndoa ya miaka kumi na mbili na watoto wadogo watatu. Sasa ninao uhakika kwamba mume wangu si mwaminifu kwangu. Siku chache zilizopita nilimwona anatembea mtaani na mwanamke wa kuvutia. Nikasoma gazeti la kila wiki lenye ukurasa wa utabiri wa nyota. Kila wiki, utabiri wa nyota ya mume wangu unasema kwamba angefurahia maisha na watu waliozaliwa mwezi wa juni. Mimi nimezaliwa mwezi wa Februari; Kwa hiyo mimi si mmojawapo wa watu waliotajwa kwenye utabiri. Zaidi ya hayo ninahisi mume wangu hanipendi kama alivyokuwa ananipenda zamani." Mume wa mwanamke huyu akasema: "Tafadhali niambie nifanye nini. Ningependa magazeti haya yangewafikiria wasomaji kama mke wangu, na hayangesema uwongo mwingi sana. Naomba kuaminiwa ninaposema kwamba huu utabiri wa nyota umeyafanya maisha yangu na yale ya watoto wangu kuharibika. Kama mojawapo ya utabiri huu unasema kwamba wiki hii nitapata kiasi kikubwa cha fedha halafu mke wangu huja kwangu na kuniuliza fedha nilizopata nimezifanyia nini? Au endapo utabiri wa nyota unasema kwamba ningepokea barua, basi Mwenyezi Mungu na anikoe! nadhani labda ni vizuri zaidi tutengane kwa sababu mke wangu hataki kukabiliana na ukweli."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 60

Mwanaume alisema mahakamani: “Ilikuwa mwezi uliopita nilipokuwa narudi kutoka kwenye karamu, mfanya kazi mwenzangu aliniomba nimpe lifti yeye na mke wake hadi nyumbani kwao. Siku moja mke wangu aliniomba nimnpeleke kwa wazazi wake. Wakati tupo njiani, mke wangu alipotazama nyumba ya gari akaona unywele wa mwanamke kwenye kiti cha nyuma. Akauliza unywele huo ulikuwa wa nani. Nilihangaika na sikuweza kumpa maelezo yanayo faa. Nilimfikisha nyumbani kwa wazazi wake na mimi nilikwenda kwenye kazi yangu. Nilipokwenda kumchukua usiku huo akakataa kuondoka na mimi. Nilimuuliza kwa nini? Aliniambia kwamba afadhali niendelee kuishi na mwenye huo unywele.”

Mwanamke mwenye umri mdogo alilalamika mahakamani na akasema: “mume wangu huchelewa kurudi nyumbani kila siku usiku kwa sababu ya kufanya kazi saa za ziada. Nina wasi wasi kuhusu hili na tuhuma yangu imeongezeka kwa sababu ya hayo yanayo semwa na majirani zetu. Wanasema kwamba mume wangu anadanganya na hafanyi kazi usiku na kwamba huenda kwenye starehe zake. Matokeo yake ni kwamba sipo tayari kuishi na mwongo.”

Katika nukta hii, mume alichukua barua chache kutoka mfukoni mwake na akaziweka kwenye kaunta mbele ya jaji na akamwomba azisome ili athibitishe kwamba yeye hana hatia na kumsitisha mkewe asiendelee na msimamo usiofaa.

“Jaji alianza kusoma barua kwa sauti. Mojawapo ya barua hizo ilionesha kwamba yeye hufanya kazi saa za ziada kuanzia saa 10 hadi 2 usiku. Barua nyingine pia zilihusiana na kazi yake ambapo aliombwa kuhudhuria semina fulani.

Mke wake alikuja mbele na baada ya kuona barua hizo alisema; “Nilikuwa nikipekua mifuko yake lakini zikuziona barua hizi.”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 61

Jaji alisema; “Inawezekana aliziacha ofisini kwake.”

Mume akasema: “Tuhuma ya mke wangu kwangu imekuwa kubwa mno hivyo kwamba ninamtuhumu yeye. Kila siku usiku ninapatwa na majinamizi, ninadhani kwamba mke wangu anaye bwana mwingine na anataka tutengane ili akaolewe na bwana huyo.”

Kufikia hapo, mke alimkimbilia mume wake kwa haraka huku analia kwa furaha, alimwomba msamaha na wote wakaondoka mahakamani.

Mtaalamu wa meno alilalamika mahakamani na kusema: “Mke wangu ana wivu kupita kiasi. Mimi ni mtaalamu wa tiba ya meno na wapo wagonjwa wanawake ambao huja ofisini kwangu kwa ajili ya matibabu. Hali hii imeamsha wivu wa mke wangu na kila siku tunabishana kuhusu jambo hili. Mke wangu anaamini kwamba nisingewatibu wagonjwa wanawake. Lakini haiwezekani mimi nipoteze wateja wangu na yeye ananipenda mimi, lakini matumani yake yasio na maana yanaharibu maisha yetu. Siku chache zilizopita alikuja kwenye chumba changu cha upasuaji na akanilazimisha tuondoke. Tulikwenda na tukagombana. Aliniambia: ‘Nilikwenda kwenye chumba chako cha upasuaji na nikaketi karibu na msichana mdogo kwenye chumba cha wanaosubiri. Mimi na msichana huyu tukazungumza kuhusu wewe bila kujua kwamba mimi ni mke wake, alisema; Huyu bwana mganga wa meno ana sura nzuri na anatabia njema.” ’

Mganga wa meno aliendelea kusema: “Kwa sababu ya maoni ya msichana, mke wangu aliniburuza nje ya sehemu yangu ya kazi kwa njia ya kunivunjia heshima.”

Mwanamke alilalamika mahakamani na alisema: “Mmojawapo wa marafiki zangu aliniambia kwamba mume wangu huenda kwenye nyumba ya wageni wanawake. Siku moja nilimfuata na kugundua kwamba ilikuwa

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 62

kweli. Sasa nataka mahakama imwadhibu." Mume katika kukubali yale yaliyosemwa na mke wake, aliiambia mahakama: "Siku moja nilikwenda kwenye duka la dawa kununua dawa. Nilimuona mwanamke humo kwenye duka la madawa ananunua maziwa ya unga. hakuwa na fedha ya kutosha kununua maziwa, kwa hiyo nikajitolea kumsaidia. Baadaye nilitambua kwamba ni mjane ambaye alikuwa masikini. Kwa hiyo niliamua kuendeleza msaada wangu." Majaji walitambua ukweli baada ya kuchunguza jambo hili na wakawasuluhisha wanandoa."

Matukio kama haya hutokea kwenye familia nyingi. Hali ya familia hubadilika na huwa na mazingira ya kutazamia taabu tuhuma na uadui. Watoto watapata mateso na athari za kisaikolojia ni mbaya sana.

Kama wanandoa wanaendelea katika hali hii, basi wote watateseka na wakioneshana kiburi, hakika wataelekea kutalikiana. Inapotokea kutalikiana, wote wawili mume na mke watahasarika, kwa sababu kwa upande moja mume hatawaza kupata mke mwingine ambaye atakuwa bora zaidi kuliko wa kwanza. Kwa upande mwingine, watoto watateseka na hawatafurahia maisha mazuri. Watoto wanaweza hata kupata matatizo mapya kwa sababu ya baba wa kambo au mama wa kambo.

Mwanamume anaweza kudhani kwamba kwa kumtaliki mke wake, anaweza akamuoa mke, 'bora' ambaye ataishi naye kwa amani. Lakini hii ni ndoto tu na kuitambua ni vigumu sana. Kwa kumtaliki mke wake, anaweza akakutana na matatizo mapya kutoka kwa mke mpya.

Kutalikiana si njia ya kuielekea kwenye faraja na furaha kwa mwanamke. Licha ya kwamba anaweza kuhisi kwamba amelipiza kisasi, kuolewa tena haitakuwa rahisi kwake. Anaweza kuishi peke yake katika maisha yake yote na labda hatafurahia hata kuwa nao watoto wake. Hata kama ataolewa tena, hakuna uhakika kwamba mume wake mpya atakubaliana na

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:23 PM Page 63

matarajio yake. Anaweza hata akajikuta analea watoto wa mume wa mke aliyefariki. kwa hiyo wala si talaka ama ubishi na ugomvi vinaweza kuwaokoa wanandoa. Lakini ipo njia inayoweza kuwakomboa.

Msimamo mzuri kushinda yote ni kwamba mwanamume na mke wake wanaacha kubishana na kujaribu kuwa na mantiki. Wanamume wanayo wajibu mkubwa zaidi katika jambo hili na kwa kweli ufunguo wa suluhu upo mikononi mwao. Kwa kufuatia uvumilivu na usamehevu, wanaume wanaweza kujiokoa kutoka kwenye matatizo na pia kusaidia kuondoa kabisa dalili za tuhuma kwa wake zao.

Sasa maneno machache kwa wanaume:

Kwanza, mpendwa bwana! Lazima ukumbuke kwamba mkeo hata kama anakutuhumu, anakupenda. Anavutiwa sana na watoto wako na nyumba yenye familia. Anaogopa kutengana. Kwa hakika atateseka kwa sababu ya hali yako ya maisha ya kusikitisha. Kama angekuwa hakupendi, hangekuonea wivu. Kwa hiyo mkeo hapendezwi na hali ya sasa, lakini atafanya nini endapo yeye ni mgonjwa? Wagonjwa wengine wanayo maradhi ya baridi yabisi na wengine wanaugua saratani. Mke wako anaumwa maradhi ya kuvurugikiwa na akili na kama huamini, basi mpeleke kwa mtaalamu wa maradhi ya akili. Unatakiwa kuwa na huruma na mpole. Usimkasirikie au kubishana na mkeo. Hapana mtu anayeweza kugombana na mtu mgonjwa. Usiwe mkali kwa ajili ya matendo yake yasio na adabu au madai. Usiishie kupigana naye. Usimpeleke kwenye mahakama yoyote. Usimdharau. Usizungumze habari ya talaka au kutengana. Baina ya matendo haya, hakuna mojawapo linaweza kutibu maradhi yake, kwa kweli maradhi hayo yanaweza kuwa mabaya zaidi. Kutokuwa mwema kwake inaweza kuwa chanzo cha tuhuma yake.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 64

Lazima uwe mwema kwa mkeo kadiri iwezekanavyo. Unaweza kumkasirikia mkeo sana kwa sababu ya msimamo wake, lakini hakuna njia nyingine yoyote. Lazima umtendee kwa namna hivyo kwamba anakuwa na uhakika wa wewe kutokuwa na hatia.

Pili, unatakiwa kujaribu kutengeneza uelewano baina yenu. Usimfiche kitu chochote. Mruhusu asome barua zako hata kabla wewe hujasoma. Usifiche funguo za meza yako ya faragha au sefu, Mruhusu apekue mabegi na mifuko yako. Mruhusu akufuatilie. Usioneshe kutokufurahishwa na mambo yaliyotajwa hapo juu, lakini yafikirie kama utaratibu wa kawaida katika maisha ya familia iliyo imara na kuelewana.

Baada ya kazi, kama hauna shughuli nyingine, rudi nyumbani haraka iwezekanavyo. kama jambo la haraka linajitokeza ambalo linahitaji kushughulukiwa, basi mwambie mkeo na mjulishe unakokwenda na wakati ambao atakutarajia kurudi nyumbani. Halafu jaribu kurudi muda huo. Endapo unachelewa kurudi nyumbani, basi haraka mwambioe mkeo sababu ya kukucheleweshe. Uwe mwangalifu, usidanganye, vinginevyo ataanza kukutuhumu. Omba ushauri wake kuhusu mambo yako. Usimfiche kitu chochote. Mpe uhuru wa kukuuliza kuhusu suala lolote lisiloeleweka na kumtatiza yeye.

Tatu, wewe unaweza kuwa huna hatia ya jambo ambalo anakutuhumu, lakini pia tuhuma za wanawake zilizo nyingi si kwamba hazina uthibitisho. Labda, kwa kutokuwa mwangalifu umefanya jambo ambalo limemwathiri kiakili na kumfanya akutuhumu. Lazima utafakari kwa uangalifu kuhusu matendo yako ya nyuma. Inawezekana ukatambua sababu ya tuhuma yake. Kwa njia hii unaweza kutatua tatizo vizuri zaidi. Mathalani, kama wewe unataniana sana na wanawake wengine, jaribu kusitisha tabia hiyo kabisa.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 65

Kuna umuhimu gani wewe kusifiwa kuwa unayo sura nzuri na tabia njema kwa hasara ya kutuhumiwa na mkeo na kutokukuamini? Kwa nini uchokoze tuhuma ya mke wako kwa kutaniana na katibu muhtasi wako au mfanyakazi mwenzako mwanamke? Kwa nini umwajiri mwanamke? Usitaniane na wanawake wengine, kwenye karamu.

Kama unataka kumsaidia mwanamke mjane, kwa nini usimjulieshe mke wako? Unaweza hata kumsaidia mjane kupitia kwa mke wako. Usijifikirie kwamba wewe ni mtumwa, au mtu aliyefungwa minyororo. Hutakiwi kuwa mtumwa, lakini mwanamume mwenye busara baada ya kufanya mkataba na mke wake, ana mtunza. Unatakiwa umsaidie aondokane na tatizo hili. Kwa uvumilivu na busara, unatakiwa uondoe hatari zinazo tishia msingi wa maisha safi ya familia yenu. Hapo utakuwa umetibu maradhi ya mke wako na kuwaokoa watoto wenu kutoka kwenye huzuni. Utakuwa umetoa huduma kubwa kwako kiakili na kimwili. Zaidi ya haya, Mwenyezi Mungu huwapa thawabu wanamume ambao wapo tayari kujitoa mhanga kwa nyakati muhimu kama hizi.

Imamu Ali (a.s) alisema: “Kila wakati wafanyieni wanawake wastani katika mambo yenu. Semeni nao kwa wema ili matendo yao yawe mazuri”

Imamu Sajjad (a.s) alisema: “Mojawapo ya haki za mwanamke kwa mume wake ni kwamba mume anatakiwa kusamehe ujinga na upumbavu wa mkewe (na kinyme chake).”

Mtume wa Mwenyezi Mungu(s.a.w.w) alisema: “Mwanamume yeyote anayeweza kuvumilia upungufu wa mkewe, kwa uvumilivu wake (kwa mke wake) wa kila mara, Mwenyezi Mungu Mweza wa yote, atampa thawabu za uvumilivu wa Hadhrat Ayub (a.s)”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 66

Sasa wanawake wanakumbushwa kuhusu mambo machache:

Kwanza: Mpendwa Bibi! Suala la mume wako kutokuwa mwaminifu, kama masuala mengine yoyote, linahitaji kuthibitishwa. Almuradi hajathibutishwa kuwa anahatia, huna haki ya kumtia hatiani. Wala si sheria ama dhamira ya mtu humruhusu mtu kumshtaki mtu kwa sababu ya welekeo wa uhalifu kufanyika. Wewe hungehisi uchungu kama mtu angekushtaki kuhusu kitu fulani bila ya uthibitisho wowote? Inawezekana kufikiria nadharia zako za kipumbavu na zisizo na msingi kama ndio uthibitisho wa uhalifu mkubwa kama zinaa?

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱجْتَنِبُواْ كَثِيرًا مِّنَ ٱلظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ ٱلظَّنِّ إِثْمٌ ﴿١٢﴾ ﴾

“Enyi mlioamini! Jiepusheni sana na dhana, kwani baadhi ya dhana ni dhambi…” (49:12).

Imam Sadiq (a.s) alisema: “Uzito wa kumshitaki mtu asiye na hatia kwa kumsingizia ni mzito zaidi ya milima mirefu.”

Mtume (s.a.w) wa Mwenyezi Mungu alisema: “Mtu yeyote anayemshitaki muumini kwa kumsingizia, Mwenyezi Mungu, siku ya Ufufuo atamweka kwenye lundo la moto ili apate adhabu anayostahili.”

Mpendwa Bibi! Usiwe mpumbavu na usifanye haraka kuamua mambo. Unapokuwa na wakati, keti na andika uthibitisho wote na hoja kuhusu mumeo kuvunja uaminifu kwako. Halafu mbele ya kila jambo, andika vipengele vingine kwenye tatizo hilo na uwezekano wa mambo hayo kujitokeza tena. Kitakachofuata, jiweke wewe katika nafsi ya jaji na utafakari kwa undani sana kuhusu mambo yaliyoandikwa. Kama hazikushawishi kwamba ana hatia, basi ama unaweza kusahau jambo hilo au ufanye uchunguzi zaidi.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 67

Mathalani kuwepo kwa unywele wa mwanamke kwenye gari ya mume wako ni jambo ambalo linaweza kuelezeka kwa urahisi kwa mojawapo ya haya yafuatayo:
Unywele huo unaweza kuwa ni wa mmojawapo wa ndugu za mumeo kama vile dada yake, mama yake, changazi yake au watoto wao.

Unywele huo unaweza kuwa ni wako.

Inawezekana alimpa lifti rafiki au ndugu yake akiwa na mke wake na unywele huo ukawa ni wake.

Inawezekana alimpa lifti mwanamke ambaye alikuwa hajiwezi.

Inawezekana mmojawapo wa maadui zake ameangusha unywele huo kwenye gari lake kwa makusudi ili kukufanya wewe uwe na wasiwasi na mumeo.

Inawezekana aliyempa lifti ni mmojawapo wa wafanyakazi wanawake kwenye gari lake.

Pia uwezekano upo kwamba alitoka nje kimatembezi na hawara yake. Lakini mfano huo upo mbali mno kuliko ile iliyo tangulia kwa hiyo si wa kuzingatiwa sana. Si lazima mtu aufikirie kama ushahidi madhubuti wa kumtia mtu hatiani wakati ambapo anasahau uwezekano mwingine katika orodha hiyo hapo juu.

Kama mumeo anachelewa anarudi nyumbani, inawezekana alikuwa anafanya kazi za ziada; au labda alikuwa nyumbani kwa rafiki yake; au alikuwa anahudhuria semina au mkutano wa kidini; au inawezekana alitembea kwa miguu kurudi nyumbani.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 68

Kama mwanamke anamuona mumeo kuwa ana sura ya kuvutia, hilo si kosa la mumeo. Kuwa na tabia njema si uthibitiosho wa kuwa na hatia! Je, ungependa mumeo kuwa mtu mkali na kukimbiwa na kila mtu?

Kama mume wako anamhudumia mjane na watoto wake, mfikirie kuwa ni mtu mwenye kupenda kusaidia ambaye anafanya hili kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Kama mume wako anayo meza ya faragha au sefu nyumbani; na kama hakuruhusu kusoma barua zake usimfikirie kuwa anaye kimada. Kwa kawaida wanamume wanayo tabia ya usiri na wastani. Hawapendi watu wengine wajue mambo yao, labda wanayo mambo ya siri yahusuyo kazi zao. Labda hakuona wewe kama mtu unayeweza kuweka siri. Kwa vyovyote vile, uwezekano ni huo tu na usifikirie kuwa uthibitisho madhubuti.

Pili: Wakati wowote unapodhania jambo lolote ni lazima ulizungumze na mume wako kwa namna ambayo utapata ukweli wa jambo lenyewe, na si kwa njia ya ugomvi. Uwe muwazi kwake na muombe akueleze kuhusu suala la dhana yako ili usafishe moyo wako na utulie katika amani. Halafu msikilize kwa uangalifu. Tafakari kuhusu maelezo yake. Kama unaridhika nayo basi jambo hilo liishe. Lakini kama bado una wasi wasi, basi chunguza jambo hilo wewe mwenyewe hadi ukweli ujulikane. Kama wakati wa kupeleleza unapata kipengele ambacho mumeo alidanganya, basi usikifikirie kama ndio uthibitisho wa kuwa na hatia. Hii ni kwa sababu licha ya kuwa hana hatia, inawezekana kwa makusudi alikuwa hasemi kweli ili usije ukawa na wasi wasi zaidi. Tena ni bora zaidi kumwendea na kumhoji kwa nini hakusema kweli yote. Kama mambo yalivyo, si vema mtu kudanganya, lakini mumeo alifanya kosa hili, basi wewe usifanye upumbavu. Muulize kwa ushupavu akwambie ukweli. Kushindwa kwake kukueleza kuhusu suala la tuhuma yako si dalili ya yeye

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 69

kuwa na hatia. Inawezekana kwamba kwa hakika anaweza kusahau jambo au anaweza kuwa amehangaika. Wakati huu, usiendelee kufuatilia jambo hili tena na liache hadi wakati mwingine unaofaa. Akikwambia kwamba amesahau kitu fulani, kubali. Hata hivyo, kama bado unayo mashaka, fanya upelelezi kupitia njia nyingine.

Tatu: Usimwambie kila mtu unayemuona dhana yako kwa mumeo, kwani wanaweza kuwa maadui zako. Maadui mara nyingi huthibitisha madai yako na wanaweza hata kuongeza uwongo juu yako ili waharibu maisha yako. Wanaweza kuwa si maadui, lakini kundi la watu wapumbavu wenye kuvutiwa kiakili kwa rahisi na watu wasiokuwa na uzoefu ambao wataimarisha madai yako kwa namna ya kukuhurumia. Watu hawa wanaweza kuwa ni ndugu zako au marafiki zako wa karibu. Ushauri unaofaa unatakiwa kutolewa na watu wenye busara, werevu na wenye huruma halisi. kama unataka kupata ushauri, basi waendee watu wanao stahiki na uwazungumzie jambo hili.

Nne: Kama ushahidi wa hatia ya mume wako si madhubuti; kama marafiki zako na ndugu zako wanadhani kwamba ushahidi huo hautoshi, endapo mume wako anajihisi kwamba hana hatia na hatimaye kama bado unamtuhumu, basi uwe na uhakika wewe unayo maradhi. Maradhi hayo ni kuvurugika kwa akili ambamo dalili za tuhuma zimeongezeka na kushindwa kuzidhibiti. Ni muhimu uende umuone mtaalamu wa magonjwa ya akili ambaye atakutibu ipasavyo.

Tano: Kwa hiyo, si busara wewe kubishana na mume wako au kupeleka malalamiko mahakamani. Usizungumze kuhusu talaka na usimshushe hadhi yake. Msimamo wa aina hiyo unaweza tu kuongeza hasira zaidi na ugomvi ambao unaweza kusababisha kuachana. Uwe mwangalifu usifanye mambo kipumbavu au kuamua kujiua. Kujiua mwenyewe si tu kwamba utapoteza maisha, lakini pia utaadhibiwa huko akhera.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 70

Je, si jambo la kusikitisha kupoteza maisha yako kwa sababu ya fikra isiyo na msingi? Je, si vema kutatua matatizo yako kwa uvumilivu na busara?

Sita: Kama bado unamdhania mume wako au una hitimisha kwamba kwa hakika anaye mpenzi nje ya ndoa, bado wewe unalaumiwa, kwa sababu hujajaribu vya kutosha kuvuta moyo wake. Unaweka ufa katika maisha yake ambapo wanawake wengine wanaweza kuona ni mahali pa wazi na wakakaa hapo. Lakini, usikate tamaa; bado muda upo. Angalia upya msimamo wako na fanya mambo yako kwa namna ya kumvuta mume kwako.

Usisikileze mazungumzo ya uwongo

Mojawapo ya tabia hasi ya watu wengine ni kuwasema wengine kwa ubaya. Tabia hii si tu ni mbaya kwa jinsi ilivyo, lakini pia ni chanzo cha fitina. Husababisha dhana, kukosa rajua (kushutumu kila kitu), kutotangamana na migongano miongoni mwa watu. Huharibu mazingira ya kirafiki na kupanda mbegu ya kutokuelewana miongoni mwa familia. Huwatenganisha wanamume kutoka kwa wake zao na inaweza kusababisha mauaji.

Kwa bahati mbaya tabia hii imeenea miongoni mwa watu hivyo kwamba haionekani kuwa ni mbaya tena. Kwenye mkutano utawaona watu wanateta na kusengenya. Hususan kwenye mkutano wa wanawake, ishara za kuteta huwa zimejazana. Wanawake wawili wakikutana, huanza kuteta. Wanawasengenya wenzao kama vile ni mashindano. Wakati mwingine huwasema waume zao. Mathalani wanawasema jinsi waonekanavyo au kazi zao, na kuona dosari za mume wa nwanamke mwingine. Mwanamke mmoja anaweza kumlaumu mwenzake kwa kuolewa na makenika au fundi viatu. Kama mume ni dereva atasema; “Mumeo kila mara yupo safarini, unawezaje kuvumilia hali hiyo? Kama mume anauza nyama, atasema mumeo kila mara hunuka mafuta.”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 71

Kama mume hana kipato cha kutosha, atasema; "Unaishi vipi kwa fedha ndogo kiasi hicho? Kwanini uliolewa naye? Si inasikitisha kwamba wewe na uzuri wote huo umeolewa na mtu mfupi na dhalili kama huyo? Wazazi wako walikuruhusu vipi kufanya hivi? Walichoka kuishi na wewe? Ungeweza kuolewa na mwanamume yeyote ambaye ungemtaka. Kwa nini ulimchagua mwanammume huyu? Hakupeleki mahali popote, hakupeleki sinema, popote.

Pamoja na hayo mumeo ni mtu mwenye uso wa kuotisha. Unawezaje kuishi naye? Ni vipi wewe, na elimu yako, ulikubali kuolewa na mkulima?"

Mazungumzo ya aina hii yanaweza kusikika katika asiliamia kubwa miongoni mwa vichimbakazi wa kike katika jamii yoyote. Wanawake wenye mazoea ya namna ya kuzungumza, kwa kweli, hawafikirii kuhusu matokeo mabaya sana yanayofuata baadaye. Hawafikiri kwamba kuteta kwao na kutafuta na kuona makosa ya watu ni tabia inayoweza kusababisha kuvunjika kwa ndoa au hata mauaji.

Wanawake wa aina hii kwa kweli ni mashetani katika umbo la binadamu. Wao ni maadui wa familia. Hutengeneza migongano miongoni mwa familia na kuzibadili nyumba zao kuwa gereza la chini ya ardhi lenye giza na kutisha. Mtu anaweza kufanya nini? Hii ni sehemu ya jamii zetu. Licha ya kwamba Uislamu umetukataza kabisa kufanya vitendo kama hivi, hatupo tayari kuacha.

Mtume (s.a.w.w) alisema: "Enyi watu mnaodai kuwa ni Waislamu, lakini mlishindwa kuiruhusu imani iingie kwenye nyoyo zenu, msiwaseme Waislamu kwa ubaya na msitafute dosari zao. Yeyote anayetafuta mapungufu ya watu, basi Mwenyezi Mungu Mweza wa yote atakuwa anafanya kama anavyofanya mtu huyo kwa wengine; na katika hali ile watafedheheshwa miongoni mwa watu, licha ya kuwa watakuwa majumbani mwao."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 72

Wanawake wenye tabia mbovu wanaweza kuwa wanafuatilia lengo moja au mengi. Wanateta kwa ajili ya kulipiza kisasi ili wavunje familia. Wanaweza wakafanya hivyo kwa sababu ya husuda au kujifaharisha wenyewe. Pengine walitaka kuficha upungufu wao wenyewe au kuwadanganya wanawake walio wepesi kudanganywa. Wanaweza kujifanya kuwa wanahuruma. Wakati mwingine wanateta kwa sababu ya kujifurahisha na hawafuatilii lengo lolote zaidi ya kuridhisha matamanio yao ya kuchukiza. Lakini mtu anachoweza kuwa na uhakika nacho ni kwamba matendo ya aina hii hayafanywi kwa lengo la kuwasaidia wengine na kwamba matendo kama haya yanaweza kusababisha athari za maangamizi.

Wasomaji kwa hakika wamekutana na matuko fulani ambayo yametokea kutokana na utesi. Ufuatao ni mfano wa matukio hayo:
"Mwanamke alisema mahakamani: "Bwana… alikuwa na tabia ya kumteta mume wangu kwa lengo la kusababisha ugomvi baina yangu na mume wangu. Alikuwa akiniambia kwamba mume wangu hakuwa mtu mzuri vya kutosha na kwamba hakunielewa mimi au sikuwa na mshtuko wowote. Kila mara alitaka mimi nipewe talaka na niolewe na yeye…. matokeo ya ushauri wake wa udanganyifu nilipotoshwa na siku moja mimi na yeye tulimuua mume wangu."

Bibi mpendwa! Sasa umetambua nia mbaya zilizojificha kwenye usengenyaji na kama unampenda mume na watoto wako, basi usije ukavutiwa na ndimi za mashetani yenye umbo la binadamu. Usikubali urafiki wao wa udanganyifu. Hakikisha wao si marafiki zako, ila ni maadui zako ambao wanataka kukuona wewe unatengana na familia yako. Usiwe mwepesi kudanganywa na usiwaamini.

Jaribu kupata malengo yao maovu kwa kutumia akili. Waambie waache haraka sana wanapoanza kumshutumu mume wako. Usione aibu kuwaambia: "kama mnataka muwe marafiki, basi acheni kuzungumza

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 73

habari zinazohusu mume wangu. Si haki yenu nyinyi kumshutumu mume wangu. Ninampenda na hana dosari yoyote."

Mara watakapo tambua kwamba unampenda mume wako na watoto wako kwa kutumia uimara wa ulimi wako, basi wanaweza wakatahayari kwa kukupotosha na hutasumbuliwa tena. Usidhani kwamba watakasirika, au kwamba utapoteza marafiki zako. Kama wao ni marafiki zako wa kweli, basi hawatakudhuru na sana watakushukuru. Kama ni maadui zako, basi, ni kipi kizuri zaidi cha kufanya kama sio kuwaepuka. Kama ukikutana na wale ambao wanang'ang'ania matendo yao maovu, vunja uhusiano wako nao.

KUMRIDHISHA MUME WAKO NA SI MAMA YAKO

Msichana anapokuwa nyumbani kwa wazazi wake anawajibika kuwaridhisha. hata hivyo, mara aolewapo, wajibu wake hubadilika.

Anapokuwa nyumbani kwa mume wake, mwanamke lazima ayapatie kipaumbele mahitaji ya mume wake. Hata hapo ambapo matakwa ya mume wake na wazazi wake yanatofautiana lazima amtii mume wake, hata kama wazazi wake hawakuridhika. Kutomtii mume ni kitendo ambacho kinaweza kuharibu uhusiano wa ndoa ya mtu, na kinyume chake. Aidha, kinamama wengi hawafaidi ilmu sahihi na busara.

Mama wengine, hawajatambua kwamba wanatakiwa kuwaacha mabinti zao wafikie maelewano na wanaume zao wenyewe. Wanandoa lazima waachwe wapange mambo yao wenyewe na kama wakipata tatizo lolote walitatue wao kwa kutumia uwezo wao.

Kwa kuwa mama wa wake hawajui jambo hili, basi wao katika akili zao hujaribu kumfanya mkwe wao afuate wanavyotaka wao. Hujaribu kufanya

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 74

hivyo moja kwa moja au kwa kuzunguka, kuingilia mambo yao ya familia. Wanawatumia mabinti zao ambao hawajapata uzoefu na hawafahamu vizuri hali yao, kwa lengo la kumvuta mkwe wao. Mama wakwe huwaambia mabinti zao kila wakati jinsi ya kutekeleza nini cha kufanya, kusema na asichotakiwa kusema. Binti ambaye anamuona mama yake kama mwenye huruma na mwenye uzoefu anamtii na anajiingiza mwenyewe kwenye matamanio ya mama yake pia.

Kutakuwa hakuna matatizo yoyote kama mume atakubali matakwa ya mama mkwe wake. Hata hivyo, akionesha kukataa, basi ugomvi huanza kutokea. Kwa sababu ya ujinga wa mama mkwe anaweza kuwa jeuri ambayo inaweza kuharibu familia mabinti yake. Mama mjinga, badala ya kumpa matumaini binti yake kujitolea maisha yake kwa mume wake, anamfanya ampinge mume wake. Mama anaweza kumwabia binti yake: "Umeharibu maisha yako. Mume gani mbaya hivi! Wanaume wazuri kiasi gani walikuwa tayari kukuoa! maisha mazuri yalioje anayoishi binamu yako! Bahati iliyoje ya dada yako! ni nini walicho nacho ambacho nyinyi hamnacho! Kwa nini uendeshe maisha ya namna hii? Binti yangu masikini!"

Mama ambaye maneno yake yanafikiriwa kama yenye huruma, husababisha ugomvi na ubishi baina ya binti yake na mume wake. Binti anawekwa katika hali ya kuanzisha ugomvi na mume wake. Wazazi wake binti watakuwa upande wake ili hatimaye washinde ugomvi, huonesha kuwa wako tayari mtoto wao apewe talaka.

"Mwanamke wa miaka thelathini alimshambulia mama yake mwenye umri wa miaka hamsini kwa sababu alisababisha kuvunjika kwa ndoa yake. Mwanamke alisema; 'mama yangu alimsengenya mume wangu sana hivyo kwamba alisababisha mabishano mengi sana kati yangu na yeye. Hatimaye nikaachika lakini nilijuta baada ya muda mfupi. Lakini nilichelewa sana

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 75

kwa sababu saa sita baada ya kutalikiana aliyekuwa mume wangu akamchumbia binamu yangu. Nilikasirika sana hivyo kamba niliamua kumpiga mama yangu.' "

"Mwanaume wa miaka thelathini na tisa alimkimbia mke wake na mama mkwe wake na akajiua, aliacha barua isemayo; 'Kwa sababu ya msimamo wa mke wangu na kwa sababu hakuwa tayari kwenda Abdan na mimi, niliamua kuiaga dunia hii. Mke wangu na mama yake wanahusika na kifo changu.' Hivyo mwanaume ambaye alichoshwa na uingiliaji wa mama mkwe wake, alijiua."

Mwanamume ambaye alikuwa amechoshwa na uingiliaji wa mama mkwe wake, alimtupa nje ya teksi.

Bila shaka, mabinti ambao huwatii mama wa aina hii na kukubali matakwa yao, wanaweza kusababisha pigo lisiloweza kurudishwa kwao.

Kwa hiyo, mwanamke yeyote ambaye anajali familia yake, asivutiwe na matakwa ya mama yake na lazima asiyafikirie kwamba matakwa hayo ni sahihi asili mia kwa mia.

Mwanamke mwenye busara na mwerevu kila mara atapima ushauri na usemi wa mama yake kabla ya kutekeleza katika maisha ya familia yake. Anaweza kuyatekeleza kama hayakupingana au kuhatarisha mkataba wa familia yake. Kwa vyovyote vile binti atalazimika kukubali matakwa ya mama yake. Vinginevyo, kama binti akifikia hitimisho kwamba mama yake si mjuzi, na ushauri wake unaweza kusababisha ugomvi na mabishano, basi anaweza kuukataa ushauri wake.

Kwa vyovyote vile, upo uchaguzi wa aina mbili kwa binti:
Kuendelea kutekeleza matakwa ya mama yake na katika hali hiyo,

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 76

kitakacho fuatilia ni mabishano ya kifamilia; au Ampuuze mama yake na kukubali kutekeleza matakwa ya mume wake.

Ni wazi kwamba, mtu hatachagua mfano wa (a) kwa sababu kama akichagua, basi ama itamlazimu aishi maisha ya kuteseka na mume wake au amtaliki. Kama ikitokea wakiachana labda mwanamke atakwenda kuishi na wazazi wake. Kwa vyovyote vile hawatamkubali kuwa kama mmoja wao wa familia na watajaribu kumfukuza. Atashushwa hadhi mbele ya watu wengine wa familia. Pia si rahisi kuishi peke yake. Pia haitakuwa rahisi kuolewa kwa mara nyingine. Anawezaje kuwa na uhakika kwamba ndoa nyingine itakuwa nzuri kuliko ya kwanza? Vipi watoto? Vipi watoto wa mume wa ndoa nyingine?

Anaweza kukata tamaa sana hivyo kwamba anaweza akajiua. Anaweza akawa mwanamke ambaye hatoweza kuishi naye hivyo kwamba mwanamume mwingine anaweza kumkimbia au hata kujiua.
Mara mwanamke akitafakari matokeo ya kuendekeza matakwa ya ubinafsi na ya yasio na maana ya mama yake au watu wengine, basi lazima afanye uamuzi thabiti wa kudharau mazungumzo yote ili asihatarishe uhusiano wake na mume wake.

Angeweza akamwambia mama yake kwa hekima na adabu: “Sasa mimi nimeolewa, ni vema zaidi mimi nikijaribu kuilinda ndoa yangu na kumridhisha mume wangu. Ningependa kuwa mwema kwake, kwa sababu ni mwenzangu. Anaweza kunifurahisha na anaweza kunisaidia. Mazuri na mabaya ya maisha yanatupata tukiwa wote. Yeye ni chaguo langu na kama tukipata matatizo yoyote tutajaribu kuyatatua sisi wenyewe. Tunaweza kupanga sisi wenyewe, bila ya kupuuza ushauri wako mzuri mama. Kuingilia sana kwenye mambo yetu, inaweza kuwa sababu ya kuongeza ubaya juu ya hali mbaya ikawa mabaya zaidi.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 77

"Kama unataka sisi kuwa na uhusiano mzuri na wewe, basi usiyaingilie maisha yetu, usimseme kwa ubaya mume wangu. (Mama naomba unielewe hivyo) vinginevyo nitalazimika kusitisha uhusiano wangu na wewe."

Kama mama, yako kutokana na ushauri wako, anaacha kuingilia familia yenu, basi hutasumbuliwa tena. Hata hivyo, kama mama yako hayupo tayari kutilia maanani matakwa yako, punguza kumtembelea, na usiache kumshawishi mara chache hizo utakazomtembelea mpaka auone ukweli wa mambo.

Ambapo kutokana na wewe kuvunja uhusianao na wazazi wako, unaweza kupoteza kiasi fulani cha heshima yako miongoni mwa watu wa familia yako. Hivyo uwe na busara na hekima katika kumshauri mama yako, usiwe fedhuli kwake.

Mtume (s.a.w.w) alisema: "Mwanamke mzuri zaidi miongoni mwa wanawake ni yule anayezaa watoto wengi, ana upendo na safi; ambaye hakubali kutekeleza matakwa ya ndugu zake lakini mtiifu kwa ajili ya mume wake tu na hujilinda mbele ya wageni, humsikiliza mume wake na kumtii, hutimiza matamanio yake ya faragha na hapotezi staha yake kwa namna yoyote ile."

Mtume (s.a.w.w) aliongeza: "Mwanamke mbaya zaidi miongoni mwa wanawake ni yule anaye watii ndugu zake lakini hakubali kutekeleza matakwa ya mume wake, mgumba na asiye samehe, haogopi kufanya matendo maovu, hujiremba wakati mume wake hayupo, hatimizi matakwa ya mume wake katika faragha, mume wake akimwomba msamaha hataki kumsamehe makosa yake."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 78

UWE SAFI NA MREMBO NYUMBANI PIA

Ni desturi ya wanawake wengi kwamba huvaa nguo zao nzuri na kujipamba sana, wakati wanapokwenda kwenye hafla au mikutanoni. Hata hivyo, wanaporudi nyumbani wanavua hayo mavazi mazuri na kuvaa nguo za zamani na chakavu. Wanawake hawa hawako makini na usafi nyumbani na hawajipambi. Wanapokuwa nyumbani nywele zao zinakuwa timtim, nguo zenye madoa na soksi zilizotoboka. Kwa kweli hali inatakiwa ibadilishwe kabisa kwa kiasi kikubwa kabisa, kwamba mwanamke anatakiwa ajipambe akiwa nyumbani na awe mchangamfu kwa mume wake ili aweze kuvutia moyo wake na ili asiache ufa wowote ambao unaweza kujazwa na wanawake wengine. Kwa nini mwanamke aoneshe uzuri wake kwa watu wengine? Hivi inastahiki mwanamke kuonesha uzuri wake kwa wanaume wengine na kusababisha matatizo kwa vijana?

Mtume (s.a.w.w) wa Uislamu alisema: “Mwanamke yeyote anayejipaka manukato na kuondoka nyumbani hawezi kupata neema za Mwenyezi Mungu Mweza wa yote hadi anaporudi nyumbani.”

Mtume (s.a.w.w) pia alisema: “Mwanamke bora zaidi miongoni mwa wanawake ni yule ambaye ni mtiifu kwa mume wake, hujiremba kwa ajili ya mume wake lakini haoneshi urembo wake kwa wageni na mwanamke mbaya kuliko wote miongoni mwa wanawake wenu ni yule anayejipamba wakati mumewe hayupo.”

Bibi mpendwa! kuuteka moyo wa mwanaume hususan kwa muda mrefu si rahisi, Usifikirie hivi kwamba: “Ananipenda, hivyo Sihitaji kuonekana mrembo kwake au kujaribu kushinda moyo wake au kumshawishi.” Lazima udumishe mapenzi yako kwake kila siku. Uhakikishe mume wako atafurahi kuwa na mke safi na mrembo hata kama hawezi kutamka. Kama ukishindwa kuridhisha matamanio ya moyo wake na huvai nguo za

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 79

kuvutia unapokuwa nyumbani, anaweza akawaona wanawake wazuri wenye kuvutia nje ya nyumba. Anaweza akakatishwa tamaa na wewe na anaweza kuelekeza mapenzi yake nje ya njia iliyo nyooka. Akiwaona wanawake wazuri anawalinganisha na wewe. Kama wewe ni mchafu, mzembe, na nywele zako ni matimtim, anaweza akadhani kwamba wanawake wengine ni malaika ambao wameteremka kutoka mbinguni. Kwa hiyo jaribu kuonekana unapendeza na kuvutia wakati ukiwa nyumbani na uhakikishe kwamba atavutiwa na wewe kila wakati.

Soma barua ifuatayo iliyoandikwa na mume:
"Mtu hawezi kubainisha mke wangu na mtumishi wangu wa ndani ya nyumba. Ninaapa kwa jina la Allah kwamba wakati mwingine hufikiri: natamaani angevaa nyumbani mojawapo ya mavazi haya yalioshonwa kwa ajili ya karamu. Natamani angetupa zile nguo zilizochakaa. Nimemwambia mke wangu mara kadhaa; Mpenzi angalau vaa zile nguo nzuri hapa nyumbani unapokuwa likizo. Akajibu kwa ukali ' Sihitaji kwa tofauti ninapokuwa nyumbani, lakini kama siku moja ninaonekana mchafu, mbele ya wafanyakazi wenzangu, nitaona aibu.' "

Msomaji anaweza kuamini kwamba wakati mwanamke anaangalia usafi wa nyumba na kupika hawezi kuvaa vizuri na kupendeza. Hii inawezekana kuwa kweli lakini mama wa nyumba anaweza kuwa na nguo tofauti za kuvaa wakati wa kufanya usafi wa nyumba; na anaweza akabadilisha nguo zake za kufanyia kazi anapokuwa mbele ya mume wake au anapokuwa amerudi nyumbani. Wakati wote unaweza kuchana nywele zako na kujiweka katika hali ya usafi baada ya kufanya usafi wa nyumba.

Imamu Baqir (a.s) alisema: "Ni wajibu wa mwanamke kujipaka manukato na kuvaa nguo nzuri sana, kujipamba kadiri iwezekanavyo, na kukutana na mume wake katika hali hii mchana na usiku."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 80

Imamu Sadiq (a.s) alisema: "Wanawake hawatakiwi kuacha kujiremba iwe hata kuvaa kidani tu. Usiwe na mikono isiyo tiwa rangi kidogo, hata kama ni hina kidogo tu. Hata wanawake wazee wasiache kujipamba."

UWE KAMA MAMA KWAKE

Wakati wa kazi nyingi na kuumwa maradhi, mtu anahitaji kutunzwa na watu wengine. Muuguzi anaweza kusaidia kupona kwa mgonjwa vizuri mno kwa sababu ya kumwangalia mgonjwa kwa wema na mapenzi. Wanamume ni watoto wadogo ambao wamekuwa. Watahitaji matunzo kama ya mama. Mwanamume akioa mwanamke, anatarajia mke wake kuwa kama mama yake kwake wakati akiugua na matatizo.

Bibi mpendwa! Kama mume wako anaugua, muangalie zaidi kuliko ilivyo kawaida.

Onesha huruma yako kwake na uoneshe kwamba umefadhaishwa sana na ugonjwa wake huu. Mliwaze, tayarisha mahitaji yake yote na wanyamazishe watoto ili mgonjwa apumzike. Kama anahitaji daktari au dawa, basi fanya atakavyo. Mpikie chakula anacho kipenda na ambacho ni kizuri kwake. Muulize kuhusu afya yake mara kwa mara. Jaribu kukaa karibu naye kadiri iwezekanavyo. Kama anaumwa sana hivyo kwamba hawezi hata kupata usingizi na wewe usilale kadiri iwezekanavyo. Mara utakapo amka, mwendee.

Muulize hali yake inaendeleaje. Kama usiku huo hakulala kabisa, basi onesha masikitiko yako. Hakikisha chumba chake kipo kimya wakati wa mchana. Matunzo yako kwake yatasababisha mgonjwa kupata nafuu haraka. Atafurahia juhudi zako na kukupenda zaidi. Zaidi ya hayo angefanya hivyo kwako endapo ungeugua.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 81

Mtume (s.a.w) wa Mwenyezi Mungu alisema: “Jihadi ya mwanamke ni kumtunza vizuri mume wake.”

HIFADHI SIRI ZA FAMILIA

Wanawake mara nyingi kupenda kujua siri za waume zao, kipato chao, maamuzi yao kuhusu maisha ya siku zijazo, na kazi zao. Wanatarajia wanamume hawataficha chochote kutoka kwao.
Kinyume chake, wanaume hawapo tayari kuwaambia wake zao kila kitu. Matokeo yake ni kwamba waume wengine na wake wengine wakati wote huwa wanabishana kuhusu suala hili.

Baadhi ya wanawake wanasema kwamba waume zao hawana imani nao, hawataki wasome barua zao; hawataki wajue idadi ya kipato chao; wanaficha mambo mengi, hawajibu maswali yao inavyo stahili; na mara nyingine husema uwongo.

Katika hali ya kawaida, wanaume wanaweza kuwaambia wake zao siri zao. Lakini wanaume wanamini kwamba wake zao hawafichi siri; kwamba huwaambia watu kila kitu wanacho jua na wanaweza hata kusababisha matatizo kwa waume zao.

Kama mtu anataka kujua siri za watu wengine inatosha kwenda kwa wake zao. Baadhi ya wake za watu, baada ya kujua siri za waume zao, huwasaliti na kwa hiyo hutumia vibaya imani ya waume zao kwao.

Ni dhahiri kwamba wanaume kwa kiasi fulani wanayo hoja. Wanawake, wakilinganishwa na wanaume, wanazidiwa zaidi na nguvu za mvuto wa hisia. Wanawake wanapo kasirika, hushindwa kujidhibiti, na kwa kuwa wanajua siri za waume zao, huwaingiza kwenye matatizo kwa kutoa siri zao.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 82

Kwa hiyo, kama mwanamke anataka kujua siri za mume wake, lazima awe mwangalifu sana kwamba asiwaambie watu isipokuwa kwa idhini yake. Hatakiwi kuwaambia hata marafiki zake wa karibu sana au ndugu zake. Huko si kuweka siri kama ukimwambia mtu kuhusu siri hiyo, na kumwambia asiseme kwa mtu yeyote, vinginevyo kila mtu atajua siri hiyo.

Kwa hiyo mtu mwenye busara ni yule ambaye hasemi siri yake kwa mtu yeyote.

Imamu Ali (a.s) pia alisema: "Kifua cha mtu mwenye hekima ni kasiki ya siri zake."

Imamu Ali (a.s) pia alisema: "Wema wa ulimwengu huu na ule ujayo umo katika mambo mawili; Kuwa msiri, na kufanya urafiki na watu wazuri; na maovu yote yamo kwenye mambo mawili kushindwa kuwa msiri na kufanya urafiki na watu wabaya."

KUBALI UONGOZI WAKE

Kila taasisi, kiwanda na shirika huhitaji meneja muajibikaji. Kwenye kila kitengo cha jamii na shirika, ushirikiano baina ya wafanyakazi ni muhimu. Hata hivyo, kuendesha mambo ya kitengo cha aina hiyo huhitaji meneja ambaye anaweza kuratibu kazi.

Mojawapo ya kitengo muhimu sana cha jamii ni familia; Kuendesha mambo ya kitengo hiki ni jambo la lazima na gumu.

Bila shaka, lazima pawepo na uelewano wa kina sana, na ushirikiano baina ya watu wa familia, lakini pia lazima pawepo kiongozi ambaye anaweza kuwajibika kwa ukamilifu kuhusu mambo ya familia. Ni wazi kwamba,

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 83

kama familia haimfurahikii mtu anayeweza kuwapanga wengine, itapata usumbufu wa vurugu na ghasia. Hivyo ama mume lazima awe kama mkurugenzi na mke awe chini yake au kinyume chake.

Hata hivyo, kwa kuwa kipengele cha mantiki ya wanaume kinatawala kipengele cha hisia za wanawake, wanaume wanaweza kuwa viongozi bora zaidi.

Mwenyezi Mungu Mweza wa yote anasema kwenye Qurani Tukufu:

﴿ ٱلرِّجَالُ قَوَّٰمُونَ عَلَى ٱلنِّسَآءِ بِمَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ وَبِمَآ أَنفَقُوا۟ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ ۚ فَٱلصَّٰلِحَٰتُ قَٰنِتَٰتٌ حَٰفِظَٰتٌ لِّلْغَيْبِ بِمَا حَفِظَ ٱللَّهُ ﴿٣٤﴾ ﴾

“Wanamume ni wasimamizi wa wanawake, kwa kufadhiliwa na Mwenyezi Mungu baadhi yao juu ya baadhi, na kwa mali yao wanayotoa. Basi wanawake wema ni wale wenye kutii ….” (Qurani 4:34).

Hivyo, ni kwa manufaa ya jamaa wa familia kumheshimu mwanaume kama mlinzi wao na mkuu wao, na kutaka usimamizi wao katika matendo yao.

Hata hivyo, mtu asihitimishe kwamba hadhi ya mwanamke ndani ya nyumba inadunishwa, lakini ni kweli kwamba kudumisha utaratibu na nidhamu ndani ya nyumba ni majukumu yanayohitaji utendaji wa mume. Wanawake wanaoweza kufikiri bila upendeleo, wanaweza kuthibitisha tendo hili.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 84

Mwanamke alisema: "Tulikuwa na desturi nzuri Iran ambayo kwa bahati mbaya imefifia pole pole. Kwenye mila hii mwanaume alikuwa ndiye mkuu wa mambo ya familia. Alikuwa ndiye msimamizi. Siku hizi hata hivyo hali imebadilika na familia haziwezi kufanya uamuzi kuhusu nani awe mkuu. Ninaamini kwamba mwanamke wa leo, ambaye kwa namna moja au nyingine anayo hadhi sawa na ya mwanaume katika jamii, anaweza kukubali mume wake kama mkuu wa kaya…Desturi hii ya zamani inatakiwa ipendekezwe kwa mwanamke kijana wa leo, ambaye anayo nia ya kuolewa.
Anatakiwa kuingia nyumbani kwa mumewe akiwa amevaa vazi la harusi na kutoka ndani ya nyumba hiyo akiwa amevaa sanda."

Ni kweli kwamba shughuli za maisha ya kila siku hazimruhusu mwanaume kushiriki katika mambo yote ya familia na kwamba kwa kawaida mke ndiye anaye endesha familia kufuatana na atakavyo, lakini hata hivyo haki ya kuamuru hubaki kwa mwanaume, na kwa hali hiyo lazima ahishimiwe.

Kwa hiyo, inapotokea mwanaume kutoa maoni yake kuhusu jambo lolote la familia au anashauri kitu chochote, mke hatakiwi kumpinga au kumnyima mume wake haki yake kuamuru kwa namna yoyote ile. Vinginevyo, mwanaume atajifikiria yeye hana mamlaka na kumuona mke wake kama mwanamke asiye na adabu na shukrani. Mwanaume anaweza kujenga kinyongo dhidi yake na katika hatua ya baadaye, anaweza hata kukataa matakwa ya halali ya mkewe.

Mtume (s.a.w.w) wa Mwenyezi Mungu alisema: "Mwanamke mzuri atajali matakwa ya mumewe, na atafanya kwa mujibu wa apendavyo mumewe."

Mwanamke alimuuliza Mtume (s.a.w): "Mwanamke anawajibu gani kwa mume wake?" Mtume (s.a.w.w) alisema: "Mwanamke lazima amtii mume wake na asikiuke amri zake."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 85

Mtume (s.a.w.w) pia alisema: “Mwanamke mbaya sana miongoni mwa wanawake ni yule ambaye ni mkaidi na sugu.”

Mtume (s.a.w.w) pia alismema: “Mwanamke mbaya zaidi miongoni mwa wanawake ni yule ambaye ni mgumba, mchafu, sugu na asiye mtiifu.”

Bibi mpendwa! Kubali mamlaka ya mume wako. Taka usimamizi wake kuhusu mambo yenu ya familia. Usikiuke amri zake. Usikatae au kuweka pingamizi, yeye hushiriki katika mambo ya nyumbani na familia. Usikatae kushiriki kwake hata kwenye yale mambo ambayo wewe una utaalamu nayo. Usifanye vitendo vya kuonesha kwamba yeye hana mamlaka. Mruhusu ashiriki katika kazi zako mara chache. Wafundishe watoto wenu kuhishimu mamlaka yake na waambie lazima waombe ruhusa kutoka kwa baba yao kuhusu mambo yao. Watoto wenu lazima watambue kwamba hawatakiwi kukiuka amri zake tangu utoto wao. Kwa njia hii watoto wenu watakuwa na malezi ya kuwatii wazazi wao.

UWE MUELEKEVU WAKATI WA HALI NGUMU

Maisha yamejaa hali ya kupanda na kushuka kuhusu kipato. Magurudumu ya bahati njema hayazunguki mara zote kufuatana na vile tunavyotaka. Mtu kupita kwenye hali ngumu mara nyingi. Kila mtu huugua maradhi. Hupoteza kazi zao na wengine wanaweza kupoteza utajiri wao wote. Mambo mengi yasiyo furahisha hutokea katika maisha ya kila mtu.

Mwanaume na mwanamke ambao wametoa kiapo cha kuaminiana wao wawili na kusaini makubaliano ya ndoa, wanatakiwa kupita kwenye njia ya maisha kwa kuelewana. Makubaliano yanatakiwa kuwa imara sana hivyo kwamba yanaweza kuwawoka pamoja katika hali ya maradhi na afya njema, katika hali ya neema na shida ya kipato na wakati wa raha na shida.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 86

Bibi mpendwa! Kama mume wako anafilisikia na kuwa fukara, hivi ni lazima uongeze kwenye matatizo yake kwa kuwa na tabia isiyo kubalika. Kama anaugua, na kulala kitandani, ama nyumbani au hospitalini, ni hatua ya kupendeza wewe ukizidisha wema kwake. Lazima umuuguze, shughulikia mahitaji yake, na tumia fedha kwa ajili yake. Kama unazo fedha za kwako mwenyewe, lazima ulipie matibabu yake. Kumbuka kama wewe ungekuwa mgonjwa, angelipa fedha yake kwa ajili ya afya yako. Je, ni haki wewe uzuiye mali yako kwa kuipendelea zaidi kuliko afya njema ya mume wako? Kama ukishindwa kumridhisha katika wakati mgumu kama huu, basi utamkasirisha, na anaweza hata kupendelea kukutaliki.

Hapa kuna kesi ifaayo kusoma:
"Mtu alikuja mahakamani kumwacha mke wake. Alisema: 'Siku chache zilizopita niliugua na daktari wangu aliniambia kwamba nilitakiwa kufanyiwa upasuaji. Nilimwomba mke wangu anikopeshe fedha alizokuwa nazo kwenye akiba yake. Alikataa na aliondoka nyumbani kwangu. Matokeo yake nilifanyiwa upasuaji kwenye Hospitali ya taifa. Sasa nimepona na afya yangu ni njema sitaki kuishi na mwanamke ambaye anapenda zaidi fedha yake kuliko mume wake. Mtu atamwitaje mwanamke huyu, mke?"

Kila mtu aliye makini katika mambo yake atakubali kwamba kwenye mfano uliotajwa hapo juu, mwanaume ndiye aliyekuwa na haki. Mwanamke kama huyo ambaye hataki kutumia fedha yake kwa ajili ya tiba ya mume wake, hastahili kuwa kwenye nafasi inayo heshimiwa ya 'mke wa mtu.'

Bibi mpendwa! Uwe mwangalifu, usiwe katili wakati mume wako akiumwa maradhi ya kudumu; hivi ni lazima umwache yeye na watoto wenu kwa sababu hii? Unawezaje kumkimbia mwanamume ambaye umekuwa naye mchana na usiku wa starehe ya siku nyingi? Unajuaje

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 87

kwamba labda hatima ya aina hii inakungojea wewe? Unawezaje kuwa na uhakika kwamba mwanamume mwingine atakuwa bora zaidi kuliko huyu? Usiwe sugu na mbinafsi. Ujitolee mhanga na uwe na moyo wa kumuabudu Mwenyezi Mungu, uilinde heshima yako na watoto wako. Uwe mvumilivu na uwafundishe watoto wako somo la moyo wa upendo, mapenzi na ustahamilivu. Unaweza kuwa na uhakika kwamba, katika dunia hii na ile ijayo, utapata thawabu nyingi sana. Moyo wako wa kujitolea ni njia bora sana ya kuonesha unamjali mume wako tabia ambayo inawekwa kwenye kiwango sawa na Jihadi.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Jihadi ya mwanamke ipo katika kumtunza mume wake."

USIKATAE KUSEMA NA USINUNE

Ni kawaida ya wanawake wengine kwamba, wanapo tibuliwa na waume zao, hununa, hukataa kusema, hukataa kushughulikia kazi za nyumbani, hawataki kula, huwapiga watoto, au hulalamika. Wanaamini kwamba kuacha kusema au kuanzisha ugomvi ndizo njia nzuri sana kulipiza kisasi kwa waume zao. Msimamo huu si tu unashindwa kumwadhibu mwanaume, lakini unaweza kusababisha naye kulipiza kisasi. Maisha huanza kuwa magumu kwani hugeuka kuwa na mfululizo wa ugomvi. Mwanamke hupiga kite, halafu mwanamume naye hufanya hivyo. Mwanamke hukataa kusema na mwanamume hulipa kisasi. Mwanamke hufanya kitu kingine, na mwanamume hufanya hivyo hivyo hadi wanachoka na kupitia upatanishi wa ndugu au marafiki, huelewana. Lakini hii si mara ya kwanza wao kugombana. Watagombana tena na tena na patakuwepo na siku chache za machungu.

Kwa hiyo, kuishi maisha yenye ugomvi wa familia litakuwa si jambo la kufurahisha kwa ama wazazi au watoto. Vijana wengi waliozikimbia

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 88

familia zao wanatoka kwenye familia za aina hii ambao baadaye huingia kwenye uhalifu na uovu.

Kijana ambaye alikamatwa kwa tuhuma ya wizi, aliwalaumu wazazi wake kwa uhalifu wake na alisema: “Wazazi wangu walikuwa wakibishana kila siku na baadaye kwenda kwa ndugu zao na mimi nilikwenda kuzurura mitaani. Halafu nikadanganywa na vijana wengine na hatimaye nikafanya uhalifu wa wizi.”

Msichana mwenye umri wa miaka kumi aliwaambia wafanya kazi wa usitawi wa jamii: “Sina uhakika lakini nakumbuka kwamba siku moja wakati wa usiku wazazi wangu walibishana kuhusu kitu fulani. Kesho yake, mama yangu aliondoka na baada ya siku chache, baba alinipeleka kwa shangazi yangu. Baada ya kipindi fulani mwanamke mkongwe alinichukua kutoka kwa shangazi na akanileta Tehran. Ni miaka michache iliyopita hadi sasa, ambapo nimekuwa ninaishi naye na niliteseka sana hivyo kwamba sitaki kurudi kwake.”

Mwalimu wa msichana huyo alisema; Huyu msichana ni mmojawapo wa wanafunzi wangu. Hana maendeleo mazuri katika masomo yake na inaonesha kama vile anaumizwa na jambo fulani. Wakati wote anafikiri. Amekuwa hata anakaa kwenye ua wa shule na kuonekana hayuko tayari kurudi nyumbani. Siku mbili zilizopita nilimuuliza kwa nini hataki kwenda nyumbani? Akajibu kwamba alikuwa anaishi na mwanamke mzee ambaye alikuwa mbaya sana kwake na kwamba hakutaka kurudi nyumbani kwa bi kizee huyo. Nilimuliza kuhusu wazazi wake na akasema walitengana.”

Bibi mpendwa! Lazima ukumbuke kwamba kama mume wako anakuwa mkali sana kwako na hataki kusema na wewe, halafu anaweza hata kuchukua hatua kali zaidi kama vile kukupiga. Inawezekana labda

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 89

utaondoka kwenda kwa wazazi wako kwa sababu ya ukali wake. Kitakachofuatia ni kwamba wazazi wako wanaweza wakaingilia kati, na ugomvi wako na mume wako utazidi kupanuka. Hatimaye labda unaweza kuachika ambapo wewe utapata hasara zaidi kuliko mume wako. Inawezekana ukaendelea kuishi peke yako katika uhai wako wote. Kwa hakika utajuta kutalikiwa.

Mwanamke alisema: "Kipindi fulani kilichopita niliolewa. Sikuwa na uelewa mzuri kuhusu kumtunza mume wangu na yeye hakuwa na ujuzi wa kutosha kunitunza mimi. Ilikuwa tabia yetu kugombana kila siku. Wiki moja nilikiwa sisemi naye na wiki moja baadaye alikuwa hataki kusema na mimi. Mnamo siku za Ijumaa tu, tulikuwa tunaelewana, kupitia kwa upatanishi wa marafiki na ndugu. Pole pole mume wangu alikasirishwa na mimi na alifikiria kunitaliki na kuoa mke mwingine. Kwa kuwa nilikuwa na umri mdogo, sikuwa tayari kubadilika na sikukataa kutalikiwa. Tuliachana na mimi nilipanga nyumba ya kwangu mwenyewe. Baada ya muda mfupi nikatambua hatari. Watu wengi niliokutana nao lengo lao kubwa lilikuwa kunidanganya. Niliamua kupatana na mtaliki wangu na nilikwenda nyumbani kwake. Huko nilimkuta mwanamke ambaye alijijulisha kwangu kama mke wa mtalaka wangu. Nililia njia yote nilipokuwa narudi kwangu. Nilijuta kwa nini nilikubali kuachika, lakini nilichelewa sana."

Mwanamke mwenye miaka ishirini na mbili, alimpeleka mtoto wake kwa wazazi wake, baada ya kuachika, alijaribu kujiua muda wa usiku, siku ya harusi ya dada yake.

Mama mpendwa! Lazima kwa kweli uepuke kumnunia na kukataa kusema na mumeo. Kama mumeo amekutibua uwe mvumilivu. Ukisha tulia na kuwa makini, ongea naye kwa upole kuhusu kukasirika kwako. Mathalan, unaweza kumwambia: "Ulinifedhehesha jana,

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 90

au ulikataa kusikiliza matakwa yangu… Hivi ni haki kwamba unaweza kunitendea hivyo?"

Njia kama hivyo, si tu inakupumzisha kwenye hisia zako, bali pia itampa onyo. Kwa hiyo, mumeo atajaribu kurekebisha tabia yake na atakuheshimu kwa tabia yako njema. Matokeo yake atapitia upya tabia yake, na atajaribu kuwa na nidhamu.

Mtume (s.a.w.w) alisema: "Wakati Waislamu wawili wakikataa kusemeshana na wasipopatana kwa muda wa siku tatu, wote wawili watakuwa wamevua joho la Uislamu, na hapatakuwepo na urafiki wowote baina yao. Halafu yeyote miongoni mwao ambaye ataanza kupatana na mwenzake, siku ya ufufuo ataishia Peponi (haraka kuliko mwenzake.)"

MUME WAKO AKIKASIRIKA, WEWE NYAMAZA

Mwanaume hukutana na watu wengi anapokuwa katika shughuli zake na hukabiliana na matatizo mengi. Anaporudi nyumbani, huwa amechoka na anapokutana na tukio dogo sana lisilofurahisha hukasirika na anaweza kuwa mkali kwa. familia yake.

Mwanamke mwenye busara atanyamaza wakati mume wake anajitapa kwa makelele yenye matusi. halafu mwanaume atanyamaza na kutulia na kujuta kwa matusi yake. Akiona kwamba hakuna jibu lolote kuhusu hasira yake, anaweza hata kuomba msamaha. Kwa msimamo huu, familia hurudi kwenye hali yake ya kawaida baada ya saa moja au mbili tu.

Hata hivyo, kama mwanamke wa nyumbani hakuelewa nafasi nyeti ya mume wake basi anaweza kupiga makelele, kuapa laana na kukasirika kwa ukali.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 91

Kwa njia hii, mume na mke wanaweza kupigana na hatimaye kuchukua hatua ya kuachana. Familia nyingi huvunjika kwa sababu ya matukio madogo kama haya. Ipo hata mifano ambapo wanaume hukasirika sana hivyo kwamba hulipuka kama volcano na kufanya mauaji.

Mwanaume alimpiga risasi mke wake na mama wa kambo, na yeye mwenyewe akajipiga hadi kufa. Inafahamika kwamba wanandoa hao wana ugomvi mwingi na mabishano tangu mwanzo wa ndoa yao. Usiku wa tukio hilo mume alirudi nyumbani kutoka kwenye shughuli zake ambapo wanandoa hao walianza tena ubishi mwingine. Mume akampiga mke wake na mwanamke aliamua kwenda polisi. Haraka mwanaume alichukua bunduki, akamuua mke wake, mama yake wa kambo na halafu akajiua yeye mwenyewe kwa risasi."

Si ingekuwa bora zaidi kama mwanamke angenyamaza wakati mume wake alikasirika? Kama mwanamke angevumilia, maisha ya watu watatu wangepotea? Wewe ungependelea vipi? Dakika chache za kimya au matokeo yote mabaya kwa kuendeleza ubishi na mume wako? Unadhani hata kwa dakika moja kwamba nafasi ya mwanaume inalindwa na kwa hiyo hana hatia. Si hivyo kabisa. Kama mambo yalivyo, anayo hatia. Hakutakiwa kumaliza hasira yake kwa kumaliza familia yake. Kwenye sura ijayo, jambo hili litazungumziwa kwa kina zaidi lakini hapa tunasema kwamba mwanamke anatakiwa kuwa na busara na asijibu hasira ya mume wake hata kama mume yupo sawa au si sawa. Katika hali kama hii, mwanaume atashindwa kuthibiti hasira yake, kwa hiyo ni muhimu kwamba mke, anyamaze kimya ili aokoe familia yake.

Kwa kawaida wanawake hudhani kwamba kunyamaza kimya wanapokabiliana na hasira za waume zao, ni namna ya kudhalilishwa, na kwa hiyo wangepoteza hishima yao. Hata hivyo, hali hii ni kinyume chake. Mwanaume asiyeona jibu lolote anapomtukana mke wake, kwa

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 92

hakika atajuta. Atamfikiria mke wake kuwa anampenda, ambaye licha ya uwezo wake wa kulipa kisasi alipendelea kusamehe. Mapenzi yake kwa mke wake yataongezeka mara nyingi. Ataomba msamaha na kwa hiyo mkewe atapata heshima zaidi.

Mtume (s.a.w.w) alisema: "Mwanamke yeyote ambaye huvumilia hasira mbaya ya mume wake Mwenyezi Mungu atampa thawabu zinazolingana na zile Alizompa Asiya binti Muzahim."

Mtume (s.a.w.w) alisema: "Mwanamke aliyebora zaidi miongoni mwa wanawake zenu ni yule ambaye, akiona hasira ya mume wake humwambia; Nina jisalimisha kwako. Siwezi kulala hadi utakaporidhika na mimi."

Mtume (s.a.w.w) alisema: "Usamehevu na uvumilivu ungeongeza heshima na hadhi ya wahusika. Uwe msamehevu ili Mwenyezi Mungu akuhifadhi."

BURUDANI ZA WANAMUME

Baadhi ya wanamume hupenda kuwa na burudani zao nyumbani. Wanapenda, kwa mfano, kukusanya stampu au vitabu, kushughulikia bustani au kupiga picha wakati wa muda wao binafsi nyumbani.

Burudani kama hizo zimeainishwa kuwa ni shughuli bora zaidi. Burudani za aina hiyo zinafaa sana kwamba huwavutia wanaume kuwa nyumbani mwao, na halikadhalika husababisha akili na mwili kutulia. Mtu anaweza kufadhaika na kuchukizwa kwa sababu ya kukaa bila kufanya kazi. Ni ukweli kwamba njia mojawapo ya kuwatibu watu wenye maradhi, ya akili ni kuwashughulisha na kazi fulani. Wale miongoni mwetu wanaofanya kazi zaidi ya wengine, kwa ujumla hawaathiriwi na kuvurugikiwa na akili na hawaathiriwi na kazi za hatari.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 93

Kwa hiyo, mwanamke lazima ahishimu burudani nzuri za waume wao na wasidhani kwamba burudani za kupitisha muda ni za kipumbavu, duni na zisizofaa. Wanawake lazima wawatie moyo waume zao kujishughulisha na burudani hizi na inapowezekana na wao washiriki.

UTUNZAJI WA NYUMBA

Nyumba, licha ya kwamba ni eneo dogo, ni neema yenye thamani kubwa. Ni hifadhi ya mwanamume ambaye hukimbilia humo baada ya kazi. Ni mahali pa kupata faraja hata wakati wa likizo, mtu huhisi kupumzika nyumbani kwake. Hakuna mahali panapolingana na nyumbani na hakuna mahali ambapo mtu anaweza kupata amani kama nyumbani kwake. Ni mahali pa urafiki, upendo, uaminifu, faraja, mapumziko na ambapo wanaume na wanawake wenye maadili mema huelimishwa na kuelekezwa. Ni karakana ya kuelekeza wanadamu na kuwasomesha na kuwalea watoto. Ni jamii ndogo ambayo humo jamii kubwa zaidi huundwa.

Nyumba inayo dhamana kubwa zaidi. Mazingira ya familia ndogo, licha ya kwamba ni sehemu ya jamii kubwa kufurahia uhuru wa ndani, ndio maana kazi ya kurekebisha taifa lazima ianzie kwenye familia.

Jukumu la elimu, uelekezaji na uendeshaji wa msingi huu nyeti wa jamii upo mikononi mwa wanawake. Kwa hiyo, kupitia kwenye matendo yao na tabia zao kwa familia zao, ni sifa zinazoweza kuashiria kudumaa au kuendelea kwa taifa. Hivyo, kazi ya mama wa nyumbani ni nyeti, yenye kuhishimiwa na inayostahili kutukuzwa.

Watu wanaoshindwa kupima nguvu ya kitengo cha familia na wanaona aibu kufanya kazi hii, kwa kweli hawajui thamani na manufaa yake. Mama wa nyumbani anatakiwa kujivunia nafasi yake. Anayo nafasi ya heshima na kujitoia mhanga kwa manufaa ya jamii.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 94

Wanawake wasomi wanayo dhamana kubwa zaidi katika kazi hii na hivyo wanatakiwa kuwa mifano kwa wengine. Wanatakiwa kuthibitisha kwa vitendo kwamba kusoma si pingamizi ya mwanamke kuwa mama wa nyumbani, lakini ni kwamba pia husaidia kuwa mama wa nyumba bora zaidi.

Mwanamke msomi anatakiwa kuongoza maisha ya familia kwa jinsi iliyo nzuri kadiri iwezekanavyo. Anatakiwa kujivunia kazi ya kuwa mama wa nyumbani na athibitishe kwamba mke msomi ni bora zaidi kwa asiye msomi.

Sio sahihi yeye kuacha kazi ya kutunza familia kwa kisingizio cha kuwa msomi. Elimu haikusudiwi kumfanya mtu aliye nayo akwepe wajibu wake, lakini lengo lake ni kumsaidia mtu atimize wajibu wake vizuri zaidi.

“Mwanaume alioa msichana aliyehitimu elimu ya sekondari ya juu, alisema mahakamani, Mke wangu hataki kufanya kazi yoyote ya nyumbani. Kila nilipolalamika alisema kwamba kazi ya kutunza familia si kazi ya mwanamke aliyesoma. Hayupo tayari kubadilika na hata ananiomba nimpe talaka na badala yake nioe mtumishi wa nyumbani! Siku mbili zilizopita niliwaalika ndugu na marafiki zake mke wangu kwa chakula cha jioni. Wakati wa chakula niliitandaza nguo ya meza na kuweka fremu ya cheti cha mke wangu cha sekondari ya juu katikati ya meza. Halafu nikamwambia kila mmoja wao aangalie kwa makini chakula cha jioni ambacho mke wangu hunitayarishia kila jioni!”

Sasa tusome maoni ya wanawake wasomi wachache kuhusu kuwa mama wa nyumba:

Bibi F.N Shamirani msomi mwenye digrii, alisema: “Mke wa nyumbani anatakiwa kuwa stadi wa kushughulikia mambo haya, mwandani mwema

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 95

wa mume wake, mama mwema kwa watoto wake na mwenyeji mwema kwa wageni."

Mke wa Fasihi ambaye ni bingwa wa tiba ya maradhi ya watoto, alisema: "Ninaamini kwamba mama wa nyumbani halisi ni yule ambaye hafanyi kazi ofisini, kwa ssababu kazi za ofosi nchini mwetu hazina vifaa muhimu kuhusu mahitaji ya lishe na vyumba vya watoto. Mwanamke anaye fanya kazi ofisini wakati wote anao wasi wasi kuhusu watoto wake au chakula cha mume wake."

Mke wa S. Yakita, ambaye ni mrakibu wa Ufundi kitivo cha Tiba, alisema.: "Mama wa nyumbani anatakiwa awe na uwezo wa kutengeneza nyumba safi na inayovutia kwa kutumia bajeti za furaha na huzuni na mume wake. Asidharau hadhi ya mume wake kiakili na kijamii."

Mke wa I. Naimi alisema: "Mama wa nyumbani ni yule anaye punguza sana burudani zisizo na umuhimu na ambaye atajaribu kuendeleza mambo ya nyumbani. Pia lazima awe na uwezo wa kulinganisha kipato na matumizi."

USAFI

Mojawapo ya wajibu muhimu wa mama wa nyumbani ni kudumisha usafi ndani ya nyumba. Usafi ni ufunguo kwa elimusiha na afya. Huzuia maradhi mengi na huwavutia watu wa familia. Ni chanzo cha heshima kwa familia.

Mtume (s.a.w.w) alisema: "Dini ya Uislamu msingi wake ni usafi."

Mtume (s.a.w) pia alisema: "Uislamu ni safi kabisa, kwa hiyo lazima ufanye jitihada kuwa safi kwa sababu ni watu walio safi tu ndio watakaoingia Peponi."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 96

Kila mara iweke nyumba yenu katika hali ya usafi na kupanga vizuri. Futa vumbi mara moja kila siku na ondoa madoa yote na uchafu wote kutoka kwenye kuta, milango, madirisha, fenicha na vitu vingine. Weka taka kwenye pipa la taka lenye mfuniko, liweke mbali na vyumba vingine na jiko. Takataka zikijaa kwenye pipa la taka zimwage panapostahili. Kila mara usiweke taka mbele ya nyumba yenu. Usiwaruhusu watoto wenu wakojoe kwenye bustani au ua, na wakifanya hivyo, safisha sehemu hiyo kwa maji haraka. Usilundike vyombo vichafu. Vioshe haraka iwezekanavyo. Usisahau kwamba virusi vya hatari hukua kwenye uchafu na vinaweza kuwa vya hatari kwako na familia yako. Osha vyombo kwa maji safi, na baada ya hapo viweke kwenye sehemu iliyo safi. Kusanya nguo zote chafu, hususan nepi za watoto kutoka kwenye vyumba vyote na jiko na uzifue haraka iwezekanavyo.

Weka nguo za familia zote hususan nguo za ndani, safi na nadhifu. Osha nyama na mboga za majani na mchanganyiko wote wa chakula kabla ya kupika. Osha matunda yote kabla ya kula kwa sababu baadhi yao hupuliziwa sumu ya kuua wadudu.

Nawa mikono kabla na baada ya kula na wafundishe watoto wenu kufanya hivyo. Baada ya kula chakula nawa mikono na modomo. Kama inawezekena piga mswaki meno kila baada ya mlo. Kupiga mswaki ni jambo muhimu, angalau mara moja kwa siku, ni vema zaidi kabla ya kulala.

Kata kucha zako mara moja kwa wiki. Kucha ndefu si elimusiha, kwa sababu virusi vinaweza kuishi kwenye kucha ndefu. Oga, angalau mara moja kwa wiki au kama inawezekana kila baada ya siku moja.

lazima unyoe nywele kwenye kwapa pamoja na sehemu zingine. Nywele zilizojificha kwenye mwili ni mahali panapoweza kuishi virusi vinavyokua. Usiruhusu nzi watue kwenye chakula kwa sababu nzi ni wasafirishaji wa vijiumbe hatari vya maradhi.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 97

Dini Tukufu ya Uislamu inapendekeza kwa kusisitiza watu waangalie usafi. Imam Sadiq (a.s) alisema: "Mwenyezi Mungu Mweza wa yote hupenda mapambo, sura ya kuvutia na hapendezewi kuona hali ya kujifanya maskini. Hupenda kuona athari za neema zake kwa mja wake, yaani, kumuona akiwa safi, nadhifu na kutumia manukato, kuremba nyumba yake, kupangusa vumbi kwenye mazingira ya nyumba yake kuwasha taa kabla ya jua kuchwa kwa sababu kitendo hiki huondoa umasikini nyumbani na kuongeza riziki."

Mtume (s.a.w) alisema: "Mtu mchafu ni mja mbaya (kwa Mwenyezi Mungu)"

Imamu Saiq (a.s) alisema: "Iweke nyumba yako katika hali ya usafi na kuondoa utando wa buibui kwa sababu utando wa buibui husababisha umasikini."

Mtume (s.a.w.w) alisema: "Usiache uchafu ndani ya nyumba wakati wa usiku kwa sababu shetani huishi humo (yaani, kwenye uchafu na najisi)."

Mtume (s.a.w.w) alisema: "Nguo za mtu lazima ziwe safi kila mara." 101

Akiongezea, Mtume wa Mwenyezi Mungu(s.a.w.w) alisema: Usiache nguo yenye mafuta ndani ya nyumba, kwa sababu shetani hufanya makazi yake hapo."

Imam Sadiq (a.s) alisema: "Kuosha vyombo na kusafisha mazingira ya nyumba huongeza riziki."

Imam Sadiq (a.s) pia alisema: "Usiache vyombo bila kuvifunika, vinginevyo shetani huvitemea mate na kuvitumia."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 98

Kwa kuongezea Imam Sadiq (a.s) alisema: "Matunda hupulizwa madawa yenye sumu, kwa hiyo, yakosheni kabla ya kula."

Imam Kazim (a.s) alisema: "Kuoga kila baada ya siku moja humnenepesha mtu."

Mtume (s.a.w) wa Mwenyezi Mungu alisema: "Usiache uchafu nyuma ya mlango wa mbele wa nyumba kwa sababu shetani hufanya masikani hapo."

Mtume (s.a.w.w) wa Mwenyezi Mungu pia alisema; Kama ingekuwa si jambo la usumbufu kwa wafuasi wangu, ningewaagiza kupiga mswaki meno yao kila wanapochukua wudhu kwa ajili ya sala (yaani mara tano kwa siku)."

Imamu Sadiq (a.s) alisema: "Kukata kucha kila siku ya Ijumaa huzuia maambukizi ya ukoma, kichaa na kupofuka macho." 109
Imesimuliwa kwamba shetani hulala usingizi chini ya kucha ndefu."

Imamu Ali (a.s) alisema: "Kunawa mikono kabla ya kuanza kula chakula, hurefusha maisha, huzuia nguo za mtu kuchafuka na kung'arisha macho ya mtu."

NYUMBA NADHIFU

Nyumba nadhifu hupendwa zaidi kuliko nyumba chafu katika njia nyingi:

Kwanza: unadhifu husaidia kuifanya nyumba ionekane safi, inavutia na mandhari ya kupendeza. Nyumba yenye mpangilio wa vitu, haimchoshi mtu, lakini itakuwa chanzo cha shangwe na furaha.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 99

Mbili: kazi ya utunzaji wa nyumba ingekuwa rahisi kwenye familia inayofuata maagizo ipasavyo, na mama mwenye nyumba kwa kujua kwa usahihi mahali vilipo vitu vya nyumbani, haungepotezwa muda kuvitafuta. matokeo yake ni kwamba mwanamke hatachoshwa na kazi yake.

Tatu: humvutia mwanamume nyumbani kwake na mke wake. Nyumba yenye mpangilio mzuri ni mwakilishi wa sifa ya mwanamke.

Nne: nyumba nadhifu ni chanzo cha majivuno ya familia yote. Yeyote anayeitembelea, atapendezwa nayo, na kuvutiwa na ubunifu na ladha ya mwanamke.

Kuwa na vitu vya anasa si chanzo cha kuifanya nyumba kuwa nzuri, lakini ni jinsi ambavyo vitu vya ndani ya nyumba vilivyopangwa, huifanya nyumba iwe ya kuvutia. Lazima utakuwa umewaona watu matajiri ambao nyumba zao, licha ya kuwa na vitu vingi vya anasa, huchosha na wapo watu ambao ni masikini ambao nyumba zao, kwa sababu ya kuwa na mpangilio mzuri wa vitu, hufurahisha kuziangalia.

Kwa hiyo, kuipanga nyumba ni mojawapo ya wajibu wa mama wa nyumbani. Wanawake wenye vipaji na ladha nzuri wanajua namna ya kuziweka nyumba zao katika mpangilio mzuri, lakini kutaja mambo machache ni jambo linalofaa.

Ainisha vyombo vyako; usiviomekeze vyombo vyote pamoja. Weka vyombo vya kulia chakula yaani visu, vijiko, na kadhalika weka mahali pengine. Weka vyombo vinavyotumika wakati wageni wakiwepo, mahali tofauti na vyombo vinavyotumika kila siku. Fanya hivyo kwa kila kitu. Kila kitu lazima kiwekwe mahali pake hivyo kwamba watu wote wa familia wanaweza kuvipata kwa urahisi hata kwenye giza.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 100

Baadhi ya wanawake wanaweza kuamini kwamba utaratibu wa namna hiyo ni kwa ajili ya watu matajiri. Lakini hii si sahihi hata watu masikini lazima wapange vyombo vyao pamoja na vyombo vya jikoni, vitanda, nguo na vitu vinginevyo. Mathalani, mke lazima awe na mahali pa kuweka nguo zake tu na nguo za mume ziwekwe mahali pengine na nguo za watoto mahali pengine. Nguo za kuvaa wakati wa baridi lazima ziwekwe mahali tofauti na zile za kuvaa wakati wa joto. Nguo chafu lazima ziwekwe mahali pake. Mapambo kama vile; bangili, vidani, heleni, vibanio vya nywele na kadhalika lazima viwekwe sehemu yake. Wafundishe watoto wenu wawe nadhifu kuhusu nguo zao, vitabu vyao, wanasesere na kadhalika. Unaweza kuwa na uhakika kwamba kwa kuwa nadhifu, watoto wenu watajifunza na kuwaiga nyinyi wazazi wao.

Wanawake wachafu huwalaumu watoto wao kwa uchafu wa nyumba, ambapo watoto wanatakiwa kujifunza kutoka kwa wazazi wao.

Kama wazazi ni nadhifu, basi watoto watajifunza, na watoto kwa kawaida wapo tayari kukemewa kinidhamu.

Weka fedha yako yote, hati muhimu mapambo ya vito na vyeti mahali pa salama au mahali ambapo watoto hawafikii. Si sahihi kumwadhibu mtoto kwa sababu ya kugusa, kuharibu au kupoteza kitu chochote cha thamani ambavyo umeviweka mahali ambapo watoto wanaweza kufika. Wazazi ndio wenye hatia na wanatakiwa kutambua vema zaidi.

Mwanamume aliacha fedha na akamwambia mkewe aziweke mahali pa salama na akaziweka kwenye maungio ya shubaka na akaondoka. Baada ya muda mfupi mwanamume akarudi na hakuzikuta fedha hizo alizoziacha. Aliangalia sehemu mbali mbali ndani ya nyumba kwa shauku lakini hakuzipata na akamuona mwanae wa umri wa miaka mitano alikuwa anachoma kitu bustanini. Mama wa mtoto huyo alimwendea kwa hasira,

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 101

akamnyanyua juu, na halafu akamtupa mtoto huyo chini kwa nguvu sana hivyo kwamba mtoto huyo alikufa papo hapo. Mama aliogopa sana alipokuwa anaiangalia maiti ya mtoto wake. Mwanamke huyo alipotoka bustanini, mumewe alianza kumpiga na halafu akaamua aende polisi. Akapanda pikipiki yake lakini alipokuwa anaelekea polisi alipata ajali. Sasa yupo kwenye chumba cha wagonjwa mahututi!

Unadhani ni nani mwenye makosa kwenye tukio hili? Unaweza kuamua wewe mwenyewe. Lakini unajua tukio lingine linalofanana na hili.

Dawa, mafuta ya taa, petroli na vitu vingine vyenye asili ya sumu lazima viwekwe mahali ambapo watoto hawawezi kuvipata. Watoto hunywa na kula chochote kinachoonekana kama chakula au maji. Usihatarishe maisha yao kwa uzembe wako. Wapo watoto wengi ambao hufa kwa sababu ya uzembe wa wazazi wao.

Watoto wawili, kaka na dada, wenye umri wa miaka 6 na 4 walikunywa D.D.T ya kuyeyushwa. Mtoto wa kike wa miaka minne alikufa na kaka yake alipona. Watoto hao walikuwa peke yao ndani ya nyumba. Walikunywa myeyuko huo kwa sababu ya kukata kiu. Mama yao watoto hao alisema hospitalini kwamba myeyuko huo ulitengenezwa kwa lengo la kuua panya ndani ya nyumba yake."

Watoto wawili walikunywa mafuta ya taa kwa makosa wakidhani kwamba ni maji. Mtoto mwingine alimeza vidonge kumi miongoni mwa vidonge vya mama yake. Watoto hawa wote walipelekwa hospitalini kutibiwa.

Hatimaye unakumbushwa kwamba nidhamu inafaa tu hadi kiwango fulani ili isiwe sababu ya kukunyang'anya faraja. Usije ukashikwa sana na shauku kuhusu unadhifu, kwa sababu kuwa na shauku sana kwenyewe ni tatizo.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 102

Mwanaume alisema: “Nimechoshwa na tabia ya mke wangu kushikilia usafi na unadhifu. Kila siku ninaporudi nyumbani saa 10:30 alasiri, mke wangu huniamuru ninawe mikono na miguu mara kadhaa. Anataka niweke nguo zangu mahali panapostahili. Haniruhusu nivute sigara kwenye vyumba vyote. Wakati wote nilikuwa naishi kwa uhuru, lakini wakati wa miaka minne ya ndoa, nimekuwa ninaishi jela. Kwa nini mtu ajali sana kuhusu usafi na unadhifu. Hii ni shauku iliyozidi mno, nami siipendi tabia hii.”

Tabia ya wastani ni bora sana katika vipengele vyote vya maisha ya mtu. Mtu hatakiwi kuwa na vurumai sana hivyo kwamba inakuwa haiwezekani kuishi maisha ya kawaida, na pia si lazima mtu adekeze usafi hadi kwenye kiwango cha shauku iliyozidi mpaka.

KUTAYARISHA CHAKULA

Wajibu mwingine muhimu sana wa mama wa nyumba ni kutayarisha chakula cha familia yake. Mama mwenye nyumba mzuri, pia ni mpishi mzuri ambaye anaweza kutayarisha chakula kitamu kwa fedha kidogo, ambapo mama wa nyumba mbaya hupika chakula kibaya kwa kutumia viungo vya gharama kubwa. Chakula kitamu ni njia ya kumvutia mume wako aelekee kwako. Mwanaume ambaye mke wake hupika vizuri, hafurahii zaidi kwenda kula nje.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: “Mwanamke bora zaidi miongoni mwa wanawake zenu ni yule anayejipuliza manukato, hutayarisha chakula kwa ustadi na hadekezi tabia ya kutumia fedha kwa israfu. Mwanamke wa aina hii ni kundi la wafanyakazi wa Mwenyezi Mungu na mtu anayefanya kazi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kamwe hatapatwa na majuto au kushindwa.”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 103

Haiwezekani kuandika orodha ya aina za mapishi, lakini vipo vitabu vingi vizuri kuhusu somo hili ambavyo vinaweza kupatikana na kutumiwa kupika chakula kitamu.

Lakini mambo machache ya kukumbuka: Nia ya kula chakula si kujaza tumbo lakini pia kwamba hugawia mwili lishe yote inayohitajika kuendeleza kazi yake. lishe muhimu inayohitajiwa na mwili ipo kwenye nyama, matunda, mboga na nafaka na inaweza kuainishwa katika makundi sita:
Maji.

Madini; kama vile kalisi/chokaa,fosforasi, chuma, shaba na kadhalika.
Vitu vyenye wanga yaani kabohaidreti.
Mafuta.
Protini.
Vitamini kama A, B, C, D, E na K.

Sehemu kubwa ya uzito wa mtu ni maji. Maji huyeyusha chakula kigumu ili kiwe tayari kufyonzwa na utumbo mdogo. Maji pia hurekebisha joto la mwili.

Madini ni muhimu kwa kukua mifupa, meno, na kurekebisha utendaji wa misuli.

Kabohairdate hutengeneza nguvu na joto.

Protini husaidia mabadiliko ya seli mpya kushika nafasi ya zilizozeeka au zilizokufa na kusababisha kukua kwa mwili.

Vitamini pia ni muhimu kwa kukuza na kuimarisha mifupa, kurekebisha majibizo ya kemikali kwenye mwili na ni muhimu kudumisha mfumo mzuri wa neva nzuri.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 104

Kila kitu kilichotajwa hapo juu ni muhimu kwa mwili. Utapiamlo husababisha maradhi mengi na unaweza kuua. Ubora wa chakula ni muhimu na upo uhusiano wa uwiano wa urefu wa kipindi cha maisha ya mtu, furaha na huzuni, uzuri na ubaya na neva zenye afya au maradhi ya akili.

Tunaonekana tulivyo kufuatana na tulicho kula. Kama mtu anafuatilia chakula chake na kujali mazoea ya ulaji wake, hatapata maradhi mara kwa mara. Si busara kula chakula kitamu bila kutafakari ubora wake. Mara afya ya mtu inapoharibika kwa sababu ya chakula kibaya, lazima atafute daktari wa kumtibu, lakini bahati mbaya mwili wa binadamu kamwe hautarudi katika afya yake ya ya mwanzo.

Mtume wa Mwenyezi Mungu(s.a.w.w) alisema: “Tumbo ni kituo cha maradhi yote.”

Kwa kuwa chaguo la chakula ni jukumu la wanawake, kwa hiyo, wanao wajibu wa afya ya familia. Uzembe mdogo sana kwa upande wa mwanamke, utaiweka afya ya familia yote katika hali ya kushambuliwa na maradhi mengi.

Kwa hiyo, mama mwenye nyumba, pamoja na yeye kuwa mpishi mzuri, lazima awe na uwezo wa kutambua ubora wa chakula.

Kwanza: Atalazimika kutayarisha chakula ambacho kina lishe muhimu kwa mwili wa binadamu kufanya kazi inavyostahili.
Mtume (s.a.w) wa Mwenyezi Mungu alisema: “Wajibu wa mwanamke kwa mume wake ni kuwasha taa ndani ya nyumba na kutayarisha chakula kizuri na kinachofaa.”

Mwanamke alimuuliza Mtume (s.a.w) wa Mwenyezi Mungu: “Ni thawabu nzuri kiasi gani zinazomngoja mwanamke anayetimiza wajibu wake kwa

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 105

mume wake?" Mtume (s.a.w) alisema: "Kwa kila shughuli anayoifanya ambayo inahusu mambo ya familia, Mwenyezi Mungu humtazama kwa jicho la wema, na yeyote anayefurahia neema za Mwenyezi Mungu hatateswa."

Pili: Mahitaji ya chakula ya watu hutofautiana. Umri, saizi ya mwili na vipengele vingine hubainisha kiwango cha mahitaji yetu ya lishe. Mathalani mtoto ambaye anakua huhitaji kalisi/chokaa zaidi ikilinganishwa na mahitaji ya madini ya aina hiyo ya mtu mwenye umri wa utu mzima. Vijana wanahitaji lishe yenye kuongeza nguvu zaidi kwa sababu wana shughuli nyingi zaidi.

Kazi ya mtu pia ni kipengele kinachobainisha aina ya chakula ambacho mtu anatakiwa kula. Mathalani, anayefanya kazi ngumu anahitaji chakula cha mafuta zaidi, sukari na wanga kwa sababu anashughulika sana.

Hali ya hewa ni kipengele kingine. Mahitaji ya lishe yetu kutofautiana kufuatana na msimu wa joto na baridi. Pia mtu mgonjwa chakula chake hutofautiana na kile cha mtu mwenye afya njema. Mpishi mzuri lazima akumbuke mambo yote haya.

Tatu: Ni kweli kwamba mtu anapofika umri wa miaka arubaini na zaidi, upo uwezekano wa kunenepa. Labda baadhi ya watu huona kuwa na kitambi ni dalili ya afya njema, lakini fikra hiyo si sahihi. Kuota kitambi ni ugonjwa ambao unaweza kusababisha athari mbaya sana kwenye moyo, shinikizo la damu, mafigo, kibofu cha nyongo, ini, na huweza kusababisha maumivu kifuani na kisukari.

Takwimu kutoka kwenye vyanzo vya tiba na kampuni za bima hushauri kwamba watu wembamba huishi kwa muda mrefu kuliko wanene.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 106

Baada ya miaka arobanini, mtu hupunguza shughuli kwa hiyo anahitaji mafuta, sukari na wanga kidogo. Kalori hazigeuzwi kuwa nishati kwa wingi kama mwanzo kwa hiyo huchangia mwili kunenepa. Kwa hiyo ni bora kupunguza kula vitu hivi.

Mwanamke anayejali afya ya mume wake anatakiwa amtengenezee lishe maalum ili asinenepe. Lazima apunguze kula vitu vitamu, vinono na, lakini azidishe kula mayai, ini nyama ya kuku, nyama isiyo na mafuta, samaki na jibini. Bidhaa za maziwa pia zinazo manufaa. Akiruhusiwa na daktari mtu mwenye uzito mkubwa anatakiwa kula matunda na mboga kwa wingi.

Kama umechoshwa na mume wako, kama unataka kuwa mjane, au kama unataka kumuua mume wako bila hatari ya kushtakiwa na polisi - basi unatakiwa kufanya jambo dogo tu. Mpe chakula kingi kitamu na cha kunenepesha. Mhimize ale mkate, wali na keki kwa wingi iwezekanavyo. Matokeo yake utamwondoa na si tu kwamba utakuwa mjane bali atakuwa amekushukuru kwa kumlisha vyakula vyote hivi vitamu.

Unaweza kushauri kwamba utaratibu wa aina hii unaweza kutekelezwa na watu matajiri ambao wanaweza kununua aina yoyote ya chakula wanachotaka. Unaweza kufikiria haiwezekani kwa watu wasio matajiri kuweka utaratibu kama huu.

Lakini mtu asisahau kwamba manufaa yote ya lishe yamejificha kwenye vyakula rahisi vya kawaida. Mwanamke ambaye amejifunza kuhusu mapishi atakwambia kwamba mtu anaweza mahitaji yote ya lishe ya mwili kutoka kwenye vyakula kama vile matunda, nafaka, mboga na bidhaa za maziwa.

Mtu anaweza kupika mlo kwa viambato hivi ambavyo vinaafikiana na elimusiha, afya na bila gharama.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 107

KUPOKEA WAGENI

Mojawapo ya kazi isiyoepukika ya kila familia ni kuwafurahisha wageni wakati moja au mwingine. Hii ni mila inayofurahisha kwani matokeo yake ni kwamba urafiki huwa karibu zaidi na watu husahau matatizo yao kwa kipindi kifupi. Kuwa na marafiki na ndugu ni jambo bora sana kwa kupitisha muda.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Riziki ya mgeni huteremka kutoka mbinguni na baada ya kuliwa, dhambi za Mwenyeji husamehewa."

Imam Raza (a.s) alisema: "Mtu mwema hula chakula alichopewa na wenzake ili na wao wale chakula chake. Lakini mtu bahili hatakula chakula alichopewa na wengine kwani wasije kula chakula chake."

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema: "Ushirikiano na marafiki husababisha wema (miongoni mwao)."

Imamu Muhammad Taqi (a.s) alisema: "Kushirikiana na marafiki hukomaza akili ya mtu kuchangamsha moyo wa mtu hata ni kidogo tu."

Kwenye bahari ya maisha yenye ghasia, roho ya mtu huhitaji utulivu, na amani ya akili inaweza kupatikana mtu anapokuwa na marafiki zake. Watu husahau matatizo yao wakati wapo kwenye mkusanyiko wa kirafiki si tu urafiki unaweza kuimarika, lakini unaweza kutia nguvu hamasa yake.

Kukirimu wageni ni desturi njema na mara chache mtu anaweza kukanusha sifa zake lakini yapo matatizo mawili humo ambayo huyafanya familia zingine kusita kushiriki kwenye mila hii ya muda mrefu.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 108

Kwanza: Vitu vya anasa na kuonana ana kwa ana vimefanya maisha ya wengi kuwa magumu miongoni mwa wengi wetu. Bidhaa za familia ambazo kazi yake ni kuhudumia faraja yetu zimegeuka kuwa namna ya maonesho kwa wengine na majivuno. Hivyo, watu wamepunguza nyakati za kushirikiana na wengine. Licha ya kwamba wengi ambao wapo tayari kukusanyika, hukataa kufanya hivyo, kwa sababu wanayo fikira potofu kwamba hawana vitu vingi vya anasa nyumbani kwao, kwamba ni vema wakae mbali na wengine na wajiokoe na aibu. Tafakari ya namna hii huharibu hali ya mtu baada ya maisha ya hapa duniani, pia humweka katika hali ngumu katika dunia hii.

Bibi mpendwa! Hivi marafiki zako hukutembelea nyumbani ili waone vitu vyako vya anasa? Kama ndivyo, washauri waende kwenye maduka yanayouza vitu hivyo na majumba ya makumbusho badala ya kukutembelea wewe. Kushirikiana na watu wengine inamaanisha kuongeza urafiki na watu wengine pamoja na kufurahi nao. Maana yake si kujionesha au kujaza tumbo la mtu. Kila mtu anachukizwa na uanasa na mashindano ya aina hiyo. Lakini hawathubutu kuitupa mila hii yenye makosa.

Kama ulikuwa tayari kuwakirimu wageni wako kwa jinsi iliyo rahisi, ungeona kwamba wangekufuata. Kwa njia hii unaweza kushirikiana na marafiki zako kwa urahisi na bila usumbufu mkubwa. Hivyo, ufumbuzi wa tatizo hili ni rahisi. Badala ya kujaribu kulinganisha vyombo vyako na vile vya wengine, fanya juhudi kuzidisha nguvu ya mshikamano wa urafiki na wao kwa kuwafanyia wema.

Mbili: Tatizo lingine ni kuhusu kukirimu wageni wako. Mama wa nyumbani anajisumbua kutengeneza chakula cha wageni wachache kwa muda wa saa chache. Wakati mwingine mwanamke hawezi kutayarisha chakula kitamu, ambacho kitamtibua mume baadaye. Mume wake anaweza kuonesha kutokupendezwa na mapishi yake. Kwa hiyo, karamu

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 109

zingine hufuatana na wasi wasi, wa wanandoa wenyeji na matokeo yake ni kwamba watu wanakuwa na mazoea ya kutokutayarisha karamu.

Kama mambo yalivyo, ni kweli kwamba kutayarisha karamu si jambo rahisi, lakini tatizo kubwa zaidi ni kutokeza pale ambapo mama wa nyumba hana ujuzi wa kutosha kuhusu namna ya kuwakirimu wageni wake.

Kuwakirimu wageni inakuwa rahisi kama mtu yupo tayari kujifunza ustadi muhimu. Hapa ni mifano miwili inaoneshwa unaweza kutumia wowote utakaopenda wakati wa kuwakirimu wageni wako:

Mfano wa (a) mwanaume anamtaarifu mke wake kwamba Ijumaa usiku kuna marafiki zake kumi watakuja kula chakula cha jioni.

Mke wake ambaye amepata kukutana na tukio lisilopendeza kwenye karamu zilizopita, ghafla hukasirika na kumpinga mume wake. Baada ya mazungumzo ya kina na mume kumwomba mke wake, hukubali kwa kusita kutayarisha chakula usiku kwa ajili ya wageni wake. Wanapitisha siku zao katika hali fulani ya wasi wasi na shauku hadi siku ya Ijumaa.

Siku hiyo ya Ijumaa mmojawapo anakwenda kununua vitu. Anakumbuka vitu vya muhimu vya kununua na baada ya kununua vitu vichache anarudi nyumbani.

mama wa nyumbani huanza kazi yake baada ya chakula cha mchana. Ghafla anakutana na matatizo mengi. Anatakiwa apike, aoshe vyombo, afagie, afute vumbi, apange chumba cha wageni na kadhalika. Pia, anatakiwa afanye yote haya yeye mwenyewe au mtu mmoja tu wa kumsaidia. Anaanza kushughulika akiwa na wasi wasi sana. Anatafuta kisu cha kukata vitunguu, anatafuta chumvi kila mahali na kadhalika. Anatambua kwamba hakuna hata nyanya moja hapo nyumbani kwa hiyo

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 110

anamtuma mtu kwenda kununua. Lazima sasa akaange nyama, aloweke mchele, aoshe mboga… na kadhalika.

Mke anakuwa na hamaki na fadhaa na halafu anamuita mtumishi kwa kelele, anamlaani mtoto wake wa kike, anampiga mtoto wake wa kiume na halafu anaishiwa gesi au mafuta ya taa. "Ee Mungu! Nitafanyaje?"

Ghafla kengele ya mlangoni inagonga wageni wamefika! Wanafika moja baada ya mwingine. Mume ambaye anatambua wasi wasi wa mke wake, anawakaribisha wageni ndani ya nyumba na kuwapeleka kwenye chumba cha wageni. Sasa anataka kuwahudumia kwa kuwapa chai, lakini haijawa tayari. Anamwita binti yake au mtoto wake wa kiume kwa kupiga kelele akihoji kwa nini birika la chai halijawekwa kwenye jiko. Chai inapokuwa tayari, anagundua kwamba hakuna sukari ya kutosha. Baada ya kununua sukari nyingine ya nyongeza, anachukua vikombe vichache vya chai na kuwapelekea wageni. Anawatazama wageni lakini akili yake ipo jikoni. Anajua nini kinachoendelea hapo. Hawezi kukaa kwa raha au kuzungumza na wageni kwa amani. Ana wasi wasi kuhusu chakula. Inakuwa mbaya zaidi endapo miongoni mwa wageni wapo wanawake ambao wanauliza kila mara kuhusu mama wa nyumba. Mwanaume lazima ajibu kwamba mke wake anashughulika na mapishi na baada ya muda mfupi atatokea na kuwa nao.

Mke, mara kwa mara anakwenda kwa wageni lakini hawezi kuketi na kuwa nao. Wakati anaomba msamaha kutoka kwao kwa mara ngingine anarudi jikoni. Haiwezekani mke kutayarisha chakula kitamu hasa katika hali kama hii.

Mara chakula kikiwa tayari, lazima atafute vyombo, atangeneze kinywaji, lazima atafute vyombo atenge vinywaji, atafute gilasi ajaze pilipili na chumvi kwenye vitikiso na kadhalika.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 111

Baada ya wageni kula chakula chao hatimaye wanaaga 'kwa heri' kwa wenyeji wao na kuondoka.

Hitimisho: Ama chakula kilikuwa na chumvi sana au hakina chumvi, kiliungua au kuliwiva nusu. Pia baadhi ya vitu labda vilisahauliwa na mama mwenye nyumba na kwa hiyo havikuwekwa mezani ili viliwe na wageni.

Sasa ni katikati ya usiku na mke amechoka. Amekuwa hana hata dakika ya kupumzika tangu adhuhuri. Pia hakuweza kuwahudumia wageni inavyostahili.

Mume amekuwa na wasi wasi sana ametumia fedha nyingi sana kwa karamu lakini jioni hiyo haikumfurahisha inawezekana hata akamlaumu mke wake.

Wana ndoa, si tu kwamba hawakufurahia karamu, lakini inaezekana pia kwamba watakuwa na mabishano kuhusu suala hili na inawezekana hata wasitengeneze karamu tena.

Wageni hawakufurahia karamu, kwa sababu walihisi kwamba walisababisha usumbufu mkubwa kwa wenyeji wao na labda walitamani kwamba hawangekuja kabisa.

Bila shaka, wasomaji hawangependa hali kama hiyo na hawangekuwa tayari au kuwa radhi kupitia kwenye hali kama hii.

Unajua chanzo cha tatizo hili? Vema, sababu halisi, moja tu ni mke kutokuwa na uzoefu na ujuzi kuhusu jinsi ya kukirimu wageni wake. Vingenevyo, kutayarisha karamu si kazi ngumu kiasi hicho.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 112

Sasa chaguo la pili:
Mfano (b), mwanamume anamwambia mke wake kwamba marafiki kumi miongoni mwa marafiki zao watakuja kula chakula cha usiku Ijumaa. mke anakubali kwa kusema: "Sawa kabisa, tutayarishe nini chakula cha usiku siku hiyo?"

Wanandoa hawa wanaamua kuhusu jambo hili wote pamoja na wanaorodhesha vitu vyote vya muhimu kwa maandishi. Wanaangalia kwa makini mahitaji yao kwa mara nyingine na kwa kuweka alama vile vitu ambavyo tayari wanavyo nyumbani, wanaandika orodha nyingine ya vitu vinavyotakiwa kununuliwa.

Siku ya Alhamisi, siku moja kabla ya karamu, wanamaliza baadhi ya kazi kama vile kukata vitunguu, kuosha viazi, kuweka chumvi na pilipili mahali pake, kutayarisha vyombo vya mezani na kadhalika.

Siku ifuatayo, asubuhi, mama wa nyumba baada ya kustaftahi, anafanya baadhi ya kazi zake kama kuosha, kukata na kukaanga nyama, nyama ya kuku na viazi. Baada ya chakula cha mchana anaweza kumpumzika na baadaye anamalizia kazi zilizobakia.

Kwa hiyo anaweza kumaliza kazi yote ya mapishi, kupanga nyumba ionekane nadhifu bila ya mkurupuko au wasi wasi. Kusingekuwa na mabishano yoyote au kuchanganyikiwa.
Angekuwa na muda wa kutosha wa kutayarisha chai baada ya wageni kuwasili. Anaweza kuwakaribisha wageni akiwa na mume wake na hata kuketi na kuzungumza nao. Angekwenda jikoni kwa sababu ya kuhakikisha kila kitu kinakwenda kama ilivyo pangwa.

Anaweza kumuomba mume wake na watoto kumsaidia kutenga chakula mezani. Kwa hiyo, kila mtu angeweza kufurahia chakula chao kitamu kwa starehe.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 113

Hitimisho: Wageni wamefurahia fursa ya kuwa na wenyeji wao. Wamezungumza na urafiki wao umezidi kuwa imara. Wamefurahia mlo na wamevutiwa na uwezo wa mama mwenye nyumba wa kuwakirimu wao. Hatimaye, wamefurahia jioni ambayo wangeikumbuka kwa muda mrefu ujao.

Mume ameweza kushirikiana na wageni. Amekuwa na muda mzuri na marafiki zake na amefurahi mke wake hakumshusha hadhi. Wametiwa moyo wa kuendelea kuwaalika marafiki zao mara kwa mara.

Hatimaye, mwanamke ambaye kwa uvumilivu na ujuzi wake, ameweza kuwakirimu wageni kama kawaida na bila ya tatizo, ameridhika na alivyo fanya. Anahisi furaha na mume wake na amethibitisha kwamba yeye ni mama wa nyumba bora.

Sasa unaweza kuchagua kufuata mfano wowote kati ya hiyo miwili.

MDHAMINI WA NYUMBA

Kwa kawaida wanaume ni wafadhili wa familia. Hufanya bidii na hutumia mapato yao kwa wake zao na watoto wao. Wanaona huu ni wajibu wao na hawako tayari kuonesha kutokupendezwa na tatizo hili.
Lakini pia wanaume wanategemea wake zao kutumia fedha zao kwa uangalifu na si kwa kufuja. Wanawake wanategemewa kuainisha mahitaji muhimu na kutumia fedha zao kwa uangalifu na si kwa kufuja. Wanawake wanategemewa kuainisha mahitaji muhimu na kutumia fedha kwa ajili ya vitu kama chakula, nguo, dawa, pango la nyumba, umeme, simu, moto wa gasi na maji. Kuweka vitu kama hivyo kama mahitaji ya anasa katika orodha ya vitu muhimu hufikiriwa kuwa ni ufujaji. Wanaume hawapendi wake zao kutumia vibaya fedha zao katika kununua vitu visivyo vya muhimu au matumizi yanayo zidi kiasi.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 114

Kama mwanaume anamuona mke wake mwaminifu katika kutunza fedha yake, kama anao uhakika, mke wake hatumii fedha kupita kiasi na kama anao uhakika kwamba fedha yake inayo patikana kwa shida haipotei bure, kwa hiyo, atafanya bidii zaidi na hatafuja fedha zake.

Kwa upande mwingine, kama mwanamke hutumia fedha za mume wake kununua nguo zake na mapambo yake au kama mke anatumia fedha katika kununua vitu visivyo muhimu na hadi waanze kukopa ili waweze kukidhi maisha, au kama familia, kama adui kafiri, hufuja utajiri wake basi mwanaume atakata tamaa. Hatapendelea kufanya kazi na kufadhili familia yake. Atadhani hakuna mantiki ya kufanya kazi na kusaidia watu ambao hawavutiwi na juhudi zake. Anaweza hata kukengeuka na kufuata njia yenye uovu. Tabia ambayo inaweza kuvunja misingi ya familia.

Bibi Mpendwa! Licha ya kwamba fedha za mume wako zimo katika utumiaji wako, usifikirie kwamba ni zako binafsi. Utajiri huo ni wa mumeo kisheria na wewe ni mdhamana. Kwa hiyo, kuchukua kitu chochote na kukifanya chako binafsi, kutoa kitu chochote, kutoa zawadi au kuuza kitu cha mumeo chochote, unahitaji ruhusa yake. Wewe unawajibika kwa mali ya mume wako na kwa vyovyote vile unatakiwa kuilinda. Ukikwepa wajibu wako, utakuwa na hoja ya kujibu Akhera.

“Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: “Mwanamke ni mlinzi na mdhamini wa mali ya mume wake na katika hali hiyo anawajibika.”

“Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) pia alisema: Mwanamke bora kuliko wote miongoni mwa wanawake wenu ni yule anayejipuliza manukato, hutayarisha chakula kitamu na hatavuka mpaka katika matumizi. Mwanamke wa aina hii ni mwakilishi na yu katika kundi la wafanyakazi wa Mwenyezi Mungu na mtu anayefanya kazi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kamwe hatapatwa na majuto au kushindwa.”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 115

"Mwanamke alimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w): "Ni zipi haki za mume kwa mke wake?" Mtume (s.a.w.w) alisema: "Mke lazima awe mtiifu kwa mumewe, asikiuke amri zake na asitoe kitu chochote bila ya ruhusa yake."

Mtume wa Mwenyezi Mungu pia alisema(s.a.w.w): "Mwanamke bora kuzidi wote baina ya wanawake zenu ni yule anayetumia fedha kwa uangalifu."

KAZI ZA WANAWAKE

Ni sahihi kwamba kutafuta na kupata kipato cha familia ni wajibu wa mwanaume na kwamba wanawake hawaruhusiwi na sheria ya Kiislamu kuwajibika kwa kitendo hiki. Hata hivyo, wanawake pia wanatakiwa kufanya kazi. Katika Uislamu kukaa bure ni fedheha na hukemewa.

Imam Sadiq (a.s) alisema: "Mwenyezi Mungu Mweza wa yote anachukia kulala sana na kupumzika sana."

Imam Sadiq (a.s) pia alisema: "Kulala sana hupoteza na kuharibu maisha ya mtu hapa duniani na Akhera."

"Hadhrat Zahra (a.s) pia alikuwa akifanya kazi nyumbani"

Mtu yeyote mwenye kuhitaji na asiye hitaji, anatakiwa kuwa na kazi. Asipoteze bure maisha yake kwa kutofanya lolote, lakini anatakiwa kufanya kazi na kutoa mchango wake katika kujenga dunia iliyo bora.

Kama ni muhimu, mtu anatakiwa kutumia kipato chake kwa ajili ya familia yake na yeye mwenyewe, lakini kama kipato hicho hakihitajiki basi atoe msaada kwa wale wanao hitaji. Kukaa bure huchosha na mara nyingi husababisha maradhi ya kiakili na kisaikolojia na pia ufisadi.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 116

Kazi iliyo bora zaidi kwa wanawake walioolewa ni kutunza nyumba. Utunzaji wa nyumba na watoto na kadhalika ni kazi nzuri na rahisi zaidi ambazo zinaweza kufanywa na wanawake.

Mwanamke aliyeolewa mwenye kipaji na bidii kwenye kazi anaweza kuibadili nyumba yake na kuwa mahali pa Pepo kwa watoto na mume wake; na hii ni kazi inayofaa na yenye thamani.

Mtume (s.a.w.w) alisema: "Jihadi ya mwanamke ni hapo ambapo humwangalia na kumtunza mume wake vema."

Umm-e-Salamah alimuuliza Mtume (s.a.w.w.w): "Ni thawabu kiasi gani zimekadiriwa kwa kazi ya nyumbani kwa mke wa mtu?" Mtume (s.a.w.w) alijibu: " Mwanamke yeyote ambaye anaipanga nyumba ionekane nadhifu, anachukua kitu fulani kutoka mahali fulani na kukiweka mahali pengine atafurahia neema za Mwenyezi Mungu, na mtu yeyote mwenye mvuto wa neema za Mwenyezi Mungu, hatateswa na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu."

Umm-e-Salamah akasema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Wazazi wangu na watolewe muhanga kwa ajili yako, tafadhali taja thawabu zingine kwa ajili ya wanawake." Mtume (s.a.w.w) alisema: "Mwanamke anapokuwa mja mzito, Mwenyezi Mungu humpa yeye thawabu nyingi kama zile ambazo angepata mtu anayepigana vita vya Jihadi kwa kutumia utajiri wake na uhai wake. Halafu mwanamke anapojifungua mtoto wake, wito humfikia na kusema, 'dhambi zake zote zimesamehewa; anza maisha mapya tena.' Kila anapomnyonyesha mtoto wake maziwa yake, Mwenyezi Mungu humpa thawabu sawa na zile anazompa mtu anapomwacha huru mtumwa katika kipindi anacho mnyonyesha."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 117

Hata hivyo, hata wanapokuwa hawashughuliki na kazi za nyumbani, wanatakiwa kutafuta kitu cha kufanya, wanaweza kusoma vitabu, kufanya utafiti wa kitu chenye manufaa, ili wajiongezee ujuzi na kustadi wao. Wanaweza kuandika makala na hata vitabu. Wanaweza kuwa wachoraji, mafundi wa kupaka rangi, ufundi cherehani na kadhalika. Matokeo yake ni kwamba wanaweza kusaidia familia zao kiuchumi na pia kutoa mchango kwa jamii yao kwa kudhihirisha mafanikio yao kwa umma.

Kufanya kazi huzuia kuendelea kuwepo kwa maradhi ya akili.

Imam Ali (a.s) alisema: "Mwenyezi Mungu humpenda mchamungu ambaye kwa uaminifu anajishughulisha na kazi."

Wakati ambapo baadhi ya wanawake hufanya kazi nyumbani, wapo wengine ambao hupenda kazi ya nje. Upendeleo huu ama unaweza kuwa kwa sababu ya kiuchumi au zingine. Kwa vyovyote vile, kazi nzuri kuliko zote ni zile za kitamaduni au uuguzi. Shule za vidudu, msingi, sekondari na sehemu zinazofaa kwa wanwake kufundisha na kuongoza wanafunzi wanawake. Mahospitali pia ni sehemu ambazo zinafaa kwa wanawake kutoa huduma ya uuguzi na udaktari. Kazi kama hizi zinakubalika kwa maumbile ya kike; na pia mara chache sana, inapobidi wao kukutana na wanamume ambao si *mahram* (wanaume ambao sio ndugu wa karibu na ambao imeharamnishwa kufunga ndoa nao).

Yafuatayo ni mapendekezo kwa wanawake wenye nia au wanaofanya kazi nje ya nyumba zao:
Pata ushauri kutoka kwa mumeo kabla ya kuanza kufanya kazi. Ni haki ya mueo kukabali au kukataa kukupa ruhusa ya kufanya kazi. Kuanza kufanya kazi bila ruhusa ya mumeo inaweza kusababisha madhara kwenye mazingira tulivu ya kupendana katika familia yenu. Wanaume pia wanashauriwa kuwa wagumu kukubali wake zao kufanya kazi nje ya nyumba zao, isipokuwa kazi husika iwe haifai kwa wanamume.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 118

Wanawake lazima wawe waangalifu kuhusu vazi la Hijabu ya kiislamu wanapokuwa nje ya nyumba zao. Lazima waende kazini bila kujipodoa na wavae nguo zisizo na urembo. Lazima waepuke kuchanganyika na wanaume ambao si *mahram* kwao kadiri iwezekanavyo. Ofisi ni mahali pa kazi si mahali pa kujionesha au mashindano. Sifa njema na heshima ni sifa zisizoletwa na kivazi chako, lakini husababishwa na matendo yako, na matendo hayo unayafanua vema kiasi gani. Matendo yako yawe kama mwanamke wa kiislamu anaye heshimika. Dumisha tabia ya kujiheshimu mwenyewe, na usiziumize hisia za mume wako; mapambo yako na nguo zako nzuri sana, vaa unapokuwa nyumbani kwa ajili ya mume wako.

Wanawake wanatakiwa kuwa na tahadhari kwamba licha ya wao kufanya kazi nje ya nyumba zao, bado wanategemewa na waume zao na watoto wao kutoa huduma za shughuli, kama utunzaji wa nyumba, kupika, kufua na kadhalika. Shughuli hizi zinaweza kufanywa kwa ushirikiano wa kifamilia. Kazi ya nje ya nyumba isiwe sababu ya kuitibua familia yote. Wanaume pia wanashauriwa kuwasaidia wake zao kuhusu utunzaji wa nyumba. Waume wasiwategemee wake zao kufanya kazi nje na nyumbani pake yao. Matumaini ya aina hii wala si halali ama haki. Wanaume na wanawake lazima wagawane kazi za nyumbani.

Kama mwanamke, ambaye anafanya kazi nje ya nyumba anaye mtoto, basi anatakiwa amwache mtoto kwenye shule ya chekechea au mtu anayeaminika na mwema. Wala si haki au busara kuwaacha watoto nyumbani bila mtu wa kuwatunza, kwani watoto wengi huwa waoga au kujihisi hawana msaada wanapo kabiliana na hali ya hatari.

Kama mwanamke anahisi kwamba, zaidi ya kazi zilizotajwa hapo juu na wajibu uliotajwa hapo juu, lazima afanye kazi nyingine, basi ni lazima aelewane na mume wake wazi wazi na aanze kufanya kazi hiyo kwa ruhusa yake na ushauri wake. Kama mume atakataa, mke lazima aache mpango

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 119

huu. Kama mume atakubali mke wake afanye kazi, lazima achague kazi ambayo itamkutanisha na wageni wanaume wachache sana. Hii ni kwa manufaa yake na jamii. Kwa vyovyote vile, anapokuwa nje ya nyumba yake, lazima awe makini kufuata kanuni za vazi la kiislamu la Hijabu na asijipodoe kabisa.

USIPOTEZE MUDA WAKO WA AKIBA

Kazi za nyumbani huwa za aina nyingi mbali mbali. Kama mke anayo nia ya kufanya kazi kwa ubora zaidi hatoweza kuwa na muda wa kutosha wa kufanya kitu kingine. Huu ni ukweli hususan ambapo pia mama wa nyumbani anatakiwa kuwatunza watoto. Lakini wanawake walio wengi ambao wameolewa hupata muda wa akiba.

Kila mtu hutumia muda wake wa akiba kwa njia moja au nyingine. Wanawake wengine hupoteza muda wao wa akiba. Wanaweza tu kutembea mtaani au anazungumza na mwanamke mwingine. Mara nyingi mazungumzo yao ya saa chache hayana thamani yoyote. Wanaweza kusikiliza maneno ya kurudia rudia ambayo huthibitisha ni ya kupoteza muda na fadhaa. Porojo za bure kama hizo husababisha kuvunjika heshima na maadili. Wanawake wanaopitia maisha ya namna hii, hakika wanapata hasara katika dunia hii na ile ijayo. Ni ajabu ilioje kwamba kama mtu yeyote anapoteza fedha, anatibuka sana, lakini watu hawafikirii hata kidogo kuhusu kupoteza muda wao wenye thamani katika maisha yao.

Mtu mwenye busara hujitahidi sana kutumia saa zenye thamani za maisha yake kwa manufaa. Ni mafanikio ya thamani kiasi gani mtu anaweza kuwa nayo!

Uvivu una madhara na husababisha maradhi ya akili na kuchanganyikiwa. Mtu mvivu wakati wote huwa katika mawazo na hutafuta njia za kuhisi

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 120

huzuni. Hupata aina nyingi za wasi wasi na baadaye akili yake huvurugika. Mtu mwenye furaha ni yule ambaye wakati wote anashughulika kufanya kitu fulani. Mtu mwenye bahati mbaya ni yule ambaye ni mvivu sana na hutumia muda wa ziada wa kutosha kufikiri raha na taabu za maisha yake. Kujishughulisha ni jambo la kufurahisha na uzembe ni chanzo cha mfadhaiko.

Je, si jambo la kusikitisha kwamba mtu anaweza kupoteza maisha yake yenye thamani au kutumia kiasi cha muda wake bila kunufaika kwa namna yoyote?

Bibi mpendwa! Unaweza kutumia kwa manufaa makubwa muda wako wa akiba. Unaweza kufanya kazi za kisayansi. Unaweza kununua vitabu vinavyo husiana na taaluma hiyo na kwa msaada wa mume wako, utaongeza ujuzi. Masomo ya kozi yoyote inawezekana, fizikia, kemia, Qur'ani, falsafa, historia, fasihi, saikolojia na kadhalika. Ungefurahia muda huo na labda siku moja ungetoa mchango wako kwa jamii kwa ujuzi wako. Unaweza kuandika makala au hata vitabu ambapo baadaye jina lako litaendelea kudumu. Pia unaweza kujipatia fedha.

Usidhani ya kwamba wanawake wote mashuhuri katika historia wanakuwa wakizembea. Wao pia waliolewa lakini ni hao ambao hawakupoteza bure muda wao wa akiba.

Bibi Dorothy Carnegie, alikuwa ameolewa na ambaye aliandika kitabu kizuri. Alikuwa akifanya kazi za nyumbani na pia alimsaidia mume wake (Dale Carnegie) kuandika kitabu chake maarufu; "How to make friends and Infuluence People." Ameandika kwenye kitabu chake kuhusu kanuni za kumtunza mume: "Nimeandika kitabu hiki wakati mwanangu anapolala kwa muda wa saa mbili. Nilikuwa nasoma sana wakati ambapo nywele zangu zilikuwa zinakaushwa kwenye chumba cha kutengeneza nywele."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 121

Wapo wanawake wengi ambao wameandika vitabu maarufu wanapata mafanikio mengi katika uwanja wa sayansi.

Kama wewe ni mtu mwenye shauku, ungekuwa mmojawao. Kama mume wako ni mtafiti basi msaidie katika taaluma yake. Je, si jambo la kusikitisha kwa mwanamke msomi kutokutumia ujuzi wake wote?

Imamu Ali (a.s) alisema: "Hakuna hazina iliyo bora zaidi ya ujuzi."

Imamu Baqir (a.s) alisema: "Yeyote anayetumia mchana na usiku kwa kutafuta ujuzi, kwa hakika ataunganishwa na neema za Mwenyzi Mungu."

Kama wewe hupendelei kusoma au kutafiti basi jishughulishe na kazi za mkono au uchoraji kama kushona nguo, kupaka rangi, kufuma, mapambo ya maua, na kadhalika.

Unaweza kujifunza sanaa za aina hii na kuzifanyia mazoezi. Itikadi hizi zinaweza kukusaidia kiakili na kiuchumi. Uislamu pia umependekeza kazi za mikono zifanywe na wanawake wakati wa muda wao wa akiba. "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Kusokota na kufuma ni burudani nzuri kwa wanawake."

UMAMA (UTUNZAJI WA WATOTO)

Mojawapo ya wajibu wa wanawake ni kutunza watoto wao. Hii si kazi rahisi lakini ni nyeti na muhimu. Ni wajibu wenye heshima na thamani kubwa uliowekwa kwa wanawake kwa amri ya muumbo. Yapo mambo machache ambayo yametajwa hapa kuhusu suala hili:
Tunda la Ndoa - licha ya kwamba mwanaume na mwanamke wanaoana kwa sababu chache kama vile kwa sababu ya ushawishi wa kijinsia, mapenzi na kadhalika, kupata mtoto si sababu mojawapo muhimu ya ndoa.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 122

Lakini huwa haipiti muda mrefu kabla ya nia ya kweli ya maumbile ya asili kudhihirika na mapenzi ya kupata mtoto hukua ndani ya nyoyo zao. Kuwepo kwa mtoto ni tunda la mti wa ndoa na matamanio ya asili ya wanaume na wanawake. Ndoa isiyokuwa na mtoto ni sawa na mti usiokuwa na tunda. Mtoto huimarisha mfungamano wa mapenzi baina ya wanandoa. Huwa kama msukumo kwa maisha ya mwanamume kufanya kazi na hutia moyo wazazi kutunza familia yao.

Wakati mwingine ndoa hutokana na matamanio ya kijinsia ya papo kwa papo. Msingi wa aina hiyo si sahihi na haudumu na kila mara huelekea kwenye uharibifu. Kipengele kinachoimarisha msingi huu ni kuwepo kwa mtoto. Matamanio na msukumo wa kijinsia hufifia haraka sana. Kumbukumbu moja tu inayoendelea kuwepo kuhusu matamanio ya kijinsia ingekuwa watoto, ambao kuwepo kwao huchangamsha nyoyo za wazazi.

Imamu Sajjad (a.s) alisema: “Furaha ya mtu ni kupata watoto wachamungu ambao anaweza kupata msaada kutoka kwao.”

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: “Mtoto mcha Mungu ni mmea unao nukia harufu tamu kutoka miongoni mwa mimea ya Peponi.”

Mtume (s.a.w.w) alisema: “Ijumlishe kwenye idadi ya watoto wenu, kwa sababu mimi, Siku ya Hukumu, nitahisi nimeheshimiwa kuhusu ukubwa wa idadi yenu kuzidi umma zingine.”

Ni wajinga kiasi gani wale ambao, wakiwa na udhuru mbali mbali hukataa kupata watoto, na hivyo hupinga kanuni ya uumbaji!

Kumwelimisha mtoto: Wajibat ambazo ni nyeti kuliko zote za mama ni kazi ya kumwelimisha mtoto na kuwaelekeza. Licha ya kwamba wazazi

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 123

wote wawili wanatakiwa kugawana wajibu huu, uzito mkubwa zaidi upo kwa mama. Hii ni kwa sababu mama anao uwezo wa kumlinda na kumfuatilia mtoto wakati wote. Kama mama, kwa kupitia kwenye utaratibu ulio sahihi hujaribu kulea watoto wao, halafu taifa lote na hata dunia ingepita kwenye mabadiliko ya kimapinduzi. Hivyo, maendeleo au kutokuendelea kwa jamii ni mambo ambayo yapo mikononi mwa wanawake. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Pepo iko chini ya nyayo za mama." Watoto wadogo wa leo ndio wanaume na wanawake wa kesho. Masomo yoyote wanayo jifunza sasa, watayafanyia mazoezi katika jamii zijazo. Kama familia zinaendelea, jamii itaendelea kwa sababu jamii itaendelea kwa sababu jamii ni mkusanyiko wa familia nyingi. Dunia ya kesho itaumia kwa sababu ya kuwepo watoto wenye hasira, jeuri, wajinga, woga, wapenda dunia, wabaya, wazembe, wachoyo na katili.

Kinyume chake dunia ya kesho itafaidika kwa sababu ya kuwepo leo watoto ambao ni waaminifu, wenye tabia njema, wema, jasiri, wapenda haki, wa kutegemewa na kadhalika.

Kwa hiyo, kwa ujumla, wazazi na hasa zaidi mama wanao wajibu kwa jamii zao. Wanaweza kuhudumia jamii zao kwa kulea na kukuza watoto wachamungu. Kwa upande mwingine, uzembe katika utekelezaji wa wajibu wao utahojiwa Siku ya Hukumu.

Imamu Sajjad (a.s) alisema: "Haki ya mtoto wako ni kwamba unatakiwa kutambua kwamba anatoka kwako. Awe mzuri au mbaya anao uhusiano na wewe. Wewe unawajibika kumlea, kumsomesha na kumuonesha njia inayo elekea kwa Mwenyezi Mungu na kumsaidia awe mtiifu. Unatakiwa kumshughulikia kwa namna ambayo kwamba ukimtendea wema, utakuwa na uhakika wa kupata thawabu na kama ukimfanyia ubaya, uwe na uhakika wa kuadhibiwa."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 124

Kama mambo yalivyo, si mama wote ambao wanatambua umuhimu wa stadi za kumwelekeza mtoto na ndio sababu wanatakiwa kujifunza na kuzijua stadi hizo.

Si katika eneo la kitabu hiki kuweka maelezo ya kina kuhusu malezi ya mtoto. Kwa bahati nzuri, vipo vitabu vingi ambavyo vimeandikwa na waandishi na wasomi kuhusu somo hili. Wanawake wanaweza kununua vitabu hivi na kwa msaada wa uzoefu wao wenyewe, wanaweza kuwaelimisha watoto wao na hata kuwa mabingwa katika fani ya malezi ya mtoto. Mama mmoja bingwa anaweza kuwasaidia mama wengine katika kazi zao kuhusu watoto wao.

Hapa linatakiwa kutajwa jambo moja. Watu wengi hufanya kosa kuhusu maneno mawili: 'elimu' na 'maelekezo,' au hudhani yana maana moja. Lakini mtu anatakiwa kujua kwamba kumfundisha mtoto masomo mbali mbali kama vile hadith zinazo faa, mashairi, Qur'ani, Hadith za Mtume (s.a.w.w) na Maimamu (a.s) si kumwelimisha. Masomo kama haya yanafaa lakini mtoto si tu ajifunze kuhusu watu waaminifu, lakini yeye mwenyewe anatakiwa kuwa mwaminifu.

Hivyo, lazima tutengeneze hali ya mazingira ya maisha ambayo mtoto kwa kawaida atakuwa mtu mwaminifu na mchamungu. Kama mtoto atakuwa mtu mwaminifu na mchamungu. Kama mtoto atakuwa kwenye mazingira ya uaminifu, ukweli, ujasiri, nidhamu, usafi, wema, upendo, uhuru, haki, uvumilivu kutegemewa, utiifu na kujitoa muhanga, basi hujifunza yote hayo. Kwa upande mwingine, mtoto anayepata makuzi akiwa katika mazingira ya uovu, udanganyifu, hasira, chuki, uaminifu na uasi hataepuka kuathiriwa na mambo hayo. Mtoto kama huyu anaweza kujifunza hadith nyingi, lakini hatanufaika nazo. Wazazi wasio waaminifu kulea na kukuza watoto waaminifu kwa kuwafundisha Qur'ani na Hadith. Mama na baba waovu kwa kweli humfundisha mtoto wao kuwa muovu. Mtoto huzingatia zaidi matendo ya wazazi wake na si maneno yao.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 125

Kwa hiyo, wale miongoni mwetu ambao wapo makini kulea watoto waaminifu na wema, lazima kwanza warekebishe tabia zao wenyewe. Hii ndio tu njia ya kumwelimisha mtoto anufaike yeye mwenyewe na jamii yake.

LISHE NA AFYA

Wajibu mwingine muhimu wa mwanamke aliye olewa ni kuwapa chakula watoto. Afya nzuri au ugonjwa, uzuri au ubaya, hata tabia njema au mbaya na ujanja wa watoto, vyote hivi vina uhusiano na lishe wanayopewa.

Watoto wana mpangilio tofauti wa kula kulinganisha na watu wazima.

Watoto wanayo mahitaji mbali mbali katika umri tofauti na kwa hiyo mama wanatakiwa kulifikiria jambo hili wanapo wapa chakula watoto wao.

Chakula kizuri sana na chenye kurutubisha sana ni maziwa. Maziwa yana kila kitu kinachohitajiwa kwa ajili ya mwili wenye afya. Hivyo, hakuna chakula kinachomfaa mtoto mchanga isipokuwa maziwa ya mama yake. Kwa kuwa maziwa yana viambato ambavyo vinafaa kwenye mfumo wa mmeng'enyo wa chakula wa mtoto mchanga, kwa hiyo hakuna matatizo ya kumlisha mtoto mchanga maziwa ya mama yake. Zaidi ya hayo, mama hahitaji kuchemsha, kuondoa, vijidudu au kuyasafisha kabisa maziwa hayo. Hakuna wasi wasi wa uhalisi wake.

Imamu Ali (a.s) alisema: "Hakuna chakula kizuri zaidi na kingi zaidi kuliko mazia ya mama kwa mtoto mchanga."

Daktari A.H. Mkuu wa Eastern Maditeranean Region of World Health Organization wa zamani alisema: "Mojawapo ya kipengele muhimu

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 126

ambacho husababisha mtoto apatwe na maradhi mengi ni kutokupata maziwa ya mama yake ambayo ndio tu bima ya maisha ya mtu."

Hivyo, mama wanao nyonyesha watoto wao maziwa yao lazima wakumbuke lishe muhimu kwa watoto wao imo kwenye maziwa hayo.

Lakini maziwa yenye lishe bora ni yale tu yanayotokana na lishe bora ya mama, ubora wa maziwa yake yanahusiana na ubora na wingi wa chakula cha mama. Mama akipata chakula bora zaidi ndivyo na maziwa yake yatakavyokuwa. Mama wanao wanyonyesha watoto wao maziwa yao, kutokana na uzembe wao kuhusu lishe bora wanaweza kuharibu afya zao na zile za watoto wao.

Baba wanaolea watoto wachanga pia wanao wajibu wa kuwapa wake zao chakula cha kutosha na kilicho bora. Utapiamlo ni tatizo kubwa kwa watu wengi kuboresha na mtu hatakiwi kudharau jambo hili au vinginevyo awe tayari kulipa, kugharamia tiba ya maradhi yanayosababishwa na hali hii.

Unaweza kupata taarifa ya kutosha kuhusu somo hili kutoka kwa daktari wako wa tiba au vitabu vinavyo husiana nalo. Lakini kama sharti la ujumla mama anaye nyonyesha anatakiwa kula aina zote za vyakula kuanzia nyama, matunda, vyakula vitokanavyo na maziwa… mpaka mboga za majani.

Ukweli ulio muhimu ni kwamba maziwa ya mama huathiri tabia ya mtoto na ndio sababu Imamu Ali (a.s) alisema: "Msichague wanawake wapumbavu kunyonyesha watoto wenu maziwa yao, kwa sababu maziwa hufanya asili ya ubora wao kupenyezwa kwa mtoto."

Imam Baqi (a.s) alisema: "Chagueni wanawake waungwana kunyonyesha watoto wenu maziwa yao, kwa sababu asili ya ubora wa maziwa unapitishwa kutoka kwa mnyonyaji hadi kwa mtoto."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 127

Lazima umnyonyeshe mtoto kwa vipindi. Mtoto wako hupata mazoea kutokana na ulinganifu huu na kumsaidia kuwa mvumilivu. Pia humsaidia kuhusu kuboresha mpangilio wa mmeng'enyeo wa chakula na tumbo. Kwa upande mwingine, kama utamnyonyesha mtoto kila anapolia basi, hatajifunza kuwa na nidhamu. Kama mtoto akizoea kupata atakacho kwa njia ya kulia basi ataichukua tabia hii na kuutumia hata atakapokuwa mtu mzima.

Hatakuwa na umuhimu wa kuvumilia atakapo kabiliwa na shida. Ama atatumia nguvu ili afanikishe matamanio yake au atafadhaika akipatwa na matatizo.

Usidhani kwamba kumfundisha mtoto nidhamu ni kazi ngumu. Lazima uwe mvumilivu na utaratibu unaofaa wa kumwelekeza kufuatana na kiwango chako. Wataalam wa lishe ya mtoto wanasema kwamba mtoto mchanga lazima anyonyeshwe kila baada ya saa tatu au nne.

Mpakate mtoto unapomnyonyesha. Kwa kumkumbatia mtoto anahisi mapenzi yako na inaweza kuathiri hata utu wake. Usimnyonyeshe mtoto mchanga wakati umelala chini kwa sababu imeonekana kwamba mama wengine hulala usingizi wakati wa kunyonyesha na matokeo yake watoto wengine wamekosa hewa kwa sababu matiti ya mama zao yaliwazuia kupumua.

Kama wewe mwenyewe huna maziwa kabisa unaweza kutumia maziwa ya ng'ombe ni mazito zaidi ya binadamu, pia lazima uongeze maji kiasi fulani. Pia unaweza kutumia maziwa yaliyosafishwa, ambayo lazima uyachemshe kwa muda wa dakika ishirini au hadi yanapokuwa salama kutumiwa na mtoto.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 128

Usimnyonyeshe mtoto mchanga maziwa ya baridi au moto, lakini yanatakiwa yawe na joto sawa na yale ya binadamu.

Kila baada ya kunyonya lazima chupa na nyonyo zichemshwe kwenye maji na uangalifu wa ziada lazima ufanywe wakati wa majira ya joto. Uwe mwangalifu usitumie maziwa yaliyobakia au yaliyochacha. Ni vema kupima wingi wa maziwa katika kila kipindi cha kunyonya ili kuhakikisha kwamba mtoto wako anapata maziwa ya kutosha.

Katika kutumia maziwa ya unga unatakiwa upate ushauri kutoka kwa bingwa wa magonjwa ya watoto. Kila mara lazima utumie maziwa ya unga mapya.

Baada ya mwezi wa nne wa umri wa mtoto, unaweza kuanza kumyonyaesha maji ya matunda. Baada ya umri wa miezi sita, pia unaweza kuanza kumlisha vyakula vikavu na supu. Unaweza kumlisha bisikuti na mkate mtamu. Maziwa mtindi na jibini hufaa. Pole pole unaweza kuanza kumpa mtoto kiasi kidogo cha chakula chako.

Kumbuka kwamba mtoto wako mchanga huhisi kiu mara nyingi kama wewe. Kwa hiyo, mnyweshe maji, lakini sio chai au kahawa. Matunda, mboga na supu ni vyakula vyenye manufaa maalum kwa mtoto mchanga anayekua.

Usisahau kuwa safi kuhusu malazi ya mtoto, nguo zake na nepi zake. Mnawishe uso na mikono yake mara nyingi. Muogeshe katika vipindi vya kawaida, kwa sababu watoto wachanga ni rahisi sana kuugua kwa sababu ya uchafu na vijidudu.

Lazima watoto wapate chanjo ya kinga dhidi ya maradhi ya ndui, tetekuwanga, kifadulo, kiharusi cha watoto (polio), homa ya vipele

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 129

vyekundu, surua, dondakoo. Kwa bahati nzuri chanjo zipo zinapatikana kwenye hospitali na vituo vya afya kwa urahisi.
Unaweza kuwa na watoto wenye afya njema kwa kushika kanuni za elimusiha na usafi.

SEHEMU YA PILI

WAJIBU WA MWANAMUME

MLEZI WA FAMILIA

Mwanaume na mwanamke ni nguzo mbili za msingi wa familia, lakini kwa kuwa wanaume wamepewa sifa maalum kwa amri ya uumbaji, na kwa sababu ya uwezo wao wa mantiki ni imara zaidi ya ule wa wanawake, wao huchukuliwa kama walezi wa familia zao.

Mwenyezi Mungu Mweza wa yote amewaweka wanaume kuwa walezi wa familia zao na anasema kwenye Qur'ani:

﴿ ٱلرِّجَالُ قَوَّٰمُونَ عَلَى ٱلنِّسَآءِ بِمَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بَعۡضَهُمۡ عَلَىٰ بَعۡضٍ ﴿٣٤﴾ ﴾

"Wanaume ni wasimamizi wa wanawake, kwa kufadhiliwa na Mwenyezi Mungu baadhi yao juu ya baadhi … (4:34)"

Kwa hiyo, wanaume wana jukumu kubwa na zito zaidi katika kuzisaidia familia zao.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 130

Ni mwanaume ambaye kwa kutumia busara yake, anaweza kuisadia familia yake na kutayarisha mazingira kwa ajili ya furaha yao, na ni yeye ambaye anayeweza kuigeuza nyumba kuwa Pepo na mke wake kuwa kama Malaika.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Mwanaume ni mlinzi wa familia yake na kila mlezi anao wajibu kwa hao waliopo kwenye ulinzi wake."

Mwanaume ambaye anaisaidia familia yake, lazima atambue kwamba mwanamke pia ni binadamu kama mwanaume. pia mwanamke anayo matamanio na haki ya uhuru na maisha. Kumuoa mwanamke si kukodisha mtumishi, lakini ni chaguo la mwenza na rafiki ambaye atakuwa tayari kuishi pamoja katika maisha yote. Mwanaume lazima amtunze na amtimizie matakwa yake. Mwanaume si mmiliki wa mke wake, kwa kweli mwanamke anazo haki fulani kwa mume wake.
Mwenyezi Mungu anasema kwenye Qurani Tukufu:

وَلَهُنَّ مِثْلُ ٱلَّذِى عَلَيْهِنَّ بِٱلْمَعْرُوفِ ۚ وَلِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ ۗ
وَٱللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٨﴾

"...Nao wanawake wanayo haki kwa sharia kama ile haki iliyo juu yao. Na wanamume wana daraja zaidi kuliko wao…" (2:228)

UTUNZAJI WA MKE WAKO

Siri ya ustawi wa familia inategemea na jinsi mtu anavyomtunza mke wake, na hii ni kama ilivyowajibu wa mke kwa mume wake ambao unaeleweka kuwa katika kiwango sawa na Jihadi, pia unatambua kama tendo jema na lenye thamani sana. Lakini mwanaume ajifunze namna ya

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 131

kumshughulisha mke wake, katika namna ambayo atageuka kuwa na tabia kama Malaika.

Kuhusu jambo hili, mwanaume lazima atafiti kuhusu tabia na matakwa ya mke wake. Lazima apange maisha yake kufuatana na matakwa ya mke wake na mahitaji sahihi. Mwanaume anaweza kwa tabia na msimamo wake kumshawishi mke wake katika njia ile ambayo inampendeza yeye (mke wake), kwake yeye mume na nyumba yake.

Hili ni somo ambalo linahitaji maelezo zaidi na mazungumzo ya kina yatawasilishwa baadaye kwenye kitabu hiki.

MPENDE MKEO

Mwanamke ni kituo cha wema na ni kiumbe chenye hisia kubwa sana. Kuwepo kwake hutegemea huruma na upendo. Huwa na shauku ya kupendwa na wengine na jinsi anavyopendwa zaidi ndivyo anavyofurahi zaidi. Hujitolea sana ili apendwe na wengi. Tabia hii ina nguvu sana ndani mwake hivyo kwamba akigundua kwamba hakuna mtu anaye mpenda, basi atajitambua kama ameshindwa. Atakasirika na atahisi kuvunjika moyo. Kwa hiyo, kwa hakika mtu anaweza kudai kwamba siri ya mwanamume aliyefuzu katika maisha ya furaha ya ndoa ni jinsi anavyo onesha mapenzi kwa mke wake.

Bwana mpendwa! Mke wako kabla ya kuolewa na wewe, alikuwa anafaidi mapenzi ya wazazi wake na wema wa wazazi wake. Sasa ameingia kwenye mkataba wa ndoa na wewe na sasa amechagua kuishi na wewe katika maisha yake yote, anatarajia wewe umtimizie matakwa yake ya mapenzi na huba. Anatazamia wewe kuonyesha mapenzi zaidi kwake kuliko alivyopokea kutoka kwa wazazi wake na marafiki zake. Amekuamini wewe sana na ndio sababu amekupa udhamini wa maisha yake.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 132

Siri ya ndoa yenye furaha hutegemea jinsi unavyodhihirisha mapenzi yako kwa mkeo.

Ukitaka kuuvutia moyo wake, ukitaka awe mtiifu kuhusu matakwa yako kama kuimarisha ndoa yenu, ukitaka mkeo akupende wewe, au adumishe uaminifu kuliko au… basi lazima kila mara uoneshe mapenzi na huba yako kwake.

Usipokuwa mwema kwa mke wako, basi anaweza kupoteza mvuto kwenye nyumba yake, halikadhalika na watoto pia. Na zaidi ya yote kwako wewe mwenyewe. Wakati wote nyumba yako itakuwa katika hali machafuko. Hatakuwa tayari kufanya juhudi kwa ajili ya mtu asiyempenda.

Nyumba ambayo ndani yake haina mapenzi, hufanana na jahanamu inayowaka moto, hata kama ni nadhifu sana na iliyojaa vitu vya anasa.

Mke wako anaweza kuugua au kupatwa na mfadhaiko. Anaweza kutafuta kupendwa na wengine kama hatoshelezwi na wewe. Anaweza asikuthamini wewe na nyumba yako pia, kiasi kwamba anaweza hata kuomba talaka!

Unawajibika kwa yote haya kwa sababu umeshindwa kumtosheleza mkeo. Kwa hakika ni kweli kwamba taratibu zingine za kutalikiana hutokea kwa sababu ya ukatili wa mume au kinyume chake.

Angalia takwimu zifuatazo. Mahitaji ya saikolojia ya mapenzi, uzembe wa waume kuhusu matakwa ya wake zao na kutokuzingatia umuhimu wa hadhi ya kiakili ya wanawake, ni vipengele ambavyo vimekuwa sababu ya kesi nyingi za kutalikiana.

Mnamo mwaka 1969 miongoni mwa kesi za kutengana 10372, katika kesi 1203 wanawake walionesha sababu ya kutaka kutalikiana kuwa ni

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 133

kuvunjwa moyo kimaisha, kujihisi hathaminiwi na upungufu wa waume kutokujali matakwa na hisia kubwa za wake zao." 146

Mwanamke alisema mahakamani; "Nipo tayari kuacha mahari yangu na hata kumlipa mume wangu fedha ili akubali kunipa talaka. Mume wangu anawapenda zaidi kasuku wake ndio sababu sitaki kuishi naye zaidi ya sasa."

Mapenzi na urafiki wa familia ni thamani kubwa zaidi kuliko chochote na ndio sababu Mwenyezi Mungu ameiona hiyo kama mojawapo ya alama za uwezo na neema kubwa ambayo mwanadamu amepewa. Qurani Tukufu inasema:

﴿ وَمِنْ ءَايَـٰتِهِۦٓ أَنْ خَلَقَ لَكُم مِّنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَٰجًا لِّتَسْكُنُوٓا۟ إِلَيْهَا
وَجَعَلَ بَيْنَكُم مَّوَدَّةً وَرَحْمَةً ۚ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَـَٔايَـٰتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١﴾ ﴾

"Na katika ishara zake ni kuwa amekuumbieni wenza kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo ishara kwa watu wanaofikiri (30:21)."

Imamu Sadiq (a.s) alisema: Yeyote ambaye ni rafiki yetu huonesha wema zaidi kwa mke wake."

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Jinsi mtu anavyozidi kuwa mwaminifu ndivyo anavyozidi kuonesha wema kwa mke wake."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 134

Imamu Sadiq (a.s) alisema: "Mmojawapo ya sifa bainifu ya Mitume wa Mwenyezi Mungu ni kwamba wote ni wema kwa wake zao."

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Maneno ya mwanaume anaye mwambia mke wake; 'Ninakupenda kweli' kamwe hayaondoki moyoni mwake."

Kama mambo yalivyo, mapenzi na huba lazima yawe halisi na kuvutia kwenye moyo wa mwingine, lakini hata kupenda sana kwa mtu haitoshi, kwa kuwa ni muhimu kuonesha huba. Kwa kuonesha hisia zako kwa maneno na vitendo vyako, mapenzi unayoonesha, yatapata jibu zuri kutoka kwa mkeo na nyoyo zenu zitaimarisha muungano wa mapenzi.

Uwe wazi na udhihirishe mapenzi yako kwako bila kusita. Wakati yupo au hayupo, msifie. Mwandikie barua unapokuwa safarini na mtaarifu kwamba kutokuwa karibu naye unajihisi mpweke sana. Mara kwa mara mnunulie kitu kama zawadi. Mpigie simu unapokuwa ofisini au shughuli zako na umuulize hali yake.

Kitu kimoja cha muhimu sana kwenye akili ya mwanamke ni namna hizi za kuonesha mapenzi kwake.

Bibi fulani wakati analia kwa masikitiko alisema. "Niliolewa na mume wangu usiku mmoja wa majira ya kupukutika kwa majani. Tuliishi pamoja kwa amani kwa muda fulani. Nilihisi kuwa nilikuwa mwanamke mwenye bahati kubwa sana hapa duniani. Niliishi kwenye nyumba yake ndogo kwa miaka sita. Nilihisi ninayo furaha mara mia moja nilipogundua kwamba nilikuwa mja mzito. Nilipomtaarifu mume wangu alidondokwa na chozi la furaha wakati amenikumbatia mikononi mwake. Alilia sana hivyo kwamba karibu angeshindwa kujizuia. Halafu akatoka nje na akaninunulia mkufu wa almasi kwa fedha yake ya akiba. Alinipa mkufu na akasema:

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 135

'Ninatoa hii kwa mwanamke bora kuliko wote ambao ninewaona hapa duniani.' Lakini baada ya muda mfupi alikufa kwenye ajali ya gari."

MHESHIMU MKE WAKO

Mwanamke hujivunia utu wake kama ilivyo kwa mwanamume. Anapenda kuheshimiwa na watu wengine. Ataumia sana kimawazo kama akitukanwa au kudhalilishwa. Hufurahi anapo heshimiwa na huwachukia wale wanaojaribu kushusha hadhi yake.

Bwana mpendwa kwa hakika mke wako anatarajia kuheshimiwa na wewe zaidi kuliko watu wengine. Anayo haki kumtarajia mpenzi wake wa maisha na rafiki mzuri zaidi ya wote kumtunza yeye.
Mke wako kufanya kazi kwa ajili ya faraja yako na watoto wenu na kwa hiyo anakutarajia wewe kumthamini yeye na juhudi zake.

Kumheshimu mkeo si jambo la kukushusha hadhi yako ila kwa kweli itakuwa ni uthibitisho wa mapenzi na huba yako kwake. Kwa hiyo, mheshimu mkeo zaidi ya wengine na sema naye kwa upole. Usiingilie kati au kumkemea anapozungumza. Mwite kwa majina ya heshima na uadilifu. Onyesha heshima yako anapotaka kuketi chini.

Unapoingia nyumbani, akisahau kusema 'Salaamu aleyk' (yaani kukusalimia), basi anza wewe kumsalimia kwa kusema 'salaamu aleyka.'

Sema 'kwa heri' unapoondoka nyumbani. Usiache kuwasiliana naye unaposafiri au unapokuwa haupo nyumbani. Mwandikie barua.

Dhihirisha heshima yako kwake unapokuwa kwenye mikusanyiko. Kwa dhati kabisa, epuka kumtusi kwa namna yoyote na kumfedhehesha. Usitumie lugha chafu au hata kumchokoza kwa kumtania. Usidhani ya

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 136

kwamba kwa sababu upo karibu naye sana kwa hiyo hatojali ukimtania. Kinyume chake ni kwamba atachukia msimamo wa aina hiyo bila kukuonesha ishara yoyote.

Mwanamke mwenye hadhi mwenye umri wa miaka 35, anasema kuhusu ombi lake la talaka; Ni miaka 12 tangu nimeolewa. Mume wangu ni mwanamume mwema na zipo tabia nyingi za mtu mwema na mpole ndani mwake. Lakini kamwe hajataka kutambua kwamba mimi ni mke wake na mama wa watoto wake. Yeye ana dhani kwamba ni mtu anayeweza kuchanganyikana na kuzoeana na watu bila taabu, lakini maonesho yake hayo kuyafanya kwa kunitania na kunidhalilisha. Huwezi kuamini ni kiasi gani nimeumia katika hisia zangu. Neva zangu zimeathiriwa sana hivyo kwamba imenibidi niende kupata ushauri kutoka kwa bingwa wa maradhi ya akili ili nipate tiba. Nimezungumza na mume wangu kuhusu jambo hili mara nyingi. Nimemwomba asinifanyie hivyo. Nimemkumbusha kuhusu nafasi yangu kama 'mke wake' na umri wangu na kwamba si stahili yake kunitania mimi mbele ya watu wengine hadi wanacheka au wanafurahia kitendo hicho. Nina hisi kuaibika mbele ya kila mtu na kwa sababu sijawahi hata wakati mmoja kuwa mcheshi, siwezi kushindana naye. Kwa kuwa matakwa yangu hayatekelezwi na mume wangu, ninataka kutengana naye. Ninajua sitakuwa na furaha nikibaki peke yangu, lakini siwezi kuishi na mwanaume ambaye hushusha hadhi yangu kila wakati .."

Wanawake wote huwa na matamanio ya kuheshimiwa na waume zao na wote huchukia fedheha. Kama wanawake wengine kunyamaza wakati waume zao wanawadhalilisha huo si uthibitisho wa kuridhika kwao na tabia hiyo.

Ukimheshimu mke wako, na yeye atafanya hivyo kwako na uhusiano wenu utazidi kuimarika. Wewe pia utapata heshima zaidi kutoka kwa watu wengine. Kama ukimtendea vibaya mke wako na yeye alipe kisasi, hili tena si kosa lake ni kosa lako.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 137

Bwana mpendwa! Kuoa si sawa na kupata mtumwa. Huwezi kumtendea mtu aliye huru kama mtumwa. Mke wako amekubali kuolewa na wewe ili aishi na wewe na kugawana maisha yake na mtu ambaye anampenda. Anatazamia mambo kama hayo kutoka kwako kama vile unavyotarajia kutoka kwake. Kwa hiyo, mtendee kwa namna ambayo wewe ungependa kutendewa.

Imamu Sadiq (a.s) akimnukuu baba yake, alisema: "Yeyote anayeoa, lazima amheshimu mke wake."

Mtume (s.a.w) wa Mwenyezi Mungu alisema: "Mtu yeyote anaye mheshimu Mwislamu, Mwenyezi Mungu atampa heshima yake mwenyewe."

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) pia alisema: "Hapana yeyote ambaye angewaheshimu wanawake isipokuwa watu wakarimu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akaongeza kwa kusema: "Mtu yeyote anaye tukana familia yake, atapoteza furaha katika maisha yake."

UWE NA TABIA NJEMA

Dunia huchukua mkondo wake kufuatana na mpangilio linganifu. Matukio hutokea na kujidhihirisha moja baada ya lingine. Kuwepo kwetu katika ulimwengu huu mpana ni kama chembe ndogo ilioko kwenye mwendo na kuathiri chembe nyingine papo hapo.

Uendeshaji wa dunia huu haupo katika uwezo wetu na matukio ya dunia hii hayatokei kufuatana na utashi wetu. Tangu hapo ambapo mtu hutoka nyumbani kwake asubuhi hadi hapo anaporudi jioni, inawezekana hukabiliana na mamia ya mambo yasiyofurahisha.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 138

Mtu hukutana na matatizo mengi sana katika uwanja wa maisha. Inawezekana mtu akakutukana, na mfanyakazi mwenzake asiye rafiki, utangojea basi kwa muda mrefu mno, umeshutumiwa kwa sababu ya kitu fulani ofisini, umepoteza fedha, au umekabiliwa na tukio lolote ambalo linaweza kumtokea mtu mwingine yeyote popote.

Inawezekana ukakasirishwa sana na matukio ya kawaida ya kila siku katika maisha yako hivyo kwamba unafanana na bomu lililotegwa na kulipuka wakati wowote.

Vema, inawezekana ukadhani kwamba huwezi kuwalaumu watu wengine au dunia kwa sababu ya bahati yako mbaya, hivyo kwamba unaporudi nyumbani, unajaribu kutoa nje hasira yako kwa mke wako na watoto wako.

Unaingia nyumbani kwako kama vile 'Ziraili' (malaika wa kifo) amewasili. Watoto hutawanyika kama panya wadogo mbele yako. Mungu na apishe mbali kwamba uone kitu fulani kilicho kosewa! Chakula, ama inawezekana kina chumvi nyingi au hakina chumvi, au kikombe chako cha chai hakijawa tayari, inaewezekana nyumba chafu, au watoto wanapiga kelele na kwa hiyo unapata kisingizio cha kulipuka kwa hasira ndani ya nyumba yako.

Halafu unamkasirikia na kumpigia kelele kila mtu, unawatukana unawapiga watoto na kadhalika. Wakati huo utakuwa umeigeuza nyumba ya huba na urafiki kuwa jahanamu iwakayo moto ambamo wewe na familia yako mtateseka.

Kama watoto wanaweza kukimbia kutoka nyumbani na kwenda mitaani, watafanya hivyo, na kama hawawezi kufanya hivyo, basi watahesabu sekunde hadi hapo utakapoondoka nyumbani.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 139

Inaeleweka dhahiri ni mazingira ya kusikitisha na kutisha yalioje yanayotawala familia za aina hii. Kila mara upo ugomvi na mabishano. Nyumba yao kila mara imevurugika. Mke anachukia kuona uso wa mume wake.

Mwanamke anawezaje kuishi kwa furaha na mwanamume mkali na mwenye hasira?

Baya zaidi kuliko yote ni hatima ya watoto ambao watakulia kwenye mazingira hayo. Ugomvi wa wazazi wao kwa hakika utatia kovu kwenye roho na nyoyo zao zilizo nyepesi kuhisi. Watoto wanao wanaopata matatizo kama haya huendeleza tabia ya kuwa aina ya watu wenye hasira, wagomvi wenye huzuni na kuona kila jambo ni baya wakati watakapofika umri a utu uzima. Hukatishwa tamaa kwenye familia yao na hukengeuka. Inawezekana wakakutana na mitego ya watu waovu na kuanza kufanya uhalifu wa aina mbali mbali. Inawezekana wakawa na tabia ngumu sana kuelezeka na kuvurugikiwa akili hivyo kwamba wanaweza kuhatarisha maisha ya watu wengine kwa kuua au kujiua.

Msomaji anashauriwa kufanya utafiti wa historia ya maisha ya wahalifu. Takwimu na taarifa za kila siku za matukio ya uhalifu yote yanaonesha ukweli huu.

Yote haya yapo kwenye wajibu wa mlezi wa familia ambaye ameshindwa kudhibiti tabia yake na ameitendea vibaya familia yake. Mtu kama huyu kamwe hawezi kuwa na amani katika dunia hii na ataadhibiwa akhera.

Mpendwa bwana! Hatuna nafasi na hatuwezi kudhibiti mambo ya dunia hii. Mabalaa, shida, na matukio ya kusikitisha yote ni mambo yanayo ambatana na maisha haya. Kila mtu hupata matatizo wakati mbali mbali. Ni ukweli wa mambo kwamba, mtu hufika kwenye umri wa balekhe kwa kukabiliana na

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 140

taabu. Mtu lazima apambane nayo kwa nguvu na lazima ajaribu kutafuta ufumbuzi wake. Binadamu wanao uwezo wa kukabiliana na mamia na matatizo madogo na makubwa na bila kukata tamaa chini ya mbinyo wa balaa.

Matukio ya dunia si ndio tu sababu ya kutibuliwa kwetu, isipokuwa hasa zaidi ni mpangilio wetu wa neva ambao huathirika na matukio kama haya na husababisha sisi tukose furaha. Kwa hiyo, kama mtu angeweza kudhibiti hali wakati anapokabiliwa na matukio ya maisha yasiyofurahisha, hangekasirika na kuchukia.

Tudhani ya kwamba umepatwa na tukio lisilofurahisha. Tukio hili ama ni matukio ya kila siku yalioambatana na hali ambayo hatuna uwezo wa kuingilia au hatuwezi kusaidia. Au inawezekana tukio hili ni lile ambalo sisi tunaweza kufanya uamuzi wetu.

Ni dhahiri kwamba katika mfano wa kwanza, hasira yetu hainge saidia kwa njia yoyote. Tutakuwa tunakosea kukasirika au kuhamaki. Lazima tukumbuke kwamba sisi hatukusababisha kutokea kwa tukio hilo na hata tujaribu kulikaribisha kwa uso wenye furaha.

Lakini kama tatizo letu ni la mfano wa pili, basi tunaweza kutafuta ufumbuzi unaofaa.

Kama hatutakata tamaa tunapokabiliwa na shida na kujaribu kujizuia, kwa kutumia busara, tunaweza kuyashinda matatizo yetu. Kwa njia hii hatuta kimbilia hasira ambayo inaweza kuwa tatizo juu ya tatizo.

Tunao uwezo wa kushinda matatizo yote kwa kutumia uvumilizu na hekima. Hivi si jambo la kusikitisha kwamba tunashindwa kudhibiti mambo yanayotokana na matukio yasioepukika maisha?

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 141

Zaidi ya haya kwa nini umlaumu mke na watoto wako kwa mabalaa yako? Mke wako anatekeleza mgawo wa wajibu wake. Anatakiwa kutunza nyumba na watoto. Anatakiwa kufua, kupika, kunyoosha pasi kufanya usafi na kadhalika. Unatakiwa kumtia moyo mke wako kama vile unavyomtendea.

Watoto wako pia wanafanya kazi yao. Wao pia wanamngojea baba yao wajifurahishe. Wafundishe mambo yaliyo sahihi na uwape hamasa wajifunze zaidi. Je, ni haki kwamba unakutana na familia yako ukiwa na uso wa kikatili na chuki?

Wanakutarajia wewe kuwatimizia matakwa ambayo ni haki yao. Wanatazamia wema kutoka kwako na wanataka uzungumze nao kwa upole na uoneshe furaha.

Watakuchukia sana kama ukidharau hisia zao na kama utaigeuza nyumba kuwa mahali pa giza ambamo hakuna furaha hata kidogo.

Unajua watateseka kiasi gani kutokana na tabia yako isiyopendeza na ya kikatili? Hata kama hutaichukulia familia yako kwa uzito uanostahili angalau ujihurumie wewe mwenyewe. Uwe na uhakika kwamba unaweza kuharibu afya yako kwa kuendeleza ukali.

Unawezaje kuendelea kufanya kazi na unawezaje kufuzu kupata mafanikio? Kwa nini uigeuze nyumba yako iwe jahannamu?
Hivi si vizuri zaidi kwamba wewe uwe na furaha kila mara na uyakubali matatizo yako kwa busara na si hasira?

Hungetaka kuamini kwamba hasira haiwezekani kutatua matatizo yako, isipokuwa hasa zaidi matatizo yataongezeka? Hungekubali kwamba unapokuwa nyumbani unatakiwa kupumzika na kurudisha nguvu zako ili

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 142

uweze kupata ufumbuzi unaofaa kwa matatizo yako akili yako ikiwa imetulia? Kutana na familia yako ukiwa na uso wenye tabasamu; taniana na watu wa familia yako kwa namna nzuri na jaribu kutengeneza mazingira ya furaha nyumbani kwako. Ule na kunywa pamoja nao na upumzike.

Kwa njia hii wewe na familia yako mtafurahia maisha na mtashinda matatizo yenu kwa urahisi. Ndio sababu dini tukufu ya Uislamu inaona tabia njema kuwa sehemu ya dini na ishara ya kiwango cha juu sana cha imani.

Mtume (s.a.w) alisema: "Mtu mwenye tabia njema amekamilika zaidi katika imani yake. Mtu mwema zaidi miongoni mwenu ni yule anayeitendea mema familia yake."

Mtume (s.a.w) pia alisema: "Hakuna tendo jema zaidi kuliko tabia njema."

Imamu Sadiq (a.s) alisema: "Kuwatendea wema watu na kuwa na tabia inayostahili unapokuwa nao kufanya miji huwa na watu wengi zaidi na umri wa raia huongezeka."

Imamu Sadiq (a.s) pia alisema: "mtu muovu hubakia kwenye mateso na uchungu."

Luqman mwenye hekima alisema: "Mtu mwenye busara lazima afanye mambo kama mtoto mdogo wakati anapokuwa na familia yake, na kuendelea na tabia ya kiwanamume anapokuwa nje ya nyumba yake."

Mtume wa Mwenyezi Mungu(s.a.w.w) alisema: "Hakuna furaha iliyo nzuri zaidi kuliko tabia njema."

Mtume (s.a.w.w) pia alisema: "Tabia njema ni nusu ya dini ya Uislamu."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 143

Imesimuliwa kwamba alipokufa Sad bin Maadh mmojawapo wa sahaba mashuhuri wa Mtukufu Mtume (s.a.w), Mtume (s.a.w) alishiriki kwenye maziko yake bila kuvaa viatu, kama vile alipoteza mmojawapo wa watu wa familia yake.

Mtume (s.a.w) aliweka maiti ya sahaba huyo karibuni kwa mikono yake iliyotakasika halafu akaufunika. Mama yake Sad ambaye alikuwa anaangalia heshima ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kwa mwanae alimwambia Sad: "Ewe Sad! furahia Pepo" Mtume (s.a.w.w) alimwambia:

"Ewe mama wa Sad, usiseme hivyo, kwa sababu Sad sasa hivi amepata mateso kwa njia ya kugandamizwa kaburini na kadhalika. Baadaye, Mtume (s.a.w.w) alipoulizwa kuhusu sababu ya mateso ya Sad, Mtume (s.a.w.w) alijibu; "Ilikuwa kwa sababu alikuwa anaitendea mabaya familia yake."

KULALAMIKA KUSIKO NA LAZIMA

Matatizo ya maisha ni mengi. Hakuna mtu ambaye anayo furaha kamili na hali yake. Lakini baadhi ya watu ni wavumilivu zaidi kwa matatizo yao kuliko wengine. Hujaribu kuyaweka katika kumbu kumbu ya akili zao na hawayataji isipokuwa kama ipo sababu ya kuyafichua.

Kwa upande mwingine, wapo watu ambao ni wadhaifu mno hivyo kwamba hawawezi kuishi na matatizo yao bila ya kuyafichua. Wanayo mazoea makubwa kulalamika hivyo kwamba kila wanapokutana na watu wengine, huanza kulalamika. Popote wendapo na wakati wowote wanapokuwa kwenye mkusanyiko, hulalamika kuhusu matukio ya kila siku ambayo yameathiri maisha yao. Inakuwa kama vile wametumwa kwenye misheni na shetani mwenyewe, kuharibu furaha ya wengine. Ndio maana marafiki wengi sana na ndugu hawapendi kutiwa wasi wasi na watu wenye tabia hii na hujaribu kuwakwepa kadiri iwezekanavyo.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 144

Lakini lazima watu wawasikitikie wake zao, na watoto wao ambao wanatakiwa kuvumilia tabia yao. Kwa sababu hakuna mtu mwingine ambaye yupo tayari kusikiliza malalamiko yao, watu hawa hutoa matatizo yao mbele ya familia zao.

Wakati mwingine hulalamika kuhusu matumizi yao, kodi marafiki zao na wakati mwingine hulalamila kuhusu wafanya kazi wenzao biashara zao, maradhi, madakitari na kadhalika.

Watu hawa ni wenye kuona kila kitu kuwa kibaya hawaoni chochote kizuri katika dunia hii. Wanateseka wao na wengine, pia na hususan familia zao huteseka pia.

Mpendwa Bwana! Kuna maana gani kulalamika wakati wote? Unafanikiwa nini katika kulalamika? Kwa nini familia yako iteseke kwa sababu wewe umekasirishwa na dereva wa teksi? Kwa nini umlaumu mke wako kwa sababu biashara yako haiendi haraka?"

Usisahau kwamba msimamo wako utaifukuza familia yako kutoka kwako. Watakukasirikia na kukata tamaa. Wanaweza hata wakakimbia kutoka kwako na inawezekana wakaangukia kwenye mtego wa uovu na ukhalifu

Jambo la mwisho ni kwamba tabia hii huweka kovu la kiakili kwa watu wako.

Je, huoni kwamba sio jambo jema zaidi kutokuharibu furaha ya familia yako? Unaporudi nyumbani, jaribu kusahau matatizo. Furahi na familia yako. Kula nao cheka nao na furahia kuwa pamoja nao.

Pia Uislamu unachukulia uvumilivu na kutokulalamika kuwa ni tabia njema na hata umetenga thawabu kwa sifa hii. Imamu Ali (a.s) alisema:

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 145

"Matatizo yanapo mpata Mwislamu, si vizuri alalamike kuhusu Mwenyezi Mungu kwa watu wengine, isipokuwa anachotakiwa kufanya ni kumpelekea Mwenyezi Mungu matatizo yake ambaye ndiye mwenye ufunguo wa matatizo yote."

Imamu Ali (a.s) pia alisema: "Imeandikwa kwenye Taurati; yeyote anaye lalamika kuhusu tatizo ambalo limempata kwa kweli atakuwa analalamika kuhusu Mwenyezi Mungu."

Mtume (s.a.w.w) wa Uislamu alisema: "Yeyote anayepata matatizo ya afya yake na halalamiki kuhusu jambo hilo kwa watu, basi ni wajibu Mwenyezi Mungu kumsamehe dhambi zake zote."

KUANZISHA UGOMVI

Baadhi ya wanaume wakati wote hutafuta visingizio vya kuona kosa katika kila kitu. Hulalamika kuhusu kila jambo dogo. Kwa nini meza hii chafu? Kwa nini chakula cha mchana hakipo tayari? Kwa nini jagi la maua lipo hapa? Hivi sijasema kabla kwamba visahani vya majivu visiwekwe chini? Na kadhalika.

Wanaume hushikilia msimamo huu hadi kufika kiasi cha kusababisha ugomvi na migongano ndani ya familia zao, na wakati mwingine familia huvunjika kwa sababu ya tabia yao.

Kama mambo yalivyo hatusemi kwamba wanaume hawana haki ya kuwaambia wake zao nini cha kufanya. Mwanzoni mwa kitabu hiki, wanawake walishauriwa kukubali haki hii. Tumesema kwamba wanawake hawatakiwi kuonesha kiburi kwa ushauri wa waume zao kuhusu mambo ya familia. Hata hivyo, wanaume wanatakiwa kutumia mantiki na busara zao. Wao ni walezi wa familia zao na kwa hali hiyo, wanatakiwa kuwa na mwenendo unaostahili.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:24 PM Page 146

Kama mwanaume anataka kushiriki kwenye mambo ya familia basi anatakiwa kuwa na mwenendo unaostahili.

Kama mwanaume anatakiwa kushiriki kwenye mambo ya familia basi anatakiwa kufanya hivyo kwa namna iliyo fanywa.
Kwa kweli, kwa kuwa mwanaume hana muda wa kutosha kushiriki katika mambo yote yahusuyo nyumba yake na kwa sababu hana utaalamu muhimu kuhusu shughuli hizo, basi ni kwa manufaa yake kumwachia mke wake kazi za nyumbani. Mwanaume anatakiwa kumwacha mke wake afanye shughuli za nyumbani kwa uhuru.

Hata hivyo, wanaume kwa kisingizio cha kutoa ushauri, wanaweza kuwakumbusha wake zao kuhusu mambo fulani bila kuwalazimisha. Mara mwanamke mwenye busara anapoona matakwa ya mume wake kufuatana nayo. Kwa hiyo, mwanaume na mwanamke ambao hujaliana wao kwa wao na familia yao.

Kwa kuzungumza pamoja kwa jinsi ilivyo wanaweza kukubaliana mambo yote. Kwa njia hii, wanawake wengi wapo tayari kukubaliana na matakwa ya waume zao ya mara kwa mara.

Lakini kama kushiriki kwake ni kutafuta dosari na kulalamika mfululizo, basi huzoea na kwa hiyo, basi mke huzoea na kwa hiyo msimamo huu unakuwa jambo la kawaida na hakuna lolote la maana litakalo tokana na hali hiyo.

Mwanamke mwenye mume mlalamikaji, hatakuwa makini naye. Mke anaweza hata asijali mambo yake yanayofaa na muhimu. Atajishauri yeye mwenyewe: “Kwa nini nipoteze nguvu zangu, kama mume wangu hatosheki hata kidogo na kazi yangu?”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 147

Si tu kwamba hatajali shutuma za mume wake, lakini anaweza hata akalipiza kisasi.

Hapa ndipo ambapo nyumba yao hugeuka kuwa uwanja wa vita. Kushutumiana mfululizo wao kwa wao kutatayarisha uwanja wa kutengana na hivyo familia huvunjika. Katika tukio hili mwanamke hatalaumiwa kwa sababu hata mke aliye na busara na mvumilivu atashindwa kuendelea kuvumilia kwa sababu ya msimamo wa mume wake wa kudhalilisha.

“Mwanaume alipiga simu kwenye kituo cha polisi na kudai kwamba mke wake aliondoka nyumbani kwake miezi miwili iliyopita na kwamba alikuwa anaishi na wazazi wake. Baada ya uchunguzi zaidi, mke wa huyu mwanaume alisema; ‘Mume wangu hapendi mtindo wangu wa kutunza nyumba. Wakati wote hunilaumu kuhusu mapishi yangu na uendeshaji wa mambo ya nyumbani. Kwa hiyo nimemwacha ili nipate amani mahali pengine.’ ”

Wanaume lazima wakumbuke kwamba kazi za nyumbani ni eneo la wake zao kutekeleza wajibu wao. Ni makosa kuwanyang’anya haki yao au kuwageuza kuwa vibaraka. Ni busara zaidi kuwaacha waendeshe mambo ya nyumba jinsi watakavyo.

Matokeo yake, mke wako hufanya kazi kwa shauku kubwa, utafurahi na nyumba yako itakuwa makazi ya familia yenye furaha.

MRIDHISHE NA MLIWAZE MKE WAKO

Pia mwanamke, kama ilivyo kwa mwanamume, hupata mabadiliko ya hisia kubwa. Huhisi furaha, hasira, huzuni na kadhalika. Huchoka kutokana na kazi za nyumbani na inawezekana akaudhiwa na watoto.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 148

Watu wengine wanaweza kumtibua kwa shutuma zao. Inawezekana akaingia kwenye mashindano na wengine. Kwa ufupi, mwanamke hukabiliana na matatizo mengi ambapo mengine miongoni mwa hayo humuathiri sana hivyo kwamba anaweza kukata tamaa kwa kiwango ambacho kitasababisha atoe majibu yasiyofaa hata kwa mambo madogo.

Hususan mfano huu ni kwa upande wa wanawake, kwa sababu wao ni wepesi sana na hutoa majibu kwa umakini zaidi kwa matukio yasiyo pendeza ikilinganishwa na wanume.

Wanawake ambao hupata matatizo huhitaji kutulizwa. Wanaume lazima wawafariji kwa sababu ni wenzi wao na wao ndio wanaoaminiwa na wake zao.

Mpendwa bwana! Unapomwona mke wako katika huzuni na hasira basi jaribu kuelewa hali yake. Kama ukiingia nyumbani kwako na hakusalimu, wewe mtolee ‘salaam’. Tendo hili halita kudhalilisha wewe. Ongea naye ukiwa katika tabasamu. Epuka ukali. Msaidie kazi za nyumbani. Uwe mwangalifu usimuudhi kwa namna yoyote. Usimtanie. Kama hajisikii kuzungumza, basi mwache. Usiseme: “Unasumbuliwa na nini?”

Kama anayo hali ya kutaka kuzungumza, msikilize na mliwaze. Jifanye unahusika zaidi na tatizo lake kuliko yeye. Mruhusu akwambie malalamiko yake kwako. Halafu, kama vile baba mwema au mume mwenye huruma jaribu kumsaidia apate ufumbuzi wa tatizo lake. Mpe moyo wa kuwa mvumilivu. Kwa busara na mantiki mfanye ayaone matatizo yake kama madogo. Imarisha tabia yake na msaidie kushinda sababu ya hasira yake, uwe mvumilivu na mtendee kufuatana na mantiki yako. Kwa hakika atauona, msaada wako kuwa unafaa na maisha yatarudi katika hali yake ya kawaida baada ya muda mfupi kwenu nyinyi wote.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 149

Kinyume chake, ukimwendea isivyo sahihi, inawezekana ukasababisha mateso zaidi kwake. Pia wewe utateseka na inaweza kusababisha ugomvi mkubwa ambao utawapa usumbufu wote wawili.

USITAFUTE MAKOSA YAKE

Hapana mtu yeyote hapa duniani ambaye anazo sifa zote na hana makosa. Watu wengine wanweza kuwa wanene sana au wembamba sana. Wenye midomo mikubwa pua kubwa au meno makubnwa. Wengine wanakuwa wachafu, hawana adabu, wenye haya, fidhuli, wenye kuvunjika moyo, hasira, wivu au wachoyo. Wanawake wengine si wapishi wazuri au mwanamke mwenye kipaji. Watu wengine wanaweza kuwa walaji sana au kutumia kwa fujo. Kwa ufupi, hakuna mtu ambaye hana mapungufu, na hakuna mtu yeyote hapa duniani anayeweza kuchukuliwa kama kiumbe kilichokamilika.

Kwa kawaida, wanaume, kabla ya kuoa hudhani kwamba atakaye muoa awe hana dosari yoyote. Hawajali ukweli huu kwamba hakuna kiumbe kifananacho na malaika hapa ulimwenguni. Wanaume hawa, mara waoapo huwaona wake zao waliodhani wakamilifu, si wakamilifu na hivyo huanza kuonesha mapungufu yao. Hudiriki kuona kuwa ndoa zao hazikufuzu na wao wenyewe kuwa na ‘bahati mbaya.’

Wanaume hawa hulalamika kila mara na hawaachi kulalamika hata dosari ndogo za wake zao.

Wanaume wengine hukuza dosari sana hivyo kwamba kila mara huziona kubwa kama milima mirefu. Mara kwa mara huzitaja dosari hizo kwa wake zao na kuwadhalilisha. Pengine huzitaja hata mbele ya marafiki na ndugu.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 150

Matokeo ni kwmaba, msingi wa maisha yao ya ndoa huanza kutetemeka. Mwanamke hufadhaika na hupoteza shauku kwa mume wake na familia yake. Atadhani hakuna mantiki yoyote kufanya kazi kwenye nyumba ya mtu ambaye humshutumu. Inawezekana akalipiza kisasi.

Mwanaume anasema kwa mke wake: "Tazama pua yako ilivyo kubwa, na mbaya ilioje!" Na mwanamke atajibu: "Si mbaya kama uso wako mbaya na kiwiliwili chake kilicho kwenda kombo!"

Halafu mwanaume atasema: "Meno yako yananuka harufu mbaya! Na mwanamke anajibu: "Funga domo lako kubwa." Na kadhalika.

Kuendelea kwa mazungumzo haya hufungua mlango wa shutuma na kuigeuza nyumba kuwa uwanja wa vita ambamo wanandoa hutukanana na kushushiana hadhi.

Wakiendelea kuishi namna hii, hawatafurahia maisha yao tena hata kidogo, kwa sababu nyumba isiyokuwa na mapenzi ya familia na uaminifu, si mahali pa faraja.

Zaidi ya haya, mwanaume anayejihisi kwamba yeye hana bahati na ndoa yake imeshindikana, na mwanamke ambaye hudhalilishwa wakati wote, wote wawili wanaweza kupata maradhi ya kiakili na mengineyo.

Kama ukubwa wa ugomvi wao unazidi kuongezeka basi kila mara huwepo uwezekano wa hatari ya kutalikiana au kutengana. Kutalikiana ni hatua isiyosaidia sana kwa pande zote zinazohusika, haswa kama wapo watoto katika familia.

Jamii haingeheshimu mtalaka mwanaume au mwanamke. Zaidi ya hayo kutalikiana ni hatua inayosababisha hasara ya kiuchumi kwa mwanaume;

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 151

ambayo si rahisi kurekebishwa hasa zaidi hii ni kweli hapo mtalaka anapotaka kuoa tena, kwani pia atahitaji kutumia fedha tena kwenye ndoa

yake ya pili. Zaidi ya hayo, hakuna uhakika wa mtalaka kupata mwanaume ambaye atamridhisha kufuatana na matumaini yake.

Kufunga ndoa mara ya pili haitakuwa rahisi kwa sababu ya historia yake. Hata kama mwanamume atapata mwanamke mwingine, bila shaka atakuwa na mapungufu fulani pia. Anaweza hata akawa mbaya zaidi kuliko mke wake wa kwanza. Atakuwa hana budi kumvumilia. Hii ni kwa sababu wanaume wengine wanayo majivuno makubwa kukubali dosari zao. Ni mara chache sana utamuona mwanaume ambaye ameridhika kabisa na ndoa yake ya pili. Imewahi kutokea kwamba baadhi ya wanaume hurudi kwa wake zao wa mwanzo.

Bwana mpendwa! Kwa nini umwangalie mke wako kwa lengo la kutaka kugundua dosari zake; na kwa nini utilie maanani sana kuhusu mapungufu madogo? Kwa nini uyakuze sana makosa yake hivyo kwamba husababisha mateso kwako wewe na familia yako?

Umepata kumuona mwanamke asiye na dosari kabisa? Wewe mwenywe ni mbora kiwango gani? Ni dosari zipi ndogo ndogo zinazostahili kuhatarisha kuvunjika kwa ndoa yenu?

Uwe na uhakika kwamba kama ukimuona mke wako kwa makusudio yenye mantiki na haki, itagundua mambo mengi mazuri kuhusu yeye. Wewe tazama na uone kwamba sifa zake zitazidi dosari zake.

Uislamu unauona msimamo huu kuwa na madhara na haupendezi na kwa hiyo unakataza watu wote kutafuta na kugundua makosa ya wengine.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 152

Mtume (s.a.w) alisema: "Enyi mnao sema, kwa ndimi zenu tu kwamba nyinyi ni Waislamu lakini imani haijaingia nyoyo zenu! Usiwaseme vibaya Waislamu na usianze kutafuta makosa yao kwa sababu yeyote anaye tafuta na kugundua dosari za wenzake, atashutumiwa na Mwenyezi Mungu na hata kama mtu kama huyu yupo nyumbani kwake, atafedheheka."

PUUZA MAZUNGUMZO YA UONGO YA WAKOSOAJI

Baadhi ya watu wanayo mazoea ya kuwazushia uongo watu wengine. Tabia hii isiyo pendeza hutengeneza uadui miongoni mwa marafiki, na ndugu na inaweza kuvunja familia. Imeweza hata kusababisha mauaji. Zipo sababu mbali mbali kuhusu tabia ya aina hii, kama wivu, hasira, kisasi na uadui.

Baadhi ya watu hukimbilia kutamka maneno ya kashifa ili waridhishe nafsi zao. wasikilizwe na watu wengine au kujifanya wanamuonea huruma mtu fulani. Lakini ni mara chache sana kwamba maneno ya kashifa huwa na makusudio mazuri.

Kwa hiyo, mtu mwenye hekima na mjanja anatakiwa kupuuza maneno kama hayo. Lazima afanye uchambuzi wa maneno ya msemaji kila mara ili aepuke kudanganya au kuvutiwa na uovu wake wa masingizio.

Jambo moja ambalo wanamume wanatakiwa kukumbuka ni kwamba kwa kawaida mama zao, dada zao, kaka zao, licha ya kuonesha urafiki, huwa hawafurahii uhusiano mzuri na wake zao.

Sababu ni kwamba, kabla ya kuoa mwanaume huishi na wazazi wake kwa miaka mingi ambapo huwa hana uhuru wa kutosha. Wazazi wake ambao wamefanya bidii kumlea wanayo matarajio ya kupata msaada kutoka kwake pindi wanapofika kwenye umri wa uzeeni.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 153

Wazazi hata baada ya kumuoza mtoto wao wa kiume na kumpa uhuru bado wanayo matumaini kwamba atafuata ridhaa yao na matakwa yao. Hupenda mtoto wao wa kiume kuwatunza wao zaidi kuliko mkewe. Lakini ukweli ni kwamba, mwanaume anapoanza maisha ya ndoa, hujitahidi sana kwa ajili ya familia yake mpya, mke na kujitegemea. Huelekeza mapenzi yake kwa mke wake na hufanya bidii kuhusu lengo hilo. Jinsi anavyozidi kuingia upande wa ndoa, ndivyo anavyozidi kuwa mbali na wazazi wake.

Hivyo mama yake na dada zake hususan hujihisi wamekosewa. Humuona bibi harusi kama tishio kwao kwani atakuwa amemchukua kijana wao kutoka kwao. Inawezekana wamlaumu bibi harusi kwa kumtenganisha kijana wao kutoka kwenye familia yake.

Wakati mwingine mama wa waume hudhani kwamba njia iliyo nzuri sana ya kukabiliana na hatari hii ni kutekeleza njia za kusababisha watoto wao (waume) wapunguze huba kwa wake zao. Mama wa aina hii, ataanza kuonesha mapungufu ya mke wa mwanae, kutangaza uongo kuhusu bibi harusi, kusema maneno ya kashfa na kufanya njama dhidi ya muolewaji na kadhalika.

Kama mwanaume anadanganyika kwa urahisi na mjinga, inawezekana akakubaliana na maneno ya kashifa ya mama yake. Hapo sasa mume atakuwa kitendea kazi kilichomo mikononi mwa familia yake ambapo matokeo yake baadaye atapoteza mvuto kwa mkewe. Akiwa kwenye ushawishi wa wazazi wake mwanaume ataanza kulalamika na kuonesha makosa ya mke wake. Atamlaumu mke wake wakati wowote itakapo wezekana.

Matokeo yake, nyumba ya familia itageuka kuwa baridi na isiyopendeza. Uchochezi wa wanaume kutoka kwa mama na dada zao huwaelekeza wanandoa kwenye ugomvi na hata kupigana. Katika hali hii, mke anaweza kukimbilia kuchukua hatua kali zaidi kama kujiua!

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 154

Mwanamke ambaye alikuwa katika siku zake za mwanzo wa ndoa, alimeza pini. Baada ya kufanyiwa upasuaji kwa lengo la kuondoa pini kutoka tumboni mwake, alisema; Kama juma moja hivi lililopita, niliolewa. Siku nilipoingia nyumbani kwa mume wangu, nilihisi kuwa na bahati kama wanawake wengine walioolewa. Lakini baada ya siku chache tu, mume wangu na dada yake walianza kunilaumu. Msimamo wao ulifanya maisha yangu kuwa magumu sana. Hatimaye niliamua kujiua na nikameza pini chache."

Mwanamke ambaye alikasirishwa na lawama za mume, shemeji yake, alijichoma moto na kufa kwa sababu ya majeraha makali."

Mwanamke ambaye alikuwa katika siku zake za mwanzo za kuolewa aliudhiwa sana na msimamo mbaya wa mama mkwe wake hivyo kwamba alijichoma moto hadi kufa."

Kwa hiyo, lawama, msimamo mbaya na maneno ya kashfa kutoka kwa mama, dada na kaka zao waume ni tabia ambazo zinaweza kuwa na madhara makubwa sana na hivyo mwanaume lazima atahadhari kuhusu usumbufu wao. Kama mambo yalivyo, haiwezekani kuwazuia watu wasiseme lakini inawezekana kutangua mazungumzo yao.

Mwanaume lazima atambue kwamba lawama zinazo elekezwa kwa mke wake na mama yake, dada zake na kadhalika hazina maana ya kuhurumiwa na kuwa na nia njema, isipokuwa sababu kubwa ni wivu, uadui uchoyo na kadhalika.

Mwanaume lazima akumbuke kwamba kwa sababu ya mke kwa kufanya uzingativu wa mume wake uelekee kwake, familia yake humuonea wivu na kumchukulia kama mporaji wa kijana wao. Kwa hiyo, hukimbilia kutumia njia za kuzuia mapenzi yao yasisitawi.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 155

Mabwana wapendwa kwa ufupi, mama, dada na kaka zenu wa aina hii hawajali furaha yenu katika ndoa, lakini hususan wao wanaangalia matakwa yao. Kama wangekuwa wanahusika na furaha yako na mke wako wangefanya vinginevyo.

Ni jambo la kushangaza kwamba wazazi hutoa sifa nyingi sana kwa mwanamke anayetarajiwa kuolewa na mtoto wao wa kiume, lakini mara mtoto wao anapooa wazazi hao hugeuka na kuwa kinyume.

Mabwana wapendwa msidanganywe. mapungufu hayo ambayo familia yako huyapachika kwa mke wako hayana umuhimu wowote; na hata kama si madogo, kumbuka kwamba hakuna mtu aliye kamilika.

Kwa vyovyote vile, je, dada na mama yako au wengine wanao mlaumu mke wako, wao ni viumbe vilivyo kamilikia?

Kuzingatia maneno yao ya kashfa ni hali ambayo itaathiri maisha ya familia yako. Inawezekana ukaishia kuachana, na matokeo yake ni kwamba unaweza kuteseka kiakili na kiuchumi.

Kuoa mara nyingine haitakuwa rahisi. Hata kama utapata mwanamke mwingine wa kuoa, haileweki kabisa kwamba atakuwa mkamilifu kuliko yule wa kwanza. Utahakikishaje kwamba familia yako hawatamtendea vibaya kama walivyofanya kwa mkeo wa kwanza?

Kwa hiyo, ni vema umwambie mama yako, dada yako na wengine kuanzia sasa kwamba mke wako anakufaa na kwamba unampenda. Lazima uwatangazie kwamba lazima waache kumlaumu mke wako au vinginevyo mke wako au wewe mwenyewe utasitisha uhusiano nao. Pindi watakapo hisi msimamo wako imara wataacha msimamo wao wa uchochezi na wewe na mke wako mtapata amani.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 156

Lakini, bahati mbaya, baadhi ya mama na dada hawaachi tabia hiyo kwa urahisi na hukimbilia kwenye mashtaka yenye nia mbaya kama vile ugoni.

Tatizo linakuwa kubwa sana hivyo kwamba mwanaume anaweza akamtaliki au hata kumuua mke wake kwa sababu ya maneno ya mama yake.

Wanandoa vijana waliomba kutalikiana kwenye mahakama ya Tabriz. Mwanaume alisema mahakamani: "Mke wangu huandika barua za mapenzi kwa kaka yangu anayeishi Isfahan. Niliziona baadhi ya barua hizo chache jana usiku." Mke wake alisema huku analia: "Mama mkwe wangu na wifi yangu hawanipendi na kunisumbua kila wakati. Lakini sasa kwa sababu matendo yao yenye fitina hayakumuathiri mume wangu, wameghushi barua kadhaa za mapenzi na wameziweka kwenye kabati langu la nguo ili wanichochee aniache." Mahakama iliwasuluhisha wanandoa hao na kumshauri mume kumwambia mama na dada yake kuacha kufanyia vitendo viovu kwa bibi harusi wao.

Mwanamke mwenye umri wa miaka thelathini na nne alijimwagia mafuta ya taa na kujichoma moto. Majirani waliuzima moto haraka na walimpeleka hospitalini. Alipokuwa hospitalini mwanamke huyo alisema: "Mimi huishi na mume wangu na mama mkwe. Kila wakati huniona mimi nina makosa. Hutoa visingizio na kwa kawaida yeye ni mkali sana. Wakati wote haachi kusababisha ugomvi baina yangu na mume wangu. Jana nilikwenda madukani kununua vitu na ghafla nilikutana na rafiki yangu wa siku nyingi tulipokuwa tunasoma. Tulizungumza kwa muda mfupi halafu nilirudi nyumbani. Mama mkwe wangu alianza kuniuliza kwa nini nilichelewa? Nilimweleza lakini hakutosheka. Aliniambia kwamba nilikuwa ninasema uongo na kwamba mwenye duka la nyama mtaani kwetu ni hawara yangu. Nilikasirika na kukata tamaa hivyo kwamba niliamua kujiua!"

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 157

Kwa hiyo, mwanaume kila mara anatakiwa kuwa na tahadhari na madai ya aina hiyo ambayo yanaweza kusababisha hatima ya hatari. Mume analazimika kufanya upelelezi kuhusu madai hayo kwa uvumilivu na asifanye uamuzi wa haraka.

Kama mambo yalivyo, wazazi wa mtu hufanya bidii na huteseka sana katika kumlea na kumkuza mtoto wao na hivyo huwafanya kuwa kituo cha matumaini yao yote. Wanamtegemea mtoto wao kuwa msaidizi wao watakapo kuwa wazee na mategemeo yao ni hayo tu. Kwa hiyo si haki mtu anapojitegemea asahau wajibu wake kwa wazazi wake. Lazima awatimizie matakwa ya hali zao hata baada ya kuoa. Lazima adumise heshima yao na kuwa mnyenyekevu kwao. Anao wajibu wa kuwasaidia kwa kuwapa fedha endapo wanazihitaji. Si vema kusitisha uhusiano wake na wazazi wake na lazima awe anawaalika nyumbani kwake. Lazima amuamuru mke wake na watoto wake waoneshe heshima kwao. Lazima amwelekeze mke wake aelewe kwamba endapo atawaheshimu wazazi wake, hawataona, umuhimu wa kumuudhi na wanaweza hata kujivunia yeye na kumsaidia.

Mwisho, wanawake wanakumbushwa kwamba hawana haki ya kutarajia waume zao kuwaacha wazazi wao. Matarajio haya wala hayawezekani kuwa ya haki. Mwanamke mwenye busara anaweza kuwatembelea wazazi wa mume wake kwa namna ambavyo kwamba wanaweza kumchukulia yeye kama mwenzie muhimu katika familia yao. Hii inawezekana tu kama atawaheshimu, atataka ushauri kutoka kwao, akiwapa msaada na kadhalika.

Mazungumzo haya yameandikwa kwa kina kwenye sehemu ya kwanza ambapo unaweza kufanya rejea kwa taarifa zaidi.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 158

SAMEHE MAKOSA YA MKE WAKO

Zaidi ya wale ambao Mwenyezi Mungu amewapa kinga wasifanye dhambi, hakuna mwanadamu aliyekamilika na sote sisi hufanya makosa mengi. Kama mambo yalivyo, hii ni kweli kwa wanamume na wanawake.

Kwa upande wa wanawake, anaweza kufanya makosa kwa kutokuwa na adabu kwa mume wake, kufanya kitu kinyume na matakwa yake kuwa mkali kwake, au kumwingiza kwenye hasara kiuchumi kwa sababu ya kuwa mzembe na kadhalika.

Kama mambo yalivyo, ni kweli kwamba wanandoa lazima waridhishane na waepuke kabisa kuudhiana wao kwa wao: Hata hivyo, hutokea mara chache kwamba mmoja wapo au wote watashindwa kukwepa kipengele hiki.

Baadhi ya wanaume hudhani kwamba wanatakiwa kuwa wakali kwa makosa ya wake zao kwa kuwa wanaamini hii kuwa ndio njia ya kuzuia kurudia kosa la aina hiyo.

Hata hivyo, uzoefu mara nyingi unaonesha matokeo kuwa kinyume chake kabisa. Mwanamke, ambaye mume wake ni mkali kwake, anaweza kuvumilia ukali wake kwa kipindi fulani, lakini hatimaye anaweza kuamua kujibu dhidi yake ikiwa kama matokeo ya kukatisha tamaa. Mke atazoea msimamo wake polepole hadi hapo atakapokuwa sugu.

Mume ambaye hatakuwa msamehevu kuhusu makosa ya mke wake, ni kwamba anamhamasisha mke wake kuwa jeuri na kukosa nidhamu. Anaweza kutaka kuendelea na msimamo huu ambapo kwa hakika atakabiliana na ugomvi mwingi wa mke wake. Wote wataishi katika hali ya uchungu kwa maisha yao yote.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 159

Au anaweza akamwacha mke alivyo na asijihusishe naye kwa ukamilifu. Katika mfano huu mke wake, ambaye atahisi ameshinda, atakuwa hajali ridhaa na matakwa ya mume wake. Hali hii inaweza kufika kiasi kwamba hata hapo mke anapofanya makosa makubwa ya kudhamiria, atanyamaza. Hapo tena ndoa yao itakuwa imepoteza uchangamfu na wanaweza kukimbilia kutalikiana.

Kumbuka kwamba talaka husababisha madhara pande zote mbili kwa sababu kuanza maisha mapya si rahisi. Itakuwa hakuna uhakika wa kuwepo furaha baada ya kutalikiana.

Kwa hiyo, ukali haufai kutumika kila wakati na mara nyingi husababisha matukio yasiopendeza ambayo mtu anaweza kuyasoma kwenye magazeti. Njia nzuri kuliko zote ni kuwa mwenye kiasi na kutenda kimantiki. Samehe makosa yote madogo na yasio ya kukusudia yanayofanywa na mke wao. Hakuna haja ya kupiga kelele kwa ajili ya kosa la mke wako ambalo limefanyika bila kukusudia.

Kama mambo yalivyo, mara kwa mara mtu anaweza kuwashauri wenzake ili kuwasaidia wasirudie tena kosa la aina hiyo.

Watu hufanya makosa mengi kwa kutokujua, kwa hiyo ni vizuri zaidi kuwa shauri kwa uvumilivu kusahihisha matendo au maoni yao yaliyopotovu.

Kwa hiyo, mke wako hawezi kulazimishwa kurekebisha makosa yake; lakini badala yake unatakiwa kumpa maelezo kuhusu kosa, ili aweze kufanya uchaguzi, yeye mwenyewe asirudie tena kosa hilo. Hivyo, si tu kwamba uelewano na kuheshimiana unabakia kama zamani, lakini pia kosa hilo litazuiwa na halitafanywa tena.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 160

Ni busara kwa mwanamume kumzuia kimantiki mke wake asifanye makosa, lakini kama ataendelea kufanya makosa, basi kwa mara nyingine amsamehe na asijali makosa yake. Si rahisi kwa mume kuendelea kumpa adhabu mke wake au kujaribu kuonesha hatia yake ili amweke katika hali ya kuomba msamaha. Hii ni kwa sababu wanawake ni wajeuri kwa kawaida; na ukali usio stahili huwafanya watoe majibu zaidi kuliko ya hapo mwanzo. Hii inaweza kufatiwa na matukio yasiyopendeza na ya kuhofisha, kama vile kuachana au mauaji.

Uislamu umelielewa jambo hili nyeti, ambapo wanamume wamepewa wajibu kwa wanawake zao.

Imamu Ali (a.s) alisema: “Wavumilieni wanawake katika hali zote na semeni nao vizuri; na kwa kufanya hivyo wanaweza kurekebisha matendo yao”

Imamu Sajjad (a.s) alisema: “Ni haki ya mke wako kwamba unamtendea wema, kwa sababu yupo chini ya dhamana yako na unatakiwa kumlisha na kuvesha na unasamehe makosa yake ya kijinga.”

Imamu Sadiq (a.s) aliulizwa: “Mwanamke anazo haki gani kwa mume wake, ambazo kama akizitimiza ipasavyo, ataonekana kuwa mtu mwenye matendo mema?” Imamu alijibu: “Lazima ampe chakula na nguo na amsamehe makosa yake aliyoyafanya bila kukusudia.”

Imamu Sadiq (a.s) pia alisema; “Yeyote anaye waadhibu wale walioko chini yake, asitarajie kuheshimiwa au kupata cheo cha juu.”

Mojawapo ya sababu za ugomvi miongoni mwa wanamume na wanawake ni kwamba mama wakwe huingilia mambo ya familia zao.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 161

Mama kabla ya kumuoza binti yake kwa mume, hudhani ya kwamba mkwilima wake kuwa mkamilifu na humthibitisha kwa binti yake kwamba ndiye atakaye mfanya awe na furaha. Atamheshimu na kumfanyia wema kwa matumaini ya kuwa na uwezo wa kurekebisha dosari zake ndogo ndogo baadaye.

Wakati mwingine mama mkwe humuona mkwilima wake hufuata matarajio yake na wakati mwingine hafuati. Katika mfano wa mwisho, anayo nia ya kumtengeneza mkwilima wake hadi hapo atakapo kubalika naye na katika utekelezaji wa hili hutumia kila njia zinazo wezekana kama vile za kwake mwenyewe na za uzoefu wa wengine na huanza kupanga namna ya kuwendea.

Wakati mwingine mama mkwe hujifanya mwenye huruma na wakati mwingine mkali. Anaweza akafanya mambo kama vile yeye ni mlezi na mfawidhi au anaweza akalalamika. Hata hivyo, chaguo zuri zaidi ni lile la kufanikisha lengo lake kwa kumvuta binti yake kwa kumfanya asifuate matakwa ya mume wake.

Huanza kumtumia binti yake na kwa hiyo humuamuru afanye tofauti nyakati mbali mbali. Kwa hiyo mwanaume humuona mke wake humlaumu leo na kesho kumuomba afanye kitu fulani.

Mwanamke mwenye uzoefu atafikiria kwamba mama angekuwa na huruma kuhusu ndoa yake na angefuata ushauri wake.

Hivyo kama mume wake hatafuata matakwa ya mama mkwe wake, ugomvi utaanza baina ya wanandoa na matokeo yake yanaweza kuwa kutalikiana au hata mauaji.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 162

Hii ndio sababu wanamume wengi hawaelewani na mama wakwe zao. Huwalaumu kwa utovu wa adabu wa wake zao na huamini kwamba mama wakwe zao huwafundisha mabinti zao tabia mbaya.

Haitakuwa wazo mbaya kama mtu anajifunza kuhusu malalamiko ya wakwilima wachache.

Bwana M. Javda ameandika: "Mama mkwe wangu ni pepo mbaya, zimwi na joka la vichwa viwili. Mungu na amwepushe asiliwe na mbwa mwitu. Ameyafanya maisha yangu kuwa machungu sana hivyo kwamba ninapata wendawazimu na ninahisi kama vile nikimbie niende milimani na majangwani. Si mimi tu, ambaye nimechoshwa na hali hii. Huu ni mfano wa kawaida na ninadhani asilimia tisini na tano ya wanamume wana athiriwa na hawa mama wakwe na asilimia tano nyingine labda hawana mama wakwe." Bwana F. Mohammed ameandika: "Mama mkwe wangu kila mara huingilia maisha yangu. Husababisha maudhi bila ya sababu ya maana. kila wakati husema maneno ya kashfa kuhusu familia yangu. Wakati wowote ninaponunua kitu chochote kwa ajili ya mke wangu, mama mkwe wangu, huanza kuonesha dosari kuhusu kitu hicho. Hukosoa rangi yake au mtindo na hujaribu kuthibitisha kwamba kitu hakina thamani kwa mke wangu." Bwana K. Parvis amendika: Mama mkwe wangu amenitendea kwa njia ambayo kwamba nimebakia kidogo nimtaliki mke wangu mara tatu. Huuma kama nge. Humfundisha mke wangu kuwa jeuri kwangu, kuacha kazi za nyumbani au kutarajia kisichowezekana kutoka kwangu. Wakati wowote anapokuja kututembelea, nyumba yetu hugeuka kuwa jahanamu. Kwa kweli sipendi hata kumuona."

Wanaume wengi hujaribu kukabiliana na mvuto wa wakwe zao kwa wake zao kwa kuwekea mipaka uhusiano wao. Huwakataza wake zao wasiende kwa wazazi wao. Kwa ufupi, wanaume hawaelewani kabisa na mama wakwe zao na huonesha kutokupenda kwao kwa kila namna iwezekanayo.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 163

Hata hivyo, mtazamo huu licha ya kwamba ni wa kawaida, si wenye mantiki na busara. Hii ni kwa sababu uhusiano wa mama na binti yake una nguvu sana na wa kimaumbile ambao hauwezi kuvunjwa kwa urahisi.

Inawezekanaje mwanaume kutarajia mke wake, kuwaacha wazazi wake ambao walitumia miaka mingi kumlea?

Matumanini haya hayatekelezeki na hata kama inatokea itakuwa kwa muda mfupi tu, kama ilivyo kwamba tendo lolote lisilo la kawaida halidumu muda wote.

Zaidi ya hayo kama mwanamke anahisi kwamba mume wake hawapendi wazazi wake, anaweza kuchukua msimamo kama huo kuhusu familia ya mume wake. Anaweza akawa hamtii, hamheshimu na kadhalika.

Juu ya hayo, msimamo huu wa mwanaume hutoa mwanya wa kisingizio kwa mama mkwe wake huingilia ndoa yake kwa ukali zaidi. Kwa ufupi, msimamo huu unaweza kusababisha matokeo mabaya na huenda yakawaelekeza wanandoa kutalikiana.

Kwa vyovyote vile kwa nini mwanaume ambaye anaweza kufaidika kutokana na kuelewana na wazazi wa mke wake, akimbilie hatua ya aina hiyo ambayo inaweza kumdhuru yeye na familia yake?

Mamlaka ya polisi wa India yalitoa taarifa kwamba mnamo mwaka 1971, sababu kubwa ya idadi ya matukio 146 ya watu kujiua wenyewe katika jiji la New Delhi ilikuwa uhusiano mbaya baina ya waume na mama wakwe zao."

Mwanaume ambaye alikatishwa tamaa na mama mkwe wake kwa sababu ya kujiingiza kwake, alimtupa nje ya teksi."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 164

Mwanaume alivunja fuu la mama mkwe wake kwa nyundo. halafu kaka wa huyo mtu akakasirika na baada ya kumjeruhi kwa kisu akatoroka na kupotea."

"Bwana…ambaye alikasirishwa na mama mkwe wake, alimwagia supu ya moto kichwani. Mama mkwe alipiga kelele na kupoteza fahamu. Alipelekwa hospitalini baada ya kupona akasema kwamba binti yake amemwambia mume wake kwamba anataka talaka na hakutaka kuishi naye zaidi ya hapo."

Mwanaume ambaye alichoshwa na mama mkwe wake, alijiua mwenyewe.

Labda inafaa kutaja mambo mawili hapa:
Ni dhahiri kwamba mama mkwe si tu ni adui kwa mkwilima wake, lakini ni kawaida yeye kumpenda mkwilima wake kama ilivyo jionesha mwanzoni mwa ndoa. Zaidi yake ni kwamba mama mkwe anajikuta yupo karibu na mkwilima wake kwa sababu ya kutaka kuona binti yake anafurahi. Kwa hiyo, mama mkwe anapoingilia maisha ya ndoa ya binti yake, haiwezekani kumaanisha kuwa kitu chochote isipokuwa kiwe na nia njema. Anamaanisha kuwa na huruma lakini wakati mwingine kwa sababu ya ujinga, huchukua hatua zisizo sahihi au hutoa ushawishi wenye madhara. Kwa hiyo, mtu asiwakosoe sana wake wa aina hii.

Uhusiano wa mama na mtoto ni wa asili ya maumbile ambao hauwezi kuvunjwa kwa urahisi, na yeyote anayefanya bidii ili kufanikisha hilo, kwa hakika atashindwa. Juhudi za aina hiyo ni kinyume cha kanuni za maumbile na haziwezi kuhalalishwa kwa vyovyote vile.

Kama vile mtu mwanaume anavyo wapenda wazazi wake, ndivyo ilivyo kwa mwanamke. Kwa hiyo, ni vizuri zaidi kuwa na uhusiano na wazazi wa wanandoa ambao unanufaisha pande zote mbili. Hii inawezekana tu kama

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 165

mtu anaonesha heshima na wema. Mwanaume anaweza kwa kutumia busara, heshima, utiifu na kadhalika kuwa na uhusiano mzuri na wazazi wa mke wake. Lazima aoneshe mapenzi yake kwa mtoto wao. Asimlaumu mke wake mbele ya wazazi wake. Aombe ushauri na msaada wa kiroho kutoka kwao. Inapotokea wanatoa ushauri au kukosea kitu fulani, mkwilima anatakiwa kuonesha hilo kwa upole na kimantiki kwamba hapo wamekosea. Asiseme nao kwa ukali.

Mwanaume aliyeoa anatakiwa kuona uhusiano mzuri baina yake na wazazi wa mke wake kama wajibu wake na siri ya mafanikio ya ndoa yao. Matokeo yake ni kwamba matatizo mengi ya kifamilia yanazuiwa yasitokee na mengine mengi zaidi hupatiwa ufumbuzi.
Kwa ufupi, si kila mara mama mkwe ndiye anayekuwa na hatia lakini wanamume wanatakiwa kuwa na busara ya kutosha na kuwa fanya kuwa na marafiki.

Wapo wanaume wengi ambao hufurahia uhusiano mzuri na mama wakwe zao.

Bwana Munuchehr ameandika: “mama mkwe wangu ni malaika au hata huzidi. Ninampenda zaidi ya ninavyompenda mama yangu mzazi, kwa sababu ni mwema na muelewa. Kila mara hutusaidia kutatua matatizo yetu. Kuwepo kwake ni dhamana na furaha ya familia yangu na ustawi wetu.”

Hata kama mtu anaye mama mkwe ambaye ni jeuri, mjinga na haiwezekani kuelewana naye, asimfanyie ukali. Wanawake wa aina hii wanaweza kufanya maisha ya mtu kuwa magumu, lakini ni vizuri kila mara kutoa majibu kwa upole dhidi ya tabia yao isiyofaa. Hii ni kwa sababu, kwa kuwa mwema kwao, mtu anaweza akapunguza hatari inayoweza kutokea kwenye ndoa yake.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 166

Wakati huo huo, mwanaume anatakiwa kuwa karibu na mke wake na amfanye mke amwamini yeye. Lazima azungumze naye kuhusu matendo mabaya ya mama yake na kuthibitisha kimantiki kwake matokeo yasiyopendeza yanayoweza kusababishwa na tabia ya mama mkwe wake.

Ikiwa mtu anaweza kutengeneza maelewano ya kina na mke wake, basi matatizo mengi ikiwa ni pamoja na lile la mama mkwe wake litatatuliwa.

Kwa hiyo usidharau tabia njema, uwe na busara na uifanyie wema familia ya mke wako ili mpate kufuzu katika ndoa yenu.

Imamu Ali (a.s) alisema; "Kukuza urafiki ni nusu ya busara."

Imamu Ali (a.s) pia alisema; Kujumuika na watu na kuwafanyia tabia njema humzuia mtu asifanye matendo mabaya na fitina."

Imamu Ali (a.s) alisema; Jumuikeni na mfanye wema. Jiepusheni na kununa na kufarakana."

UWE MSIKIVU

Mwanamke ni kiumbe mwenye hisia kubwa ambazo hutawala mantiki yake. Mwanamke ni mjinga na mwepesi kuhisi kuliko mwanamume. Mwanamke anaweza kudanganywa kwa urahisi zaidi na hawezi kudhibiti matashi ya hisia zake. Hawezi kuamua kwa busara pindi anapotibuliwa. Anaweza kufurahishwa au kutibuliwa kwa urahisi sana. Hivyo kama mwanaume ana usimamizi wa tabia na matendo ya mke wake, hatari za watu wengi zingeepukwa.

Ndio sababu dini tukufu ya Uislamu imemteua mwanamume kuwa kama mlezi wa familia yao na hufanya kuwa na wajibu kwa mambo ya familia.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 167

Mwenyezi Mungu anasema kwenye Qurani Tukufu:

﴿ ٱلرِّجَالُ قَوَّٰمُونَ عَلَى ٱلنِّسَآءِ بِمَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ
وَبِمَآ أَنفَقُوا۟ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ ۚ فَٱلصَّٰلِحَٰتُ قَٰنِتَٰتٌ حَٰفِظَٰتٌ لِّلْغَيْبِ بِمَا
حَفِظَ ٱللَّهُ ﴿٣٤﴾ ﴾

Wanamume ni wasimamizi wa wanawake kwa kufadhiliwa na Mwenyezi Mungu baadhi yao juu ya baadhi, na kwa mali yao wanayo yatoa. Basi wanawake wema ni wale wenye kutii na wanao jitihada hata katika siri kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameamrisha wajilinde." (4:34).

Kwa hiyo mwanaume anayeonekana kama mlinzi wa familia yake, asifanye uzembe kuhusu matendo ya mke wake. Kila mara lazima afawidhi mambo ya mke wake na kufuatilia matendo yake. Lazima mume ahakikishe kwamba mke wake hapotoki au kujumuika na aina ya watu wabaya. Mume lazima amweleze mke wake kimantiki kuhusu madhara ya rafiki mbaya. Asimruhusu kuondoka nyumbani akiwa amevaa nguo zisizofaa au zile zinazosababisha ashiki ya kijinsia. Asimruhusu mke wake ashiriki kwenye shughuli ovu au kuhudhuria mikutano isiyofaa.

Ni kweli kwamba kama mwanamke akiachwa peke yake katika matendo yake na kuchanganyikana na watu, inawezekana akanasa kwenye mtego wa watu wenye akili potovu na huishia kwenye upotovu.

Wanaume wanashauriwa kuangalia idadi ya wanawake ambao kwa sababu ya uzembe wa waume wao wamenasa kwenye mtego wa uovu. Wapo wanawake wengi ambao wamedanganywa kwenye karamu za usiku. Familia nyingi zimevunjika na watoto wengi wamepoteza familia zao. Kwa sababu ya mikusanyiko hiyo.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 168

Mwanaume anaye mruhusu mke wake kuondoka nyumbani akiwa amevaa nguo zisizofaa, kuwa na marafiki wabaya na hamzuii kuhudhuria mikusanyiko yenye uharibifu, kwa kweli atakuwa anafanya kosa kubwa sana la uhaini kwake, kwa mke wake na kwa watoto wake.

Msimamo huu ungemwelekeza mke wake kwenye mamia ya sehemu za hatari ambamo hawezi kujinasua kwa urahisi. Petroli hushika moto kwa urahisi sana, kwa hiyo ni tendo la kipumbavu kuacha petroli karibu na moto na kudhani kwamba haitashika moto.

Ujinga ulioje wa watu ambao huwaruhusu wake zao au mabinti zao kujionesha mitaani huku wakiwa wanavaa nguo zisizofaa na wakati huo huo hawapendi nadhari au kutupiwa macho na wanaume kwa sababu ya mavazi yao!

Uhuru usio sahihi wa aina hii unayo matokeo mabaya sana. Kama mwanamke amefaulu kumshinda mume wake kuhusu matamanio yake yasiyo halali, ataongeza matakwa hayo hadi kwenye kiwango ambacho atafanya mambo yake kwa uhuru bila kumjali mume wake. Hii itasababisha matukio ya uovu kwenye familia.

Ndio maana Mtume (s.a.w.w) alisema: “Mwanaume ni mlezi wa familia yake na mlezi yeyote anao wajibu kwa wale walio chini kuwatimizia mahitaji yao.”

Mtume (s.a.w.w) pia alisema: “Waamrisheni wanawake kufanya mema kabla hawajakufanyieni ninyi uovu.”

Kwa nyongeza Mtume alisema: “yeyote anaye mtii mke wake, Mwenyezi Mungu atamtupa kwenye moto akitanguliza uso wake.”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 169

Mtume aliulizwa: “Aina gani ya utiifu unaomaanishwa hapa?” Mtume (s.a.w.w) alijibu: “Ni hapo ambapo mume humruhusu mwanamke ambaye humwomba mume wake ruhusa ya kwenda kwenye hamamu ya nje, watu kuhudhuria harusi, sherehe na mikusanyiko ya kutoa rambi rambi akiwa amevaa nguo za kumfedhehesha.”

Imamu Sadiq (a.s) alisema: “Furaha kamili ya mwanaume ni kwamba awe mfawidhi na kiongozi wa familia yake.”

Mtume (s.a.w.w) wa Uislamu alisema: “Mtu yeyote anayemruhusu mke wake ambaye amejipamba, kuondoka nyumbani kwake ni mtu mwenye roho ya kikatili na yeyote atakaye mwita hivyo, atakuwa hakufanya dhambi. Na mwanamke yeyote ambaye mume wake humruhusu kutoka nyumbani kwake akiwa amejipamba na kujipulizia manukato, kila hatua atakayo tembea, Mwenyezi Mungu atamjengea nyumba mume wake huyo katika Jahannamu.”

mwisho ninawakumbusha kuhusu mambo mawili:
Ni sahihi kwamba mwanaume anatakiwa kuwa na hadhari kwa mke wake lakini zoezi hili linatakiwa kufanywa kwa uangalifu na busara. Mume hatakiwi kukimbilia kukasirika au matumizi ya nguvu. Asimwoneshe mke wake kwamba anaamuriwa au vinginevyo atatoa jibu kwa njia isiyopendeza. Njia iliyo nzuri kabisa, kwa mwanaume ni kuwa na huruma na uelewa. Lazima atekeleze zoezi hili kama mwenza mwenye upole na amwambie mke wake kuhusu madhara ya matendo maovu. Lazima atengenezewe mazingira ya kuchagua njia iliyo nyooka yeye mwenyewe kwa shauku na hamu.

Mwanaume anatakiwa kuwa na wastani, ni kwamba wala asiwe mkali sana na kiherehere ama asiwe mzembe.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 170

Mwanamke, kama alivyo mwanaume, anahitaji uhuru na anatakiwa apewe uwezo wa kujiamulia la kufanya kwenye makundi yake kwa usawa unatakiwa.

Lazima mwanamke awe huru awe huru kuwasiliana na wazazi wake, kaka zake na dada zake, na lazima aruhusiwe kuwa na watu wa aina inayofaa.

Kwa ufupi, ipo mifano isiyo ya kawaida ambapo mwanamke ananyang'anywa utashi wake. Lakini hata kwenye mifano kama hiyo mtu hatakiwi kuvuka mpaka uliowekwa na kuwa mkali sana. Ukali wa kupita kiasi unayo madhara. Huharibu mazingira ya urafiki na husababisha maudhi. Mwanamke anaweza akajibu kwa ukali zaidi kutokana na ukali wa mume wake. Mke anaweza hata kuomba talaka.

Mwanamke kijana, mke wa… alimwambia mwandishi wa habari mahakamani: "Niliolewa na Bwana….Miaka mitano iliyopita. Tunao watoto wawili; mmoja wa kiume na mwingine wa kike. Wakati fulani mume wangu amekuwa anamchukulia kila mtu kwa namna ya ubeuzi. Haniruhusu mimi kushirikiana na mtu yeyote. Hata hufunga milango ya nyumba anapoondoka nyumbani. Sisi ni wafungwa ndani ya nyumba yake. Sasa, siwezi hata kwenda kwa wazazi wangu. Watu wa familia yangu hawatutembelei, kwa sababu yake. Sijui nifanye nini! Kwa upande mmoja ni kwamba siwezi kuishi naye, na kwa upande mwingine, nina wasi wasi kuhusu hatima ya watoto. Kwa hiyo, niliamua kuleta shauri langu kwenye mahakama hii; labda wanaweza wakapitisha uamuzi fulani."

Wanaume kama mume wa huyu mwanamke, kwa bahati mbaya ni wakali sana na si watu wa kawaida hivyo kwamba wake zao, licha ya kutaka kuishi pamoja na waume zao, huomba talaka. Wake zao huudhika sana, licha ya kuwa na watoto, wapo tayari kutengana nao.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 171

Kwa nini mwanaume amkatae mke wake asishirikiane na ndugu zake wa karibu? Kwani haelewi kwamba ukali ukizidi kiasi, hutayarisha uwanja kwa baadhi ya wanawake kukengeuka? Kwani hajasikia au hajaona familia zilizosambaratika kutokana na tabia ya aina hii?

Hata kama mke wa mtu atavumilia ukali wa mtu, patakuwepo upungufu wa huba inayo changamsha mazingira ya familia ndani ya nyumba. Inawezekanaje mtu kutarajia mke aliyeko kifungoni kuwa mwema kwa mume wake na watoto au kufuatilia kazi za nyumbani kwa hamu?

HAKI ZA KINIDHAMU ZA MUME

Ingawaje mume na mke ambao hutengeneza maisha ya pamoja ya familia, hugawana na kushirikiana katika kuendesha mambo ya nyumba yao, wanaweza kuwa na maoni tofauti kuhusu mambo fulani. Mwanaume anaweza kuhisi kwamba ni yeye ndiye anayetakiwa kuwa na uamuzi wa mwisho kuhusu mambo ya familia, bila kupata upinzani kutoka kwa mke wake. Wakati huo huo mke wake anaweza akakataa kazi yake kama upande uliomtiifu. Ubishi na ugomvi unaweza ukaanza kwa sababu kila upande unajaribu kuanzisha mamlaka juu ya upande mwingine. Suluhu nzuri zaidi ya tatizo kama hili ni kwamba pande zote zinatakiwa kuacha kujionesha kama unao mamlaka makubwa zaidi kuzidi upande mwingine, na kujaribu kupata ufumbuzi wa matatizo yao kwa njia ya mazungumzo na uelewano wa kina. Hii inawezekana tu kufanikiwa kama pande zote zinaacha ukaidi.

Baadhi ya wanamume huwaamuru wake zao kufanya mambo mengi na kama wakikabiliwa na upinzani, wanadhani ni sahihi kuwashika, kuwaadhibu au hata kuwapiga wake zao. Msimamo huu si sahihi kabisa. Mwanaume wa kipindi cha ujahiliya ambaye alipungukiwa ubinadamu, alifanya mazoea ya kuwapiga na kuwaumiza wake zao.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 172

Mtukufu Mtume (s.a.w) alipiga marufuku kuwapiga wanawake, isipokuwa katika hali isiyozuilika ambapo adhabu huwa wajibu."

Mtume (s.a.w) pia alisema Nina shangazwa na mwanaume anaye mpiga mke wake, ambapo ni yeye mwenyewe, zaidi ya mke wake ambaye anastahili kupigwa. Enyi watu, msiwapige wanawake zenu kwa kutumia fimbo kwa sababu tendo la namna hiyo lina ulipizaji kisasi."

Kumuonea mwanamke ambaye kwa utashi wake amekubali kuolewa na mwanamume, ambaye anataka kupata faraja na utulivu na yeye, na ambaye anamtarajia mume wake kushirikiana wote katika matatizo, si sahihi. Kwa kweli Mwenyezi Mungu anamdhamini mwanamke kwa mume wake kwa njia ya ndoa na maonevi ya mwanaume kwa mke wake ni kutokuwa mwaminifu kwa dhamana ya Mwenyezi Mungu.

Imam Ali (a.s) alisema; Wanawake wamedhaminiwa kwa wanamume na kwa hiyo, wao si wamiliki wa bahati zao au mabalaa yao. Wao wapo na nyinyi kama dhamana ya Mwenyezi Mungu, kwa hiyo msiwaumize na msifanye maisha yao kuwa magumu."

Mwanaume ambaye humpiga mke wake, hulazimisha uharibifu kwenye roho hivyo kwamba anaweza akapata mateso yasiyo elezeka na upendo wa familia na uchangamfu unaweza ukatoweka kabisa. Mwanamume mwenye ghadhabu anaweza kudunisha uhusiano mzuri wa ndoa na mke wake na kushushiwa hadhi? Hii kwa kweli ni aibu.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Enyi wanaume! Inawezekanaje yeyote miongoni mwenu ampige mke wake na baadaye amkumbatie?"

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 173

Mwanaume, isipokuwa awe na haki ya pekee kwa mke wake, inayofanana na zile ambazo zitatajwa kwenye sura hii haruhusiwi kisheria kumlazimisha mke wake kufanya jambo lolote au kukimbilia matumizi ya kipigo kuhusu utovu wa utiifu. Mathalani mwanamke kisheria hawajibiki kufanya kazi za nyumbani kama kufagia, kupika, kufua, kutunza watoto, kushona na kadhalika. Licha ya kuwa wanawake walio wengi hufanya kazi hizi za mama wa nyumbani kwa kutaka wao wala si za lazima.

Wanaume wanatakiwa kuwashukuru wake zao kwa kazi zao za ndani ya nyumba. Kwa hiyo, hapana mwanamume mwenye haki ya kuhoji au kumwadhibu mke wake anapokabiliwa na kukataa kwake kutekeleza kazi za nyumbani.

Uislamu unapendekeza adhabu ya kipigo kwenye mifano miwili tu ambapo hali zake hukiukwa:

Mfano wa kwanza; Mwanaume ameruhusiwa kisheria katika Uislamu kupata na kutoshelezwa na tendo la Ndoa na kupata starehe ya kila aina kutokana na uhusiano huu na mke wake. Mke anawajibika kisheria kukubali matamanio ya ngono kutoka kwa mume wake. Kama mwanamke anakataa kumtosheleza mume wake, mume katika hatua ya kwanza anatakiwa amshawishi katika njia na mpangilio unaostahili. Hata hivyo, kama mwanaume anahisi kwamba mke wake anataka kuleta hali hiyo, basi kwa kuchunguza hatua zilizo bainishwa anaweza kumwadhibu.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ ٱلرِّجَالُ قَوَّٰمُونَ عَلَى ٱلنِّسَآءِ بِمَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ وَبِمَآ أَنفَقُوا۟ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ ۚ فَٱلصَّٰلِحَٰتُ قَٰنِتَٰتٌ حَٰفِظَٰتٌ لِّلْغَيْبِ بِمَا حَفِظَ ٱللَّهُ ﴿٣٤﴾ ﴾

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 174

Wanaume ni wasimamizi wa wanawake kwa kufadhiliwa na Mwenyezi Mungu baadhi yao juu ya baadhi, na kwa mali yao wanayo yatoa. Basi wanawake wema ni wale wenye kutii na wanao jitihada hata katika siri kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameamrisha wajilinde." (4:34).

Kwa hiyo, Qura'ni inamruhusu mume kumpiga mke wake kama hatua ya mwisho ya kutoa adhabu, kama inatokea mke anaonesha tabia mbaya kwa mume wake kuhusu matakwa yake ya ngono. Hatua ya kwanza ni kutoa ushauri. hatua ya pili; Mwanaume aache kulala kitanda kimoja na mkewe au amgeuzie mgongo na kwa njia hii anatakiwa kuonesha hasira yake. Kama hakuna jibu linalotarajiwa hadi mwishoni mwa hatua ya pili na bado mwanamke anaendelea kukataa, mume anaruhusiwa kumpiga mke wake kidogo.

Mume, hata hivyo, haruhusiwi kuvuka mpaka uliowekwa na kukimbilia kumuonea. Wanaume wanakumbushwa kuhusu yafuatayo:
Lengo la adhabu ya kipigo kwa mke wa mtu linatakiwa kuwa njia ya kumuelimisha na si kulipiza kisasi.

Kipigo kinatakiwa kufanywa kwa kutumia mkono au mti mwembamba na mwepezi.

Kipigo kikali cha kuweza kubadilisha rangi ya ngozi kuwa buluu au nyekundu hakiruhusiwi na mhusika lazima apigwe faini (dia).

Kupiga sehemu nyororo na nyeti za mwili kama vile macho, kichwa tumbo na kadhalika, hakiruhusiwi.

Adhabu ya kipigo haitakiwi kuwa kubwa mno hivyo kwamba haitasaidia kuanzisha hasira na fikra mbaya miongoni mwa wanandoa kumwelekeza mke kwenda kwenye kiasi cha kutotii zaidi.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 175

Mwanaume (anaye nuia kumwadhibu mke wake kwa kutumia njia hii) anatakiwa kukumbuka kwamba ataendelea kuishi na mke wake na kwamba upendo wa familia usiharibiwe.

Mwanaume haruhusiwi kumpiga mke wake kama zipo sababu halali zilizomfanya asikubali matakwa yake. Mathalani kama mke yupo kwenye siku zake za hedhi, saumu ya mwezi wa Ramadhani, awe amevaa vazi la Hija (Ihram) au mgonjwa. Sababu hizi zinakubalika na mwanamume hawezi kumwadhibu mke wake kwa kukataa matamanio yake kwa sababu hizo zilizotajwa.

Mfano wa pili; Mwanamke anaweza kutoka nje hapo tu ambapo ameruhusiwa na mume wake. Akitoka nje bila ruhusa hairuhusiwi kisheria na kufanya hivyo ni dhambi.

Hadith imesimuliwa kwamba Mtume (s.a.w.w) hakumruhusu mwanamke yeyote kutoka nje ya nyumba yake bila ruhusa ya mume wake. Alisema; Mwanamke yeyote ambaye hutoka nje ya nyumba yake bila ruhusa ya mume wake, atapata laana kutoka kwa malaika wote walioko mbinguni na wote wale wanao muona, wawe majini au wanadamu, hadi anaporudi nyumbani kwake."

Hii ni hali ya mume yeyote ambayo lazima iangaliwe na wake zao.

Lakini wanaume hawatakiwi kuwa wakali sana kwa wake zao. Ni bora zaidi wao kuwaruhusu wake zao kutoka nje kila inapowezekana.

Hali hii ya wanaume haimaanishi kuonesha nguvu au kujaribu kuwashinikiza wake zao, lakini ni njia ya kuwazuia wanawake wasiende kwenye sehemu zisizo pendeza na zisizofaa.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 176

Kuwa mkali sana si tu kwamba ni jinsi isiyofaa, lakini inaweza kuathiri uhusiano wa familia au hata kumsukuma mwanamke kuelekea kwenye utovu wa nidhamu na uovu.

Mwanaume lazima amzuie mke wake asiende kwenye sehemu za mikusanyiko zenye uovu na zisizofaa. Huu ni wajibu wa kidini kwa wanawake kuwatii waume zao. Mwanamke asiye mtiifu anaweza kuadhibiwa na mume wake. Hapa tena adhabu inatakiwa kutekelezwa hatua kwa hatua.

Hata hivyo, mwanamke anaweza kutoka nje ya nyumba yake kwa sababu maalum bila ya ruhusa ya mume wake na wanamume hawaruhusiwi kuwaumiza wake zao katika mifano kama hiyo:
Kutoka nje kwa ajili ya kujifunza amri muhimu za dini.

Kutoka nje kwa ajili ya Hija pale ambapo anao uwezo muhimu wa kifedha na kutekeleza Hija.

Kutoka nje ya nyumba kwa ajili ya kulipa deni almuradi deni hilo haliwezi kulipwa bila kutoka nje.

WANAMUME WA KUTUHUMU

Ni haki ya wanaume kuchunguza wake zao lakini si kwenye kiwango cha tuhuma na kutokuaminiana. Wanaume wengine hutuhumu na kutilia shaka uaminifu wa wake zao. Hii ni hatari na kufanya maisha kuwa magumu kwa familia yote.

Mwanaume anayesumbuliwa na tabia hii, wakati wote hutafuta dosari na kukusoa. Humfuatilia mke wake kwa karibu sana kwa humfuata kila

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 177

aendako. Hupata ushahidi wa kusaidia sababu yake ya kutuhumu kutoka kwenye kila kitu. Kama akimuona au akiona picha ya mwanaume kwenye vitu vyake au akiona barua aliyoandikiwa na mwanaume au akimwona mwanaume anamtazama, atapata uhakika kuhusu kutokuaminika kwa mke wake. Kama mke wake akificha barua kutoka kwake, atadhani ni barua ya mapenzi. Asipoonesha mapenzi yake kama ilivyokuwa zamani atatilia shaka uaminifu wake.

Anaweza hata kufikiria kwamba kwa kuwa binti yake hafa nani na yeye, mke wake lazima alizini.

Mifano yote ya aina hii inaweza kuonekana kama uthibitisho imara wa udanganyifu wa mwanamke wa mume anayemtuhumu mke wake. hali huwa mbaya sana kama ndugu au rafiki akikubaliana na tuhuma yake.

Familia nyingi ambazo zimeathiriwa na maradhi haya, huteseka sana. Mwanaume anaweza kujishughulisha kama mpelelezi ndani ya nyumba. Na mke wake anaweza kuhisi kama vile alikuwa amefungiwa jela. Wote wawili wanaweza kupata maradhi ya kiakili na ndoa yake kuwa hatarini. Wanaweza hata kukimbilia kutalikiana au mauaji.

Ipo mifano mingi ya kuua na kujiua ambayo imetokea kutokana na tuhuma. Katika hali hii mwanaume na mke wake lazima watahadhari kuhusu uwezekano wa matokeo mabaya sana na kwa kutumia busara na utambuzi, huondoa hatari yoyote, ambayo ingetisghia ndoa yao au hata uhai wao. Wanatakiwa tu kuwa na tahadhari ya uwezekano wa hatari na kuweza kufikiri bila wasi wasi ili waweze kushinda matatizo yao.

Mwanaume anatakiwa kuacha ushabiki wake na wivu wa kupindukia. Lazima atumie mantiki. Lazima atambue kwamba kumtia hatiani mke

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 178

wake kwamba ni mgoni si jambo dogo na kwamba madai ya aina hii huhitaji uthibitisho uliokamilika.

Mwenyezi Mungu amesema kwenye Qurani Tukufu:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱجْتَنِبُواْ كَثِيرًا مِّنَ ٱلظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ ٱلظَّنِّ إِثْمٌ ﴿١٢﴾ ﴾

"Enyi mlioamini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi . . ."(49:12).

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema: "Yeyote awaye, ambaye atamshitaki kwa kumsingizia mke wake kwa kuzini atapoteza thawabu zake zote za matendo mema kama vile ambavyo nyoka huvua ngozi yake ya zamani. Na kwa kila unywele kwenye mwili wake, dhambi elfu moja zitaandikwa kwenye rekodi yake (kwa ajili ya siku ya hukumu)."

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) pia alisema: "Mtu yeyote ambaye atamshitaki mwanaume au mwanamke muumini kwa kumsingizia, Mwenyezi Mungu atamning'iniza kwenye lundo la moto ili apate adhabu ya dhambi yake siku ya Hukumu." 201.

Alimuradi kutokuaminika kwa mwanamke hakujathibitishwa kwa ushahidi ulio thabiti, mwanaume hana haki yoyote ya kumshitaki, vinginevyo atakuwa anafanya dhambi ambayo, kufuatana na Uislamu ataadhibiwa kwa kuchapwa viboko themanini.

Ushahidi utokanao na dhana hauoneshi lolote. Barua za zamani, picha na kadhalika hazithibitishi lolote.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 179

Kutunza vitu kama hivyo si sahihi, lakini hili ni kosa ambalo hufanywa na vijana wengi na si jambo la kujihusisha nalo kabisa.

Kama mwanamke anaonekana anazungumza na mwanaume mgeni, licha ya kwamba si sahihi yeye kufanya hivyo, jambo hili haliwezi kuaminika kuwa uthibitisho wa kutokuaminika kwake.

Hii ni kwa sababu inawezekana alifikiria ingekuwa ni jeuri kutokuzungumza na mwanaume huyo, au inawezekana mwanamume huyo hakuwa mgeni lakini alikuwa rafiki yake baba yake au kaka.

Kama mwanamke anampongeza mwanaume, ingawa asingefanya hivyo, inawezekana kuwa hiyo ilikuwa kurahisisha na kwa hiyo haiwezekani liwe tendo la kuonesha kutokuaminika kwake.

Kama mwanamke anasema uongo kuhusu uhusiano fulani au akificha barua zake, inawezekana iwe kwamba ipo sababu nzuri ya kufanya hivyo au anaweza kuogopa mashtaka ya mume wake yasio na maana.

Kama mwanamke amekuwa hamchangamkii mume wake, inawezekana ametibuliwa naye, inawezekana ni mgonjwa au anaweza kuwa na matatizo mengine.

Kwa ufupi, katika mazingira yote ambayo yanaweza kuonesha dalili za kutokuwa mwamnifu anaweza kupata sababu nyingi na nzuri zinazotengeneza uwezekano wa makosa yeyote kuwa bure.

Bwana mpendwa! Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu acha tabia ya kutuhumu. Jione wewe mwenyewe kuwa mwamuzi wa haki na ulione tatizo kimantiki. Pima kiwango cha uwezekano wa mkeo kutokuwa mwaminifu na uelewe kama ndivyo, ni tuhuma tu au hata la kuaminika?

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 180

Sisemi kwamba wewe usijali na uwe mzembe lakini unatakiwa kuchukua hatua kufuatana na ushahidi ulio nao na si zaidi ya hapo. Kwa nini ukuze tatizo kwa kufuata tuhuma isiyo na msingi na uyafanye maisha kuwa magumu kwako na familia yako. Wewe ungejisikiaje kama mtu yeyote angekushitaki kwa jinsi isiyo ya haki? Kwa nini ujifedheheshe mwenyewe na mke wako? Kwa nini usimhurumie mke wako? Imepata kukujia fikira kwamba hatimaye mke wako anaweza akukengeuka kwa sababu ya wewe kutokumwamini na mashitaka ya kumsingizia?

Imamu Ali (a.s) alimsimulia mwanae Imamu Hasan (a.s): "Uwe mwangalifu usifanye mambo kama mtawala ambapo haupo hivyo kwa sababu hii inawezekana kuwaelekeza watu wanaofaa kwenye dhambi"

Kama unamtuhumu mke wako, usimwambie mtu yeyote unayemuona, kwa sababu wanaweza kuthibitisha tuhuma yako kwa vile ni maadui zako, wepesi kuamini au uzembe. Wanaweza hata kuimarisha hutuma yako na kukusababishia ukosefu wa furaha katika dunia hii na akhera. Hususan, usimwambie mama yako au dada yako kwa sababu ni kawaida watakubaliana na wewe na kwa hiyo kuongezea tuhuma yako. Lazima utafute ushauri kutoka kwa watu wenye busara na marafiki na ndugu wenye uzoefu.

Msimamo mzuri zaidi, hata hivyo, ni wewe mume kuzungumza na mke wako na mwambie akueleze. Lakini usitake kuthibitisha uhalifu wake. Sikiliza yale ambayo wanakuambia na uamue kama mwamuzi mwenye haki ambaye hana upendeleo.

Angalau ujaribu kumuamini na uchukulie kana kwamba shemeji yako wa kiume anakuletea ushahidi juu ya dada yako wewe kutokuwa muaminifu. Kwa nini ulishughulikie jambo hili bila huruma na kumuona mhusika kuwa mhalifu aliye thibitishwa?

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 181

Uwe na busara na uvumilivu, vinginevyo utamwacha bila sababu ya maana. Kama unavumili mateso ya kuwa mtalaka lakini unao uhakika gani kuhusu mke wa ndoa ijayo? Bado utaendelea kuwa unatuhumu. Kosa lao ni nini kama ni wewe ambaye unasumbuliwa na maradhi haya? Uwe na busara na jaribu kuelewa tatizo lako mwenyewe.

Uwe na tahadhari usije ukajiua au kumua mke wako. Kwa sababu, utaharibu maisha yako hapa duniani na Mwenyezi Mungu Mweza atakuwadhibu huko Akhera.

Lazima uelewe kwamba kumwaga damu siku moja kitendo hicho kitajulikana halafu ama utanyongwa au utafungwa kifungo cha maisha.

Kama hutakubaliana na jambo hili basi tazama takwimu za waliotiwa hatiani.

Wake za wanaume wenye ugonjwa wa kutuhumu pia wanao wajibu mkubwa kuhusu familia zao. Wanawake hawa lazima wajitolee muhanga na kuthibitisha uwezo wao katika hali ngumu kama hiyo.

Mama mpendwa kwanza kabisa mume wako ameambukizwa ugonjwa wa hatari ambapo yeye, kwa kutaka yeye mwenyewe, huchukua hatua zisizo sahihi ambazo zingehatarisha familia yenu.

Lazima uoneshe mapenzi yako kwake kadiri uwezavyo. Lazima awe na uhakika kwamba ni yeye tu katika maisha yako. Uwe mvumilivu kuhusu tabia yake, usimpigie kelele, usikatae kusema naye na usiwe kaidi kwake.

Ukihisi kwamba anafuatilia barua zako au anadhibiti kurudi na kutoka kwako nyumbani, usifanye upinzani. Mwambie kila kitu, mwambie ukweli. Epuka kusema uwongo au kukanusha matukio ambayo yametokea.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 182

Kama akigundua kwamba umemdanganya kuhusu suala lolote, ataona hilo kama uthabitisho kuhusu udanganyifu wako, ambapo haitakuwa rahisi kurekebisha uharibifu wake.

Kama mume wako mwenye maradhi ya kituhuma akikuzuia ushirikiane na mtu fulani au anataka ufanye kazi fulani, basi kubali neno lake vinginevyo sababu ya wasi wasi wake kwako itaimarika. Kwa ufupi epuka matendo yote ambayo yanaweza kumfanya akutuhumu.

Imamu Ali (a.s) alisema: "Yeyote anayejiweka wazi kwa shutuma, asiwalaumu wale wanao mtuhumu."

Kama mume wako anaonesha chuki kwa mtu yeyote, lazima uache mawasiliano na mtu huyo kabisa.

Bibi mpendwa! Ni bora zaidi wewe kuiweka familia yako pamoja kwa lengo la kudumisha urafiki na watu wengine. Usidhani kwamba wewe ni mtumwa kwenye minyororo ya mume wako, lakini tambua kwamba bado wewe ni mke wa mwanaume.

Kumbuka ulipofanya mapatano ya ndoa na mume wako, ulikubali mgawo wote wa nyakati za furaha na huzuni katika maisha. Hivi itakuwa haki wewe kumtendea mabaya mume wako ambaye anaumwa maradhi ya kutuhumu? Weka pembeni mawazo yasiyo pevuka na uwe na busara. Kwa jina la Mwenyezi Mungu kujitolea kwako kwa kiwango chochote kwa ajili ya familia yako ni kitendo cha manufaa. Mwanamke mzuri ni yule anaye weza kuvumilia hali ngumu.

Imamu Ali (a.s) alisema: "Jihadi ya mwanamke ipo kwenye kuvumilia matendo ya kashifa na hamasa ya mume wake."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 183

Usifanye jambo lolote ambalo lingemfanya mume wako akutuhumu. Usiwatazame wanaume wengine.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: Mwenyezi Mungu atamkasirikia sana mwanamke aliyeolewa anayependa kuwatazama wageni."

Usishirikiane na wanaume wageni. Usiondoke nyumbani bila ruhusa ya mume wako. Usipande magari ya wageni. Usafi wako tu peke yake hautoshi, lakini ungeepuka kitu chochote ambacho kingeamsha tuhuma ya mume wako. Inawezekana akutuhumu kwa mambo madogo sana kutokana na tabia yako.

Mwanamke mwenye umri wa miaka 27 alisema mahakamani; Ilikuwa wakati wa baridi ya mwaka 1963, ambapo ilikuwa siku ya barafu niliingia kwenye gari la mjomba wa rafiki yangu. Aliniambia kwamba mjomba wake angenipeleka hadi nyumbani kwangu kwa gari lake. Nilikubali nikaingia kwenye gari lake. Tulipofika nyumbani mume wangu alikuwa amesimama karibu na mlango wa nyumba na kwa vile sikutaka mume wangu kuniona ndani ya gari la mtu mwingine nilimwomba mjomba wa rafiki yangu aendelee na safari na alifanya hivyo. Baadaye mume wangu ambaye alikwisha niona ndani ya gari hilo, aliniuliza kuhusu suala hili, lakini nilikanusha kila kitu. Akawa ananituhumu zaidi na ilifika kiwango ambapo hakuamini hata ushahidi wa rafiki yangu. Sasa ni miaka minane wala haishi na mimi ama kunipa talaka. Sijui hata la kufanya."

Unadhani ni nani wa kulaumiwa katika hadith hii? Ningesema kwamba mwanamke ana hatia zaidi kuliko mume wake. Ni mwanamke ambaye kwa uzembe wake na wepesi wa fikira, alijiweka yeye na mume wake katika hali hii.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 184

Kwanza, kabisa mwanamke hangekubali msaada wa lifti ya gari la mgeni kwani hilo si jambo sahihi kufanywa na mwanamke yeyote. Haistahili na ingeweza kuwa hatari.

Pili, hangefanya alivyofanya baada ya kumuoana mume wake. Angesimamisha gari na kumpa mume wake maelezo ya kina.

Tatu, mojawapo ya makosa ya mwanamke ilikuwa kumwambia dereva kuendelea na safari.

Nne, hangekataa baada ya kuulizwa. Angeeleza kila kitu katika hatua hii ya kuchelewa na ingesaidia kupata ufumbuzi wa tatizo.

Kama mambo yalivyo, pia mwanaume alikosea. Si lazima aone tukio hili kama ndio ushahidi wa kutoa uamuzi kuhusu hatia ya mke wake. Lazima afikirie uwezekano kwamba mke wake inawezekana alipanda gari la mgeni kwa uzembe na halafu labda kwa sababu ya woga alimwambia dereva asisimamishe gari na kama ilivyo kawaida akakanusha jambo lote.

Lazima apeleleze jambo hili mara atakapo hakikisha kwamba hana hatia, lazima awe msamehevu.

MWANAMKE ASIYE MWAMINIFU

Mara tu mwanamke akionekana ana hatia ya kuzini, kwa kutumia uthibitisho madhubuti, mume wake atakuwa katika hali ngumu sana. Kwa upande moja heshima yake inakuwa hatarini na kwa upande mwingine kuvumilia fedheha ya aina hii si rahisi. Anahisi amenasa kwenye mtego wa kutokuafikiana ambamo si rahisi kujinasua.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 185

Mwanamume aliyeko kwenye hali hii anaweza kuchagua kufanya mojawapo ya haya yafuatayo:
(a) Anaweza kunyamaza kimya kuhusu jambo lenyewe ili aokoe heshima yake na kwa ajili ya familia yake. Lakini lazima ataishi akikumbuka jambo hili katika maisha yake yote. Kama mambo yalivyo chaguo hili halikubaliki kwa mtu yeyote mwenye kuheshimika, kwani haitakuwa rahisi kuvumilia kuishi na mke wake mzinzi na uwezekano wa kupata mtoto wa haramu. Mapenzi makali ni sifa inayopendeza sana kwa mwanamume hivyo kwamba mwanamume ambaye hana sifa hiyo hawezi kufurahia neema ya Mwenyezi Mungu Mweza. Ni maisha ya fedheha na aibu ilioje watu hao walio nayo ambao hawajali kutokuaminika kwa wake zao.

"Mtume (s.a.w.w) alisema: 'Harufu nzuri ya Peponi yaweza kunuswa katika umbali wa safari ya miaka mia tano, lakini makundi mawili ya watu yatanyimwa; nayo ni wale watu ambao wamelaaniwa na wazazi wao na mume wa mke aliye zini.' Swali liliulizwa; 'Ewe Mtume (s.a.w.w) wa Mwenyezi Mungu; nani huyu mume wa mke aliyezini? Mtume alijibu: 'Mwanaume ambaye anamjua mke wake kuwa ni mzinzi, na hunyamaza kimya kuhusu suala hili.' "

(b) Angeweza kumuua mwanaume aliyezini na mke wake au wote wawili mke wake na mwanaume mzinifu. Anaweza kulipa kisasi na kupata amani. lakini tendo hili ni la hatari kwani halingekuwa na mwisho mzuri, kwa sababu mauaji hayangefichwa daima milele. Muuaji lazima angejulikana na kuadhibiwa. Hangeweza kuthibitisha kutokuaminika kwa mke wake ndani ya mahakama; na kwa hiyo uwezekano wake kuachiliwa kutoka jela ungekuwa mdogo sana. Ingewezekana hata kupewa adhabu ya kifo. Hivyo angepoteza maisha yake na watoto wake wangekengeuka. Kwa hiyo, si busara kwa mwanaume kuhatarisha maisha yake kwa sababu ya kulipa kisasi. Mwanaume anatakiwa kuwa na busara na mtaratibu na kuweza kudhibiti hasira yake hadi apate ufumbuzi unaofaa kwa tatizo lake.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 186

Angejiua ili asiendelee kuona kutokuaminika kwa mke wake na aishi maisha ya fedheha. Tendo la kujiua wala si lenye busara kwa sababu upande moja amejiua, ambayo yenyewe ni dhambi kubwa katika Uislamu na muuaji lazima aadhibiwe na Mwenyezi Mungu mnamo Siku ya Hukumu. Kwa upande mwingine amejinyima maisha. Hii ni mantiki ya aina gani ambayo ingeshawishi kujiua kama kisasi cha uhalifu wa mtu mwingine. Angeteseka katika maisha yajayo na pia kumpa uhuru mkubwa zaidi mke wake kuendelea kuzini zaidi.

Angemtaliki mke wake. Hiki ni kitu cha busara zaidi kufanya. Ni sahihi kwamba talaka ingeharibu maisha ya familia yake na ingeleta madhara zaidi kwake na watoto wake, lakini hakuna njia nyingine yeyote. Ni bora zaidi yeye kumtaliki mke wake na achukue watoto wake, kwa sababu si sawa kuwaacha waishi na mama yao mwovu.

Kama mambo yalivyo, kulea watoto si kazi rahisi kwa mwanaume, lakini lazima ahakikishe kwamba Mwenyezi Mungu angemsaidia. Angemsaidia yeye kuendesha tabia ya kuheshimika.

USITAMANI WANAWAKE WENGINE

Mwanaume lazima ajitahidi sana kuchagua mwanamke ambaye atamfaa. Yupo kwenye fursa ambapo anaweza kuwa mwangalifu na kuchukua tahadhari katika kumpata mwenza ambaye ataishi naye katika maisha yake yote. Hata hivyo, baada ya kuoana, si sahihi yeye kuanza kutamaani wanawake wengine. Ni sharti asifikirie wanawake wengine isipokuwa mkewe.

Lazima atambue kwamba msichana ameacha familia yake ili aishi naye na si sahihi kwa mume kuendekeza matamanio ya kitoto. Lazima afanye

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 187

jitihada kuiweka familia yake mpya pamoja na lazima ajaribu kutengeneza mazingira ya kirafiki nyumbani.

Mwanaume ambaye anataka kuwa na furaha yake mwenyewe, baada ya kuoa lazima aache mawazo ya kijinga na lazima abadilike ili aendane na maisha mapya.

Haina maana kwa mwanaume aliyeoa kutaniana na wanawake wengine au kuonesha mapenzi kwao. Mwanaume pia hangetaka mke wake ataniane na wanaume wengine. Mwanamke naye hangetaka msimamo wa aina hii kuendekezwa na mume wake kwa wanawake wengine.

Mwanamke anayemuona mume wake anakuwa karibu na kuwazoea wanawake wengine, ataona wivu na kukata tamaa. Hataipenda nyumba na familia yake. Huenda akalipa kisasi kwa kufanya kitendo cha aina ile ile au ataomba kutalikiwa.

Mwanamke alilalamika mahakamani kuhusu mume wake. Alikuwa ameolewa kwa miaka thelathini na tatu akasema kwamba mume wake kila mara anayo mazoea ya kutaniana na wanawake wengine."

Mwanamke alilalamika mahakamani kwamba kila mara mume wake alikuwa anaonekana kuvutiwa na marafiki zangu. Akasema kwamba aliacha kuwaalika marafiki zake nyumbani kwake kwa sababu walifikiri mume wake alikuwa anavutiwa nao na kwamba yeye-mke alikuwa anaona aibu kwa sababu yake."

Haistahili kwa mwanaume aliyeoa kutupa jicho la mapenzi kwa wanawake wengine. Kuwatazama wanawake wengine kwa matamanio husababisha shauku, mfadhaiko na kutokujali familia.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 188

Mwenyezi Mungu anasema katika Qurani Tukufu:

﴿ قُل لِّلْمُؤْمِنِينَ يَغُضُّوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ ۚ ﴿٣٠﴾ ﴾

“Waambie waumini wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao. . (24:30).

Imamu Sadiq (a.s) alisema: ‘Mtazamo wenye matamanio ni mshale wenye sumu uliotupwa na shetani. Upo uwezekano mkubwa kwamba mtazamo kama huo ungekuwa sababu ya huzuni na masikitiko kwa muda fulani.’

Kuonesha mapenzi, mabingwa wa maradhi ya akili wanasema ni ugonjwa. Jicho ambalo limezoea tabia hii, haliwezi kutosheka. Kutazama kwa njia hii huwa sababu ya uharibifu mwingi, ambapo vijana wanaweza kukengeuka na kuacha njia iliyonyooka. Kile ambacho macho hayakioni moyo hauwezi kutamani.

Mtu anaweza kujizuia katika hatua za mwanzo kuhusu matokeo mabaya ya mitazamo iliyozuiwa, lakini hatimaye atashindwa na kuvutiwa na kile anachokiona.

Imamu Sadiq (a.s) alisema; ‘Mitazamo iliyokatazwa ya mara kwa mara huamsha matamanio katika moyo wa mtu na hiyo inatosha kumpotosha mtazamaji.’

Uislamu, kwa kutambua madhara ya mitazamo ya kizinifu kama hiyo, umeharamisha moja kwa moja.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 189

Mwanaume ambaye ghafla anapomuona mwanamke huko barabarani au mahala pengine, anatakiwa kuelekeza macho yake mahali pengine au afumbe macho yake. Asiwaangalie wanawake kwa muda mrefu. Hii inaweza kuwa ngumu mwanzoni, lakini akifanya zoezi kidogo anaweza kumudu.

Watu wenye busara wanatambua kwamba kujizuia kwenye mitazamo iliyokatazwa ni zoezi ambalo lingewatokeza kama vile mauaji, uhalifu, kujiua, kuchanganyikiwa kiakili, mfadhaiko, kudekeza tamaa ya moyo, kuondoa hatari nyingi ambazo zingejitokeza wazi, ugomvi wa famili na kadhalika.

Ninatambua matatizo ambayo yana wakabili vijana katika kipindi hiki, na ninajua kwamba kufumba macho ya mtu ili yasione uchafu wa mitaani na penginepo si jambo rahisi, lakini hakuna njia nyingine yoyote zaidi ya kudharau hayo.Mwanaume anayeweza kufumba macho yake ili asione wanawake wengine, atakuwa amepata ulinzi dhidi ya maovu mengi. Badala yake atafurahia familia yake na kupata utulivu wa akili.

Bwana mpendwa! Kama unataka kupata furaha, mara tu ukioa usiwatilie maanani wanawake wengine. Usiwape pongezi wanawake wengine mbele ya mkeo.
Usiseme: “Natamaani labda ningemuoa fulani… nilikosa fursa nyingi nzuri.” Maneno ya aina hiyo yanaweza kumkera mke wako na anaweza asikuchangamkie wewe na maisha kwa ujumla. Anaweza hata kufanya kama ulivyo fanya na kusema kwa mtindo huo huo.

Matokeo yake ni kwamba maisha yako yanapungukiwa furaha. Ni wa kusikitikiwa wanaume waovu na kuwaacha wake zao, kama vile hawajapata kujua mapenzi na uaminifu wa familia. Wanaume wa aina hii

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 190

ni kama wanyama ambao huelekeza juhudi zao zote kwenye kula, kulala na kuondoa hamu ya ngono. Huonekana kama vile ni wageni wa ubinadamu na mapenzi.

UWE MWENYE KUSHUKURU

Kazi ya utunzaji wa nyumba inaweza kuonekana kama kazi rahisi kwa wanaume wengine, lakini itakuwa ni jambo la kuridhisha kukubali kwamba kazi hii ni ngumu na inachosha.

Mama wa nyumbani! Hata kama atafanya mchana kutwa na usiku kucha hataweza kumaliza kazi yake yote. Kupika kufanya usafi, kufua nguo na kunyosha pasi kuosha vyombo na kuvipanga, kutandika vitanda na kupanga fenicha na zaidi ya yote kuwatunza watoto, si siku moja, lakini, ni kila siku ni ngumu sana.

Mwanaume anaweza kufikiri kwamba mke wake anapika tu mara tatu kwa siku na kusahau kazi zake zingine nyingi sana.

Ni mwanaume huyo tu ambaye atakuwa tayari kukaa nyumbani kwa kipindi cha mwezi moja na afanye kazi ya nyumbani ndiye atajua shinikizo lililopo, na hapo ndipo atakapo pendezwa na juhudi za mke wake.

Mke wa nyumbani hufanya kazi hii yote kwa furaha lakini hutarajia mume wake kupendezwa naye na kuonesha shukrani zake.

Bwana mpendwa! Kuna ubaya gani ukimpa ahsante mke wako kwa kazi ya kutunza nyumba? Kwa nini usioneshe upendo kwa chakula anachopika? Kuna ubaya gani ukimshukuru mke wako kuhusu juhudi zake za kutunza watoto? Hutambui kwamba kupendezwa kwako kwa jitihada zake ni kitendo cha kumtia moyo na kumchangamsha?

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 191

Kama hutajali jitihada zake, au hutaki kumshukuru atapoteza mvuto wa kazi ya kutunza nyumba na halafu wewe utalalamika. Lazima utambue kwamba wewe unaweza kuwa chanzo cha uvivu wa mkeo.

Kama mgeni anakupa upendeleo mdogo, ungemshukuru mara nyingi sana, lakini mke wako anayekupendelea mara nyingi, humshukuru hata mara moja! Wewe haupo tayari kumfurahia kwa kuonesha kupendezwa kwako kwa jitihada zake zote.

Mama wa nyumbani mwenye umri wa miaka ishirini na tisa aliandika kutoka Tehran. “Nimeolewa na mwanaume asiye na shukrani na asiye pendezwa ambaye hajali kabisa kazi yangu ya kutunza nyumba. Ninafua, ninafanya usafi, ninapika, ninapamba nyumba, ninafuma sweta kwa ajili ya familia, hupiga rangi viatu vyake, hupiga pasi nguo zake na kadhalika na hajawahi kunishukuru hata mara moja. Wakati wowote ninapomwambia kuhusu kazi za nyumbani huingilia kati na kusema kwamba nisisifie kazi hiyo mbele yake. Anadharau juhudi zangu, ambapo kufaulu kwake kunategemea sana bidii yangu.”

Baadhi ya wanaume hufikiri ni kitendo cha ujasiri wa kiume kutojali kazi za nyumbani za wake zao. Wanadhani kama wakitoa pongezi kwa kazi hiyo ya wake zao, wanawake wataharibika. Wanaweza hata kuamini kwamba mume na mke hawahitaji kupeana ahsante wao kwa wao.

Imani hii si sahihi, kwa sababu yeyote anaye tenda wema kutoka katika mtizamo wa kisaikolojia anahitaji kupewa shukrani na kuthaminiwa. Kufurahia jambo la mtu humpa hamasa ya kufanya vizuri na hii ni kweli hususan kwa mama wa nyumbani ambaye hufanya kazi ya kuchosha kila siku tena na tena.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 192

Hivyo Uislamu unaona kitendo cha kutoa shukrani ni sifa njema katika tabia ya mtu. Imamu Sadiq (a.s) alisema: "Yeyote anayemsifu Mwislamu, Mwenyezi Mungu humwandikia sifa nyingi hadi Siku ya Hukumu."

Mtume (s.a.w.w) wa Uislamu alisema: "Yeyote anayemheshimu Mwislamu, na kusema naye kwa uchangamfu, na humwondoshea huzuni, wakati wote atakuwa kwenye neema za Mwenyezi Mungu."

PIA UWE MSAFI NYUMBANI

Kufuata kanuni za usafi kwa kila mtu na kila mahali ni muhimu. Mtu lazima aweke mwili wake na nguo zake katika hali ya usafi, wakati wote. Lazima aoge angalau mara moja kwa wiki na lazima aoshe uso wake na mikono yake kwa sabuni, achane nywele zake, anyoe nywele, aoshe miguu yake, avae soksi safi kila siku na lazima pia avae nguo zenye tohara. Dini tukufu ya Uislamu inasisitiza sana kuhusu usafi na kuvaa vizuri.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Usafi ni sehemu ya imani (ya Uislamu)."

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alimuona mtu aliyekuwa mchafu, nywele zake hazikuchanwa na yeye hakuwa katika hali ya kuvutia. Mtume (s.a.w.w) alisema: "Kutumia neema za Mwenyezi Mungu ni sehemu ya imani ya Uislamu."

Mtume (s.a.w) wa uislamu pia alisema: "Mtu mchafu atakuwa mfanya ibada mchafu wa Mwenyezi Mungu."

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) aliongeza kwa kusema: "Jibril alisisitiza sana kupiga mswaki meno hivyo kwamba nikawa nayahofia."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 193

Imamu Ali (a.s) alisema: "Mwenyezi Mungu ni mzuri na hupenda uzuri. Na pia hupenda kuona athari za neema Zake zinapotumiwa na waja wake."

Usafi na uzuri si kwa ajili ya wanawake tu, lakini wanaume lazima pia wanatakiwa kuwa safi na wavae vizuri. Baadhi ya wanaume hawajali usafi wao na huoga mara moja kwa kipindi fulani. Hawajali nguo zao zipo katika hali gani na hawajali hata kunyoa ndevu zao. Wananuka harufu mbaya sana hivyo kwamba huwafanya wengine kuwa mbali nao.

Wanaume ambao ni waangalifu kuhusu usafi na huweka umuhimu kuhusu nguo zao, mara nyingi hufanya hivyo nje ya nyumba zao. Ni kwamba wanaonekana safi na kuvaa vizuri nje ya nyumba kwa ajili ya watu, si ndani ya nyumba zao kwa ajili ya familia zao. Huonekana nadhifu sana mitaani, kwenye mikusanyiko na kadhalika lakini mara tu wanaporudi nyumbani; huvaa nguo zilizochakaa. Mara chache sana kuangalia hali ya nywele zao na nyuso zao wanapokuwa nyumbani kwa ajili ya familia zao.

Wanaweza hata wasijali kunawa uso kabla ya kunywa chai ya asubuhi. Wanaume wa aina hii huzifanya familia zao zisiwajali.

Bwana mpendwa! Kama huwezi kumvumilia mke aliye mchafu na aliye vaa nguo zilizo chakaa na unatarajia aonekane safi na mzuri akiwa nyumbani, basi uwe na uhakika kwamba anatarajia hivyo hivyo kutoka upande wako. Mkeo pia, huchukia mume mchafu, anaye nuka na asiye nadhifu. Mke wako anataka kukuona wewe katika hali safi na nadhifu.

Kama utashindwa kutosheleza matarajio yake kuhusu unadhifu, anaweza akawaona wanaume wengine ambao wanaonekana safi na nadhifu na anaweza hata kudhani kwamba wametokea dunia nyingine. Atakulinganisha na wao na yawezekana akapoteza mvuto kwako. Kwa nini unaonekana safi kwa ajili ya wageni huko mitaani lakini unaonekana mchafu mbele ya mke wako na watoto wako.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 194

Kwa hiyo, dini tukufu ya Uislamu inawaamuru wanamume wajipambe mbele ya wake zao.

Mtume (s.a.w.w) wa Uislamu alisema: "Ni wajibu kwa mwanaume kumpa mke wake chakula na nguo na asionekane mbele yake akiwa mchafu na hapendezi. Kama angetimiza yaliyotajwa hapo juu, haitamwia vigumu kutekeleza haki za mke wake."

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) pia alisema: "Enyi wanamume lazima mjiweke katika hali ya usafi na kuweni tayari kwa wake zenu kama ambavyo nyingi mnavyotaka wake zenu kuwa tayari kwa ajili yenu."

Hasan bin Jiham anasema: "Nilimuona Hadhrat Abu al-Hasan (a.s) ambaye alipaka rangi nywele zake. Niliuliza kama kweli alipaka rangi nywele zake" Alisema: 'Ndio, mapambo ya mwanamume kwa ajili ya mke wake kusaidia kumweka mke katika uaminifu. Wanawake wanaoacha njia safi na kuanza kufanya uovu ni kwa sababu ya uzembe na makosa ya waume zao.' Hadhrat Abu al-Hasan alisema: 'Unapenda kumuona mke wako katika hali ya uchafu?' Nilijibu: 'Hapana' Halafu akaongezea: 'Hufikiria kama unavyo fikiria wewe.' "
Imamu Rida (a.s) alisema: "Wanawake wa Bani Israel waliacha njia iliyosafi kwa sababu waume zao hawakujali usafi wao na unadhifu wao." Halafu Imamu akaongeza: "Vile unavyo mtarajia mke wako, ndivyo anavyotarajia kwako."

MTUNZE MKE WAKO

Mume na mke kila mara huhitaji ushirikiano wa kila mmoja wao na kuonesha mapenzi kwa kila mmoja. Hata hivyo, haja hili huwa kubwa zaidi wakati wa ugonjwa na matukio mengine yanayo fanana na hilo. Mtu mgonjwa, kama vile anavyohitaji daktari na dawa, huhitaji matunzo

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 195

na uangalizi wenye mapenzi. Muuguzi mzuri humsaidia mgonjwa kupona vizuri na haraka.

Mwanamke pia hutegemea mume wake kumtunza yeye wakati anaugua na kulala kitandani. Mke anatarajia mume kumtunza yeye zaidi ya wazazi wake.

Mwanamke anaye fanya kazi nyumbani kama mtumishi wa nyumbani anastahili uangalizi ulio na mapenzi kutoka kwa mume wake. Anatarajia kwamba ni haki yake mume wake amuuguze.

Malipo ya tiba na dawa ni mojawapo ya matumizi ya kawaida ya maisha na mwanaume anao wajibu wa kumpa fedha hizo muhimu. Mwanamke anayefanya kazi nyumbani bila mshahara wowote, hakika anayo haki ya kumtarajia mume wake kulipa gharama ya tiba yake.

Wapo wanaume ambao hawana aibu kufanya isivyo haki. Huwatumia wake zao wakati wana afya njema na wenye uwezo, lakini hukataa kulipa fedha wanapo ugua. Fedha yoyote ndogo wanayotumia kwa ajili ya tiba ya wake zao huilalamikia sana. Baadhi ya wanaume, wakiona gharama ya tiba ni kubwa wanaweza hata kuwaacha wake zao. Tabia hii ni sawa kweli? Mwanamke mmoja alikuwa analalamika kuhusu mume wake. Alisema: “Nilikuwa nafanya kazi kwa bidii nyumbani na nilipita kwenye nyakati nyingi za furaha na shida na mume wangu. Hata hivyo, sasa nimeugua, mume wangu anataka kuniacha!”

Bwana mpendwa! Kama unapenda kuwa na furaha na maendeleo ya familia yako, lazima umpeleke mkeo kwa daktari anapougua. Lazima ulipe gharama ya matibabu yake. Zaidi ya hapo, lazima umuuguze kwa wema. Sasa amewaacha wazazi wake ili aishi na wewe, anatarajia wewe kuwa na mapenzi zaidi kwake kuliko wazazi wake. Yeye ni mwenzako na mama

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 196

wa watoto wako! Mhurumie na mpe matumaini ya kupona haraka. Mpikie chakula. Tayarisha chakula kinachofaa na nunua vifaa vilivyoelekezwa. Mlishe chakula. Yote haya yatamfanya mke wako afurahi.

Wanyamazishe watoto. Uwe mwangalifu wakati wa usiku. Wakati wowote akiamka muulize hali yake anavyojisikia. Kama hawezi kulala kwa sababu ya maumivu, basi na wewe uwe macho. Unaweza hata kuwaambia watoto wenu wakusaidie kumwangalia mama yao. Usimwache hata kidogo mke wako bila huduma, hasa zaidi anapokuwa anaumwa. Wakati kama huo, mke wako ataona mapenzi yako na yeye atakupenda zaidi. Atajivuna kwa sababu hiyo na atakuwa tayari kukuhudumia wewe na watoto zaidi, mara atakapo pona.

Mtume (s.a.w.w) alisema: "Mtu mzuri zaidi miongoni mwenu ni yule ambaye ni mwema zaidi kwa familia yake, na mimi ni mwema kuliko wote kwa familia yangu."

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) wa Uislamu pia alisema: "Yeyote anayefanya jitihada kutambua haja ya mgonjwa, dhambi zake zitasamehewa, na atakuwa kama siku aliyozaliwa." Mmoja wa maansari (wenyeji wa Madina) aliuliza: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Wazazi wangu na watolewe muhanga kwa ajili yako, ni vipi endapo mgonjwa anatoka miongoni mwa familia yako- Ahlul –bait? Hakuna thawabu nyingi zaidi katika mfano huu?"

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alijibu: "Ndio."

UCHUMI WA FAMILIA

Kufanya mpango wa sadaka ya mke ni wajibu wa mume. Ni kwamba mwanaume anawajibika kulipa gharama za mke wake kama chakula, nguo,

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 197

nyumba, daktari na dawa. Atakuwa anakosea kama hata mgharimia mke wake na anaweza kushitakiwa kisheria.

Mtu hawezi kutarajia familia iishi bila matumizi yeyote ya fedha. Watu wa familia wote wanahitaji chakula, nguo, dawa na mahali pa kuishi. Hata hivyo, wanaweza wakaomba vitu visivyo muhimu ambavyo mwanaume anaweza kukataa kuvinunua na asikubaliane na matakwa yao mbali mbali.

Mtu mwenye busara atatumia fedha kufuatana na uwezo wa kipato chake. Lazima abainishe bidhaa muhimu na avinunue katika mpango wa kipaumbele wakati wowote anapoweza. Lazima pia aweke akiba ya fedha kwa matumizi ya siku za shida. Kiasi fulani cha fedha lazima kitengwe kwa ajili ya kodi ya nyumba au kununua mahali pengine. Lazima mume asisahahu umeme, maji, nishati na simu. Kodi na ada za shule lazima zikumbukwe. Lazima kabisa aepukane na kutumia zaidi ya bajeti na kulipa vitu visivyo muhimu. Mpango mzuri wa matumizi ya fedha utamwepusha mtu asifilisike au kuwa na madeni.

Mwenyezi Mungu huona matumizi yaliyopangwa vizuri ni ishara ya imani na anasema ndani ya Qurani:

﴿ وَٱلَّذِينَ إِذَآ أَنفَقُواْ لَمۡ يُسۡرِفُواْ وَلَمۡ يَقۡتُرُواْ وَكَانَ بَيۡنَ ذَٰلِكَ قَوَامٗا ٦٧ ﴾

“Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili bali wanakuwa katikati baina ya hayo”. (25:67).

Imamu Sadiq (a.s) alisema: “Yapo makundi manne ya watu ambao sala zao hazitafika kiwango cha kukubaliwa; Kundi moja ni la watu ambao hutumia vibaya utajiri halafu humwomba Mwenyezi Mungu Mweza, ‘Ee Mwenyezi Mungu naomba riziki. Halafu Mwenyezi Mungu hujibu, si nilikuagiza uwe mwangalifu katika matumizi yako. ’ ”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 198

Abdullah bin Aban anasema: “Nilimuuliza Musa bin Jafar (a.s) kuhusu utunzaji wa familia ya mtu na akasema: ‘Ubadhilifu na uchoyo vyote ni sifa mbaya. Mtu lazima awe na kiasi.”

Mtu mwenye busara ataepuka kukopa fedha na hawezi kuchukua mkopo kwa matumizi mabaya. Uchumi unaotegemea mikopo (na riba), inayopokewa kutoka kwenye mabenki na taasisi zingine si sahihi kiislamu na kimantiki haufai.

Kununua vitu kwa mkopo, ingawa hufanya nyumba yako ionekane nzuri, lakini faraja na utulivu wa akili hutoweka. Kwa nini mtu ananunua vitu visivyo muhimu kwa bei ya juu zaidi na kujaza mifuko ya wenye mabenki kwa malipo kidogo? Ni maisha ya aina gani hayo ambapo kila kitu hupatikana kwa bei ya mkopo? Kwani si vema zaidi kwa mtu kungoja na kuweka akiba ili anunue bidhaa kwa bei nafuu?

Ni kweli kwamba kupata fedha ni vigumu na huathiri sana maisha ya mtu. Hata hivyo, la muhimu zaidi ni jinsi mtu anavyotumia fedha yake. Zipo familia zenye vipato vizuri ambazo kila mara ni wadeni wa wengine. Zipo pia familia nyingi zenye vipato vya chini ambao huishi kwa raha. Tofauti baina ya makundi haya mawili ni jinsi ya fedha inavyo tumiwa. Kwa hiyo, inafaa zaidi ama mwanaume aendeshe udhibiti wa matumizi au awe msimamizi wa mtu ambaye anawajibika nayo.

Mwisho, inakumbushwa kwamba ubakhili ni mbaya kama ufujaji, kama mwanaume anacho kipato zaidi lazima aifurahishe familia yake zaidi na kuwapa mahitaji yao muhimu kadiri iwezekanavyo.

Utajiri na fedha vyote ni vya kutumia na kuwezesha upatikanaji wa vitu muhimu vya maisha, na si vya kulundika na kuviacha hapa duniani.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 199

Ishara za utajiri lazima zionekane wazi kwenye familia ya mtu na nyumba. Kuna manufaa gani kufanya kazi kwa bidii halafu kinachopatikana kisitumike?

Mtu mzima atumie utajiri kuhusu familia yake na starehe yake mwenyewe. Inachukiza kuona mtu ambaye anao uwezo wa kifedha lakini watoto wake wanatamaani chakula kizuri na nguo nzuri. Watoto wa mtu bakhili kungoja kifo chake ili wagawane utajiri wake. Kama Mwenyezi Mungu Mweza wa yote anampa mtu neema zake, neema hizi lazima zidhihiri katika maisha ya mtu huyo.

Mtume (s.a.w.w) wa Uislamu alisema: "Si mwenzetu (si mfuasi wa Mtume s.a.w.w) ambaye anazo fedha lakini huiweka familia yake mbali na utajiri wake."

Musa bin Jafar (a.s) alisema: Jamaa ya mtu ni watu wanaomtegemea. Hivyo, yeyote anayepewa neema za Mwenyezi Mungu, lazima azisambaze kwa wale wanao mtegemea ili wafarijike, au vinginevyo neema hizo zitaondoshwa kwake."

Imamu Rida (a.s) alisema: "Ni jambo la manufaa kwa mtu kuwapa watu wa familia yake starehe itokanayo na matumizi yake, ili wasingoje hadi hapo atakapofikwa na mauti."

Imamu Ali (a.s) alisema: "Tayarisha matunda kwa ajili ya watu wanaokutegemea kila siku ya Ijumaa ili kwamba watafurahia kuja kwa Ijumaa."

SAIDIA KUFANYA KAZI ZA NYUMBANI

Licha ya kwamba utunzaji wa nyumba ni wajibu wa wanawake, lazima ieleweke kwamba kuendesha mambo ya nyumbani si kazi rahisi.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 200

Mke ambaye ni mama wa nyumbani hata akitumia muda kiasi chochote kile kwa utunzaji wa nyumba, hatoweza kumaliza kazi hiyo yote kwa wakati moja. Hii ni kweli hasa zaidi pale ambapo anatakiwa kuwakirimu wageni au anapougua na kadhalika. Kazi ya kutunza nyumba humchosha mke wa nyumbani na hivyo wanaume wanatarajiwa kuwasaidia wake zao katika suala hili.

Si haki kwamba mwanamume awe amekaa nyumbani bila ya shughuli yoyote ambapo mke wake anashughulika na kazi nyingi mbali mbali. Inafaa tu mume kumsaidia mke wake kadiri iwezekanavyo na wakati wowote awezapo. Msaada huu ni ishara ya huba ambayo humvutia mke kwa mume wake na familia yake.

Si ujasiri wa kiume hata kidogo kwamba mwanaume hapaswi kugusa kitu chochote ndani ya nyumba, bali kutoa amri tu kumpa mkewe. Nyumba ya familia si makao makuu ya kutoa amri, isipokuwa hapo ni mahali pa upendo, wema na ushirikiano.

Bwana mpendwa! Usidhani kwamba wewe ukifanya kazi za nyumbani ni kushusha hadhi yako. Kinyume chake ni kwamba, mke wako atapendezwa sana na kitendo chake cha kumsaidia.

Mtume (s.a.w.w) wa Uislamu ambaye ni mtu anaye heshimiwa sana katika historia, alikuwa na desturi ya kusaidia kazi za nyumbani.

Ayisha, mke wa Mtume (s.a.w.w) alisema: “Wakati wowote Mtume (s.a.w.w) anapokuwa hana kazi, alikuwa na desturi ya kushona nguo zake, kutengeneza viatu vyake na alikuwa anafanya kazi nyumbani kama wanaume wengine.”

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 201

RUDI NYUMBANI MAPEMA

Mwanaume asiye na mke anao uhuru wa kutumia muda wake, lakini pindi anapooa, lazima abadilishe mpango wake. Hawezi kukaa nje kwa muda wowote anaotaka. Anatakiwa kumtaarifu mke wake mahali alipo na kadhalika. Lazima asisahau kwamba mke wake huwepo nyumbani siku nzima, husafisha nyumba, huosha vyombo na hupika. Humngoja arudi nyumbani mara tu anapomaliza kazi zake, ili amuone, azungumze naye na kufurahia kuwa naye.

Watoto pia huwa na matumaini ya kumuona baba yao. Si haki kwamba mwanaume aache familia yake nyumbani na yeye afuate starehe zake mahali pengine.

Ndoa si tu kulisha chakula na kuimvisha nguo familia yako. Mwanamke ni mwenza wa mume wake na si mtumishi. Mke hayupo pale kwa ajili ya kufanya kazi mchana kutwa na kulishwa chakula lakini hasa zaidi anayo matarajio ya kuwa na rafiki wa kudumu na mwenza.

Baadhi ya wanaume kwa kweli hawafanyi sawa, hawana haki na wapumbavu. Huwaacha wake zao na watoto wao nyumbani na kutumia muda wa usiku kucha mahali pengine. Fedha ambayo wangetumia na familia nyumbani, anaipoteza mahali pengine. Wanaume wa aina hii bado hawajaelewa maana ya mapenzi na huba na huona starehe zao zisizo na thamani na chafu kama ndio njia ya maisha mazuri. Hawatilii manani ukweli kwamba vitendo kama hivyo huwadhalilisha. Wengine hutambua vitendo kama hivyo kuwa vya kipumbavu na kijeuri.

Wanaume wa aina hii ni sababu ya huzuni kwa wenyewe na familia zao. Matendo yao huwashawishi wake zao kudai talaka kutoka kwao.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 202

Mwanaume ambaye alimtaliki mke wake, alisema mahakamani: "Mwanzoni mwa ndoa yangu, nilikuwa na marafiki fulani ambao nilikuwa nikitoka nao kwa matambezi, ambapo humwacha mke wangu nyumbani… na nilikuwa na desturi ya kurudi nyumbani kesho yake alfajiri. Mke wangu ambaye alichoshwa na hali hii, alipewa talaka. Tulikuwa na watoto kumi, ambao nilitaka kukutana nao mara mbili kwa mwezi. Kipindi fulani kilipita tukitekeleza mpango huu. Lakini sasa ni muda mrefu tangu watoto wangu wajifiche na ninayo shauku kubwa kuwaona watoto wangu."

Mwanamke alisema; "Nimekata tamaa kwa upweke. Mume wangu hajali kabisa kuhusu mimi. Kwa ajili ya starehe zake huwa nje hadi asubuhi sana."

Bwana mpendwa! Sasa umeoa. Usiendekeze tabia ya kikapera. Wewe unawajibika kwa mke wako na watoto wako, acha kushirikiana na marafiki wasiofaa rudi nyumbani mara unapomaliza kazi yako. Furahia maisha ya familia na mke wako na watoto wako. Hata kama starehe zako za kila siku usiku si zenye uovu, hata hivyo, zinaweza kusababisha madhara kwako na maisha yako ya ndoa.

UWE MWAMINIFU

Baada ya mapatano ya ndoa maisha binafsi ya watu wawili yanalingana na kuwa maisha ya ushirika moja wa kijamii. Kiapo kitukufu cha ndoa kinamaanisha kwamba mwanaume na mwanamkie wanapeana ahadi kila moja kuwa pamoja katika maisha yao yote, kusaidiana wao kwa wao, kuwa mwema na mwelewa wakati wote, wakati wa neema na wakati wa shida, wakati wa ugonjwa na afya njema na huzuni na kadhalika.

Utu unadai kwamba mwanandoa anatakiwa kuwa mwaminifu kwa ahadi yake. Wanandoa hawatakiwi kusahau mkataba wao hata kwenye hali

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 203

ngumu. Msichana mdogo ambaye huchagua mwanamume mmoja kuishi naye katika maisha yake yote hatarajii kuwa amekuwa mwanamke wa makamo ya utu uzima. Si haki kwamba mwanaume atafute starehe na mwingine na kumwacha mke wake.

Mwanamke ambaye hutoa mchango mkubwa katika kujenga familia madhubuti katika mazingira mazuri ya maendeleo ya uchumi, hatarajii mume wake kumpenda mwanamke mwingine.

Mwanamke anayefanya bidii nyumbani kwa kawaida anayo matumaini kwamba mume wake hatamnyima mapenzi na huba yake wakati wa ugonjwa na kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi. Jambo la mwisho kabisa hatarajii mume wake kutafuta starehe ya kwake peke yake.

Baadhi ya wanaume kwa kweli hawashituki. Wakati wake zao ni vijana na maumbo ya kuvutia wanafurahia kuwa nao, lakini huwaacha wanapo zeeka.

Mwanaume alimtaliki mke wake kwa sababu ya kuwa na kisirani, kwani tangu walipooana baba yake alikufa na mjomba wake akafilisika.

Mwanaume aliye muoa mwanamke kijana kwa kumpenda, alimtaliki baadaye kwa sababu hakumpenda tena.

Mwanamke… alilalamika mahakamani: “Nimeishi na mume wangu kwa miaka mingi, lakini sasa nimepata maradhi anasema kwamba hataki mke mgonjwa!”

Bwana mpendwa! Wewe si hayawani ambaye maisha yake yote ni kula na kukidhi matamanio ya kimwili. Wewe ni binadamu mwenye mchomo wa moyo, dhamira na tabia ya kujitolea. Hivi ni haki kweli kwamba wewe unafuatilia starehe zako nje ya nyumba yako?

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 204

Kama ndio, basi wewe ni muonevu na kwa hali hiyo wewe utaadhibiwa hapa hapa duniani. Ukitumia muda wako na mwanamke mwingine, basi, kwa ajili ya starehe utulivu wa akili yako na utapata maradhi ya kuharibikiwa akili. Watoto wako hawatakubali na watajibu kwa kukukashifu.

Kama mke wako anaugua, chukua hatua muhimu za kumtibu, na kama anayo maradhi yasiotibika, basi endelea kuishi naye, jitolee kumsaidia na usioe mke mwingine akingali hai.

Usimuudhi wakati huo mgumu. Ungetarajia nini endapo wewe ungekuwa katika hali hiyo? Ni haki kabisa kwamba yeye angetegemea hivyo hivyo kutoka kwako.

Ni sahihi kwamba wewe unapo ugua mke wako atataka umtaliki? Je hujafedheheka mbele ya marafiki na ndugu? Kwa hiyo kama unakubali kwamba uaminifu na unyofu ni sifa nzuri, basi jaribu kuwa mwaminifu.

ELIMU NA MAFUNDISHO

Mwanamke kijana ambaye ndio kwanza kaolewa anao wajibu wa kuendesha mambo ya mume wake na katika hali hiyo atahitaji ujuzi wa kupika, usafi, kunyosha nguo, kushona, kupanga fenicha, kukaribisha wageni wake, kushirikiana na watu wengine, kumtunza mtoto wake na kadhalika.

Mume wake atatarajia mke wake kujua yote haya. Hata hivyo, mategemeo yake yanaweza yasifanikiwe takriban muda wote kwa sababu ujuzi wa mke wake kijana kuhusu utunzaji wa nyumba ama haupo kabisa au upo kidogo sana.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 205

Mtu afanyeje? Hili ni tatizo katika jamii zetu. Wazazi hawajali, wala mfumo wa elimu hauna mipango ya kutosha kukidhi haja hii. Hata hivyo, mtu anatakiwa kupata ufumbuzi wa tatizo hili.

Kwa vile mwanaume anakusudia kuishi na mke wake kwa maisha yake yote lazima amsaidie kumuelimisha, kwa sababu kwa kawaida wanaume huwa na umri mkubwa kuzidi wa wake zao na hivyo wanao uzoefu zaidi.

Mwanaume kwa uvumilivu anaweza kumuelemisha mke wake na kumfundisha vitu ambavyo anavijua. Anweza hata kumuuliza mama yake, dada au shangazi zake kuhusu mambo ambayo hayajui, au anaweza hata kununua vitabu vinavyohusu masomo kama ya kupika, ushonsji, utunzaji wa nyumba na kadhalika.

Mwanaume vile vile lazima amhimize mke wake kusoma vitabu ambavyo vitaonesha kimaadili kuwa ni vyenye manufaa. Lazima asahihishe upungfu wake wa maadili kwa adabu nzuri na sio kwa upinzani, au vinginevyo atageuka dhidi yake.

Mwanaume, kwa kutumia uvumilivu wake, anaweza kumwelimisha mke wake kwa mujibu wa njia yake ya maisha katika kipindi cha miaka miwili ya mwanzo wa ndoa yao. Inawezekana asifaulu asili mia kwa mia lakini bila shaka atakaribia kutosheleza mahitaji.

Elimu ya aina hii inahitaji uvumilivu, muda na busara, lakini mwanaume lazima ajaribu kuipata. Hii ni kwa sababu mwenza mzuri ni mama mzuri kwa watoto wake ni neema kwa mwanaume.

Mojawapo ya mambo muhimu ambayo mwanaume Mwislam aliyeoa anatakiwa kukumbuka ni ukweli kwamba mke wake pia ni Mwislam, na inawezekana awe hatambui utaratibu wa maisha ya Kiislamu na sheria zake. Inawezekana asijue hata kuhusu wudhu, kusali na kadhalika.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 206

Kwa kweli ni wajibu wa wazazi kuwafundisha watoto wao mambo yote muhimu ya Kislamu na maadili. Kwa bahati mbaya, hata hivyo, wazazi hawajui kabisa kuhusu ukweli huu, na bila kuwafundisha mabinti wao kitu chochote kuhusu Uislamu, wanawaozesha. Hivyo wajibu wao huangukia kwenye mabega ya waume wanaowaoa.

Bwana mpendwa! Ni wajibu wako kumzoeza mke wako maadili ya Kiislamu na kumfundisha mambo yaliyohalalishwa na yale yaliyo haramishwa katika dini. Mfanye ajifunze kuhusu tabia za Kiislam. Kama huwezi kufanya hivi, basi tafuta msaada kutoka kwa wengine au fanya mpango wa vitabu na makala zenye elimu ya Uislamu na mwambie asome na kufanya kwa vitendo. Unaweza hata kufanya mpango wa elimu na maelekezo yake kupitia kwa mtu mwaminifu na aliyeelimika.

Kwa ufupi, ni wajibu wa mwanaume kumtia moyo mke wake kumuamrisha kufanya mema na kumkataza kufanya mabaya. Kama mwanamume atafuata wajibu wake huu, basi atafurahia kuwa na mwenza mwenye tabia njema, mwema, muaduilifu na mke mwenye busara.

Hata hivyo, kama mwanamume anaamua kutojali wajibu wake atateseka kwa kuwa na mke mjinga ambaye imani yake ni dhaifu na ambaye hana kinga dhidi ya uovu. Pia mume ataulizwa na Mwenyezi Mungu huko akhera kuhusu uzembe wake huu.

Mwenyezi Mungu anasema kwenye Qurani Tukufu:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ قُوٓاْ أَنفُسَكُمۡ وَأَهۡلِيكُمۡ نَارٗا وَقُودُهَا ٱلنَّاسُ وَٱلۡحِجَارَةُ ٦ ﴾

“Enyi mlioamini jiokoeni nafsi zenu na watu wenu (wa nyumbani – wake zenu watoto wenu nk.,) kutokana na moto ambao kuni zake ni watu na mawe…” (66:6)

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 207

Imamu Sadiq (a.s) alisema: "Aya hiyo hapo juu ilipoteremshwa mmoja wapo wa Waislamu alikuwa analia na kusema; 'Mimi siwezi kujinusuru hata mimi mwenyewe kutoka kwenye moto wa Jahanamu na ninatakiwa kuwajibika kuinusuru pia familia yangu kutoka kwenye Jahanamu!' Mtume (s.a.w.) alimwambia mtu huyu: "Ingetosha kama tu ungewaagiza kufanya mambo hayo ambayo wewe unayafanya na uwakataze wasifanye yale ambayo wewe mwenyewe unajizuia kuyafanya."

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: "Wanaume wameumbwa kuwa viongozi na kuwajibika kwa familia zao, na kwa namna hiyo wanawajibu kwa watu wanaowategemea."

Mtukufu Mtume (s.a.w.) pia amewakumbusha wanawake: "Waambieni waume zenu wafanye matendo mema kabla hawajawashawishi nyinyi kufanya mabaya."

KUPATA MTOTO

Moja ya mambo ambayo huweza kuwa ni nukta zenye kuumiza kwa wanandoa ni kuhusu kupata mtoto. Ni kwamba mwanamke atataka kupata mtoto lakini mume wake anakataa au kinyume chake. Tatizo hili wakati mwingine huwa kubwa sana na matokeo yake wanandoa wanaweza kuishia katika kutalikiana.

Bibi…alilalamika mahakamani na kusema: "Niliolewa nikiwa na umri wa miaka ishirini na saba ambapo mume wangu alikuwa amemaliza masomo ya Chuo Kikuu. Alikuwa mkufunzi kwenye mojawapo ya chuo kikuu na nilihisi kuwa nilikuwa mwanamke mwenye bahati. Hata hivyo mume wangu hataki kuzaa mtoto. Simwelewi kwa sababu sote afya zetu ni nzuri na tunazo fedha za kutosha kuwa na angalau watoto wawili. Si kwamba hawataki watoto, kwani anawatunza vizuri wapwa zake. Nina umri wa

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 208

miaka thelathini na kama ilivyo kawaida ningependa kuwa mama. Mume wangu anaelewa hisia zangu lakini husema kwamba mtoto atakuwa sababu ya usumbufu katika maisha yetu na kuendelea." Mwanamke huyu, wakati anajizuia asilie, anakabiliwa na tatizo ambalo ni zito sana hivyo kwamba wanandoa hawa waliamua kutalikiana, ili yeye aweze kuolewa tena na mwanamume mwingine na yeye apate muda wa kutosha kufanya utafiti wake wa kisayansi."

Kupenda watoto na kuzaa ni matamanio ya kawaida ya binadamu na hata ya hayawani. Watoto ni matunda ya maisha na urithi mzuri kuliko wote wa mwanadamu.

Maisha ya mtu mwenye watoto hayatasitishwa na kifo chake lakini, hakika yataendeshwa kama vile maisha yalivyo panuka. Mtu asiye na mtoto au watoto atahisi mpweke na aliye tupwa na atajihisi vibaya zaidi atakapo kuwa mzee.

Nyumba isiyo na watoto ni mahali panapo chosha na haitakuwa changamfu na upendo. Ndoa isiyo na watoto, wakati wowote ipo katika hatari ya kuvunjika. Hivyo watoto ni chanzo cha uchangamfu na kudumu kwa familia.

Imamu Sadiq (a.s) alisema: "Furaha ya mtu imo katika kupata watoto."

Mtume (s.a.w.) wa Uislamu alisema: "Zaeni watoto wengi kwa sababu mnamo Siku ya Hukumu nitajivunia idadi yenu juu ya umma nyingine."

Kumpenda mtoto ni matamanio ya kawaida, lakini baadhi ya watu hupotoshwa kutoka kwenye kawaida yao na wanaathirika na maradhi ambayo huwafanya kutafuta visingizio kama vile upungufu wa fedha, kuwa ndio sababu ya kuwafanya wasipende kuzaa. Hata hivyo,

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 209

Mwenyeyzi Mungu amehakikisha kwamba atawaruzuku viumbe Vyake vyote.

Bakr bin Saleh alisema: "Niliandika barua kwa Hadrat Abu al-Hasan (a.s) nikisema kwamba nilikuwa nachukua hatua za kuzuia nisipate mtoto kwa muda wa miaka mitano; kwa sababu mke wangu alikuwa anasita kupata mtoto, na kwamba alikuwa anasema kwamba ukosefu wa fedha ungefanya kazi ya kulea mtoto kuwa ngumu.' Nilimuuliza Hadrat Abu al-Hasan maoni yake kuhusu jambo hili." Akajibu: "Usizuie kupata mtoto, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mweza atampa riziki."

Mwenyezi Mungu Anaweza hata kuongeza riziki ya familia kwa sababu ya neema za watoto. Wapo watu wengi ambao walikuwa na shida kabla ya kupata watoto, lakini walipata maisha ya raha baadaye.

Baadhi ya watu huona watoto kama usumbufu. Hii si kweli na kwa kweli watoto ni chanzo kizuri sana cha furaha na kiburudisho kwa wazazi.

Kama ilivyo, kutunza watoto si kazi rahisi na yenye matatizo, lakini maadam inaafikiana na kanuni ya asili, mtu anaweza kuvumilia matatizo na kwa hali hiyo inafaa kukubali usumbufu uliomo humo.

Ufinyu ulioje wa akili wa wanaume na wanawake ambao kwa sababu ya kutokupata watoto wanakimbilia kuachana! Je si kweli kwamba inashangaza mwanaume mwenye elimu, anakataa kukubali sheria za utaratibu wa jambo la asili kwa kung'ang'ania kiasi cha hata kuwa tayari kumpa talaka mke wake?

Wanandoa wengine hukubaliana kupata mtoto lakini hubishana kuhusu wakati wa kupatikana mtoto. Mwanamke au mwanaume wa aina hii angesema; 'Mtu lazima awe huru wakati wa umri mdogo kwani mtoto

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 210

atamnyima uhuru wa kustarehe. Ni vema kungoja hadi baadaye kupata mtoto mmoja au wawili.' Kama wote mume na mke wanatofautiana kwa maoni, basi mabishano yataanza ambayo yanaweza kuishia kwenye kutalikiana.

Na tukumbuke kwamba kama mtu anataka watoto, basi lengo hili lingetekelezwa katika kipindi cha mwanzo kabisa cha ndoa. Hii ni kwa sababu watoto wanaozaliwa na wazazi vijana kwa kiasi fulani huwa bora kuliko wale wanaozaliwa na wazazi wenye umri mkubwa zaidi. Kwanza, watoto hawa afya zao huwa njema zaidi na wanaonekana kuwa na nguvu nyingi zaidi. Pili, kwa kuwa wanatokana na wazazi vijana, wanaweza kuishi kwa muda mrefu zaidi na wazazi wao. Wanaweza kusomeshwa zaidi na kulelelewa vizuri zaidi. Lakini watoto walio zaliwa na wazazi wenye umri mkubwa hunyang'anywa uongozi na mafundisho ya wazazi wao kwa sababu ya kifo au kukosa uwezo. Tatu watoto wa wazazi wenye umri mdogo wangeweza kufika kwenye umri wa kuwa na familia zao na kuanza kufanya kazi, ambapo wazazi wao wakingali hai. Hivyo wanaweza kuwa msaada mkubwa sana kwa wazazi wao watakapo kuwa wazee.

Kwa ufupi, kuzaa watoto wakati wa ujana ni vema zaidi kuliko umri mkubwa. Lakini hiki si kipengele cha muhimu sana hivyo kwamba kisababishe ugomvi na kutalikiana. Ni vema kwa mwanaume au mke kukubaliana kwa maelewano wasiruhusu suala hili kutengeneza mwanya katika ndoa yao.

Baadhi ya wanandoa hushindwa kuelewana kuhusu idadi ya watoto ambao wangetaka kuzaa.

Mwanamke akiwa amemshikia mtoto mikononi mwake alisema: "Miaka minne baada ya kuoana, nilizaa watoto wa kike wawili na mume wangu, lakini kwa kuwa alitaka mtoto mwanaume, nilipata ujauzito kwa

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 211

mara nyingine na tena nilijifungua mtoto mwanamke. Sasa ninao watoto watatu wanawake. Mume wangu anafanya kazi benki na mshahara wake hautoshi familia yetu. Hivi karibuni amekuwa akisisitiza kwamba nibebe mimba mara nyingi hadi nizae mtoto wa kiume. Lakini mimi sipo tayari kwa mpango huu kwa sababu kipato chake hakitoshi kuwasomesha watoto wetu kwa namna tunavyotaka. Nimemwambia mara nyingi kwamba watoto wanaume na wanawake wote ni wazuri. Nina hofia kwamba kama nikibeba ujauzito tena nitazaa mtoto mwanamke tena. Nina uhakika kwamba atataka kusisitiza tupate mtoto mwingine. Hatutakubaliana katika jambo hili na hivyo tumeleta shauri letu mahakamani."

Ni sahihi kwamba kusomesha na kuelekeza watoto wengi ni vigumu na hii hususan ni kweli wako ambao hawana kipato cha kutosha.

Kwa hiyo, ni vema wanandoa kuamua kuhusu idadi ya watoto kwa mujibu wa kimaadili na uwezo wa kifedha. Lazima waelewane na waweze kupata ufumbuzi wa matatizo yao kwa kutumia busara na wema. Si sahihi kwa yeyote miongoni mwao kusisitiza kitu kisicho na mantiki.

Zipo familia nyingi ambazo ama wanao watoto wengi au zinatosheka na mtoto mmoja au wawili.

Baadhi ya wanandoa hutofautisha kuhusu jinsia ya mtoto (watoto) wanaotaka kuzaa. Wanandoa wengine, wanaume na wanawake hupenda kuzaa mtoto mwanaume na hawapendi kuzaa watoto wanawake. Kuzaliwa kwa mtoto mwanamke ni tukio ambalo lingemfanya mzazi mwanamke ajihisi ana hatia na kwa hiyo angenyamaza kwa sababu ni yeye ndiye amezaa. Lakini mwanamume huenda akaonesha kutokuridhika kwake. Wanaume wapo tofauti. Baadhi yao hawaoneshi kutokuridhika kwao wazi wazi na huishia kuonesha tu uso wa kuogofya. hawatilii maanani kuwahudumia wake zao baada ya kujifungua. Huonekana na huzuni.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 212

Baadhi ya wanamume, hata hivyo huwa wakali sana wanapopata taarifa ya kuzaliwa mtoto wa kike. Huwakasirikia wake zao na huanzisha shutuma za makosa yao. Hupinga na kuanzisha ugomvi. Wanaume wengine huamua hata kuwapiga wake zao au kuwataliki.

Mwanamke alisema mahakamani; “Niliolewa miezi kumi na tano iliyopita na nikapata ujauzito miezi sita baadaye. Hivi karibuni, muda wa kujifungua ulipokaribia, mume wangu aliniambia kwamba nizae mtoto mwanaume. Lakini nilihisi kwamba ningezaa mapacha au hata watatu. Siku chache zilizopita nilijifungua mapacha wa kike. Nilifurahi sana kuhusu jambo hili, alitibuka na akaondoka hapo chumbani. Baadaye nilimuomba awapeleke watoto nyumbani, alinikaripia na kunilaumu kwa kuzaa mapacha wanawake. Akaniambia niondoke kwake, kwa hiyo nilikwenda kwa wazazi wangu na sasa ninaomba anipe talaka.”

Bibi… alimwambia mwandishi wa habari mahakamani: “Baada ya miaka ishirini na moja ya ndoa na kuzaa watoto watano, ninalazimika kuyaacha maisha ambayo nimeyapatia mchango mkubwa sana, kwa kumpisha mwanamke mwingine ambaye ameweza kuzaa mtoto mwanaume.

“Ninao watoto wanawake watano wazuri ambao ni wenye vipaji na ambao si tatizo kabisa kwa baba yao. Ni ipi hatia yangu kama siwezi kuzaa mtoto wa kiume. Mume wangu ananilaumu kwa kutokuzaa mtoto wa kiume na anataka mimi nimruhusu kuoa mwanamke mwingine.”

Kwa bahati mbaya, sifa hii imeendelezwa na watu wengine tangu enzi za Ujahiliya (kipindi cha ujinga) kwamba hutilia shaka maumbile ya binadamu ya jinsia ya kike. Huoni aibu kuzaa watoto wa kike na huhisi wamedhalilishwa.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 213

Katika zama zaa ujinga, watu walikuwa na desturi ya kuzika watoto wa kike wakingali hai! Qurani Tukufu imesema kuhusu matendo yao ifuatavyo:

﴿ وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُم بِٱلْأُنثَىٰ ظَلَّ وَجْهُهُۥ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ ﴿٥٨﴾ ﴾

"Na mmoja wao akibashiriwa kwa msichana, uso wake unasawijika, naye kajaa chuki." (16:58),

﴿ يَتَوَٰرَىٰ مِنَ ٱلْقَوْمِ مِن سُوٓءِ مَا بُشِّرَ بِهِۦٓ ۚ أَيُمْسِكُهُۥ عَلَىٰ هُونٍ
أَمْ يَدُسُّهُۥ فِى ٱلتُّرَابِ ۗ أَلَا سَآءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿٥٩﴾ ﴾

" Anajificha asionekane na watu kwa ubaya wa aliyo bashiriwa! Je, akae naye juu ya fedheha hiyo au amfukie udongoni? Tazama uovu wa wanavyohukumu!" (16:59).

Lakini Uislamu unapinga fikira hii isiyo sahihi na kuwaona wanawake na wanamume kuwa wapo sawa.

Mtume (s.a.w.) wa Uislamu alisema: "Miongoni mwa watoto wenu walio bora zaidi ni mabinti zenu."

Mtume (s.a.w.w) wa Uislam pia alisema: "Ishara ya mwanamke mwenye bahati ni yule ambaye mwanaye wa kwanza ni mwanamke."

Kwa nyongeza, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: "Yeyote ambaye anawalea watoto wanawake watatu au dada watatu, Pepo itakuwa ya kwake."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 214

Kama mtoto mwanamke angekuwa duni, Mwenyezi Mungu hangefanya ukoo wa Mtume (s.a.w.) uendelee kupitia kwa Hadhrat Fatima Zahra (a.s).

Bwana mpendwa! Unadai kwamba wewe ni mstaarabu na binadamu wa kisasa, kwa hiyo acha fikira za aina hiyo. Kuna tofauti gani wewe ukiwa na mtoto mwanamke au mwanamume. Wote hawa ni watoto wako na wote waweza kuelekea kwenye ubora. Mtoto mwanamke pia anaweza kuwa mtu mashuhuri kwa malezi yako sahihi ya elimu.
Mtoto mwanamke ni bora zaidi ya mtoto mwanamume kwa kiasi fulani:

Kwanza, mtoto mwanamke ana huruma zaidi kwa wazazi wake anapokua na kujitegemea. Watoto wanawake, kama wazazi hawawapi upendeleo wowote zaidi ya watoto wao wanamume, wangekuwa na mapenzi zaidi kwao.

Pili, mtoto mwanamke mahitaji yake hayana gharama kubwa kama ya mtoto wa kiume, kwa sababu kwa kawaida hadumu muda mrefu nyumbani kwa wazazi wake, kwani huolewa mapema katika umri wake na huwaacha wazazi wake akiwa na vitu vichache tu vya kuanzia maisha yake mapya. lakini, wavulana huwa wa makamo ya vijana ambao huweza kuishi na wazazi wao kwa muda mrefu. Wazazi watalipa gharama ya elimu yake, wtamtafutia kazi, watalipa gharama zake wakati wa miaka miwili ya kutumikia jeshi, kama upo umuhimu, na halafu kumuoza mke, baada ya hapo angehitaji kupewa nyumba, mabusati, samani, na kadhalika. Angehitaji hata msaada wa fedha kutoka kwa wazazi wake baada ya kuoa.

Tatu, kama wazazi hawatafanya ubaguzi baina ya mtoto wao mwanaume na mwanamke, na kama watamtendea wema mkwilima wao, mkwilima wao mara nyingi huenda akawasaidia wao wakati wa matatizo na kwa kawaida huwa mwaminifu zaidi kwao kulinganisha na mtoto wao wa kiume.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 215

Kwa vyovyote vile, hivi huwa ni kosa la mwanamke inapotokea anazaa mtoto mwanamke? Mume na mke wote wanahusika katika tendo la kuzaa na mwanaume hana haki ya kumlaumu mke wake kwa jambo hili. Vinginevyo ni sawa kabisa mwanamke naye kumlaumu mume wake kuhusu jambo hili. Hata hivyo, hapana yeyote kati yao anaye laumiwa kwa jambo hilo kwani ni utashi wa Allah pekee wenye kuamua jinsia ya mtoto.

Wapo baadhi ya wataalamu ambao wanaamini kwamba jinsia ya mtoto inaweza kuamuliwa kutokana na jinsi mama anavyopata lishe yake wakati wa ujauzito wake. kwa hiyo, kama wapo watu wanaopendelea mtoto wao awe na jinsia wanayotaka wao, wanaona wataalamu na kwa hiyo watazuia hali ya kuwalaumu wake zao.

Mtu mwenye akili si lazima afadhaike kwa kupata mtoto mwanamke, lakini lazima afurahi sana. Anatakiwa kuonesha furaha yake, huba yake kwa mke wake na anatakiwa hata kumpa mke wake zawadi.

Angeweza kusherehekea kupatikana kiumbe kipya na hata kuchukua hatua za kimantiki katika kumridhisha mke wake kwamba mtoto mwanamke ni bora kama alivyo mtoto mwanaume, iwapo mke wake atakuwa amefadhaika kwa sababu ya kupata mtoto mwanamke.

Baba mwenye busara hawezi kubagua baina ya mtoto wake mwanaume na mwanamke, hangemlaani yeyote kwa kupata mtoto mwanamke na kwa hiyo angepambana na fikira za kipindi cha ujahiliya.

Mwanaume alisikia habari ya kuzaliwa mtoto wa kike wakati alipokuwa na Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w). taarifa hiyo ilimvuruga. Mtume (s.a.w.w) alisema: “Kwa nini umefadhaika?” Alisema: ‘nilipokuwa ninatoka nje ya nyumba yangu, mke wangu alikuwa katika uchungu wa kujifungua, na sasa nimeletewa taarifa kwamba nimepata mtoto

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 216

mwanamke.' Mtume (s.a.w.w) alisema; "Ardhi inayo nafasi ya kumtosha yeye, na mbingu inampa hifadhi na Mwenyezi Mungu atampa riziki. Yeye ni ua lenye kutoa harufu nzuri ambamo kutoka humo utapata furaha kubwa."

UJAUZITO NA KUZALIWA MTOTO

Muda wa kudumu ujauzito ni kipindi nyeti chenye matukio ya majaliwa kwa maisha ya mtoto. Tabia ya lishe ya mama pamoja na harakati za kimwili na za kisaikolojia ni mambo ya muhimu kwake na maisha ya kimbe kilichomo kwenye tumbo lake la uzazi.

Afya au maradhi ya mtoto, nguvu au udhaifu, ubaya wa sura au uzuri wa sura na tabia yake nzuri au mbaya na sehemu ya akili na busara, huanzishwa kwenye tumbo la uzazi la mama. Mmoja wapo wa wataalamu ameandika: "Wazazi wa watoto ama wanaweza kukua kwenye ngome ya afya au kwenye uharibifu wa maradhi. Ni wazi kwamba uharibifu wa maradhi si sehemu inayofaa kuishi roho ya milele au mwanadamu. Hii ni sababu ambayo kwamba wazazi wanaaminika kubeba wajibu mkubwa sana ikilinganishwa na uumbaji wote."

Kwa hiyo, kipindi cha mimba hakiwezi kufikiriwa au kufanywa kama cha kawaida. Mara tu mimba inapoanza, wazazi hupewa wajibu mkubwa.

Wazazi wanaweza bila kufahamu kusababisha matatizo ya aina nyingi, yaliyo mengi baina yao yanaweza kuwa magumu sana kurekebishwa, kwa sababu ya uzembe mdogo wakati wanapofanya kazi zao.

Yafuatayo ni mambo ambayoyanayofaa kuangaliwa:
Chakula: Kilengwa kilichomo kwenye tumbo la uzazi la mama yake, hula chakula na kukua kwa lishe ya damu yake. Kwa hiyo, chakula cha mama

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 217

kinatakiwa kuwa na virutubishi vya kutosha ili viweze kumpa mtoto vitu vya asili anavyo vihitaji, pia kwa ajili ya ustawi wa mama. Kwa hiyo, upungufu wowote wa vitamini, protini, mafuta, sukari au wanga katika ulaji wa mama inaweza kusababisha madhara katika afya ya mtoto. Imam Sadiq (a.s) alisema: "Chakula cha kilengwa kinapatikana kwenye lishe anayopata mama." 256. Tatizo kubwa ambalo linawapata wanawake wengi sana wajawazito ama katika kipindi fulani cha ujauzito au kipindi kikubwa cha ujauzito, hupungukiwa na ladha ya lishe bora, kwani hupatwa tabia ya tamaa ya vyakula fulani huku akisikia kinyaa kwa vyakula vingine. Kwa sababu kawaida hula chakula kidogo wakati wa kipindi hiki, lazima wahakikishe kwamba chakula chao si kizito na wakati huo huo kiwe na virutubisho vya kutosha ili kiweze kumpa mtoto vitu vya msingi.

Ufuatiliaji wa mpangilio ya chakula katika kipindi hiki cha ujauzito ni mgumu sana, hususan kwa watu wasio na uwezo wa kifedha na wale ambao hawana ujuzi wa ubora wa vyakula mbali mbali. Wajibu mkubwa anao baba ambaye anatakiwa kufanya jitihada kubwa kutoa vyakula vya msingi kwa mke wake. Kutokujali kwa upande wa baba kungeweza kusababisha madhara kwa mtoto anayekua, ambapo yeye ndiye atakaye wajibishwa hapa duniani na akhera.

Hali ya kiakili: Mama, wakati wa ujauzito anahitaji utulivu na anatakiwa apate hisia ya uzoefu wa kupenda maisha. Hii ina faida kwa mama na mtoto wake. Baba akiwa ni mwenye wajibu wa kumpa mke wake mazingira ya amani na uchangamfu, lazima ajaribu kwa bidii zaidi wakati wa kipindi cha ujauzito wake. Mume kwa wema na upendo, anatakiwa kuwa na mwenendo kwa namna ambayo mke wake anaweza kujivuna na kufurahi kuhusu yeye kuwa na ujauzito, lazima aone fahari kwamba maisha ya kiumbe kingine yanategemea kwake na kwamba anawajibu wa ustawi wake.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 218

Mjamzito aache miondoko ya kushtua. Mwanamke mwenye mimba anatakiwa kuepuka shughuli nzito na anatakiwa kupumzika sana. Kunyanyua kitu kizito au miondoko ya haraka ya mwili inaweza kusababisha madhara yasiyo rekebika kwake, mtoto au wote. Wanawake wajawazito wanatakiwa kuepuka kazi ngumu na waume zao wanatakiwa kujitolea kufanya kazi kama hizo.

Woga wa uchungu wa Kujifungua. Kujifungua mtoto mara nyingi huwa si kazi nyepesi. Maumivu ya uchungu wa kujifungua wakati mwingine huwa makali sana. Wanawake wajawazito mara nyingi huwa na wasi wasi kuhusu maumivu yaliyomo na uwezekani wa hatari yanayohusishwa na kujifungua mtoto, inayofuatiwa na kipindi cha kupata ahueni baada ya kujifungua. Ingawa wanawake wanatakiwa kustahamili ujauzito, uchungu wa kujifungua na kulisha watoto wao, wanamume pia wanatakiwa kugawana wajibu wa kulea watoto wao.

Ingawa kiinitete kinatungwa kwenye tumbo la uzazi la mwanamke pia yupo baba wa mtoto ambaye amefanya kazi muhimu katika kutungwa mimba. Kwa hiyo, wanamume wanatakiwa kuhakikisha kwamba wake zao wanapata maliwazo wakati wa kujifungua na kuwa tayari kusaidia endapo chochote kitahitajika haraka.

Ni kazi ya kibinadamu na kiislamu kwa wanaume kufanya kila wawezalo kwa wake zao wajawazito kwa kuwapa matunzo ya kitabibu na mahitaji ya kurahisisha kujifungua. Mwanaume anatakiwa kuwa na mke wake baada ya kuzaliwa kwa mtoto, lakini kama hawezi kufanya hivyo anatakiwa ampigie simu au amtumie ndugu zake wakae naye. Anatakiwa kujaribu kumrudisha nyumbani yeye mwenyewe na amsaidie kufanya kazi za nyumbani ili mke wake apate mapumziko ya kutosha na kurudisha tena nguvu iliyopotea. mwanaume anaye mfanyia mke wake wema, atazawadiwa na Mwenyezi Mungu. Mtume (s.a.w.w) alisema:

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 219

"Mwanaume aliye mbora sana miongoni mwenu ni yule anayemfanyia mke wake wema. Na mimi miongoni mwenu ni mwanaume mbora sana kuhusu kuwafanyia wema wake zangu."

Imamu Sadiq (a.s) alisema: "Mwenyezi Mungu na amrehemu mwanaume ambaye kufanya uhusiano mzuri na mke wake, kwa sababu Mwenyezi Mungu anamteua mwanaume kuwa mlezi wa mke wake."

Mwanaume anaye mtendea mke wake wema, atafanya mazingira ya familia yake kuwa machangamfu na ataimarisha misingi yake. Mke wake, kwa upande wake, kamwe hatasahau mapenzi ya mume wake na huba yake. Matokeo yake mshikamano wa ndoa unakuwa imara zaidi.

Msaada wa kuwalea watoto

Mtoto ni tunda la ndoa. Wote wawili wanamume na wanawake wametoa mchango katika kupatikana kwa mtoto na lazima wagawane matatizo na starehe zinazohusishwa kuwapo kwake. Kumlea mtoto ni kazi ya wazazi wote na si mama peke yake. Ingawa mara nyingi zaidi ni mama ndio wanaolea watoto wao na kuwalisha kuwaweka katika hali ya usafi na kadhalika, baba wasidharau juhudi hizo. Sio sahihi kwa mwanaume kudhani kwamba kazi ya kutunza watoto ni ya wanawake tu na kwamba wanaume hawana wajibu katika jambo hili. Si haki kwamba baba aondoke na kumwacha mke wake na mtoto ambaye analia na aende kupumzika kwenye chumba kingine.

Mpendwa ndugu! Mtoto wako ni wajibu wako pia. Unadhani ni haki kumwacha mkeo na mtoto anayelia ambapo wewe unapumzika kwenye chumba kingine? Hii ni njia inayofaa kufanya mambo nyumbani mwako? Kama vile unavyofanya bidii nje ya nyumba, mkeo hufanya bidii ndani ya nyumba; na anahitaji usingizi kama vile unavyohitaji usingizi. Yeye pia hafurahii kilio cha mtoto, lakini huvumilia.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 220

Ndugu yangu! Ubinadamu halikadhalika na Uislamu unakutaka wewe umsaidie mkeo katika kumlea mtoto wenu. Ama mnatakiwa msaidiane kwa pamoja au mpeane zamu. Kama mkeo anakosa usingizi kwa usiku wote na analala baada ya sala ya alfajiri, halafu usitegemee kwamba atakutayarishia staftahi kama siku zingine. Kwa kweli unatakiwa wewe mwenyewe utayarishe staftahi yako na ya mkeo ili pindi akiamka akute kila kitu tayari mezani. Mke wako hawajibiki kumlea mtoto wenu wakati wote unapokuwa haupo nyumbani au upo safarini. Kwa ufupi unatakiwa umsaidiea mkeo na mgawane wajibu wa kulea mtoto. Kwa njia hii, maisha ya familia yenu yataimarishwa.

Mwisho wanawake lazima pia wakumbuke kwamba waume zao hufanya bidii kupata riziki ya familia na wasitegemee kwamba wanaweza kuwadai zaidi ya uwezo wao. Wanawake wasitegemee waume zao ambao wamechoka kuanza kuwasaidia kulea watoto mara wanaporudi kutoka kazini.

KIKWAZO KIKUBWA KATIKA KUSULUHISHA TOFAUTI

Kikwazo kikubwa sana katika kusuluhisha ugomvi wa kifamilia ni ubinafsi na kiburi. Kwa bahati mbaya, watu wengi huathiriwa na tabia hizi. Watu kama hawa hupungukiwa na sehemu fulani ya akili ambapo hukubali tabia zao tu na kukataa za wengine na hawataki kukubali makosa yao. Hususan ni hatari sana ambapo ghasia ya tabia inafanikishwa na mtu mwingine yaani, kuwakosoa wengine kwa makosa yao. Wakati mwingine mume na mke wote husumbuliwa na tatizo hili kwa maana hiyo, watagombana kila siku. Kila mmoja atamlaumu mwenzake na wakati huo huo kila mmoja wao atakataa kuhusika kabisa na makosa yote.

Wakati mwingine kama upande moja tu utaumia kutokana na dosari hii ya kukoseana, kila mmoja atamwona mwenzake analo kosa na kwa kufanya hivyo watakuwa wanajikomboa kabisa kutokana na kulaumiana.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 221

Pale ambapo mume na mke wote wanakumbwa na usumbufu wa vurugu hii, ni vigumu sana kuwasuluhisha, kwa sababu hawatakuwa tayari kuzingatia ushauri wa mtu yeyote. Wakati ambapo kila mmojawao anasikiliza redio au anaangalia vipindi vya runinga vinavyohusu mambo ya familia, wataona dosari fulani ya tabia ambayo inaendekezwa na mwenza wake na kwa hiyo ataanzisha lawama zake hapo hapo. Lakini dosari yoyote ikizungumziwa inayogusa udhaifu wao watajifanya hawasikii na wataelekeza fikira zao kwenye mambo mengine. Wanaweza kununua kitabu kinachohusu maadili ya familia na kumpa mwenza wake, bila wao kuwa na hisia zozote za kuwa na hamu ya kusoma yaliyomo humo.

Ubinafsi unaweza kuwa mkali sana hivyo kwamba muathirika hataweza hata kutambua tatizo hilo. Katika hali kama hiyo, uhusiano baina ya wanandoa unaharibika na hata usiwezekane kuendelea. Matokeo yake ni, ama maisha yataendelea katika hali ya ugomvi, huzuni, kutokuwa na furaha au hata kutalikiana.

Kwa hiyo, inashauriwa kwamba wanandoa wote waache tabia ya ubinafsi na kiburi. Wanandoa ambao wanatatizwa na hali hii, wanatakiwa wapate muda wakae pamoja, na wawe kama majaji wawili waaminifu wazungumzie matatizo yao. Kila mmoja amsikilize mwenzake kwa umakini na bila upendeleo wowote. Kila mmoja wao anatakiwa kufahamu dosari zake bila kusahau hata iliyo ndogo sana pamoja na nia ya kuzirekebisha. Halafu wote wawili wanatakiwa waamue kujisahihisha wao wenyewe; lakini ni hapo tu ambapo wanahisi umuhimu wa uelewano wa kina na ambapo wote wanatamaani kufufua mapenzi yao na utulivu ambao ulikuwapo baina yao.

Hata hivyo, inapokuwa hakuna uwezekano wa kupatikana suluhu, wanandoa wanatakiwa kuwasilisha matatizo yao kwa mtu mwenye uzoefu, mwaminifu, mtambuzi wa kutegemewa na mwema. Kama mtu kama huyo

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 222

ni rafiki au ndugu, hiyo itakuwa nafuu yao kwa sababu wanaweza kumwambia kila kitu na kungoja hukumu yao. Lazima wamsikilize na kuupokea ushauri wake na kutia nia ya kuutekeleza kwa vitendo.

Kama ilivyo, kuamini ushauri wa jaji si rahisi, lakini mtu ambaye anajali familia yake na uimara wake, amani kudumu kwake anatakiwa kuvumilia na baadaye afurahie matokeo yake yenye manufaa.

Wazazi wa wanandoa wa aina hiyo, kama wanatambua matatizo ya kifamilia ya watoto wao, wanatakiwa kuwashauri wamuone Kadhi mwenye uzoefu, mwaminifu na nia njema. Wazazi hawatakiwi kuonesha upendeleo kwa mume au mke., Kwa njia hii, kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, matatizo yao yanaweza kutatuliwa.

Mwenyezi Mungu anasema kwenye Qurani Tukufu:

وَإِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَٱبْعَثُوا۟ حَكَمًا مِّنْ أَهْلِهِۦ وَحَكَمًا مِّنْ أَهْلِهَآ
إِن يُرِيدَآ إِصْلَٰحًا يُوَفِّقِ ٱللَّهُ بَيْنَهُمَآ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ عَلِيمًا خَبِيرًا ﴿٣٥﴾

“Na mkichelea kutakuwepo mfarakano baina ya mume na mke basi pelekeni muamuzi kutokana na jamaa za mume, na muamuzi kutokana na jamaa za mke, wakitaka mapatano mwenyezi Mungu atawawezesha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye Khabari.” (4:35)

TALAKA

Licha ya kwamba talaka ni kitendo halali, ni kitendo kinacho chukiza na ni kibaya kuzidi vitendo vyote.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 223

Imam Sadiq (a.s) alisema: “Oeni lakini msitalikiane, kwa sababu talaka inaweza kutetemesha Arsh ya Mwenyezi Mungu.”

Imam Sadiq (a.s) pia alisema: “Mwenyezi Mungu huipenda nyumba ambayo inakaliwa na wanandoa na huchukia nyumba ambayo wanandoa wametalikiana. Hakuna kitendo kinacho mchukiza Mwenyezi Mungu kuliko kutalikiana.”

Ndoa si kama kununua jozi ya viatu au soksi ambapo vitu hivi vikichujuka kwenye matamanio ya mmiliki wake, huvitupa na kununua jozi nyingine ya viatu. Ndoa ni makubaliano ya kiroho ambayo hufanywa na watu wawili kwa lengo la kuishi pamoja kama marafiki wa kuliwazana, na wapenzi hadi kifo chao. Makubaliano haya yameegemezwa kwenye matumaini haya hivyo kwamba msichana huwaacha wazazi wake na kuungana na mume wake.

Mwanaume hufanya jitihada na kufanya bidii kwa msingi wa makubaliano hayo ya kimungu. Hulipa gharama za harusi yake na hununua vitu muhimu kwa ajili ya maisha yake mapya na hufanya kazi kwa ajili ya faraja ya familia yake.

Ndoa si jambo la kukata kiu cha tamaa ya kimwili na wanandoa hawawezi kuiharibu kwa visingizio vidogo. Licha ya kwamba kutalikiana ni tendo halali, linachukiza sana na watu wanashauriwa kuepukana nalo kadiri iwezekanavyo.

Bahati mbaya, tendo hili ambalo linachukiza sana, limekuwa jambo la kawaida sana kwenye nchi za kiislamu na misingi ya familia imetikisika sana, hivyo kwamba kwa ujumla watu hawana imani tena kuhusu ndoa.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 224

Kuvunja ndoa inaruhusiwa hapo tu ambapo hali si ya kawaida na inalazimu iwe hivyo.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alisema: "Malaika Jibril aliniusia kuhusu wanawake sana hivyo kwamba nilifikiri kwamba wanamume wasiwataliki isipokuwa kama wanazini."

Kesi nyingi za kutalikiana hazina sababu za msingi, isipokuwa visingizio visivyo komaa. Yaani, sababu za kesi nyingi zaidi za talaka ni hafifu na hazifai kuwaathiri na kuwatenganisha wanandoa. Mume au mke, kwa sababu ya ubinafsi, anaweza kukuza jambo dogo na kuamua kwamba maisha yao ya ndoa lazima yakome.

"Bibi fulani mwenye umri wa miaka ishirini na nne, alimwambia mumewe awaalike wazazi wake kwenye chakula cha jioni chenye gharama kubwa. Kwa kuwa hakutekelezewa ombi hilo, alidai talaka."

"Mwanaume alimtaliki mke wake kwa sababu alikuwa anazaa watoto wanawake tu. Wanandoa hawa walikuwa na watoto wanawake watano."

"Mwanamke aliomba talaka kwa sababu mume wake aliamini mafundisho ya kumfikiri Mungu kwa njia ya tafakuri na hakuonesha kupenda maisha."

"Mwanamume alidai talaka kwa sababu alitaka kumuoa mwanamke tajiri."

"Mwanamke aliomba talaka kwa sababu mume wake alikuwa na tabia ya kuficha fedha zake kwenye mikono ya shati."

"Mwanaume alimtaliki mke wake kwa madai kwamba ana balaa tangu walipooana baba wa mume alifariki na ami yake alifilisika."

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:25 PM Page 225

Wanandoa ambao hawana heshima na busara, wanaweza wakanasa kwenye mtego wa mambo madogo kama hayo na kudai talaka.

Wanandoa wanaotaka kutengana, wasifanye haraka kutelekeza jambo hilo. Wanashauriwa wafikiri kwa uangalifu kuhusu athari na maisha yao ya baadaye kwa makini na halafu waamuwe. Hususan lazima watafakari kuhusu mambo mawili:

Jambo la kwanza: wanandoa wanaotaka kutalikiana kwa kawaida hutaka kuoa au kuolewa tena. Lakini lazima wakumbuke kwamba baada ya kutalikiana, watu wanaojulikana kama watalaka hawatakuwa na sifa nzuri kuhusu ndoa. Watu huwafikiria kuwa wenye ubinafsi na si waaminifu.

Baada ya kupata taarifa ya maisha ya ndoa ya siku za nyuma ya mwanamume na kutaliki, mwanamke anaweza kuwa na shaka kuhusu uaminifu wa mwanaume au tabia yake.

Mwanamke mtalaka ni nadra sana kupata fursa ya kuolewa tena. Kwa sababu wanaume kwa kawaida hawaoneshi kuvutiwa sana kuoa mwanamke mtalaka na hutilia shaka kuhusu uaminifu wake.

Kwa hiyo, mtalaka anawezekana akaishi peke yake kwa muda wote wa maisha yake na atateswa na upweke pia.

Kuwa mpweke ni hali ngumu sana na watu wengine wapweke hupendelea zaidi kifo kuliko maisha ya aina hiyo yasiyovumilika.

Mwanamke wa miaka ishirini na mbili ambaye aliachika, alijaribu kujiua mnamo usiku wa siku ya harusi ya dada yake. Alikuwa na mtoto mmoja.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:26 PM Page 226

Hata kama mwanaume anafaulu kuoa tena, haitajulikana kabisa kwamba maisha yake mapya yatakuwa mazuri zaidi kuliko ya mke wake wa mwanzo. Mke wake wa pili anaweza kuwa mbaya zaidi. Mwanaume wa aina hii hupendelea kumtaliki mke wa ndoa ya pili na kurudi kumuoa mke wa kwanza. Lakini kwa kawaida huwa wamechelewa sana.

Mwanaume wa miaka themanini alisema mahakamani; "Nilikuwa na maisha mazuri nilipomuoa mke wangu wa ndoa ya kwanza, takriban miaka sitini iliyopita. Lakini baada ya muda alianza kunifanyia ubaya kwa hiyo nikamtaliki. Nilioa wanawake wachache baada ya hapo lakini nilihisi kwamba mke wangu wa kwanza alikuwa mwaminifu zaidi miongoni mwao. Nilimuona na nikampa rai ya kurudiana naye. Yeye, ambaye pia alichoka maisha ya upweke alikubali na sasa tunataka kuoana tena."

Mwanaume alimtaliki mke wake wa pili kwa sababu hakutaka kuwalea watoto wawili aliozaa kwenye ndoa yake ya kwanza. Halafu akaamua kumuoa tena mke wake wa kwanza ambaye alimtaliki miaka mitano ya nyuma.'

Jambo la pili: Wanandoa ambao wanataka kutengana lazima wafikirie pia suala la watoto wao. Faraja ya watoto imo kwenye familia yenye wazazi wote wanao ishi pamoja na wanawalea kwa pamoja.

Baada ya kuvunjika kwa maisha ya familia, watoto hufadhaika sana. Kama ni baba yao tu anaye watunza, hawatakuwa na maisha na mama yao wa kambo. Mama wa kambo si tu kwamba wanashindwa kutekeleza kama mama halisi, lakini wanaweza kufikiri watoto wa kambo ni mzigo. Mama wa kambo wengine huwanyanyasa watoto wa kambo na kuwafadhaisha kwa kukusudia na baba zao hunyamaza kimya.

Bibi harusi wa miaka kumi na nne ambaye alitaka kujiua alisema akiwa hospitalini. Wazazi wangu walitengana nilipokuwa na mwaka mmoja.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:26 PM Page 227

Baba yangu alioa tena baada ya mwaka mmoja na nusu na sasa tunaishi wote. Mama yangu wa kambo alikuwa na desturi ya kunipiga na hata alinichoma moto kwa chuma mara kadhaa. Baba yangu licha ya kuwa na uwezo wa kifedha alinikataza nisisome. Takriban mwezi mmoja uliopita baba yangu alinioza kwa mtu mwenye umri wa miaka arobaini na tano.

Msichana wa miaka kumi na tatu alijinyonga. Msichana huyu aliishi na kaka zake wawili. Mmojawapo wa hao kaka zake alisema; "Wazazi wetu walitengana miaka takriban mitatu iliyopita. Mama yangu aliolewa tena na mwanamume mwingine na baba alikufa miezi miwili iliyopita. Ilikuwa saa 12:30 jana jioni nilikuja nyumbani nikamkuta dada yangu amejinyonga."

Pia, kama mama anachukua wajibu wa watoto wake, basi watakosa baba halisi ambaye angewatunza. baba wa kambo mara nyingi ndiye sababu ya kukosekana furaha kwa watoto wake wa kambo.

Mwanamke alimsaidia mume wake wa ndoa ya pili kumfunga mtoto wa kambo mwenye umri wa miaka nane kwenye kitanda. Halafu wakafunga mlango na wakaondoka kwenda matembezini. Waliporudi nyumbani,walikuta mtoto wao ameungua moto hadi kufa kwa sababu ya moto uliounguza nyumba.

Talaka huharibu familia na huwaacha watoto wanatangatanga hawana hifadhi. Watoto mara nyingi huteseka kwa sababu ya ubinafsi wa wazazi wao.

Watoto wanne wenye umri wa miaka kumi na mbili, tisa, sita na minne walikwenda kwenye kituo cha polisi. Mtoto mwanamme mwenye umri mkubwa zaidi alisema: "Wazazi wetu walitengana muda fulani uliopita. Wakati wote walikuwa wanabishana na walikuwa na tabia ya kugombana

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:26 PM Page 228

kila siku mchana na usiku. Sasa wametalikina, hapana mmojawao ambaye yupo tayari kutulea sisi."

Watoto ambao hawana mlezi anayefaa na mazingira ya familia, mara nyingi hukengeuka. Kutokupata elimu ya kutosha na mtu mwenye huruma katika maisha yao, huwafanya wasumbuliwe na hisia za udhalili. Wanaweza hata kufanya uhalifu wa viwango mbali mbali, wakati wa utoto au utu uzima.

Mtu anaweza kutambua jambo hili na kusoma matukio kwenye magazeti kila siku.

Kwenye utafiti uliofanywa kwenye kituo cha kurekebisha vijana, ni wazi kwamba katika vijana wahalifu mia moja kumi na sita wa kituo hiki, watu themanini walithibitisha kwamba mama zao wa kambo waliwanyanyasa ndio sababu wakafanya uhalifu."

Mpendwa bibi na bwana! Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kwa ajili ya watoto wako wasio na kosa, kuweni wasamehevu nyinyi kwa nyinyi wanandoa. Msikuze matatizo madogo na msipende kung'ang'ania ubishi. Msitafutane makosa nyinyi kwa nyinyi. Fikirieni mambo yenu ya siku zijazo na watoto wenu. Kumbukeni watoto wenu wanawategemeeni nyinyi na wanatumaini kupata furaha yao kutoka kwenu. Wahurumieni na msiharibu maisha yao.

Kama mkidharau matamanio yao ya ndani na kama mkivunja nyoyo zao ndogo, hamtaweza kuepuka athari ya masikitiko yao. Kwa hiyo, hamtaweza kuwa na maisha yenye faraja pamoja.

Kanuni za ndoa.qxd 7/20/2005 5:26 PM Page 229

UFAFANUZI

Hadithi zilizorejelewa katika kitabu hiki zimenukuliwa kutoka katika vitabu vifuatavyo:

1. Wasail al Shia.
2. Bihar al-Anwar, juz.
3. Dar Aghushe khushakhtih.
4. Mahajjat al- Bayda.
5. Mustadrak.
6. Shafi
7. Majma al Zawaid.
8. Usul al Kafi.
9. Makarim al Akhlaq.

Na anayetaka maelezo zaidi kuhusu hadithi hizi, anashauriwa kusoma kitabu cha Kiingereza: ***"PRINCIPLES OF MARRIEGE"***